

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Hamsini na Nne - Tarehe 24 Agosti, 2011

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kufuatia kikao cha pamoja cha Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge kilichofanyika jana mchana Wajumbe walikubaliana na kupanga utaratibu wa namna watakavyoshiriki katika mazishi ya Mheshimiwa Mussa Khamis Silima, yatakayofanyika leo tarehe 24 Mwezi wa Agosti 2011 Zanzibar. Walikubaliana kuwa mwili wa Marehemu uchukuliwe Dar es Salaam na kwenda Zanzibar moja kwa moja na Waheshimiwa Wabunge watasafirishwa kwa ndege itakayowachukua kutoka Dodoma hadi Zanzibar kwenye mazishi na kuwarudisha Dodoma baadaye leo hii.

Vile vile, wajumbe walikubaliana kuwa makundi yafuatayo ndiyo yatakayokwenda kushiriki katika mazishi hayo. Kwanza Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, pia Wajumbe wa Tume ya Huduma za Bunge, tatu wajumbe nane kutoka Zanzibar na nne ni baadhi ya Wabunge kutoka Kamati ya Nishati na Madini pamoja na Menejimenti ya Ofisi ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu utaratibu wa usafiri ni kwamba Ofisi ya Katibu wa Bunge imepata ndege mbili, moja yenye uwezo wa kubeba abiria kumi na moja na nyininge yenye uwezo wa kubeba abiria 49 hivyo jumla ya watakaohudhuria mazishi ni 60. Ndege ya kwanza itakayoondoka itabeba abiria 11 kama nilivyosema na itaondoka Dodoma saa Nne asubuhi hii. Ndege ya pili itakayobeba abiria 49 itaondoka saa nne na nusu asubuhi ya leo. Wote wanaosafiri wanaombwa kufika uwanja wa ndege wa Dodoma kuanzia saa tatu na nusu asubuhi hii.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli za ibada na mazishi zitaanza saa sita na nusu mchana huko Zanzibar na mazishi yatafanyika saa saba mchana mara baada ya mazishi ndege zitaanza kuondoka kurudi Dodoma, Ndege inayobeba abiria 49 itaondoka Zanzibar kurudi Dodoma saa tisa alasiri.

Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na ratiba ya Mkutano wetu wa Bajeti unaoendelea, Wajumbe jana walikubaliana kwamba tarehe ya kumaliza Mkutano ibakie kuwa ni ile ile tarehe 26 Agosti, 2011 siku ya Ijumaa, hivyo kilichobadilishwa ni muda wa kukamilishwa kuitishwa Bajeti ya Wizara zilizobakia.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge litakuwa linakamilisha Bajeti saa saba na robo mchana badala ya jioni kila siku kama ilivyokuwa, na hivyo tutakamilisha Bajeti ya Wizara ya Fedha tarehe 26 Agosti, 2011. Waziri Mkuu atahitimisha shughuli za Mkutano huu kwa kutoa Hoja ya Kuahirisha Bunge jioni ya tarehe 26 Agosti, 2011.

Aidha, semina ambayo ilikuwa ifanyike tarehe 27 Agosti, 2011 nayo imeahirishwa hadi mwanzoni mwa Mkutano wa Bunge wa Tano.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kuitia kwa kifupi sana wasifu wa Mheshimiwa Marehemu Mussa Khamis Silima aliyekuwa Mbunge Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuitia Baraza la Wawakilishi Jimbo la Uzini. Marehemu alizaliwa tarehe 14 April, 1951 Kijiji kwa Kiboje Mwembeshauri, Mkoa wa Kusini Unguja.

Alipata elimu ya Msingi katika shule ya Kiboje Mkwajuni kuanzia mwaka 1961 na kuhitimu darasa la saba mwaka 1968. Alipata elimu ya Sekondari katika shule ya Sekondari ya Uzini kuanzia mwaka 1969 mpaka mwaka 1970 alipomaliza Kidato cha nne alijunga na shule ya sekondari ya Karume kwa masomo ya A-level kuanzia mwaka 1971 na kuhitimu Kidato cha Sita mwaka 1972.

Aidha, Marehemu Mussa Khamis Silima alisomea Stashahada ya Ualimu katika Chuo cha Ualimu cha Nkhuruma Zanzibar kuanzia mwaka 1981 hadi 1983. Utumishi wake katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Marehemu alianza kazi katika Wizara ya Elimu Zanzibar mwaka 1973 akiwa Mwalimu wa kawaida mpaka mwaka 1988 alipopandishwa cheo na kuwa Mkuu wa shule mpaka mwaka 1999 alipopangiwa kuwa Afisa Mratibu wa wanafunzi nafasi aliyoshikilia mpaka mwaka 2001.

Marehemu Musa Khamis Silima aliendelea na utumishi wake uliotukuka katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo mwaka 2001 alihamishiwa Uwanja wa Amani kama Afisa Mkuu nafasi ambayo alishikilia mpaka alipoacha mwaka 2010 na kugombea Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Maisha yake katika Siasa, Marehemu Mussa Khamis Silima hadi anafariki dunia alikuwa ni Katibu Mkuu Msaidizi wa Jumuiya ya Wazazi, Mwakilishi wa Jimbo la Uzini na Mbunge wa Bunge la Kumi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuititia Baraza la Wawakilishi. Marehemu alikuwa ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kifo chake Marehemu Mussa Khamis Silima alifariki mnamo tarehe 23 Agosti, 2011 katika Hospitali ya Muhimbili Dar es Salaam alipopelekwa baada ya kupata ajali ya gari iliyotokea Dodoma usiku wa Tarehe 21 Agosti, 2011, ajali ambayo iligharimu pia maisha ya Mke wake Bi Mwanakheri Fakhari ambaye alifariki papo hapo ajalini na kuzikwa tarehe 22 Agosti, 2011 Zanzibar.

Waheshimiwa Wabunge, Marehemu ameacha watoto watano, watatu wa kiume na wawili wa kike. Tunaomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahala pema peponi, Amina.

Waheshimiwa Wabunge kwa kumalizia nitaje orodha ya watakaoshiriki kutegemeana na usafiri wa ndege zitakazopatikana. Ndege ya kwanza ya Wabunge kumi na moja inayoondoka saa tatu na nusu kama nilivyoeleza itaongozwa na Mheshimiwa Spika Anne Makinda, Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni Freeman Mbewe, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Agripina Buyogera, Ndugu John Joel, Kaimu Katibu wa Bunge, Ndugu Amina Magina Mhasibu, Ndugu Suzan Hokororo kutoka Ofisi ya Spika, Ndugu Alphonse Mwakasege Kutoka Ofisi ya Spika na Ndugu Herman Berege.

Waheshimiwa Wabunge ndege ya pili itakuwa na Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo Kamishna, Mheshimiwa Godfrey Zambi - Kamishna, Mheshimiwa Dokta Maua A. Daftari Kamishna, Jaji Fredrick Werema, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Zaynab M. Vullu, Mheshimiwa Agustino Lyatonga Mrema. Mheshimiwa Kabwe Zuber Zitto, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa Magreth S. Sitta, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa January Y. Makamba, Mheshimiwa Mahamoud Mgimwa, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Abia M. Nyabakari, Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi, Mheshimiwa Yusuph A. Nassir, Mheshimiwa David E. Silinde, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib, Mheshimiwa Asaa Othman, Mheshimiwa Amina Andrew Makilagi, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Said Mussa Zuber, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour,

Mheshimiwa Juma Nhunga, Ndugu Kitolina Kippa, Ndugu Abdallah Ramadhani, Ndugu Said Yakub, Ndugu George Seni, Ndugu Abdallah Mwanga, Ndugu Josse Mwakasyuka, Ndugu Pamela Pallangyo, Ndugu Eliufoo Ukhotya na Waandishi wa Habari.

Waheshimiwa Wabunge tuendelee.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatayo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU):

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2011/2012.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MHE. PINDI H. CHANA -MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka 2010/2011 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MHE. TUNDU A. M. LISSU-MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Katiba na Sheria Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zitto.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 51 ya Kanuni za Bunge, inayohusiana na masuala yanayohusu Haki za Bunge, ikinsomwa kwa pamoja na Kanuni ya 55(3) inayohusu hoja ambazo zinaweza kutolewa bila taarifa na hapa nazungumzia Kifungu cha (f) Kuhusu jambo lolote linalohusiana na Haki za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana sote, Wabunge na Watanzania, tumesikia taarifa ambayo Katibu Mkuu Kiongozi ameitoa kuhusiana na suala linalomhusu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini. Katika maelezo yake kwanza, ameonesha kwamba tuhuma ambazo Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, alizitoa hapa Bungeni dhidi ya Ndugu Jairo kwamba tuhuma zile wamezikuta hazipo. Lakini pili Katibu Mkuu Kiongozi akawa ameagiza kwamba Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini arudi ofisini leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani ya Bunge hili, alizungumza kwamba ingekuwa yeye angekuwa tayari ameshamchukulia hatua Ndugu Jairo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kusema kwamba Bunge linaweza likawa ni Mahakama likaendesha kesi na kuamuru, lakini kwa Mujibu wa taratibu za *Commonwealth* kila mhimili una majukumu yake, hasa ukizingatia kwamba katika maelezo ya Katibu Mkuu Kiongozi alisema kwamba Ndugu Jairo anaweza akashtaki Wabunge *for defamation* jambo ambalo naona ni kuingilia kabisa hadhi ya Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika nilikuwa naomba nitoe hoja kwamba Bunge lisitishe kujadili shughuli yeoyote ya Serikali iliyopo mbele yetu mpaka Serikali itakapoleta hapa Bungeni taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na suala hilo ili iweze kujadiliwa kwa

sababu aliyejkuwa *accused* ni *Civil Servant*, aliyeeweza kusimamia hilo shtaka bado ni *Civil Servant*. Kwa hiyo, Bunge nafasi yake ni kama imekuwa imepokwa, haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nitoe hoja na Wabunge wote naomba waunge mkono hoja hii, kwamba tuzuie shughuli za Serikali mpaka hapo taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali itakapokuja hapa Bungeni kwa ajili ya kujadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja

MHE. TUNDU A. M. LISSU:Mheshimiwa Naibu Spika Naafiki.

NAIBU SPIKA:Waheshimiwa Wabunge nawashukuru. Namshukuru Mheshimiwa Zitto ametoa hoja yake sote tumeisikia na imeungwa mkono vya kutosha. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge hoja hii ni nzito kweli, maana hoja iliyotolewa, unajua shida ya mambo ya kushtukizwa ndiyo hayo!(*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyotolewa hapa ni kwamba Bunge lisitishe kuendelea kujadili shughuli yejote ya Serikali hadi taarifa ya CAG iweze kufika hapa Bungeni, na ndiyo hoja ambayo imeungwa mkono. Kabla sijasema chochote naona Waziri wa Nchi amesimama tafadhalii Waziri wa Nch, i Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, najua jambo hili lina *Public Interest*, lakini pia linagusa miyo mingi ya Waheshimiwa Wabunge kama ulivyoona wameunga mkono. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilitaka njirejeshe kwenye Kifungu kile kile alichokisoma Mheshimiwa Zitto Kabwe, Kifungu cha 51.

Kwa kuwa jambo hili linahusisha Haki na Madaraka ya Bunge kifungu kinasema Mbunge anayetaka kama alivyoanza Mheshimiwa Zitto, Mbunge anayetaka kuwasilisha jambo ambalo anaamini linahusiana na Haki za Bunge atafanya hivyo wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa shughuli za Bunge uliowekwa na Kanuni hizi na atakuwa amemwarifu Spika mapema kuhusu kusudio lake hilo na jambo ambalo anataka kuwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilitaka kukumbusha tu Kiti chako kwamba jambo hili ultakiwa uwasilishiwe mapema, ili uweze kuamua kwa mujibu wa Kifungu hiki, kama jambo hili linagusa Haki na Kinga za Wabunge.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae. Wakati nasoma matangazo mbalimbali kuhusiana na kifo cha mwenzetu na mazishi yake na mpangilio wa mazisha yake nilipata taarifa fupi ya maandishi kutoka kwa Mheshimiwa Zitto ya kusudio ya kufanya hivyo. Lakini kwa kweli haikunipa nafasi ya kuweza kuifanya kazi vizuri. Tuseme kwa kweli maana ya hoja iliyotolewa imetolewa kiutaratibu na imeungwa mkono na Wabunge wengi humu ndani.

Lakini hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge ni nzito ambayo mimi peke yangu siwezi kuitolea uamuzi hapa. Ninachowaomba Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Uongozi kama mpo ninawaomba tukutane *Speaker's Lounge* sasa hivi.

Wakati Waheshimiwa Wenyejiti wanakwenda huko namwombwa Mheshimiwa George Simbachawene avae josh, kiutaratibu wakati huo mimi naendelea na session ya maswali atakapokuwa George Simbachawene atachukua nafasi hii. Tuna hakika kabla ya kipindi cha maswali kuishi, Kamati ya Uongozi itakuja kutoa taarifa ya nini kinachopaswa kuendelea. (*Makof*)

MASWALI NA MAJIBU

Na. 480

Miradi ya maji kijiji cha Jojo, Iwindi na Ihango

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE aliuliza:-

Miradi ya maji kijiji cha Jojo, Iwindi na Ihango imechukua muda mrefu licha ya Serikali kuahidi kuwa miradi hiyo ingechukua muda mfupi:-

Je, ni lini Serikali itaanza kazi ya kujenga miradi hiyo ili wananchi wa vijiji waweze kujipatia maji safi ya kunywa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mch. Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijiijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kuitia programu ya maji na usafi wa mazingira vijiji inatekeleza mradi wa vijiji 17 vilivyochanguliwa. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 jumla ya shilingi bilioni 2.2 zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji hivyo.

Aidha, mpaka sasa kiasi hiki cha fedha hakijapatikana. Halmashauri katika vipaumbele vyake imeamua kutekeleza mradi huu kwa awamu kwa kuanza na vijiji vyenye uhaba mkubwa wa maji na idadi kubwa ya wakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usanifu wa miradi hii umefanyika na kukamilika kuitia Mtalaam Mshauri Tanzania *Association of Environmental Engineers in association with NIRAS SCANAGRI* na taarifa zimewasilishwa Wizara ya Maji ili kupata kibali cha kutangaza zabuni ya kujenga miundombinu miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huu inaanza mwaka 2011/2012 kwa kuhusisha vijiji vitatu (3) vya Iwalanje, Shongo na Igale. Katika Kijiji cha Iwalanje vitajengwa vituo 10 vya maji, Kijiji cha Shongo vituo 19 na Kijiji cha Igale vituo 17. Katika mwaka huu zimeidhinishwa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya miradi hiyo ya maji.

Aidha, Halmashauri imezingatia katika vipaumbele vyake vijiji vilivybaki katika awamu ya pili, tatu na nne ya utekelezaji wa programu ya maji na usafi wa mazingira vijiji.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Naibu Spika, jibu la msingi ambalo nimejibowi ni kwamba zilikuwa zimetengwa mwaka jana shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyoko Mbeya Vijiijini na fedha hizo hazikupatikana na mwaka huu naambiwa kwamba zimetengwa bilioni 1.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo.

- (a) Je, Serikali itanihakikishie vipi kwamba fedha hizo zitapatikana kutekeleza miradi hiyo?
- (b) Kwa kuwa miradi mingi ambayo inafadhiliwa na fedha za Benki ya Dunia imekwama na haitekelezwi mara nyingi. Je, Serikali haloni kwamba sasa ni wakati muafaka kutafuta chanzo kingine cha fedha ili kutekeleza miradi yote ambayo ilikuwa inafadhiliwa na Benki ya Dunia? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Kabla ya majibu naomba sasa nimpishe Mheshimiwa George Simbachawene, Mwenyekiti wa Bunge ili aendelee na shughuli hizi kama tulivyokubaliana.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) Alikalia Kiti

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli miradi mingi iliyokuwa kwenye vijiji kumi (10) haikuweza kutekelezwa na sasa hivi Serikali kwa kuitia mpango wa miaka mitano utaelekeza fedha nyingi za ndani ili tuweze kutekeleza vile vijiji ambavyo tayari usanifu wake umekamilika.

MHE. MOSES JOSEPH MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hivi karibuni kumekuwa na miradi hii ya maji ambayo inafadhiliwa na Benki ya Dunia kama ambavyo Serikali imekuwa ikitupatia taarifa.

Kwa kuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu katika vijiji mbalimbali nya Jimbo la Kasulu Mjini vina tatizo kubwa la maji na kampuni iliyopewa kuweza kufanyakazi ya usanifu wa miradi ya maji kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu hadi dakika hii hawajaweza kuwasilisha taarifa Wizarani jambo ambalo linaashiria uzembe kwa sababu kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Maji ya mwezi Februari ilionekana bado hawajawasilisha taarifa hizi Wizarani.

Naomba kupata kauli ya Serikali inachukua hatua gani kwa uzembe wa watendaji wa Halmashauri ya Kasulu ikiwa ni pamoja na kampuni iliyopewa kazi ya kuweza kufanya usanifu wa miradi ya maji ambayo mpaka leo hii wananchi wa Kasulu hatujui hatma ya tatizo la maji litaisha lini?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ilmwajiri mtaalam mshauri na katika kutekeleza kazi zake hajamaliza ile kazi ambayo ilikuwa imepewa. Sasa kauli ya Serikali ni kwamba tutakwenda kufuatilia na tuone ule mkataba aliopewa ulikuwa unaisha lini na ni kazi zipi ambazo alitakiwa afanye kabla hatujachukua hatua zingine. (*Makof*)

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Mbeya Vijiji linafanana kabisa na tatizo lililoko llemela katika vituo viwili ambavyo usanifu ulishafanyika Igombe na Kayenze mradi upo lakini haufanyi kazi tangu mwaka 2005/2006. Je, Waziri anasema nini kuhusu mradi au akautembelee ili huo mradi uanzesha kazi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubali kwamba miradi hii ilikuwa inasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya llemela. Sasa kwa ruhusa yako naomba naomba niende nikatembelee ili niweze kuona tatizo ni nini.

Na. 481

Kuondoshwa kwa Mifugo Wilayani Kilombero

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE aliuliza:-

Kutokana na agizo la Mheshimiwa Rais kuwa Mkoa wa Morogoro uwe ghala la Taifa la Chakula, Wilaya ya Kilombero ni eneo linalotegemewa sana kwa utekelezaji wa agizo hilo:-

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya kuondoshwa kwa mifugo katika Wilaya hiyo ambayo ni mingi na inasababisha uharibifu mkubwa wa vyanzo nya maji na ardhi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mifugo iliyopo katika Bonde la Kilombero ni mingi ukilinganisha na ukubwa wa eneo lillipo. Mifugo iliyopo katika eneo hili ni 66,426 ikilinganishwa na eneo linalofaa kwa malisho ambalo ni hekta za mraba 120,000.

Serikali imechukua jitihada mbalimbali za kuondoa mifugo hiyo kufuatia agizo la aliyejukua Makamu wa Rais Dkt. Ally Mohamed Shein la kutunza mazingira na ardhi oevu katika mwaka 2006. Kati ya mwaka 2006 na 2009 idadi ya mifugo iliyondolewa ni 27,929 na mifugo mingine 8,674 ilizwa katika mnada wa Pugu, Dar es Salaam katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya Serikali ni kuimarisha utekelezaji wa mpango wa Matumizi bora ya ardhi kwa kutenga maeneo ya wakulima na wafugaji, kuendelea kuzuia mifugo kuingia ndani Wilaya bila utaratibu, kuendelea kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu ufugaji wa kisasa na wenyewe tija, kuhamasisha uanzashaji wa Vyama vya Ushirika wa wafugaji unaozingatia athari za kimazingira na kutunga sheria ndogo kuzuia wafugaji kuchunga katika vyanzo vya maji na maeneo ambayo hayamo katika Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya ni Wilaya ambayo ina vyanzo viwili vya umeme unaotegemewa. Vile vile ni ghala la chakula kitaifa. Vile vile ina mkataba wa Kimataifa wa RAMSA kwa kutunza eneo chepechepe ambalo ni hili ile ya Wilaya ya Kilombero na Serikali imekiri ya kwamba kweli mifugo iliyoko Kilombero ni mingi na mingi mno hata kupita hata maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

(a)Je, Serikali haioni sasa kwamba wao ndio wachochezi wakubwa wa migogoro kati ya wafugaji hawa Wasukuma na sisi wakazi wa Kilombero? (*Makofii*)

(b)Hivi karibuni takribani mwezi mzima kumekuwa kukiingizwa mifugo kinyemela kupita Kata za Chita, Melela na ikisambazwa kwenye Kata zingine au vijiji vingine vya Kilombero na hii mifugo imesemekana ni wale ambao wafugaji wamefukuzwa huko Iringa sasa wanaingia Kilombero. Kwa kweli ile mifugo ni mingi kuliko wakazi wenyewe wa Kilombero. Je, Serikali ina tamko gani, itatuacha hivi sisi tukigombana na wafugaji ambao ni watani zetu ni ndugu zetu mpaka lini? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linalozungumzwa hapa ni jambo kubwa na ambalo linahusu uhai wa taifa letu. Si jambo ambalo sisi tunapuuza. Anavyosema Mheshimiwa Mbunge hapa ni jambo la msingi kabisa. Maelekezo ya kuwaondoaa watu katika maeneo haya oevu yalitolewa na Serikali.

Wakati tulipoamua kwamba sasa tunasitisha zoezi la kuwachukua hawa wafugaji na kuwapeleka katika maeneo mengine maelekezo yale yalipelekwa na Serikali na yalitolewa na Serikali. Nataka niseme la kwanza hapa kabisa kwamba Serikali ndio inaendekeza jambo lile si kweli hata kidogo. Serikali ndio imekuja na mpango unaoitwa Mpango wa Matumizi bora ya ardhi. Tumemsikia hapa Waziri wa Mifugo alikuja akazungumza aliulizwa swali hapa kutoka Tanga.

Tukitaka tuwaondoe wale wafugaji walioko pale Tanga tukasema hapana akasema kwamba hawawezi kuondolewa pale isipokuwa tufanye mambo yafuatayo, ukitaka kuondokana na tatizo hili ukiwafuata hawa Wasukuma hawa wanaozungumzwa hapa watakuambia sisi kilimo kile kule cha Mpunga na Mchele Kimeendelezwa sasa hivi kwa sababu tunatumia makisai watasema hivyo. Wakisema hivyo wala simaanishi kwamba mimi nataka niwatetee hapa wafugaji.

Lakini wafugaji tunawahitaji, wakulima tunawahitaji, wavuvi tunawahitaji na wale wengine wote tunawahitaji katika nchi hii. *The bottom line is* unafanya nini lazima uzungumze habari ya ya matumizi bora ya ardhi. Useme hapa ni kwa ajili ya ng'ombe, hapa ni kwa ajili ya mbuzi, hapa ni kwa ajili ya kilimo, hapa ni kwa ajili ya uvuvi. Useme hivyo kwa sababu vyote hivi unavahitaji. Ukitaka waende wakachunge mahali popote waharibu mazingira *equally* ni makosa kwa sababu tutakosa maji na tukikosa maji hapa tutapata matatizo.

Tunataka kusema nini kama Serikali, tunachosema hapa mambo makubwa matatu, la kwanza sisitiza matumizi bora ya ardhi. Pili, sisitiza kutumia sheria na kusimamia sheria katika nchi hii. Tatoo elimu kwa watu wako waambie watu wako kwamba ng'ombe kama ameshazaar kwa muda mrefu hatoi tena maziwa vuna, ukisema ondoaa hawaelewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelieleza jambo hili kwa kirefu. Naomba nimalizie (b) yake hapa anasema kwamba kuna tatizo ambalo limetokea wako wengine wameingia *recently*. Nimezungumza na *District Commission* ni kweli anachosema Mchungaji Rwakatare, ni kweli wako watu wameingia katika maeneo yale. (*Makofii*)

Kwanza tunataka Mkuu wa Wilaya atuambie na ametueleza ni nani aliyeruhusu mifugo ile iende pale kwa wakati huu wakati sisi tulishatoa tamko hilo? Kwa hiyo, hii habari anayosema hapa Mkuu wa Wilaya amechukua hatua wamekamata ng'ombe wale, tumemwambia akamate ng'ombe wale wote na tupate maelezo ya kina kwamba ni nini kilichosababisha ng'ombe wale wakaenda pale.

Baada ya hapo tutawasiliana na Mheshimiwa Mbunge, kujua hatua gani ambazo zitakuwa zimechukuliwa hapa, nitaongea pia na Mkuu wa Mkoa kuhusu jambo hili. (*Makofî*)

MHE. MTUTURA ABDALLAH MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyeleza Mheshimiwa Waziri sisi tumetekeleza tumetenga maeneo, Kata ya Mlingoti Mashariki, Kata ya Ngapa na Kata ya Muwesi, lakini bado tuna mifugo mingi sana katika Kata ya Mchoteka na kwa kuwa wafugaji hawa wana miili mikubwa na miili ya sisi watu wa Tunduru ni midogo midogo hatuna uwezo wa kuwakabili. Je, kama Serikali imeshindwa wanaturuhusu sisi tuanze kuchukua mazoezi ili tuweze kukabiliana nao? (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu watu wenye miili mikubwa na wenye miili midogo mnafanyaje?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimwambie chonde chonde huko tusiende kabisa yaani sisi tutanza kukaa hapa tuanze kusema kwamba sasa wale Wayao wa Tunduru waanze kujandaa vizuri kwa misuli na kadhalika. Hiki kitu hatuwezi kuruhusu katika nchi yetu. Nchi hii inaamini katika utawala bora, katika utawala wa sheria.

Mheshimiwa Mtutura tumemsikia. Tunachosema hapa hakuna cha mwili mkubwa, hakuna cha watu warefu wala watu wafupi, sheria ya nchi ifuatwe, wao wametenga maeneo pale mimi nimekwenda Tunduru na mimi nimefanya kazi Tunduru miaka kumi.

Hapo anapazungumza mimi napafahamu hatuwezi kuruhusu wale watu waende pale kama wamesema Wilaya ya Tunduru tayari wametenga eneo, wamesema kwamba ardhi hii tunaitenga tunaiweka katika matumizi bora ya ardhi maelekezo tunayotoa hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa wasimamie jambo hili kuhakikisha kwamba linatekelezwa kama liliyozungumza na Mheshimiwa Mtutura atuamini tutashirikiana na ye ye kuhakikisha kwamba huo mpango wa matumizi bora wa ardhi unaufatwa.

Na. 482

Fidia kwa Mashamba yaliyochukuliwa na Jeshi la Nchi Kavu na Majini

MHE. SABREENA H. SUNGURA aliuliza:-

Serikali imechukua maeneo ya wananchi katika Kata Kibirizi, Burunge, Nyantore na Kagongo kwa ajili ya Jeshi la Nchi Kavu na majini lakini wananchi hao Hawajalipwa fidia:-

Je, ni lini wananchi hao watalipwa fidia?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, eneo lilioombwa kutumiwa na Jeshi la wananchi wa Tanzania (JWTZ) eneo la Kibirizi kuanzia *RAS* Nondwa hadi Kalalangambo lina ukubwa wa kilomita za mraba kumi (10)

Mheshimiwa Spika, kutokana na mahitaji ya kiulinzi JWTZ iliomba Serikali ya Mkoa na Wilaya na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji eneo hilo kwa ajili ya kujenga kituo cha Kijeshi kukidhi mahitaji ya ulinzi na usalama.

Aidha hatua za awali za kujua kiasi cha tathmini ya fidia ya maendelezo, yaliyo katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na mazao na mali za wananchi bado iko kwenye mchakato. Inategemewa si muda mrefu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa itatoa taarifa kwa Serikali ya Mkoa, Wilaya na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji kuhusu kuanza kwa zoezi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo eneo hilo halijaporwa kutoka kwa wananchi na wala Serikali haina mpango wa kulipora isipokuwa ni kilitwaa kwa faida ya Umma kwa faida ya wananchi wenyewe katika kuimarisha ulinzi na usalama wao na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria taratibu na kanuni zinazohusiana na mazoezi ya utwaaji wa ardhi ikiwemo ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaostahili zitazingatiwa

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na usumbufu mkubwa wa Serikali kuwa imechukua maeneo kabla ya tathimini:-

(a) Je, Waziri haoni sasa kuna haja kwamba iwe inafanyika tathimini halafu ndio wananchi wanahamishwa?

(b) Kwa kuwa ni takribani sasa ni miaka mitatu na huu unaanza mwaka wa nne eneo hilo limechukuliwa na bila kuendelezwa na bila fidia kufanya kulipwa kwa wananchi. Je, Waziri ni lini atatoa taarifa kwa Serikali ya Mkoa na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji juu ya uanzishwaji wa zoezi hili la tathimini ili wananchi waweze kupatiwa fidia zao? (*Makofii*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikubaliane naye kwamba ni muhimu sana tathimini zikawa zinafanywa kabla wananchi hawajahamishwa kwa sababu mara kadhaa imetokea matatizo pale ambapo wananchi wanahamishwa kwanza muda wa kufanya tathimini na malipo unakuwa ni mrefu sana. Kwa hiyo, tunakubaliane naye na hili litazingatiwa.

Kuhusu ni lini sasa tathimini hii itafanywa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu imeshaandaa utaratibu muda si mrefu kutoka sasa zoezi hilo litaanza na hatimaye fedha hizo zitakazohitajika zitawekwa kwenye Bajeti ili wananchi waweze kulipwa. (*Makofii*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kambi hizi zinajengwa pia Mkoa wa Singida Wilaya ya Manyoni na Wilaya ya Iramba na kwa kuwa wananchi hawajazoea kuishi na wanajeshi. Je, Serikali itakuwa tayari kutoa elimu kwanza kwa wananchi ili wajue faida watakazopata na hasara watakazokumbana nazo?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Diana Chilolo anazungumzia Kambi za JKT na Kambi za Jeshi la Wananchi na kwa kawaida utaratibu wa Kambi za JKT, hupeleka maombi Mkoani na hatimaye Mkoa ndio unatoa kibali cha eneo baada ya kuzungumza na wananchi na kuelewana kwamba utaratibu wote wa tathimini na kadhalika utafanyika.

Kwa hiyo, tutaendelea kuwaomba wenzetu wa Mikoani na Wilayani watoe elimu kwa wananchi waelewe vyema umuhimu wa kuwa na kambi hizi katika maeneo yao ili hatimaye mazoezi haya ya kuweka kambi katika maeneo mbalimbali ziwe za JWTZ au za JKT yasizue migogoro na wananchi.

Na. 483

Usikivu Hafifu wa Radio ya Taifa TBC Kalambo

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha usikivu wa *TBC* kwenye maeneo yote ya Jimbo la Kalambo na kwingineko katika nchi ambako hawapati usikivu wa chombo hicho cha Habari *cha Taifa* (*TBC*).

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana utamaduni na michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mbunge wa Kalambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua tatizo la usikivu la usikivu wa redio na uonekanaji wa Televisheni ya Taifa (*TBC*) katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Jimbo la Kalambo.

Katika kuhakikisha kuwa maeneo yote ambayo hayapati huduma ya vyombo hivyo viwili yanapata huduma hiyo Serikali imekuwa ikifunga mitambo mipya ya kurushia matangazo na kufanya matengenezo ile ya zamani utekelezaji huo umefanya katika awamu mbalimbali na kwa kadri fedha zinapopatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza imehusisha miji Mikuu ya Mikoa na awamu ya pili Serikali imeanza kwa kufunga katika Miji Mikuu ya Wilaya. Ni matarajio yetu kuwa maeneo mengine ya nchi likiwemo Jimbo la Kalambo ambalo lipo Mkoani Rukwa na ambalo halipati matangazo kuititia mtambo uliofungwa katika Mji Mikuu wa Mkoa huo, litapata huduma hiyo kuititia mtambo utakaofungwa katika Mji Mikuu wa Wilaya ya Kalambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo pamoja na mitambo hiyo kufungwa katika Miji Mikuu ya Wilaya, inawezekana matangazo yake yasisikike vizuri zaidi maeneo mengine ya Wilaya hiyo kutokana na hali ya kijiografia, hususani kuwepo kwa milima. Katika hali hiyo utafiti unafanya kuweza kuyabaini na kufunga mitambo mingine ili matangazo hayo yasikike vizuri zaidi.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natanguliza shukrani kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na majibu yake mazuri nina swali moja kama ifuatavyo:-

Ni ukweli usiopingika kwamba Jimbo la Kalambo lipo pembezoni mwa nchi na ni ukweli usiopingika kwamba hata watumishi wengi wanapopangwa kwenda kuripoti kule hawaendi kwa sababu wanakosa huduma kama hizi. Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari kuhakikisha kwamba tunaposherehekea Miaka 50 ya Uhuru na wananchi wa Jimbo la Kalambo watakuwa wamepata huduma hii ili waweze kushuhudia kwa kutazama kwenye TV na kwa kusikiliza Radio wakati wa sherehe za Uhuru wa Miaka 50?

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Naibu Waziri amelielezea vizuri sana kwenye majibu yake ya msingi naomba kumhakikishia Mheshimiwa Kandenge kwamba tutafanya kila jithada kuona kwamba watu wa jimbo lake wanaweza kunufaika na matangazo haya.

Lakini hatuwezi kumhakikishia kwamba mwaka huu wataweza kuona. Lakini awe na hakika kwamba tunachukua hatua kwa uzito unaostahili. (*Makofii*)

MHE. JOSEPH ROMAN SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la usikivu wa Redio ya Taifa katika Jimbo la Kalambo linafanana sana na tatizo hilo hilo katika jimbo la Rombo. Sehemu kubwa ya Jimbo la Rombo maeneo ya Tarakea, Useri, Mashati hawapati redio ya taifa na badala yake wanasiliza *KBC* kutoka Kenya na sehemu ndogo sana pia wanasiliza Redio binafsi ya *Radio One*.

Je, Serikali inaweza iktuambia ni kwa nini Redio ya Taifa ishindwe kusikika katika maeneo hayo na badala yake Radio binafsi isikike?

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Mheshimiwa Selasini kwamba ni kweli kwamba baadhi ya maeneo katika jimbo lake hayasikiki vizuri na ye ye mwenyewe ameniambia jambo hili na nimeshamhakikisha kwamba tunafuatilia tunapeleka watalaam kuona namna ya kusaidia kuhakikisha tatizo hili linakwisha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Selasini naomba uwe na imani kwamba yale tulioyaongea tutayatekeleza.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jimbo langu kuna milima inayoambaa Ziwa Nyasa, milima ya Livingstone ambayo imetenga usikivu kati ya Songea na maeneo mengine na Ziwa Nyasa hivyo kufanya watu wa Nyasa kusikia matangazo kwa Radio Malawi. Je, ni lini watu wa Nyasa watapata kusikia Redio Tanzania ikiwa ni pamoja na alikozaliwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza kuchukua hatua za kurekebisha mawimbi ya mawasiliano katika Mkoa wa Ruvuma na sasa hivi marekebisho yanaendelea katika Wilaya za Tunduru na Songea Mjini.

Baada ya marekebiso hayo tutafanya marekebiso katika Wilaya ya Mbinga ili kuhakikisha Mheshimiwa Kapt. Komba wananchi wake wanasikia vizuri matangazo yetu badala ya kutegemea matangazo ya nje ya nchi.

MWENYEKITI: Maana yake Serikali ifanye jitihada maana jibu limekuwa *very standard*.

Na. 484

Viwango vya Malipo ya Pensheni kwa Wastaifu

MHE. MARIAM R. KASEMBE aliuliza:-

Kiwango cha pensehni wanachopewa wastaifu kwa sasa hakiendani kabisa na kupanda kwa gharama za maisha:-

(a)Je, Serikali haioni kuna haja ya kutazama ya kutazama upya viwango hivyo ili virekebishwe kulingana na hali ya sasa ya kupanda kwa maisha?

(b)Kwa nini malipo haya hucheleweshwa sana na kuleta usumbufu mkubwa kwa wahusika?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, nakubaliana na maoni ya Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna haja ya kutazama upya viwango vya pensheni wanachopata wastaifu. Serikali muda wote imekuwa ikijitahidi kuinua viwango hivyo na itaendelea kufanya hivyo kutegemeana na hali ya uchumi itakavyoruhusu. Lakini kwa sasa uwezo wa Serikali ni kulipa kiasi cha shs. 50,114/= kima cha chini kwa mwezi.

(b)Mheshimiwa Spika, ucheleweshwaji wa malipo ya mafao pamoja na mambo mengine husababishwa na kutokamilishwa kwa taratibu zinazotakiwa kufuatwa ili mafao yaweeze kuandaliwa. Utunzaji wa kumbukumbu na mawasiliano hafifu mionganoni mwa wadau hii inajumuisha malumbano ya kifamilia kuhusu teuzi wa msimamizi wa mirathi husika.

Katika kuandaa mafao ya mstaifu kama kuna ukosefu wa waraka mmoja tu kati ya nyaraka kumi zinazotakiwa zoezi hilo haliwezi kufanyika au kwa maana nyingine haliwezi kukamilika haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utimilifu wa kumbukumbu zote za utumishi pia makubaliano mahsus ya kifamilia kuhusu uteuzi wa msimamizi wa mirathi ni muhimu sana. Kwa hiyo, endapo kutakuwa na kumbukumbu zinazotakiwa na nyaraka zote za mirathi zitakuwa zimewasilishwa kama inavyotakiwa mafao yataweza kulipwa kwa haraka bila ya usumbufu.

Aidha, Wizara imeanzisha matumizi ya mtandao wa kompyuta katika kitengo cha pensheni, kurahisisha mawasiliano pamoja na maandalizi ya mafao ya pensheni kwa kutumia teknolojia hii (*Automation of Pension Payments*). Hii nafikiri itasaidia sana ulipaji wa mafao kwa wastaifu. (*Makof*)

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kiwango kinacholipwa pensheni kwa wastaifu waliostaifu miaka ya tisini na kurudi nyuma kinatofautiana na wastaifu ambao wamestaifu kuanzia miaka ya 2000 hadi 2010 ambao cheo cha wastaifu hawa kinalingana:-

(a)Je, Serikali haioni iko haja ya kurekebisha viwango hivyo ili kuwe na kiasi cha pensheni wanacholipwa maalum ili kuwaondolea unyonge wale wastaifu waliostaifu miaka ya 1990 ya kupata shilingi 50,000 kwa mwezi wakati wenzao waliostaifu kwa cheo hicho hicho wanapata zaidi ya fedha hizo?

(b)Kwa kuwa wapo wastaifu ambao wamekuwa wamepoteza nyaraka zao na kukosa kulipwa mafao. Je, Serikali haiwezi kuona huruma kwa watu hawa walipoteza kumbukumbu zao kwa kuandaa utaratibu ambao utasaidia hawa wastaifu waweze kulipwa mafao yao ili na wao waweze kukabiliana na ukali wa maisha ulipo kwa hivi sasa? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Wabunge wote kwa kuthamini maisha ya wastaifu na kuwapigania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı lake la kwanza ambalo linahusu maafisa ambao wanastaifu lakini vyeo vinafanana halafu malipo yanatofautiana naomba tu nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba maafisa hawa wenyе cheo kimoja japo walistaifu katika cheo kimoja lakini ni wazi kwamba wastaifu hawa walikuwa wanapata mishahara tofauti. Ukokotoaji wa mafao ya kustaifu unazingatia muda ambao mtumishi anayestaifu ametumikia pamoja na mshahara wake wa mwisho kabla kustaifu.

Hivyo ni kweli usiopingika kuwa aliystaifu mwaka 1990 mshahara wake aliostaifu nao ulikuwa mdogo kuliko Afisa anayestaifu mwaka 2010 na hivyo kutofautiana katika mafao yao ya kiinua mgongo na pensheni ya kila mwezi ni suala la kawaida tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo uwezekano wa kulipwa mafao na pensheni ya viwango tofauti kwa maafisa wa cheo kimoja waliostaifu tarehe moja kutokana na tofauti za muda wa utumishi. Maafisa watakaolipwa mafao ya pensheni zinazofanana ni wale tu ambao walajiriwa siku moja na kustaifu tarehe moja katika cheo kimoja chenyе mshahara unaofanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı la pili kuhusu kwamba wale ambao wamestaifu lakini kumbukumbu zao zimepotea nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hata kama kumbukumbu za mstaifu zimepotea Serikali ina utaratibu ambao unaweza ukamsaidia huyu mtu ambaye kumbukumbu zake zimepotea na utaratibu ambao unatumika ni kwamba unaweza kwenda mahakamani halafu huyo mstaifu akala kiapo kwa maana ya zile fomu za *affidavit* zinajazwa halafu hatimaye inathibitishwa kwamba kumbukumbu ambazo zimepotea zinaweza zikarekeblishwa kwa kula kiapo mahakamani na endapo atafanya hivyo basi malipo yanaweza yakaandaliwa kwa utaratibu huu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nimpishe Naibu Spika, ili aweze kuendelea na shughuli zinazofuata. (*Makof*)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa kipindi chetu cha Maswali kwa leo umeisha, Maswali yaliyobakia yatapangiwa muda mwingine kwa wakati muafaka.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitoe taarifa ya kikao nilichokuwa nimekiitisha cha dharura cha Kamati ya Uongozi ambapo bahati nzuri Mheshimiwa Spika, ameweza kuhudhuria na kukiendesh, Mheshimiwa Anne Makinda. Kama niliviotangaza asubuhi yeye na wengine tayari wako njani wanaelekea Zanzibar kwa ajili ya Marehemu Mbunge mwenzetu.

Kamati ya Uongozi imepima hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Kabwe Zitto na kuiona ni hoja ambayo inahitaji kupata fursa ya kusikilizwa na Bunge. Kwa maana hiyo sasa namwomba Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto achukue fursa hii kutuweka sawa anasema nini kuhusu jambo hili sasa. Mheshimiwa Kabwe Zitto karibu, endelea.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa busara ya hali ya juu ambayo umeonyesha katika kuongoza Bunge hili na kuruhusu jambo hili liweze kwenda kwenye Kamati ya Uongozi, tena kwa dharura na kuweza kujadiliwa kikamilifu.

Waheshimiwa Wabunge, watakumbuka kwamba Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, alisimama hapa Bungeni na kuonyesha barua ambayo baadaye iliwakilishwa kwa Spika wa Bunge kuhusiana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kukusanya fedha kwenye taasisi zilizo chini ya Wizara yake kwa ajili ya kuwezesha Bajeti ya Wizara kuweza kupitishwa hapa Bungeni.

Baada ya malalamiko Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja ndani ya Bunge hili Tukufu na kuweza kueleza ya kwamba jambo lile limemsikitisha sana. Zaidi ya kumsikitisha ni kwamba iwapo yeye angekuwa na mamlaka angeweza kuwa amemchukulia hatua mara moja.

Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja ndani ya Bunge hili Tukufu na kuweza kueleza ya kwamba jambo lile limemsikitisha sana na zaidi ya kumsikitisha ni kwamba iwapo yeye angekuwa na mamlaka angeweza kuwa amemchukulia hatua mara moja Katibu Mkuu. Lakini bahati mbaya hakuwa na mamlaka hayo. (*Makof!*)

Jana Katibu Mkuu Kiongozi kufuatia Tume kufuatia kazi aliyokuwa amemwomba Mheshimiwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) alifanya uchunguzi na jana taarifa hiyo imetoka ya uchunguzi na imetolewa kwa waandishi wa habari na leo hivi ninavyozungumza Katibu Mkuu yule wa Wizara ya Nishati na Madini ameamriwa arudi kazini leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili lillianzia Bungeni. Bunge lilikuwa linapaswa kupewa taarifa ya uchunguzi huo ambaa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) ameutoa na baadaye kuweza kuishauri Serikali hatua ambazo zinapaswa kuchukua. (*Makof!*)

Kitendo cha Katibu Mkuu Kiongozi kuchukua taarifa ile kuitisha Mkutano na Waandishi wa Habari na kuitolea maamuzi ni dharau kwa Bunge. Kwa kuwa Waziri Mkuu alisema kwamba yeye anamsubiri Rais na Kanuni za Utumishi wa Umma na Sheria za Utumishi wa Umma kumbe zinataka Katibu Mkuu Kiongozi ndio aweze kutoa adhabu.

Kitendo cha Katibu Mkuu Kiongozi kutoa taarifa ile kwa Waandishi wa Habari bila Bunge kutaarifiwa na kuweza kuishauri Serikali ni dharau kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiye msimamizi wa shughuli za Bunge. (*Makof!*)

Kwa kweli kama mimi ningekuwa Waziri Mkuu baada ya taarifa ile ya Katibu Mkuu Kiongozi ningejuzulu Uwaziri Mkuu. Kuna dalili zote kwamba taarifa ile ya Katibu Mkuu Kiongozi imeingilia hadhi, kinga na madaraka ya Bunge. Bunge hili Tukufu linahitaji kujadili na kuitolea

maelekezo kwa mujibu wa Katiba kwa sababu sisi ndiyo wasimamizi, tunaisimamia Serikali kwa mujibu wa ibara ya 63(ii) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nawaomba Waheshimiwa Wabunge tujadili jambo hili na kuweza kama nilivyosema hapo awali kwamba tuzuie shughuli zote za Serikali. Hoja zote za Serikali ambazo zinakuja Bungeni mpaka hapo tutakapojadili taarifa hii ya Katiba Mkuu Kiongozi na kuweza kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nataka nisiwe mbali na mtoa hoja. Nilikuwa naomba nianze kwa kujadili lakini nianze kwa kuanza kuangalia kwenye Katiba kifungu Na. 63 cha Katiba ibara ya (ii) ambayo inasema: "Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi, kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii." (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niende kwenye hiyo hiyo ibara ya (ii) kifungu (b) ambacho kinasema: "Kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka la Bajeti". (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya nukuu ya vifungu hivyo viwili suala lile liliibuliwa ndani ya Bunge hili na baada ya kuibuliwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye na yeye ni Mbunge mwenzetu lilimgusa kwa machungu sana. Ni matarajio yetu baada ya utafiti uliofanyika na uchunguzi uliofanyika suala lile lingerudi kwetu. Tukalijadili, tukaona ni nini kilichotokea, tukawahabarisha wananchi wetu ni jinsi gani matumizi ya fedha za nchi hii ambazo ni jasho la wananchi zilivyotumika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuona kwamba wale waliotoa taarifa jana, kwa kweli mimi binafsi naona kama tumedhalilishwa. Bunge halikupewa haki yake kama Bunge. Tumeonekana Wabunge wote humu ndani hatujui wajibu wetu na pia mamlaka yetu yamekiukwa na yamevutwa kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako Tukufu lisimamie hoja hii na tujadili ili tuweze kupata muafaka. Naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchukua nafasi ya kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii yenye maslahi mapana kwa taifa letu na inailinda hadhi na madaraka ya Bunge yaliyopo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama Wabunge wote mnavyokumbuka tulijadili hoja ya Wizara ya Nishati na Madini na wakati wa kujadili lilijitokeza suala zima la makusanyo ya fedha yaliyoelekezwa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kwa taasisi zilizoko chini yake juu ya nini Waziri Mkuu alisema kwa niaba ya Serikali nyote mnajua na Taifa zima linajua.

Lakini matarajio ya Watanzania na matarajio ya Bunge hili ni kwamba baada ya kazi hii ambayo imefanywa na CAG na vyombo vingine taarifa ile ilipaswa ije ndani ya Bunge hili ili kwa pamoa tuweze kuitendea haki.

Sasa kwa kweli yaliyoelekezwa jana siyo tu hayawezi kukidhi matarajio ya Bunge kwa sababu ninayapingga yote kwamba ng'ombe zangu zimeibiwa hata nikisema 100 ukaenda kuzikuta tatu bado haiondoi ukweli kwamba aliyechukua hizo ng'ombe tatu ni mwizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachotaka kusema ni kulishawishi Bunge hili kwamba madaraka tulyopewa na kinga tulyopewa kwa mujibu wa ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya ya Muungano wa Tanzania na kinga nyine tulyopewa na Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296 marejeo ya Sheria za Tanzania Toleo la 2002 inasema hivi na kwa ruhusa yako Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kunukuu. “*There shall freedom of speech and debate in the Assembly and such freedom of speech and debate shall not be liable to be questioned in any Court or place outside the Assembly*”. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka haya tulyopewa na sheria ya Kinga na Madaraka ya Bunge na ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kitendo kilichotokea jana kwa kauli ya Katibu Mkuu Kiongozi siyo tu kwamba inaingilia Haki na Madaraka ya Bunge bali inafedhehesha na kumdhailisha Waziri Mkuu, inadhalilisha Bunge hili.

Sasa ili kuitendea haki hoja hii nikiungana na Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Zaynab Vullu aliyeongea kwa ruhusa yako Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutumia Kanuni ya 117 kuliomba Bunge lako Tukufu sasa liamue kuunda Kamati Teule itakayoangalia pamoja na mambo mengine kuingiliwa kwa Uhuru wa Bunge.

Lakini mchakato mzima uliosababisha fedha zile zikusanywe na kugawanywa na kukusanywa kama fedha za harusi wakati mnajua kwamba kila Waziri anapewa Kasma ya maandalizi ya Bajeti inayokuja na kwamba wale wote waliokuja waliweza kuja na mafuta kutoka katika Ofisi zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge hili liniunge mkono kwa kutoa hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 117 fasili ya (i) (ii) mpaka ya (iv) ambayo yanaweka masharti ya utaratibu wa kuundwa kwa Kamati Teule na hii itasaidia sana kuitendea haki hoja hii na kulinda hadhi ya Bunge lako Tukufu na ndiyo maana nimesimama hapa kutoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja na naomba mniunge mkono Waheshimiwa Wabunge Wenzangu wote. (*Makof*)

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wabunge mnawenza kukaa. Katika kujadili hoja hii ambayo imeibuliwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe. Sasa Mheshimiwa Ole-Sendeka ameiboresha kwa kutoa hoja ya kuundwa Tume Teule ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeiunga mkono kwa wingi sana kwa kutumia Kanuni ya 117 ambayo inasema: “Kamati Teule inaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalum kwa hoja mahususi itakayotolewa na kuafikiwa”.

Hoja hii imetolewa na imeafikiwa na kwa jinsi hiyo mimi ninakubaliana na jambo hili. Kwa jinsi hiyo kufuatana na Kanuni hii ya 117 Bunge hili litaunda Tume Teule kwa ajili ya kulichunguza jambo hili. Kwa sababu Bunge ni muhimili, haliwezi kudharaulika kirahisi. Tunaiheshimu na kuipenda sana Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Waziri wake Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda. Si rahisi kwa Bunge kuonekana Waziri Mkuu akidharaulika halafu Bunge likanyamaza, haiwezekani. (*Makof*)

Kama dharau inaweza ikatokea huko huko wanakofanya dharau hii siyo ndani ya Bunge hili. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Kabla ya kuahirishwa kwa Bunge keshokutwa jioni Mheshimiwa Spika, Anne Makinda, ataiunda rasmi Tume hii kwa kutaja majina ya wanaohusika na tunaitaka Tume hiyo ifanye kazi kwa haraka katika muda mfupi iwezekanavyo na Bunge ijalo moja ya mambo ambayo yatajadiliwa ni taarifa ya Tume hiyo maana yake lazima ijadiliwe ndani ya Bunge hili. Ahsante sana. Hilo ndiyo hitimisho la suala hili. (*Makof*)

Sasa naomba niendelee na matangazo ya wageni wetu na naomba sana Waheshimiwa Wabunge sasa mnivumilie ili ratiba ya leo iweze kwenda kama tulivyoipanga. Nawaombeni sana. Nakuona Mheshimiwa Mkono.

MHE. NIMROD E. MKONO: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuniona. Naomba mwongozo wako Mheshimiwa Naibu Spika. Katiba, Kanuni ya 68, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ibara ya 15(vi) kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya Sheria. Mamlaka ya nchi itaweka taratibu zinazofaa au zinazozingatia misingi kwamba wakati haki na wajibu kwa mtu yoyote inapohitajika kufanyiwa maamuzi na Mahakama au narudia au chombo kingine chochote kinachohusika basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu na pia haki ya kutaka kukata rufaa ama kupata nafuu nyingine ya kisheria kutokana na maamuzi ya chombo hicho kinachohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika wakati sakata hili linaanza la Ndugu yetu Jairo na wakati Waziri Mkuu anazungumza juu ya jambo hili huyu mtuhumiwa amehukumiwa na sisi wenyewe inavyoonekana bila yeche kumwuliza kinyume na utaratibu wa Katiba.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mkono nakuomba ukae. Sijakuelewa, unajadili jambo ambalo nimeshalitolea uamzi au unajadili jambo gani? (*Makofii*)

MHE. NIMROD E. MKONO: Ninaomba.....

NAIBU SPIKA: Kama ni hili ambalo nimeshalitolea uamzi, unafahamu utaratibu Mheshimiwa. Lakini niko tayari kukusikiliza kama ni jambo lingine.

MHE. NIMROD E. MKONO: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Nashukuru kwa taarifa yako. Mimi ninalolisema, ninachouliza kwako ni mwongozo.

Je, hatuoni kwamba, najua uamzi umetolewa. Lakini uchungu ni uchungu. Mimi nataka kujua, nataka kujua tu mwongozo wako kama hatutakuwa tumekwenda nje ya utaratibu wa Katiba basi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mkono. Lakini kwa kuwa umeuliza na wewe ni mtaalam wa Sheria. Nikuhakikishie kuundwa kwa Tume Teule itafanya kazi katika taratibu ambazo zitazingatia haki, itafuutilia, ina madaraka makubwa, ina uwezo wa kumwita mtu yoyote pamoja na huyo unayemsema akapata nafasi ya kusikilizwa na baada ya hapo hiyo taarifa itakapokuja hapa Bungeni ndiyo swali lako litakapokuwa na mantiki kwamba je hii Tume Teule iliyahi kumhoji na fulani na fulani. Lakini kwa wakati tumeunda chombo ambacho kinaenda kufanya kazi hiyo kwa niaba yetu na kutuletea ripoti kamilifu kuititia ripoti ya CAG na mambo mengine. Sasa tuendelee. (*Makofii*)

Wageni walipo katika jukwaa la Spika ni wageni wa Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Katiba na Sheria amba ni pamoja na familia yake Ndugu Goodluck Kombani. Goodluck yupo? Oooh atakuja jioni na Joel Kombani mtoto wake vile vile. Kwa hiyo, hawa wageni wa Mheshimiwa Waziri wote watakuja jioni? Ahsante sana. Tutawatamka jioni.

Waheshimiwa wa Ndugu John Joel - Kaimu Katibu wa Bunge ni Ndugu Ambele Mwaipopo, Kaimu Mkuu wa KKKT Diocese ya Dodoma, Ndugu Elingaya Saria, Msaidizi wa KKKT Diocese ya Dodoma, Ndugu Robert Mgaya, Katibu wa Diocese ya Dodoma. Karibuni sana. (*Maakofii*)

Wageni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 55 toka shule ya Msingi General Musuguri Dodoma. Karibuni sana wanafunzi pamoja na walimu. Wanafunzi ishirini (20) na walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari ya Mgulasi Morogoro. Ahsanteni sana. Wachezaji 11 wa timu ya wanawake wa Tanzania wa mchezo wa golf. (*Makofii*)

Wanafunzi hamsini (50) wa shule ya sekondari ya Viwandani Dodoma, karibuni sana. Wageni watano (5) wa asasi ya Kode ya Dar es Salaam amba ni wawakilishi wa mpango wa VICOBA wakiongozwa na Ndugu Ado Lusinde, karibuni sana. (*Makofii*)

Matangazo ya vikao vya kazi. Mheshimiwa John M. Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*) anaomba Kamati hiyo ya *PAC* Wajumbe wake kukutana saa saba, gorofa ya pili 231.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kushirikiana na *UN Women* watafanya Semina kwa Waheshimiwa Wabunge wanawake wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii leo saa 7.30 hadi saa 9.30 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa John Mnyika anawaomba Wabunge wote wa CHADEMA kukutana saa 7.15 mchana gorofa ya pili katika Ukumbi ule ambao tumeuzoea. Waheshimiwa Wabunge wanawake wote saa 7.30 mchana ile Semina inayoitishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Rosweeter Kasikila anaomba Wajumbe wa Kamati wa masuala ya UKIMWI saa 7.15 Pius Msekwa B. Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo saa 7.15 Ukumbi wa *Basement*. Katibu Mkuu *UPNAC*, anawaomba wajumbe wa Kamati Tendaji ya *UPNEC* kutakuwa na kikao cha Kamati Tendaji, Ukumbi 231 saa 9.00 kamili, *UPNAC* saa 9.00 kamili Kamati ya Utendaji. (*Makofii*)

Nawaomba tena wale mabinti mabingwa wa gofu, wasimame. Waheshimiwa Wabunge, nimetaarifiwa na Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo -Mheshimiwa Nchimbi kwamba timu hii ya gofu ndiyo iliyotwaa ubingwa wa Afrika Mashariki kwa mchezo wa gofu. Kwa niaba ya Bunge hili na wananchi wote wa Tanzania, tunaomba kutoa shukrani zetu kubwa sana kwa kutubeba. Kombe ndiyo hilo, eeh! Kombe ndiyo hilo ambalo wanalinyanya. Tunatumaini na timu za michezo mingine nazo zitazidi kufanya vizuri katika michezo yao. Karibuni sana hapa Bungeni. Karibuni sana. (*Makofii*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa pole Mheshimiwa Waziri Mwandosya. Mungu ampiganie arudi katika afya yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya maji inafanya kazi nzuri. Maeneo mengi Serikali imejitahidi kuchimba visima virefu na vifupi ili kusaidia wananchi kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali, Wahandisi wa Maji Wilayani wasimamie kwa uadilifu miradi/fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya uchimbaji wa visima. Mara nyingi Wahandisi wa Wilaya hawasimamii vizuri (wanashauri watia sahihi wa vijiji husika waweke sahihi kulipa kiasi kikubwa Wakandarasi wa kuchimba visima hata kabla hawajachimba). Hili nimeshudia, Wakandarasi walichimba visima viwili badala ya vinne, lakini Mkandarasi alishalipwa fedha yote ya visima vinne. Kama kiongozi, niliagiza Mkandarasi akachimbe visima viliviyobaki, au yeze na *eng/her* wa maji Wilaya, wapate kifungo. Kazi ilifanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inadhihirika kuwa *Engineer* wa Maji wa Wilaya alishirikiana na Mkandarasi kutapeli wanakijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Benki ya Dunia wa kufadhili maji katika vijiji 10 kila Wilaya unachukua muda mrefu mpaka wananchi wanakata tamaa. Nashauri Serikali iangalie tatizo liko wapi. Inawezekana Halmashauri ya Wilaya haitendi kama Benki ya Dunia inavyoshauri. Kuna haja kuititia upya makubaliano ya Serikali na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, viko vyanzo vingi vya maji katika maeneo mengi nchini Tanzania. Vyanzo vingi havitunzwi, ndiyo maana mito mingi imekauka. Nashauri Serikali irekebishe Sheria ya *distance*, ya kulima karibu na chanzo cha maji. Mita 60 au mita 200 kulima kutoka chanzo cha maji ni umbali mfupi sana. Nashauri iwe mita 1000 au kilometra moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Halmashauri za Wilaya ziagizwe wananchi wa maeneo yao wapande miti mingi katika kuzunguka vyanzo vya maji. Miti ikipandwa itatunza vyanzo na

maji yatapatikana. (Uko mfano hai ambao kule Kasulu Kigoma kila chanzo cha maji kinakabidhiwa mwanakijiji mmoja anatunza, na imekuwa *very effective*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchimba kisima ni kazi moja. Kazi kubwa na yenye kuleta tija ni kuweka bomba za kusambaza maji haya ili yatumike na kaya nyingi. Nashauri Serikali itoe agizo kwa Naibu Waziri ya kuwa miradi yote inayoibuliwa na vijiji, bomba za kusambaza maji ziwe included katika bajeti ili watakapochimbiwa kisima, maji yasambazwe, wakazi wengi wafaidi maji haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kilimanjaro una maji ya kutiririka na pia ya visima ambavyo vinaendelea kuchimbwa. Nashauri Serikali iangalie tatizo la Ziwa Jipe. Ziwa hili linakauka kwa magugu maji upande wa Tanzania. Upande wa Kenya linang'ara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ichukue hatua za haraka kulinusuru hili ziwa ili lisaidie kilimo katika Kata ya Jipe na zile zinazolizunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa la Nyumba ya Mungu nalo linazidi kuharibika kwa sababu ya undogo mwingi kuingia kutokana na mmomonyoko wa ardhi. Bwawa hili ni chanzo pia cha samaki na umeme unaopatikana Hale Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja Serikali ichukue hatua za haraka kuondoa tatizo la mmomonyoko wa ardhi. Kama ni sababu ya kilimo, basi sheria zichukue mkondo wake watu waache kulima katika vyanzo nya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Serikali iwaambie Watanzania, Kamati waliyounda kuangalia matatizo ya mto Umba, Ziwa Jipe na Nyumba ya Mungu inatakiwa kutoa ripoti lini na Serikali wana mpango gani wa kulinusuru Ziwa Jipe kutokana na magugu maji na Nyumba ya Mungu kutokana na mmomonyoko wa udongo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hoja nkipata majibu kuhusu Ziwa Jipe na Nyumba ya Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimpa Eng. Mrindoko kilio changu cha ndugu yangu Mr. Paschal N. Matunda ambaye ametumia zaidi ya Shilingi milioni 50 na muda zaidi ya mwaka mmoja kutumia *agency* ya Wizara kumchimbia kisima cha maji njia panda ya Dar es Salaam - Moshi Holili. Baada ya usumbufu wa mwaka mmoja, walichimba, lakini *pump* yao ikatumbukia. Mr. Matunda bado hajapata maji pamoja na *ku-invest that much*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaisihi Wizara isaidie katika tatizo hili. Inakatisha tamaa kwa mwekezaji na Mtanzania anayepanga kuwekeza katika kilimo. Ni vyema *pump* itolewe au achimbiwe kisima chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani zangu za dhati.

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji ni kubwa katika Jimbo la Mpwapwa. Kata zifuatazo ndizo zenye matatizo ya maji tangu tupate Uhuru mwaka 1961. Kata ya Chunyu, Iwondo, Chitemo, Mima, Sazima, Makutupa, Bumila na Lupeta.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya maeneo/Kata hizi vipo visima nya muda mrefu, lakini "pump" za maji za kuvuta maji ni za muda mrefu, mpaka sasa hazifanyi kazi (*beyond repair*).

Je, Wizara ina mkakati gani wa kuchimba visima virefu kama hatua ya kutatua kero ya maji kwa maeneo niliyoyataja? Nashauri, utaratibu wa kuvuna maji ya mvua yanayotiririka ovyo wakati wa msimu wa mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Wizara ina mpango gani wa kuzindua miradi wa maji katika mji mdogo wa Mpwapwa? Mradi huu ulikwishakamilika muda mrefu sasa. Wananchi wa mji mdogo wa Mpwapwa wanayo shauku kubwa ya uzinduzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, anisaidie tupate maji katika Jimbo la Mpwapwa. Mimi sina haja ya Shilingi.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi kuchangia bajeti ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwa kumpa pole Waziri wa Maji kwa ugonjwa, Mungu amsaidie apone haraka. Nampongeza tena Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri alioifanya, pamoja na Katibu Mkuu mzoefu wa Wizara Bwana Christopher Sayi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu, kuna maeneo mengi ambayo hayana maji tofauti na *data* za Serikali. Katika maeneo kame, Halmashauri ya Longido inaongoza kuwa na tatizo la maji nchini. Kwenye hotuba ya Waziri ametaja Wilaya za Longido, Monduli, Simanjiro na Kiteto. Halmashauri hizo zinatajwa kila bajeti, lakini hakuna kinachofanyika. Naomba kwenye bajeti ya mwaka huu iwe mkombozi wa kukumbukwa kutatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Longido Makao Makuu, ni mji mdogo wa Longido ambapo maji ni kero kubwa. Kwa sasa, debe moja ni Sh. 1,500/= jambo ambalo ni dhahiri maisha bora kwa kila Mtanzania ni ndoto kabisa. Huwezi kujenga bila kutumia maji ya kununua. Shule za Sekondari wanafunzi hawasomi, wanatafuta maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ikumbukwe kwamba kila mwaka Longido inawekwa kwenye maandishi, mwaka huu uwe ukombozi wa wananchi wa Longido. Kero kubwa za wanafunzi kukosa vipindi wakihangaika kutafuta maji ya kupikia kufulia, kuogea na ya usafi shulenii, wananchi wanashindwa kujenga. Hata miradi inashhindikana kwa ajili ya tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tatizo linalotokea ni Serikali kuelezwu wizi na ujisadi kwenye fedha za maji, Halmashauri ya Longido na kukaa kimya kana kwamba hakuna kilichotokea. Wizi mkubwa umetoka kwenye miradi ya maji Halmashauri ya Longido, hakuna mradi ambao umetekelezwa kulingana na fedha zilizotolewa, yote yametengenezwa chini ya kiwango, mengine hayapo. Mhandisi wa maji ametumia fedha za miradi kujengea nyumba zake huku wananchi wakiteseka. Fedha za kujenga uwezo, hakuna semina au mikutano iliyofanyika, lakini fedha zimefika. Huu ni ujisadi mtupu! Naomba ukaguzi ufanyike haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo mengi ambayo yana maji, bado wanajengewa mabwawa huku Longido ambapo hakuna maji, hawana mabwawa. Kuna bwawa moja la *NGODIN* liiliojengwa na Wizara kwa jumla ya Sh. 640,000,000/=. Fedha hizo zimeliwa na bwawa ni dogo sana. Mheshimiwa Waziri Mark Mwандосиа amekwenda kuzindua akashangaa kuona bwawa ambalo limetumia fedha nyingi huku bwana ni ndogo mno. Naomba bwawa kubwa lijengwe Longido kupunguza msongamano wa mifugo na watu wa mji wa Longido.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mradi wa *World Bank* wa vijiji 10 kila Wilaya, limekuwa kero tangu mwaka 2000 mpaka leo. Serikali inaweka kwenye bajeti zote, lakini hakuna kinachoendelea. Sasa hatutaki kusikia jambo la mradi huo. Serikali itoe tena kauli ya kweli kwamba bado mradi huo utaendelea au hautaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko wa tabianchi, Serikali kufanya utaratibu wa namna ya kukabiliana na hali hii ili athari kubwa ikitokea, ijulikane namna ya kukabiliana nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba masahihisho kwenye visima virefu. Visima vilivyojimbwa ni 12, visima vitano ndiyo vina maji. Naomba visima hivyo vitengenezwe wananchi watumie maji haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Wilaya ya Longido ilipokuwa wilaya moja na Monduli, Serikali ilitoa kwenye bajeti mabwawa 18 lakini mabwawa mawili tu ndio yamejengwa kwenye Wilaya ya Longido, mengine yamepelekwa Monduli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Longido wamebaki kwenye hali ngumu kwa muda mrefu. Naomba Serikali iwaokoe wananchi wa Longido, wanaangamia kwa tatizo la maji. Mheshimiwa Waziri ameahidi kujenga bwawa kubwa Wilaya ya Longido. Kuugua kwake isiwe tatizo, Longido kukosa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nategemea kupata majibu. Ahsante.

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia njia ya maandishi, nachangia bajeti ya Wizara hii muhimu kwa uhai wa wanadamu. Mchango wangu kwa kiasi kikubwa unalenga suala la hifadhi ya maji au vyanzo vya maji tulivyonavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za binadamu zinaendelea kwa kasi kuharibu vyanzo vya maji. Lipo tatizo la uchungaji wa ng'ombe kwenye vyanzo vya maji hali ambayo huharibu mabonde na uoto unaotunza maji. Shughuli za kilimo nazo ni njia nydingine inayoharibu vyanzo vya maji. Kilimo kinachochaea mmomonyoko wa ardhi na kilimo cha mabonde ya hifadhi ya maji nacho ni chanzo cha uharibifu, pia pamoja na kilimo, upandaji wa miti umekuwa tatizo. Umekuwepo upandaji miti aina ambazo hutumia sana maji, au hazina sifa ya kuvuta mvua na kuhifadhi maji. Miti na uoto wa asili umeharibiwa, hali inayopunguza fursa tulizokuwa nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu ni kuwa, Wizara ya Maji inabidi kubuni mpango na utaratibu ambao hifadhi ya vyanzo vya maji itasimamiwa. Inatakiwa kuwepo mfumo wa utendaji kati ya Wizara ya Maji, TAMISEMI, Ardhi, Mazingira na hata Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni jitihada za Serikali katika kusambaza maji. Inasikitisha kuona kuwa nguvu nyangi za usambazaji maji bado zinaelekezwa mjini. Kwa kipindi kirefu (*50 years*) juhudhi za kupeleka maji vijijini hasa Muleba Kaskazini ni ndogo sana, kama zipo. Tunapendekeza miradi ya mijini iwe makini kwa kujengwa mara moja kwa muda mrefu ili tuwakumbuke watu wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni maji kwa wananchi wanaoishi visiwani. Jamii hii inalazimika kutumia maji machafu yanayopatikana ufukweni. Jambo la kusikitisha ni kuwa suluhisho la kuwapatia maji watu wa visiwani, siyo la gharama sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni uamuzi wa kupangilia na kupata pampu ndogo za *solar* zinazoweza kuvuta maji toka mbali ziwani sehemu ambazo hazina shughuli za kibinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha muhimu hapa ni kulipa umuhimu suala la maji na kuona watu walio wengi wanashiriki katika kutatua tatizo la maji. Wataalamu wetu kwa kutumia mawazo ya wananchi, mbinu na mikakati itafutwe kuboresha maji vijijini na mijini.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kwa kuishukuru Wizara kwa kuongeza bajeti ya mwaka 2011/2012 kutoka Shilingi bilioni 30.7 hadi Shilingi bilioni 41.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iwasaidie wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini kupeleka maji katika matanki ya maji katika vijiji vya Nyololo, Igowole, Kibao, Sawala, Nyigo na Ihomas. Matanki ya maji yapo na vyanzo vya maji, vipo lakini hayapelekwi kwenye matanki ambayo yalishajengwa kwa kushirikiana na wananchi na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kuwa uchimbaji wa visima katika Viji vya Sawala na Kiponda. Naiomba Serikali kwamba visima ambavyo vimechimbwa bado havijawekwa *pump* na gharama kubwa inatumika katika uchimbaji wa visima hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kisima cha Kibao kijiji kimechimbwa, lakini hakina maji. Lakini kuna chanzo cha maji ambacho kipo jirani na kijiji. Naiomba Serikali kutega maji ambayo yapo katika kijiji cha Kibao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri wa Maji atembelee Jimbo la Mufindi Kusini ili akague matanki ya maji ambayo yalijengwa na Serikali, lakini hayatumiki na wananchi wanapata shida ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea kuhusu tatizo la maji katika Jimbo la Kasulu mjini. Nimepitia taarifa kuhusu hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya vijiji 10 kwa kila Halmashauri chini ya Programu za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini hadi kufikia tarehe 15 Agosti 2011. Kimsingi, hainishawishi kuunga mkono bajeti ya Wizara kutokana na kukithiri kwa uzembe wa hali ya juu Wizarani hadi katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu. Uzembe uliopo na wa hatari ni pale inapoonyeshwa katika taarifa ya Wizara Jedwali No. 1 ukurasa wa 17 item No. 9 inayosomeka hivi:

"Halmashauri ambazo wataalam washauri wanaandaa taarifa za awali na kuainisha taarifa za awali na kuainisha kazi zitakazofanyika (*scoping study*) Kasulu ni mojawapo ya Halmashauri tano ambazo bado wataalam washauri wanaandaa taarifa za awali. Haya ni maajabu kweli kweli. Katika Bunge la Februari mlieleza taarifa hizo hizo. Leo ni zaidi ya miezi sita mnarudia mambo yale yale! Maajabu kweli kweli! Sichelei kusema kuwa Wizara na Halmashauri wanatudharau watu wa Kasulu. Hivi kweli kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita inashindikana kufanya upembuzi na usanifu wa mradi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri na maombi ni kama ifuatavyo:-

- Wizara iache ulaghai wa kila wakati kusema kuwa bado wataalamu washauri wanafanya sijui upembuzi yakinifu na kadhalika;
- Wizara ielete ni lini tatizo la maji katika Jimbo la Kasulu mjini litakoma?
- Wizara inachukua hatua gani kwa Halmashauri na kampuni husika inayofanya kazi ya ushauri au usanifu wa miradi kwa kuchelewesha taarifa na hivyo kuendelea kusababisha kero ya maji kuwa ya kudumu Kasulu mjini na vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Napongeza Waziri wa Maji na wadogo wake wote kwa kazi nzuri na kubwa wanayofanya ya kueneza maji Jimbo la Vunjo Mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kusambaza maji katika Mji wa Himo inaendelea vizuri. Naipongeza Serikali kwa kutoa Sh. 186,006,776/= kwa ajili ya ujenzi wa chanzo cha maji, bomba kuu kutoka kwenye chanzo hadi kwenye matanki, bomba kuu la kusambazia maji kutoka kwenye matanki hadi Himo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika kipindi cha mwaka huu 2011/2012, imetenga Shilingi milioni 100 ajili shughuli za ununuzi na ujenzi wa bomba za kusambazia maji. Lakini naomba kukumbushia ahadi ya Rais ya kutoa Shilingi milioni 150 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa mradi wa maji Himo. Naomba kujua kama hizi Shillingi milioni 100 zitatosha kukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji Kirua Kahe Kata saba vijiji 30. Napongeza jitihada za Serikali kukamilisha mradi wa maji Kirua Kahe. Naomba kujua mradi wa Kirua Kahe katika Kata saba na vijiji 30 utakamilika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji Kilema Mandaka - Njia panda Himo. Napongeza Serikali kwa kusimamia mradi huu ambaa utamaliza tatizo la maji ya kunywa Himo Njia Panda.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji (vijiji vitano) *WSDP*. Vijiji hivyo ni Matala, Mwanjeni, Kilimo Makuyuni, Makame Juu na Makame Chini. Naomba kujua ni lini Serikali itaanza kujenga mradi huo.

MHE. WILLIAM V. LUKUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa la Iguluba limesimama kujengwa. Litaanza tena lini na litakamilika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba usimamizi wa tenda za mabwawa ufanywe na Halmashauri badala ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mabwawa mengine matatu Isimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dharura iliyopo mwaka huu wa ukame na uhaba wa maji Tarafa ya Isimani naomba visima 10, mimi nitachangia *pump*. Naomba wataalam wakafanye *study* ya maji ya uhakika Isimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006 nilitoa ushauri kupunguza na kumaliza tatizo la maji Dar es Salaam, Serikali ingejenga miundomimbu ya maji toka Rufiji kwa kutenga bajeti kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka Mto Rufiji mpaka Dar es Salaam ni kilomita 160. Kama kila mwaka Serikali ingejenga kilomita 33 tu, shida ya maji ingeleta historia. Kwanini Serikali haipendi kusikiliza hoja za msingi?

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa la Kawa katika Wilaya ya Nkasi Wizara ya Maji ilidharau kwa makusudi mawazo ya Mbunge wa Jimbo la Nkasi. Katika kipindi cha mwaka 2005 – 2010, Mheshimiwa Nyami aliwaleza kabla ya mradi wa hilo bwala la Kawa, Mheshimiwa Nyami aliwaeleza kuwa ni bwawa liko kwenye shamba la mtu binafsi, lakini hawakujali kabisa kwa maslahi yao kabisa.

Je, hao viongozi wa Idara ya Maji kwa nini walichukua hatua hiyo ya kutumia fedha za Serikali kwa manufaa ya mtu binafsi? Ama kweli, siyo utawala bora kabisa kutumia kodi za wananchi kwa manufaa ya mtu binafsi. Mimi siungi mkono hoja kabisa. Hii ni ubadhirifu mkubwa kabisa wa pesa za walipa kodi. Waliohusika lazima wachukuliwe hatua za kisheria siyo za kinidhamu, pamoja na kupelekwa Mahakamani mara moja

MHE. MUSTAFA HAIDI MKULO: Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kilosa, Kata ya Kidete, kuna mradi wa Bwawa la maji. Mradi huu unaendelea vizuri, lakini upelekaji wa fedha hauko makini sana. Hivi karibuni makandarasi ilikuwa karibu aondoke kwenye *site* jambo ambalo lingeugharimu mradi gherama kubwa za *remobilisation*.

Mheshimiwa Naivu Spika, ili mradi huu ukamilike kwa wakati, nashauri Wizara ya Maji na Halmashauri husika wawe na ushirikiano wa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa maji katika mijini na vijiji tunapoolekeea kusherehekea miaka 50 ya Uhuru, inasikitisha na kutia aibu kuona kwamba suala la upatikanaji wa maji mijini na vijijini linaendelea kuwa sugu kadri tunavyokaribia nusu karne ya uhuru wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji mijini linapelekeea matatizo makubwa sana katika familia nyingi. Mfano, Mkoa wa Singida, hususan mjini, wanawake na watoto wa kike wamekuwa wakipata taabu sana kutafuta maji usiku kucha, na mara nyingine wanapotafuta maji hayo, usiku

kuna watu hasa wanaume ambao sio waaminifu wamekuwa wakiwadhalilisha kijinsia pamoja na kuwabaka. Matokeo yake ni kuwaambukiza maradhi ikiwemo Ukimwi au kuwapa ujauzito watoto wetu wa kike ambao hawakuutarajia matokeo yake ni kuzalisha kizazi cha watoto wa Mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji halipo mjini tu Mkoani Singida, bali katika vijiji takriban vyote vya Singida vijiji hususan katika Jimbo la Singida Magharibi. Vijiji vya Kata za Sepuka, Ihanja, Puma, Mgungira, Mwaru, Mhifiro, Ing lanson, Mayange na kadhalika vina shida kubwa sana ya maji kiasi ambacho wanafunzi wamekuwa hawatulii mashulenii kusoma, badala yake wanahangaika kutafuta maji mchana kutwa na hasa wanafunzi wa sekondari. Athari ni kubwa sana, maana inasababisha hata watoto kutofanya vizuri katika mitihani yao na matokeo yake wanapomaliza shule wanakuwa ni watu wasioweza kujitegemea na kushindwa kukabiliana na mazingira yao yanayowazunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ufujaji mkubwa wa fedha katika mamlaka ya maji safi na maji taka. Hii imekuwa ni sababu kubwa ya kushindwa kutengeneza miundombinu ya maji. Mfano, mabomba yamekuwa chakavu kwa muda mrefu na mabomba yamekuwa yakipasuka na kusababisha kupotea kwa maji mengi na kupoteza pesa nyingi. Watumishi ambao wamekuwa sio waminifu wamekuwa wakifuja pesa kama tulivyosikia kwenye taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, lakini hawachukuliwi hatua zozote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itolee tamko kuhusu ubadhiri huu mkubwa wa fedha za Serikali na ni hatua gani imechukua kwa hao wahusika walisababisha ubadhiri huu wa fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. SEIF S. RASHIDI: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kwa neema zake za kuniwezesha kuwa na afya na kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupongeza hotuba na juhudi za Serikali kutimiza wajibu wake wa msingi wa kukusanya kodi kwa lengo la kutumia fedha hizo ili wananchi walipakodi wapatiwe huduma za msingi, moja ikiwa ni hoja ya huduma hiyo, kauli mbiu wakati wa uhuru, Serikali itatoa maji bure au bila ya malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1971, mara baada ya zoezi la uanzishaji wa vijiji vya ujamaa ambavyo lengo lake ni kuratibu na kuwapatia huduma ya maji vijiji vyote ifikapo mwaka 1999, lengo la kila mtu kuishi ndani ya mita 400 kutoka kituo cha maji safi na salama. Tumeshuhudia sababu za kupotosha za kuridhisha kushindwa kufikia lengo hili la kuendeleza huduma ya maji, kama vile ushirikishwaji, ujuzi na kusahau kusema sababu ya msingi ya utawala mbovu uliokuwa unakumbatiwa na Mhandisi wa Maji wa Wilaya na kusingizia vijiji ambavyo havikukabidhiwa madaraka, kama sababu ya kushindwa. Sababu nyingine ni kwamba Serikali wakati huo ilishindwa kudhibiti wizi uliokuwa ukifanywa dhahiri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanga ni kuchagua. Je, ipi ni busara, kutafuta chanzo cha maji kwa kila kijiji au kuwa na chanzo kimoja au viwili vyenye uwezo na miundombinu ya kuwapatia maji vijiji vingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia faida ya miradi ya namna hii ya pili kama vile Chalinze ikifikisha maji katika vijiji 20, Handeni *Trunk Main* ukitoa huduma katika vijiji zaidi ya 70, mradi wa Kahama Shinyanga, Makonde, Wanging'ombe na mingine yamefanya vizuri na kuondoa kero kwa vijiji vingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Rufiji, kwenye miaka ya sabini, vijiji karibu vyote vya ujamaa vilikuwa na maji na mifumo, lakini hivi sasa vijiji vingi sana havina maji na kumekuwa na mzigo mkubwa wa uendeshaji ambapo wanajiji wengi hawana uwezo nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inaendelea kutekeleza miradi mitatu kule utete; Ikwiriri na Kibiti na kuvacha vijiji vingi hasa katika Kata za Ngaramba, Mbwara, Chumbi,

Mkongo, Ngorongo, Ndundunyikanza na Mwaseni vikiwa havina maji na kutegemea utatuzi wa kijiji kimoja kimoja na kugharimu fedha nyingi sana, naiomba Serikali kwa ajili ya kuisaidia Wilaya ya Rufiji, Jimbo la Rufiji kutatua tatizo la maji kwa kuongeza uwezo wa mradi wa Ikwiriri ili uunganishwe na chanzo cha maji katika Kijiji cha Mkongo ambapo kisima chake kina maji mengi sana ili kuunda mtandao wa miundombinu wa kuweshesha kuvunganisha vijiji 14 kutokea Ikwiriri hadi Mloka pamoja na vijiji tisa vilivyoko Ikwiriri yenewe ili kwa pamoja vijiji 23 viondokane na tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa Serikali itaongeza nguvu katika mradi wa maji wa mji ndogo wa Utete ili maji hayo yafike katika vijiji vya Kata ya Chemchem. Naiomba Serikali kutoa msaada wa dhati wa kuwapatia maji vijiji vya Kata ya Ngarambe, Mbware pamoja na Kata ya Chumbi, ili kwa pamoja, Serikali yangu itakuwa imetekeleza ahadi ilioanzishwa katika ilani ya Chama tawala, Chama cha mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, na kupendekeza miradi ya kutatua tatizo la maji katika Wilaya ya Rufiji ili miaka iliyofuata fedha za walipakodi zifanye kazi nyingine za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ilioainishwa ni ndogo mno kutekelezaaya inayosema naiomba Serikali kuongeza fedha hizi na kupunguza utegemezi wa fedha za wafadhili katika kutekeleza huduma hii ya msingi kwa faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hoja ikiwa Serikali angalau itaeleza namna itakayoshughulikia maombi yangu haya.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuungana na wenzangu wote kumtakia Waziri wa Wizara hii afya njema ili arejee nchini kuendelea na ujenzi wa Taifa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Wassira - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais kwa uwasilishaji murua wa hotuba ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nampongeza na kumshukuru sana Naibu Waziri wa Maj, Mhandisi Gerson Hosea Lwenge kwa uchapakazi na unyenyekevu mkubwa katika kazi yake ya Unaibu Waziri na kwa wakati kufanya kazi kwa niaba ya Waziri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Simanjiro ni mionganoni mwa Wilaya zilizopo kwenye nyanda kame na kwa hakika inaongoza kwa tatizo kubwa la maji kwa ajili ya binadamu na mifugo. Ni vigumu kuorodhesha vijiji vyenye matatizo ya maji katika Wilaya ya Simanjiro, kwani karibu vijiji vyote vitakuwa kwenye orodha hiyo isipokuwa nitumie nafasi hii kutaja vijiji ambavyo vinaongoza kwa tatizo hilo ambavyo ni Losokonai, Lozbene, Olchoro onyori, Lezumo, Lendarai, Langai, Irkujit, Loonderkes, Nadorijukia, Endonyongijape, Losoito, Kimotozok, Namalulu, Okutu, Orkesumet, Mererani na Kata ya Oljoro No. 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu wa Orkesumet umekamilisha upembuzi yakinifu na kwamba tayari kuna makubaliano kati ya Serikali yetu na BADEA. Hatua hii kwa kuzingatia mazingira ya Simanjiro na urasimu wa miradi ya BADEA haiwezi kuachwa iwe njia pekee ya kutegemewa, kwani maji Simanjiro yanahitajika leo kama siyo jana. Nashauri Serikali ikamilishe makubaliano na kampuni ya Kifaransa ya *ELIPSE Project* ili mradi uanze kutekelezwa sasa, vinginevyo Serikali itafute fedha za dharura sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji Mererani unahitaji kufanyiwa upembuzi ili kuona uwezekano wa kuvuta maji kutoka *K/A* au Mlima Meru, kwani Kata zote nne za Tarafa hii ya Moipo yenye Kata za Naisenyai, Mererani, Endiamtu, Shambarai ambazo uzoefu unaonyesha kuwa maji yake hayafai kwa matumizi na ndiyo maana watoto wanapinda miguu kwa miaka yote 50 ya Uhuru wa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mradi wa maji wa Hai/Bomang'ombe utumike kama chanzo cha kuaminika, kwani umbali wake ni chini ya kilometra kumi kuingia kijiji cha kwanza (Naisenyai) ndani ya Tarafa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ione uwezekano wa kutumia sehemu ya fedha za athari za ukame kwenye maeneo ya wafugaji pamoja na Wizara ya Maji kutenga fedha kwa ajili ya kuchimba mabwawa kwa ajili ya mifugo. Mradi huu wa mabwawa uende sambamba na uchimbaji wa visima kwenye vijiji ambavyo vinaongoza kwa tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kwa wananchi wa Simanjiro, kila kiangazi kuhamisha mifugo yao kwenda Kilindi na Handeni kufuata maji ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu hali yetu ni mbaya, siyo kwa chakula tu, bali pia tatizo la maji linaongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mizengo K.P. Pinda kwa kubainisha ukweli wa hali halisi ya ukame na tatizo la maji Wilayani Simanjiro. Namshukru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo K.P. Pinda kwa kuhakikisha Shilingi billioni 1.8 kwa ajili ya dharura ya miadi ya maji Orkesumet na maeneo yanayozunguka. Ikumbukwe kwamba Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete wakati wa kampeni ya mwaka 2010 aliwaeleza wananchi wa Orkesumet kuwa wakati wowote kutoka siku hiyo fedha hizo zingekuwa zimekwishatolewa ili kunusuru tatizo hilo. Ni fedheha kubwa kuwa hadi sasa hakuna kilichofanyika. Naishauri Serikali iondoe aibu hii sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Baada ya hayo naomba kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maji Mwanza, katika Wilaya ya Illemela. Katka Wilaya ya Illemela kuna Mradi wa Igombe ambapo *pump house* ipo, Kisima (*swamp well*) ipo, *intake line* tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ulifanyiwa usanifu tangu mwaka 2003 na kazi ya kuusimika mradi huu ilianza mwaka 2005/2006, baada ya hapo kimya. Haukuendelezwa tena. Mradi huu ungemalizwa ungekuwa wa manufaa sana kwa Kituo cha Afya kilichopo Nyamwirolelwa ambacho hakitumiki kama Kituo cha Afya cha Wilaya ya Illemela.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Kayenge *pump house* ipo, Kisima (*swamp well*) hakuna, *intake line* hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ulianzishwa pia mwaka 2005/2006 baada ya usanifu wa mwaka 2003, haukuendelezwa kama ule wa Igombe. Ungemalizika, ungefaa sana kwa vijiji nya jirani, mfano, Kata ya Sangabuye na kwingineko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba jibu, kwanini mradi huu ulisimama?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nyamagana, maji yamesambaa vizuri mjini tu. Kwa mfano, mabomba yamesambazwa hadi Kata ya Buhongwa, basi. Malalamiko ya wananchi ni mabomba kutotoa maji. Je, Waziri anasema nini katika Wilaya hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, Maji Wilaya ya Magu. Mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria maarufu kwa "Mradi wa Kalemela" (1970's) – "mradi wa Milembe" ulikuwa unahudumia watu takriban 60,000 wa Kata zifuatazo:-

- (a) Kalemela - vijiji ni Kalemela, Mayega, Chamgasa, Bushigwa, Mhela hadi Mabujose;
- (b) Igalukilo - vijini ni Lunda, Ng'wamagigisi na Nyangili;
- (c) Malili - vijiji ni Malili na Ngunga; na
- (d) Mkula - vijiji ni Mkula na Lutubiga.

Mheshimiwa Naibu Spika, *pump house* ipo na matanki mawili yapo ambayo yako Igalukilo na Mula.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ombi kwa wataalam kwenda kuuona mradi tajwa ili Wizara iutolee maamuzi mwaka 2012/2013. Tafadhali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kilio kikuwa cha kila leo kwa wananchi wa Wilaya za hasa Misungwi na Kwmiba kwamba wanataka maji kutokana na bomba kuu toka Ziwa Victoria. Baada ya kupeleka maji Shinyanga hadi Kahama sasa Wizara irudi kuwatolea maji wanavijiji ambao bomba hili limepitia. Tafadhali sana, naomba jibu vijiji kama Ihelele, Mbarika, Igende, Isesa Mwagiligili, Mhambo na Gukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, natoa ushauri ufuatao:-

- (i) Kutafuta pesa za ndani ili kupunguza utegemezi wa fedha za Benki ya Dunia;
- (ii) Serikali kuhimiza taasisi zake kulipa madeni ya an kra za maji; na
- (iii) Serikali kuititia hifadhi ya mazingira kutunza vyazo vya maji

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua mambo mawili. Serikali inipe majibu, ina mkakati gani kuhusu mradi wa Ntomoko ambao unahudumia vijiji zaidi ya kumi na saba katika Jimbo la Kondoa Kusini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye kampeni aliahidi kuwa Serikali itaukarabati mradi huu. Sasa nataka nijue ni lini ukarabati wa mabomba yaliyochakaa utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, pesa zilizotengwa kwa ajili ya mradi wa maji wa bank ya dunia ni kwa ajili ya kuchimba visima tu na hakuna pesa ya kusambaza maji hayo. Je, Serikali inasemaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia kwenye hotuba ya Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuiomba Serikali iweke umuhimu mkubwa katika Sekta ya Maji kwa kuongezea bajeti ya kutosha. Tatizo kwa Watanzania kuhusu maji ni kubwa mno na kero namba moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kuwa na mipango endelevu ikiwa ni pamoja na kuwa na *Masterplan* ya maji katika Wilaya zote hapa nchini. Kutokana na mikakati hiyo, ndipo gharama zieleweke na kukamilisha miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la maandalizi na uchimbaji visima unazisababishia Halmashauri na Wizara kutumia fedha nyingi ambazo hazittoi tija yoyote. Fedha nyingi zinazotumika kwenye eneo la *Geophysical Survey* zinapotea bure, maana huwa utafiti huu hauzai matunda na kupelekea visima vingi vinavyochimbwa kuwa havina maji pamoja na utafiti ambao huwa umekwishafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ieletekeze kwenye uchimbaji wa Malambo na usambazaji wa maji kutoka kwenye vyanzo vya uhakika vilivypo kama katika Jimbo la Lulindi kuwa vyanzo vya uhakika vya maji vinne; Chiwambo, Mkululu, Mkwaya, na Miwale. Ningombwa Wizara isaidie kuongeza uwezo wa fedha na utaalamu ili wananchi wanufaikie na maji yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Mheshimiwa Waziri kwenye kuhitimisha hotuba yake wananchi wa Jimbo la Lulindi wanataka kujua kwenye bajeti hii ya mwaka 2011/2012 ametenga kiasi gani kufuatia ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa alipotembelea Jimbo hili, ya Shilingi milioni 580 kwa ajili ya mradi wa Chiwambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Waziri aeleze kuhusu Shilingi milioni 500 zilizotengwa kwa ajili ya ukamilisho wa visima 10 kutumika kwa ajili ya uchimbaji malambo na usambazaji wa maji kutoka kwenye vyanzo mbalimbali hasa kutokana na taarifa kuwa katika visima 10 ni kimoja tu ndicho kitajengewa miundombinu kutokana na visima tisa kutofaa kumaliziwa kutokana na kutokuwa na maji.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara ya Maji kuititia Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata taarifa kuhusu pesa ambazo nilipeleka maombi maalum kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa maji Nanyamba, Serikali ilitoa Shiling milioni 240 kwa ajili hiyo. Hadi leo sijui fedha hizo ambazo zilitolewa zaidi ya mwaka mmoja, sijui zimefanya shughuli gani, kwani hadi leo wananchi wa mji mdogo wa Nanyamba hawajapata maji hata tone moja kutoka kwenye mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mradi wa Maji vijiji 10 kuititia Benki ya Dunia liangaliwe upya. Mchakato wa miradi hii ni mrefu na wa gharama kubwa sana. Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, tumemaliza na washauri waelekezi na kutafuta Wakandarasi na hadi sasa tunaendelea kutafuta Wakandarasi. Hii kidogo ni ngumu kuielezea kama Serikali, nashauri tubadili mikakati ya utekelezaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wizara hii kukabiliwa na changamoto nydingi, changamoto zinazotokana na ukweli kwamba maji ni muhimu kwa uhai wa mwanadamu, lakini pia kwa maendeleo. Kutokana na umuhimu huu, napata shida kukataa kuunga mkono hoja hii kwani kwa kufanya hivyo nitakuwa siwatendei haki wananchi hasa wa vijijini, lakini pia Serikali ambayo imetenga fedha japo kidogo kwa ajili ya Wizara hii. Hivyo, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba ufanuzi wa jambo moja tu nalo ni fedha za kusambaza maji katika maeneo yote ya mji wa Kahama. Maji yapo Kahama, ya uhakika lakini mradi ule ulihusu maeneo ya katikati ya Mji tu wakati maeneo mengi ya Mji bado hayajaunganishwa katika mtandao wa maji wa Mji wote wa Kahama.

MHE. STEPHEN J. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nawapongeza kwa kuwasilisha hotuba ya bajeti. Pili, naunga mkono hoja kwa kuamini matatizo yangu ya kisera/tariffs yatapatiwa majibu ya uhakika. Nimeshaleta mapendekezo yangu mapema awali ili nipatiwe majibu. Hoja hizo ni:-

- (1) Je, Serikali imechukua hatua gani kutatua tatizo la bei ya maji katika Manispaa ya Shinyanga? Ni lini bei mpya itatajwa?
- (2) Je, Serikali ina maoni gani juu ya Muundo wa sasa wa mradi wa KASHWASA na SHUWASA hasa kimahusiano ya kazi?
- (3) Je, Serikali iko tayari kuongeza ruzuku kiasi cha Shilingi milioni 695 kwa KASHWASA ili kusaidia gharama za uendeshaji na bei kushuka?

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kazi mbalimbali nzuri, lakini hili la maji ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo langu kuna Kata nyingi tu pamoja na Vijiji vimechanga hela nyingi ziko Benki, lakini hakuna kinachoendelea. Kata hizo ni Lupembe, Matebwe, Ikondo, Kitandililo na Mahongole. Naiomba Serikali ione umuhimu wa vijiji ambavyo wamechanga hela kutatua mapema zaidi tatizo hili. Pale Makambako mradi ni wa siku nyingi sana maana wakati ule tunapata maji idadi ya watu walikuwa siyo zaidi ya 15,000 leo hii Makambako tuko zaidi ya 65,000 na miundombinu ni ile ile ya zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Makambako sasa tupatiwe maji ya kutosha kwani watu wameongezeka zaidi kutoka 15,000 mpaka 65,000, siyo kitu kidogo.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu ya Makadirio ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii vilevile kutoa pole kwa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandoza - Waziri wa Maji kwa ugonjwa amba o unamsumbu. Naamini kwa jitihada za Madaktari na baraka za Mwenyezi Mungu atapata nafuu na punde atarejea katika utumishi wake kwa Serikali na Wapiga kura wake Jimboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai na maji ambayo tunayazungumzia ni maji yaliyo safi na salama. Kama ilani ya uchaguzi ya CCM inavyosema. Naipongeza Serikali kwa jitihada kubwa inazofanya kufanikisha azma ya llani ya CCM kwa Watanzania kupata maji safi na salama kwa maeneo ya vijiji na mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirejea kwenye kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2011/2012 imegusa Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Morogoro vijiji (Uk. 31, 71 na 154).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Morogoro ina idadi ya Kata 29 na vijiji 144 ambavyo vyote bado vinahitaji huduma ya maji yaliyo safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kutenga Sh.174,202,000/= kwa ajili ya kutekeleza programu ya maji na usafi wa mazingira ni pesa kidogo sana katika Wilaya ya Morogoro. Ni pesa ndogo sana, bahati mbaya sana Wilaya ya Morogoro ni moja kati ya Wilaya mbili ambazo hadi sasa hazijakamilisha taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri katika miradi ya *World Bank* ambapo vijiji 10 vitahusika katika Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali ifikirie jinsi gani itafanya kuongeza pesa zaidi katika Wilaya ya Morogoro ili kusaidia vijiji ambavyo vimeathirika na ucheleweshaji wa kuanza kwa mradi huo. Lakini vile vile katika uhifadhi wa mazingira na uondoaji wa mifugo iliyotapaka katika Wilaya yetu ili ujenzi wa bwawa la Kidunda uweze kutoa huduma inayotakikana katika jiji la Dar es Salaam na kwingineko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kuanza ujenzi wa bwawa la Kidunda ambalo itakuwa ni suluhisho la matatizo ya jiji la Dar es Salaam, vile vile katika vijiji vitakavyozunguka bwawa hilo. Ombi langu kwa Serikali wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja za Wabunge:-

(1) Serikali itenye pesa za upimaji wa maeneo ya makazi na kilimo kwa wananchi amba o watapisha maeneo yao patakapoengwa bwawa hilo. Halmashauri yetu ipatiwe fedha hizo ili wapimaji wakapime maeneo hayo ili wakilipwa pesa waelekee huko na huduma zote umeme, maji, barabara, shule, zahanati na mengineyo yakiwepo huko.

(2) Fidia ziendane na hali halisi ya maisha kwa sasa.

(3) Ulipaji wa fidia uende sambamba na makundi wanaume amba o wameoa fidia ilipwe kwa wote, hundi iandikwe mume na mke ili kukwepa waume kudhulamu haki za wake zao. Watoto yatima amba o wanalelewa na ndugu kama wazazi wao walikuwa na mali ambazo zitalipwa, zilipwe kwa watoto hao yatima kwa majina yao na siyo walezi wao.

(4) Mwisho, katika ujenzi wa Bwawa la Kidunda Serikai iangalie uwezekano wa kuhamisha vijiji vyote katika Kata ya Selembala Jimbo la Morogoro kusini ili kuepuka mafuriko katika siku za usoni baada ya ujenzi wa bwawa hilo. Serikali imejipanga vipi katika tazito la utunzaji wa mazingira na hasa uwepo wa mifugo mingi katika vyanzo vya maji ya mto Ruvu Msonje, Mvuka Mngazi na mingineyo yote itakayokuwa inatengeneza bwawa hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia Waziri Mwandosya kheri katika afya yake, apone haraka. Nampa pole Mheshimiwa Silima kwa ajali iliyopelekea mke wake apoteze maisha, naye kupata majeraha. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mke wake mpenzi mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Hanang ni moja ya Wilaya inayokabiliwa na uhaba mkubwa wa maji. Wilaya ipo katika Bonde la ufa na mlima ambaao una *volcano*. Ukichimba visima inahitaji mita nyingi sana kupata maji. Kama hiyo adha haitoshi, maeneo mengi ya madini ya *Floride* ambayo yanafanya maji ya visima vingi isifae kwa afya ya wanadamu na wanyama. Wilaya haina mito na haina miradi ya mabwawa/lambo isipokuwa ile iliyochimbwa wakati wa ukoloni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miji yetu midogo kama maeleo katika viambatisho yanavyoonyesha nayo yana matatizo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara isaidie jitihada za Halmashauri kufanya utafiti, ili Wilaya hii ambayo upatikanaji wa maji safi na salama ya uhakika ni mdogo, ili kubaini vyanzo vya maji ili kuokoa wananchi na wanyama waliopo. Hali ilivyo sasa hivi, inatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu, ila naomba mnisaidie, kwani Ubunge huu utayeyuka. Ahsante.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tarime, siungi mkono hoja iliyopo mbele yako, kwani Serikali hii kupitia Wizara ya Maji haiwatendei haki wananchi wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwatendei haki kwa sababu Wilaya ya Tarime zamani ikijulikana kama *North Mara* ilianzishwa toka enzi za ukoloni, lakini hadi sasa miaka 50 ya Uhuru, Wilaya ya Tarime iko taabani kwa kukosa maendeleo na hata huduma za lazima kama vile maji. Wananchi wangu hawajui hata kidogo, wala hawajawahi kuona maji salama na safi ya bomba. Pia wananchi wangu hawajui hata maji ya visima safi virefu au vifupi vilivyo chimbwa na Serikali kwa ajili ya matumizi ya maji salama na safi kwa afya zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kusikia kwamba wananchi wa Tarime wanaishi kwa kutegemea chemichemi ambazo hukauka wakati wa kiangazi. Hali hii imesababisha taabu, mateso, dhiki na shida kwa wananchi wa Tarime. Maisha ya wanatarime yanategemea miujiza ya Mwenyezi Mungu. Akiwalettea mvua wanashukuru, lakini maji yanakuwa na takataka ya kila aina, halikadhalika jua likipiga ukame unakausha chemichemi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, huo ndiyo usawa wa maendeleo kwa wananchi wote wa Tanzania? Ni aibu, tena aibu kubwa kwa nchi kama hii kutowatendea haki baadhi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, napenda kumwuliza Mheshimiwa Wassira (kwa niaba ya Mheshimiwa Mwandosya) maswali machache yafuatayo:-

- Wilaya ya Tarime hasa Mjini kukosa maji safi na salama kwa muda mrefu, Serikali haioni kuwa haiwatendei haki wananchi wa Tarime?
- Ziwa Victoria ambalo liko Wilayani Rarya (Zamani ilikuwa Wilaya moja) linawanufaishaje wananchi wa Tarime? Kwanini Serikali isichukue maji toka Ziwa Victoria na kuwapelekea wananchi wa Tarime? Au ina maana wananchi wa Shinyanga waliopelekewa maji ya Ziwa Victoria na Serikali ni bora zaidi kuliko wananchi wa Tarime? Je, huu siyo usaliti na unafiki?
- Je, Serikali inawasaidiaje wananchi wa Tarime waishio vijiji kupata huduma hii ya maji safi na salama?
- Je, Mto Mara ambao kwa kiasi kikubwa unapita katika eneo la Wilaya ya Tarime, unawanufaishaje wananchi wa Tarime? Ni lini Serikali itatumia maji ya mto huu kwa manufaa ya wananchi? Je, Serikali haioni kuwa ni hekima na busara kutumia maji ya Mto Mara kwa kuyajengea matanki katika mji mdogo wa Nyamwaga na baadaye kuyasambaza hadi Tarime mjini? Je, bado fikra ipo?
- Je, visima kumi vinavyofadhiliwa na Benki ya Dunia, utekelezaji wake katika Wilaya ya Tarime unasuasua, ni kwanini?
- Je, ni lini Serikali itajenga mabwawa madogo na makubwa kwa ajili ya hifadhi ya maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu Wilayani Tarime?
- Kwanini viongozi wa kitaifa, hasa Wagombea Urais/Marais wenyewe tangu enzi za Mzee Ruksa, Mkapa na hata Kikwete wamekuwa wakitoa ahadi zisizotekelezeka juu ya utatuzi wa tatizo la maji Wilayani Tarime?
- Je, mradi mkubwa wa maji unaofanyiwa usanifu Wilayani Tarime utaanza na kukamilika lini?
- Je, ni lini Serikali itachimba visima vya maji safi na salama kwa vijiji vyote vya Wilaya ya Tarime?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuuliza maswali haya, nahitaji kupata majibu ya uhakika yenye kujitosheleza na kukidhi haja. Kwa niaba ya wananchi wa Tarime, sitaunga mkono hoja. Ila naisihi Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi (CCM) iangalie kwa makini suala la maji Wilayani Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 132 inaonyesha kuwa Wilaya ya Manyoni, kati ya visima 22 vilivyochimbwa ni visima vinne tu vyenye maji. Kwa Jimbo la Manyoni Magharibi ni kisima kimoja cha kijiji cha Rungwa na kisima kimoja cha kijiji cha Makale ndiko kuna maji yaliyopatikana, lakini vijiji vyote vilivyokuwa kwenye programu ya kuchimbiwa maji vilikosa maji. Pia hali ni mbaya sana katika kijiji cha Kuitanula, Ipalalyu, Mitunda, Kayui, Damweru, Ipande, Muhang'a, Jilimali na Mkajenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchakato wa kuchimba maji kuna yule anayepima kubaini maji na Makandarasi anayechimba maji. Hawa imeonyesha hutofautiana; wanaotafiti na kupima maji wanakuja na lao na Makandarasi wanaochimba nao wana lao *at the expense* ya wananchi. Kuna mchezo unaofanyika kwa pande hizi mbili kufuja fedha za umma kwa manufaa yao na ni *continuing process*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendelekeza Serikali ivunje mtandao huu wa kutafuna/kufuja fedha za umma kati ya Watendaji wa Serikali na Makandarasi wanaopima ni watumishi wa Serikali/maji na wachimbaji ni Makandarasi binafsi. Hivi ni kwanini kila mwaka matatizo haya hujirudia bila ufumbuzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata maelezo, Serikali inachukua hatua gani kukomesha ufujaji huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jawabu la matatizo ya maji kwenye maeneo yetu ni uchimbaji wa mabwawa zaidi kwa ajili ya matumizi ya mifugo na wanadamu. Kwa bahati mbaya hili halitiwi maanani na Serikali katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ikazie zaidi uchimbaji wa mabwawa kuokoa fedha nyingi zinazopotea kwa uchimbaji wa visima visivyotoa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa na afya njema na kupata wasaa wa kuchangia katika Wizara hii muhimu sana kama kauli isemayo "maji ni uhai." Ni kweli maji ni uhai kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu kuu juu ya maji hasa inahusu udhaifu wa Watendaji wa Wizara hii au niseme na sisi sote tunaowasimamia hawa Watendaji. Serikali hii sasa ni miaka 50 baada ya uhuru lakini wananchi tumeendelea kuteseka na kuhangaikia kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui tatizo la nchi hii ni nini! Maana kwa umri wangu huu wa miaka 60 nimeshuhudia kudidimia kwa upatikanaji wa maji kwa wananchi. Hapo zama za ukoloni na mwanzo wa uhuru wakati wa mpendwa wetu Mwalimu Julius tulikuwa tupate maji salama kutoka kwenye vyanzo salama vyaya visima na chemichemi. Pia mito ililindwa na sheria zilizosimamiwa vyema na mamlaka ya wenyeji "*native authority*." Kila mtu alikuwa anazifahamu sheria za vijiji hadi vitongoji vyaya kutotumia mazingira ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mzazi alimfundisha toka awali mtoto wake huko nyumbani kutochafua vyanzo vyaya maji. Pamoja na hilo pia watoto tulifundishwa kutokata miti ovyo hata matawi, tulizuiwa kabisa, hii ilikuwa ni sehemu ya malezi na makuzi ya jamii. Jambo hili lilifanikiwa sana. Sasa ni nini kinachofanya tabia hizi njema zisirithishwe kwa vizazi vyaya sasa na baadaye? Ni tatizo kubwa sana kuwakosesha Watanzania elimu muhimu ya kuheshimu mazingira na matumizi ya maji. Kwanini elimu ya maji haitiliwi mkazo mashulen na vyuoni?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza kwamba mkazo wa elimu ya "*package*" nzima ya maji na usimamizi wake vitiliwe mkazo toka utoton hadi ukubwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo llingine linalonishangaza sana ni suala hili la Serikali ya CCM kutotambua umuhimu wa maji kwa uhai wa watu na kisha kwa maendeleo ya nchi yetu, kwani unapozungumzia maji, maana yake ni 'kilimo bora' kama sera ya Chadema inavyotambua maji ni makazi, maji ni misitu, maji ni mvua, maji ni chakula, maji ni afya na hivyo maji ni uhai. Lakini inaelekea kuwa Serikali ya CCM haitambui hili na ikiwa inatambua, basi ni kwenye maneno tu na wala haliko moyoni, ndiyo maana mambo yanaishia kwenye vitabu vyaya ilani na mipango ya CCM bali haliko kwenye vitendo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili lisemwalo hapo juu linajithibitisha katika bajeti hii na nyingine za Serikali ya CCM, maana mipango iliyoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu lukuki lakini fedha iliyoengwa kiduchu (angalia bajeti) huwezi kuamini. Iweje kweli kama tumekamia kuondoa tatizo hili la maji tuweke kiasi kidogo hiki cha fedha? Kwanza maji yenyewe ni raslimali, pia ikipangwa vyema maji ni chanzo cha mapato na uimarishaji wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kuhuzunisha kwamba unapozungumzia maji na matatizo yake, basi ni unazungumzia matatizo makubwa yanayowakabili robo tatu ya wanawake wa vijijini na mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la maji linawahu sana wanawake kwa vile mila na desturi za jamii ya Watanzania zinaweka jukumu hili juu ya wanawake. Kwa ajili ya mfumo dume, unaathiri hata upangaji wake wa bajeti. Kwa uhalisia tu wapangaji wa bajeti walio wengi ni wanaume, lakini watumiaji ni wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanga ni kuchagua. Hawa wapangaji wa bajeti wakaona kuwa kipaumbele ni 'barabara' kuliko maji. Hili limeonyesha katika bajeti hii kwamba barabara ambazo zinawagusa wanaume ambao wengi ndiyo watumiaji wa vyombo vinavyotumia barabara, wamejipangia bajeti ya kutosha na akiba watakapohitaji. Lakini bajeti ya maji ina fungu la kusikitisha na kukatisha tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai yangu kuwa Serikali isikilize na kuzinduka kuhusu kuwapatia wananchi wake hasa wanawake na watoto wao wa kike ambao husumbuka sana na upatikanaji wa maji ya kutumika majumbani. Waokoeni wanawake na adha hii ya maji na mabinti zao kushindwa kuendelea na masomo kwa ajili ya kutumika katika kuipatia familia maji ambayo ni uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. JOHN P. J. MAGUFULI: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, hongereni kwa mipango mizuri ya maji na kazi nzuri mnazofanya. Aidha, natoa pole kwa Profesa Mwандосya, Mungu amsaidie apone haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Mheshimiwa Waziri wa Maji - Profesa Mwандосya alitoa Shilingi milioini 75 kwa ajili ya kuchimba visima vine. Visima vilivyo chimbwa ni vitatu na vyote havitoi maji, sasa ni karibu mwaka. Hakuna maji na fedha zote zimetumika *with no water* (H_2O), kwa bahati mbaya zaidi visima hivi vimechimbwa ambapo siyo mkondo wa maji. Hii siyo haki. Suala hili analifahamu Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na hata Katibu Mkuu Dkt. Sai analifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mradi huu urudiwe, kama kuna kandarasi aliusika na aliyehusika *ku-design* mradi, ni vyema wakarudia ili kutoa kero hii kwa wananchi, kwani ahadi hii alitoa Rais na Mheshimiwa Waziri mwenyewe. Fedha zilitolewa, lakini hakuna maji. *This issue is very urgent* kwani ni kero kubwa kwa wananchi wa Mji wa Chato.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji ni kubwa sana Wilayani Mbarali. Wananchi wa vijiji vya Kanganga, Mkandami, Matemela, Ipwani, Limsem, Itipungi, Manienga, Isumura na Kata ya Igava. Vijiji hivi vilichagua mradi wa maji kutoka mto Mpeng'o Wilayani Njombe. Mradi huu unafadhiliwa na Beniki ya Dunia imekuwa ikitamkwa bila kuleta matumaini ya kupatikana maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatoa tamko gani kwa wananchi wa vijiji hivi ambavyo toka nchi hii ipate uhuru hawajui maji ya bomba? Wamenitura njiwe niwasemee. Hata hivyo, naomba Serikali ichukue jukumu la mradi huu, kwa sababu kutohana na upembusi yakinifu uliofanywa na *Don Consultant* imeonekana utagharimu zaidi ya Shilingi bilioni nane, fedha ambazo kwenye Halmashauri hazipo. Je, Serikali haioni ipo kila sababu ya kutoa fedha ili kukabiliana na gharama hizi? Tafadhalii naomba njibowi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji Wilayani Mbarali ni matatizo matupu. Maji wanayotumia ni matokeo ya miradi ya *DANIDA* iliyojengwa zaidi ya miaka 20 ishirini iliyopita, kwahiyo imechakaa. Mtandao wa maji umechakaa na hivyo kufanya maji kutopatikana kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kata za Rujewa, Igawa, Ubaruku, Songwe Imalilo, Mapogoro, Utengule, Chimala, Igurusi, Mswisi, Luhanga, Itamboleo, Chimala, Mahongole, Mwatenga, Madibira, Miyombweni na Ruiwa kote maji ni tatizo. Wakati mradi huu unajengwa idadi ya watu ilikuwa kidogo. Kwa sasa watu wameongezeka mara mbili. Kwahiyo, naomba

mradi wa maji kwa Wilaya ya Mbarali kubadilisha mabomba, kuweka mabomba makubwa zaidi ili yaweze kutosheleza idadi ya watu ambayo imeongezeka kutoka takriban watu laki mbili na hamsini hadi zaidi ya watu laki nne kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua ni lini mchakato wa kubadilisha mabomba utaanza? Lipo tatizo katika kuboresha Banio la maji katika Banio la Igomelo. Jitihada za Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, katika kuboresha na kutoa maji salama, waliamua kujenga chujio la maji, lakini nasikitika, wakatokeza askari wa kipengele *Game Reserve* na kusitisha huduma hii muhimu isifanyike, kwa kisingizio kuwa eneo hilo lipo ndani ya hifadhi. Sote tulishangaa kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali hatujawahi kushirikishwa kwenye uwekaji wa mpaka huo. Mkurugenzi alipotaka utaratibu wa kufuatwa aliambiwa awasiliiane na watu wa mazingira nao wanamazingira walitaja gharama za kutisha. Hivi nchi hii tumefikia hatua hii ya kutojali huduma za wananchi? Naomba ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atembelee Mbarali afike aone hali halisi katika Kata za Mawindi, Igava, Ipwani, Rujewa, Songwe Imalilo, Chimala, Mvatenga, Ruwa na Madibira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nitaunga mkono hoja nikijibowi.

MHE. PHILIP G. MTURANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mungu kwa kupata wasaa huu ili niweze kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pole ya dhati kwa Waziri wa Maji - Mheshimiwa Profesa Mark Mwандоса na namwombea afya njema azidi tujumuike pamoja katika kulisukuma hili gurudumu la maendeleo kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazipongeza hotuba zilizowasilishwa na Waziri wa Maji, Kamati pamoja na ile ya Kambi ya Upinzani. Rai yangu, ninaiomba Serikali iyazingatie maoni yote yaliyotolewa hasa na hotuba ya upinzani ili kuyafanya kazi yale yote yaliyoainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai. Maji ni kiungo muhimu katika maendeleo. Sekta zote nyeti zinategemea bidhaa hii mfano viwandani, mashambani, katika migodi, mazingira pamoja na matumizi ya binadamu kwa maana ya mijini na vijijini, tajiri na masikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiomba pesa nydingi katika bajeti yake ya maji lakini pesa hiyo imekuwa ikifujwa na wajanja wachache na hivyo kuhujumu juhudji jitihada hizo. Mko wa Dar es Salaam ni mfano wa Mikoa ambayo imekuwa ikihujumiwa na Watendaji. Ndani ya DAWASCO kuna matatizo makubwa ya kiutendaji hali ambayo inachangia udhaifu wa DAWASCO katika kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi juu ya DAWASCO upo kuhusu malalamiko yao kwamba uongozi uliopo ni mbovu na unadhoofisha juhudji za DAWASCO. Wafanyakazi wamekuwa wakinyanyaswa, kuhamishwa ovyo, vitisho, sambamba na mambo mengine maovu. Wafanyakazi wamepeleka malalamiko yao kwa maandishi kwa Rais na nakala pia kwa Waziri. Nataka kujua Wizara imechukua hatua gani hadi sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge wa Ubungo - Mheshimiwa Mnyika ametembelea DAWASCO Januari mwaka huu ikiwa ni pamoja na kuandika barua mbalimbali kwa nyakati tofauti za kero ya maji maeneo ya Msigani, Goba, Msakuzi, Golan, Makuburi na maeneo mengine, lakini barua husika hazijapata majibu stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya wafanyakazi ndani ya DAWASCO yanapunguza kasi ya kuhudumiwa wateja katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam. Matatizo ya DAWASCO yako pia katika Ofisi mbalimbali za Kanda na Wilaya za DAWASCO zilizopo Temeke, Ilala na Kinondoni. Tunataka Wizara, DAWASA na EWURA kwa kushirikiana na Wabunge wa Dar es Salaam waunde chombo huru cha kuchunguza matatizo ndani ya DAWASCO ambayo kama yasiposhughulikiwa matatizo ya maji yataendelea hata kama fedha zitaongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, maji kwenye Manispaa ya Kigoma Mjini hakuna. Watu wanaopata maji ni asilimia 52 ya *population* yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa maji chini ya Mita tano. Yaani maji ya Ziwa Tanganyika ni safi na salama, yapo machoni mwetu, lakini kwenye mabomba hayapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yote inayosemwa ni miaka mitano mpaka 10 iliyopita, lakini hakuna kinachoendelea. Tunataka kujua lini Mji wa Kigoma utapata maji ya uhakika? *Story* ya miradi tumechoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka maji, pia msisahau kwenye ilani ya CCM 2005 – 2010, tulisema tutapeleka maji mijini kwa asilimia 90. Je, Kigoma mjini siyo mjini au ahadi haikutekelezwa?

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Maji - Mheshimiwa Profesa Mark Mwандосya, Naibu Waziri wa Maji - Mheshimiwa Eng. Gerson Hosea Lwenge, Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mkuu wa DAWASA, Mkurugenzi Mkuu wa DAWASCO, pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye mwelekeo wa kuondoa adha ya maji nchini. Vilevile nitakuwa mchoyo endapo sitampongeza Mheshimiwa Stephen Wasira kwa kuwasilisha bajeti hii kwa niaba ya Waziri mwenye dhamana ya Maji Mheshimiwa Profesa Mark Mwандосya ambaye anaumwa, ukweli amewasilisha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hii, nategemea kupata ufanuzi kutoka kwa Waziri na Naibu Waziri wakati wanajibu hoja za Wabunge hapo kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza sana Serikali kwa juhudhi zake za kutoa huduma ya maji kwa wateja mpaka kwenye makazi yao. Tatizo ni kwamba wapo wateja ambao hupewa *bili* kubwa za maji wakati maji nyumbani kwao hutoka mara moja moja sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali kuhakikisha kila mteja wa maji anafungiwa mita ili kuondoa udanganyifu wa malipo ya matumizi ya maji kwa kila mwezi. Ninasubiri jibu toka kwa Waziri wakati anajibu hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujulisha Serikali kuwa kuna matatizo makubwa sana katika kutekeleza miradi kumi ya kila Halmashauri ya maji inayotekelizwa na *World Bank*. Ninasema hivi, kwa sababu miradi hii inachukua muda mrefu sana kutekelezeka ukizingatia adha kubwa waliyonayo wananchi katika vijiji vilivyteuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali kuhakikisha usimamizi wa miradi hii iwe mizuri kuliko ilivyo sasa. Mfano, mradi wa maji Singida Mjini sasa ni miaka mingi sana bado mradi huu haujakamilika. Je, ni lini mradi utakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa masikitiko yangu kuwa katika Wilaya ya Iramba, Kata za Kinyangiri, Kyengege na Matongo zina kero ya maji kweli kweli, kwani hazijawahi kufikiriwa hata mara moja. Wananchi hususan wanawake, wanapata adha kubwa na kufuata maji mbali na huko wanakuta msururu mkubwa. Kwa kweli hadi ndoa zinayumba kwa sababu wanawake wanatumia masaa mengi kufuata maji huku waume zao wanangojea nyumbani na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Mheshimiwa Waziri awaeleze wananchi wa Kata nilizotaja kuwa kwenye bajeti hii wametengewa fedha au sivyo? Kama sivyo: Je, bajeti ijayo yaani mwaka wa fedha 2012/2013 watapewa kipaumbele? Nasubiri jibu wakati wa majumuisho hapo kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kupeleka maji mji mdogo wa Shelui pamoja na vijiji vya Kizonzo na Mseko. Tatizo katika mji huu mdogo wa Shelui ni kukosekana

kwa mtaalam wa maji ambaye angekuwepo wananchi au wateja wa maji wangekuwa wengi sana. Wananchi wengi wanahitaji kupelekewa maji kwenye nyumba zao, bali inachukua muda mrefu kwa sababu mtaalamu mpaka atoke Makao Makuu ya Wilaya. Ninaomba Serikali iniambie ni lini fundi bomba atapelekwa Shelui?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze sana wenzetu wa *DAWASA* kwa kazi nzuri ya kukarabati miundombinu ya Maji Dar es Salaam ingawa ukarabati bado haujakamilika, mfano Magomeni Mikumi, Mtaa wa Muhuto. Mtaa huu una shida ya maji sana kwani mabomba yamechakaa mno, maji yanapotoka yanakuwa na udongo. Vilevile wateja wa mtaa huu wa Muhuto wamechimba kuunga tepu za maji chini urefu wa mita mbili. Sijui Serikali inajua hili suala! Kama Serikali inajua: Je, hao wateja wanalipa bili za maji au hawalipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono bajeti nikiwa na imani nitapewa majibu kama alivyoniahidhi wakati nauiza swali la nyongeza kwenye swali la Mheshimiwa Ritta E. Kabati la Na. 451 tarehe 19 Agosti, 2011.

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa hotuba ya bajeti, japo fedha ni kidogo, lakini wamejaribu kuviainisha kwa maeneo mbalimbali ya nchi. Pamoja na mipango mizuri, naomba sana Wizara isimamie kwa karibu miradi hii, kwani uzoefu umedhihirisha kuwa Halmashauri za Wilaya siyo wasimamizi wazuri. Ulaji umezidi kipimo na hatimaye ni Wizara ya Maji ndiyo inayolaumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Busega kuna mabwawa ya Gininiga na Ilumya yamejengwa kupitia Mpango wa *DASIP*, lakini utadhani ni mtoto anajifunza kazi. Naomba Wizara ya Maji isilachie jumla jumla wajibu huu wa kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa iliyopo sasa ni ya mabadiliko ya tabia nchi inayopelekea mvua kuadimika na vyanzo vya maji kukauka. Pia matumizi ya maji ya binadamu yasiyo na usimamizi ni tatizo kubwa zaidi. Kilimo cha umwagiliaji ni muhimu sana kulisha idadi ya watu wanaongezeka, lakini bila kusimamiwa vyema, itatupeleka kwenye janga la upotevu wa maji. Hali hii inadhihirishwa na hali iliojitekeza mwaka huu kwa Mto Ruaha kukauka licha ya kuongezea maeneo ya Ihefu na Usangu katika Hifadhi ya Ruaha. Matumizi ya maji kwa kuyaondoa kwenye mkondo mkuu na kuingia mashambani bila usimamizi ni hasara kubwa. Hii ndiyo imepelekea hata Mtera kukauka na kuishia giza kuu mwaka huu nchini. Kama Taifa, lazima tuainishe matumizi ya maji kwa ajili ya kilimo na matumizi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la uharibifu wa mazingira kwenye mabonde ya mito Simiyu na Duma. Mito hii sasa inakauka mapema. Napendekeza miradi ya *LVEMP* ijielekeze pia katika kuhifadhi uasili wa mabonde haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa kuanza kuutekeleza mradi wa maji bomba wa Lamadi ukisimamiwa na Mwauwasa. Naomba mradi huu utekelezwe haraka kwa sababu sasa hivi mji wa Lamadi wenye wakazi 40,000, watu wanunua maji Sh. 200/= kwa ndoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa maji kwenye Makao Makuu ya Jimbo Nyashimo unakwamishwa na udogo wa mabomba. Tathmini ilionyesha kuwa Shilingi milioni 10 tu ndizo zinahitajika kuondoa kero hiyo. Chonde chonde, naomba Wizara itupatiate fedha hiyo ili tuondoe kero inayofanya wananchi waamini kuwa maji huwepo wanapokuja wageni wa Serikali tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa siku nyingi wa maji bomba wa Kalemela - Bushigwamhola - Nyangili - Malili - Mkula ulikuwa unahudumia takribani theluthi moja ya Jimbo. Mradi huu ulijengwa wakati wa Mbunge, Hayati Dorothea Milembe. Mradi huo sasa umeachwa tu. Naomba Waziri apeleke wataalamu ili waufanyie tathmini ili kujua mahitaji ya kuukarabati mradi huo. Ukiiondoa mradi wa Lamadi, huu ndiyo unaofuatia kwa umuhimu Jimboni Busega kwa sababu unahudumia Kata tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji wa Ngasamo uliokusudiwa kupitia *TASAF* kuhudumia vijihi nane ambao uliingiliwa na vidudu mtu. Tanki kubwa ilijengwa, ilipofika muda wa

kuleta mashine/pump, ndipo kirusi kilipoingilia na mambo yote yakasimama. Chanzo cha maji ambacho ni kisima cha Nyamagana kina maji yasiyo na ukomo. Naomba tathmini ya mashine stahili iangaliwe na mabomba yatandazwe ili vijiji vilivyokusudiwa vya Ngasamo, Sanga, Iralamote, Ng'wang'wenge, Mwamigongwa, Malili, Ngunga, Nyangoko vipate maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha hotuba, nimeona mradi wa visima kwa ushirikiano na Serikali ya Misri kwenye maeneo kame utekelezwe kikamilifu. Mradi huo utawezesha vijiji vya Mwamigongwa, Lwangwe, Mwakiloba, Mwangoba na Badugu vipate visima na kupunguza kero ya akina mama kuamka usiku wa manane kwenda kutafuta maji. Hali hii inaathiri sana mahusiano ya kifamilia, lakini pia inaathiri wanafunzi wa kike kuweza kufuatilia masomo baada ya kukesha visimani na mitoni wakisubiri maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la maji katika Shule zote za Msingi na Sekondari. Nadhani hili ni tatizo la kitaifa. Wakati wa kiangazi ambapo juu huwa ni kali, watoto huteseka sana na hata kuathirika kiafya na pia kushindwa kufuatilia vyema masomo. Napendekeza kuwa huu utaratibu wa kuvuna maji kwenye majumba, basi uanzishwe kama program ya kitaifa ya kuweka maji katika mashule yetu. Nitaomba Jimbo la Busege liwe kwenye pilot project ya mpango huo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Wizara isimamie programu zake kikamilifu badala ya kuachia Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuokoa muda naomba nichangie kwa namna ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mmoja anafahamu kuwa viumbe vyote vyenye uhai vinahitaji maji; watu, wanyama, miti, mazao na vilevile viwanda na uzalishaji wa umeme. Jambo la kushangaza ni Serikali kutenga Shilingi bilioni 446 wakati huku tukiwa na matatizo ya mabwawa ya umeme kupungukiwa na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba Serikali iongeze Bajeti ya maji kwa kukopa mkopo wa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuchukulia maanani matatizo ya maji vijiji na taabu wanayopata akina mama na wanyama, nashauri hali hii ichukuliwe kuwa ni dharura kama ile ya umeme na kwa ajili hiyo, Serikali itafute fungu la fedha la kuokoa hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwamba watu wote walioiba maji wakatiwe mabomba yao. Watumishi wa Mamlaka za Maji hasa wa Arusha wachukuliwe hatua za kinidhamu. Aidha, Serikali itoe bei ya maji, inakuwaje debe moja ya maji iuzwe Sh. 500/=?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Mbulu fedha nyingi ya miradi ya maji imetumika vibaya kutoptera na kutokuwa na utafiti makini wa kijiolojia na Haidrolojia. Visima vingi vimechimbwa na kukutwa havina maji. Visima vyote vya fedha za Benki ya Dunia havijasaidia Wilaya hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya kuwa na mifugo mingi na kilimo cha kumwagilia hasa kitunguu swaumu, naomba Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ifikiriwe kuongezewa fedha za malambo na mabwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo katika mabonde ya maji, nashauri ili kuhifadhi vianzio vya maji, kilimo kando kando ya mito na maeneo ya "Swamps" ikatazwe kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumtakia kheri na Mwenyezi Mungu amjalie afya Mheshimiwa Waziri wa Maji – Prof. Mark Mwandosya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, sitaunga mkono hoja ya Wizara hii kwani katika vijiji 68 vilivyopo katika Jimbo la Mufindi Kaskazini, vijiji vilivyokuwa na maji ya uhakika havizidi viwili. Mji wa Mafinga ndiyo unaongoza kwa kuwa na matatizo makubwa. Kuna baadhi ya vijiji havina hata kisima kimoja, hili ni jambo baya sana. Kata kama Ihanu yenyenye vijiji sita hakuna hata kisima kwenye kijiji chochote Kata kama Mdaburo yenyenye vijiji vitano, hakuna hata kisima kimoja Ifwagi, Ihelimba, Isalavanu, Igombirani, Sudani, Ikweha, Mapanda Kibengu na Rungembra.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, Waziri alidanganya kuwa Jimbo la Mufindi Kaskazini kuna visima 78, hakusema kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa tayari kuunga mkono nitakaposikia Serikali ikitoa ufanuzi na kuahidi kuleta maji angalau kisima kimoja kila kijiji.

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nawapa ponegez kwa hotuba nzuri na kazi nzuri mnayoifanya Wizarani. Tunamtakia kila la heri Mheshimiwa Waziri apone haraka. *Get well soon.* Nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tujihakikishie kupata maji endelevu, lazima tuwekeze zaidi katika utunzaji wa vyanzo vya maji. Tuhakikishe kuwa tunaanzisha Mfuko wa Maji ambao utachangiwa na wote wanaotumia maji. *TANESCO* ambao wanategemea maji katika kuzalisha umeme wachangie mapato yao katika kutunza vyanzo vya maji (*Water Resources Management*). Viwanda vya vinywaji pia wachangie kwa vile asilimia 98 ya malighafi ni maji. Huu ni mfuko ambao utasaidia sana katika kuendeleza miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa maji vijijini – *World Bank Project*, unasuasua sana vijijini kutokana na wakandarasi wa maji kutokuwa na mitambo ya kuchimbia maji. Mitambo ya kukodi ni michache, hivyo Wakandarasi inabidi wasubiri kupata mitambo. Serikali iondoe kodi kwenye *Water Rigs* ili mitambo ipatikane kwa wingi na hivyo kupunguza gharama za kuchimbia visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Pangani inapata maji toka *Bore holes*. Maji haya yana chumvi 1800 ec/per cc karibu kufikia “unacceptable levels” ambayo ni 1800 ec/per one cc. Maji haya hayafai kwa uendelezaji wa shughuli za kiuchumi bila ya *Water softener*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi yetu ni haya yafuatayo:-

- (a) Katika kipindi cha mpito tunahitaji pampu ya kusukumia maji, gharama yake ni Shilingi milioni 20 tu.
- (b) Mto Pangani uko karibu na unapita Mjini Pangani. Tunahitaji kuanzisha mradi wa maji mkubwa wa kuleta maji toka mto Pangani. Huu utaratibu wa *Clustering na Tanga Urban Water and Sanitation Authority* haujasaidia sana upatikanaji wa uhakika wa maji.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mark J. Mwandosya, Naibu Waziri – Mheshimiwa Gerson Hosea Lwenge, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi – Ndugu Bashiri Juma Mrindoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza mchango wangu kuchangia kuhusu tatizo la maji. Naomba nisisituze juu ya dhamira ya Serikali ya kuupatia mji wa Bariadi maji ya kutosha kutoka Ziwa Victoria. Mpango huu uko katika ahadi za Rais, lakini umuhimu wa mpango huu ni kuwa utatoa huduma ya uhakika kwa wananchi wa Mkoa mpya wa Simiyu, pamoja na vijiji vingi ambapo mradi huu utapitia. Pia tunaomba Halmashauri za Wilaya zisisitizwe kutenga fedha ya kutosha ili kujenga mabwawa kwa ajili ya binadamu na mifugo ili kupunguza kero kubwa iliyopo hususan

katika Wilaya za Busega Bariadi, Meatu na Maswa. Lakini pia fedha inayotengwa kwa kazi hiyo ya maji ni muhimu ikasimamiwa vyema ili kuwe na kazi inayoendana na thamani ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Busega mradi wa maji bomba Ngasamo ulianza kujengwa na TASAF, sasa umeachwa unasuasua. Mradi huu ulilenga kuhudumia vijiji nane Ngasamo, Sanga, Ngunga, Malili, Mwamigongwa, Imalamate, Ng'wang'wenge na Nyangoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kisima kina maji mengi, tenki lilijengwa, kinachokosekana ni mashine (*pump*) na mtandao wa mabomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji wa Kiloleli ulijengwa kuhudumia Kata ya Kiloleli na vijiji vyake vya Ihale, Ijitu, Masanza, Liswimila, Iluya na Mwabuduli. Mradi umeachwa umekufa wakati tenki na mabomba yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji wa Mwamanyili ambao TANESCO tayari wamepeleka umeme kwenye mashine, lakini mtandao wa mabomba umekufa. Mradi huu unalenga kusaidia vijiji vya Mwamanyili, Mwanangi, Nassa Cunnery, Chanela na Mwamakanga kikiwemo na Kituo cha Afya Mwanangi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifanye mpango kabambe wa kuweka mfumo wa kuvuna maji katika mashule na taasisi zote za Serikali kule Simiyu wakati wa kiangazi. Watoto wanateseka kwa kiu na kushindwa kusoma kwa makini. Ni wajibu wa Serikali kusaidia hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Naibu Spika, katika majumuisho ya hotuba yake, naomba atoe ufanuzi kuhusiana na masuala yafuatayo yanayohusu mradi wa maji katika visima vya Kimbiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni uamuzi wa Serikali kuhusu eneo la mradi? Je, eneo lilitotwaliwa ni ekari 60 au zile 7000 za awali?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini wananchi waliosalia watalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, maeneo mabomba yatakayopita yatanufaika vipi na mradi huu? Kigamboni ina matatizo makubwa ya maji.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasilishe maombi kwa Waziri wa Maji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Tunduru Kusini lina vijiji vingi ambavyo vina matatizo sugu ya kupata maji safi na salama. Matatizo yamegawanyika katika makundi matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji ambavyo chini kuna miamba ni Likweso, Lukumbo, Msinji, Imani na Kazamoyo. Kiasi cha pesa kinachotengewa Halmashauri hakitoshi kuwezesha kukodi mitambo yenye uwezo mkubwa kutoboa miamba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijiji ambavyo viko kwenye miinuko. Vijiji hivyo vinahitajika kupatiwa visima virefu sana zaidi ya mita 100. Hali hii inahitajika mitambo mikubwa yenye uwezo wa hali ya juu kuweza kuyafikia maji yaliyopo chini sana, pia kuwa na pampu zenye uwezo wa kuvuta maji kutoka kwenye kina kirefu. Vijiji hivyo ni Tuwemacho, Msinjewe, Namasalau, Nasya na Chilonji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji ambavyo vinaweza kupata maji kwa kutumia visima vya urefu wa kati, dhamira yangu ni kuiomba Wizara itusaidie kuiwezesha Halmashauri kifedha ili imudu changamoto kwa vijiji vinavyoangukia kundi la kwanza na la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SLYVESTER M. KASULUMBAYI: Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya kazi za lazima kwa mradi wa usimamizi wa mazingira ya Ziwa Victoria ni pamoja na kutayarisha mpango kabambe wa kukarabati mazingira ya Bonde dogo la Mto Simiyu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Bariadi, Magu, Kwimba, Meatu na Maswa na kuibua na kuandaa miradi ya jamii ya kuhifadhi mazingira na kuongeza kipato cha jamii inayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuitekeleza adhima hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Maswa ilishirikiana na wanakikundi wa Kijiji cha Ipirilo walioamua kuzitumia fursa za Bonde dogo la Mto Simiyu kwa kuanzisha mradi wa kilimo cha umwagiliaji hapo 2009/2010. Wanakikundi hao walichimba mtaro kutoka katika mto huu wenyе urefu wa kilometra 17.6 unapita katikati ya mashamba ya wanakikundi hao ukizungukia kila shamba. Uchimbaji huo wa mtaro ulichimbwa chini ya maelekezo ya wataalamu wa kilimo kitengo cha umwagiliaji mashamba. Wanakikundi hao walitumia nguvu zao nyingi wakachimba mtaro huo kwa nia ya kuwa na uwezo wa kuyatumia maji ya mto Simiyu pale mvua zinaposhindwa kunyesha na kuyatumia maji ya mto huo wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uchimbaji huo kuwa wa gharama kubwa na uliwichukua miezi mingi kuuchimba na kuumaliza, Serikali haikuweza kuwaunga mkono wanakikundi hao, hali iliyosababisha mtaro huo kubomoka katika kipindi hicho cha mwaka 2009/2010. Kama hiyo haitoshi, wanakikundi hao katika mwaka 2010/2011 waliufukua upya mtaro huo wenyе urefu wa kilometra 17.6 kwa matamanio kuwa Serikali itawajali na kuwapatia bajeti ya kuuwezesha mtaro huo kuyavuna maji ya mto huo wa Simiyu ili waweze kuboresha kilimo chao kwa lengo la kuondoa umaskini unaowazunguka.

Pamoja na juhudhi hizo, Serikali bado haijallona hilo. Je, Serikali inataka wanakikundi hao mpaka wafanye lipi ili ijue kuwa wanakikundi hao walikuwa wanatimiza yale yaliyoelekezwa katika Mradi kabambe wa usimamizi wa mazingira ya Ziwa Victoria? Kwakuwa bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2011/2012 imeishia kutoa maelezo ya miradi ya kuongeza kipato kwa vikundi na jamii mbalimbali katika eneo hilo utaanza: Je, maelezo haya maana yake ni kuongeza kipato kwa wanakikundi walitumia nguvu nyingi kuuchimba mtaro wenyе urefu wa kilomita 17.6 ambao Serikali haijataka kuuingizia kwenye bajeti tangu mwaka 2009/2010 na 2011/2012? Naomba nipate maelezo ya kina ili wanakikundi hao wasiendelee kuutamani mradi huu wa usimamizi wa mazingira ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono tu pale nitakapoona wanakikundi hao Serikali imewatambua kwa kuwapatia bajeti ya kuendeshea mradi huo ili uweze kuyavuna maji ya bonde dogo la Mto Simiyu.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuleta hotuba nzuri sana hapa Bungeni. Pia nampongeza Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifanya katika nchi yetu. Pamoja na pongezi hizi, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji vijijini ni kubwa sana. Vijiji vingi hapa nchini havina maji. Mfano halisi ni vijiji vya Jimbo langu la Karagwe. Vijiji vya Kata za Ihembe, Rugu, Nyakasimbi, Nyakahanga, Kayauga, Ihanda, Chonyonyo, Kibondo, Nyakabanga, Nyabiyonza, Ndama, Kituntu, Chanika, Kanoni na Igurwa havina maji hata kidogo. Hata maeneo ya mijini ikiwemo Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe, yaani Kayanga na Omurushaka hayana maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu, mifugo na umwagiliaji. Kwa ufupi Jimbo la Uchaguzi Karagwe lina tatizo sugu la maji maeneo ya vijijini na mijini. Upatikanaji wa maji siyo zaidi ya asilimia 20. Hii ni hatari kwa afya ya wananchi wa Jimbo la Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Karagwe imejaliwa kupata vyanzo vingi vya maji ikiwemo mito, maziwa na kadhalika, mfano halisi ni Ziwa Victoria, Ziwa Kajungu Kata Bweranyange Wilayani Karagwe, Ziwa Burigi, Ziwa Kaberenge, Ziwa Songambеле, Ziwa Chenjubu pamoja na mito mingi yenye maji yasiyokauka muda wote. Tunao mto Kagera unaopita Wilayani Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni kwamba Wilaya hii haina maji safi kwa ajili ya wananchi wake. Tunaomba ijengwe miundombinu ya kutosha angalau kwa kuanzia maeneo ya mijini kama Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe (KAYANGA) na mji mdogo wa Biashara wa (Omurushaka). Ili kumaliza tatizo hili ni kujenga mradi mkubwa wa maji kama ulivyo mradi wa *Wami River* Wilaya ya Bagamoyo maeneo ya Chalinze. Wananchi wa Karagwe wanausubiri mradi mkubwa wa jinsi hii. Serikali ikiamua inaweza, kwani fedha siyo tatizo hata kidogo. Tatizo ni nia thabiti ya kuwapa maji wananchi wa Wilaya ya Karagwe. Mradi mkubwa wa kutatua tatizo hili kwa kukadiria unawenza kugharimu shilingi za kitanzania bilioni 20 hadi 50 tu. Kiwango hiki kimahesabu kinaonekana kuwa kikubwa lakini ukihesabu faida na manufaa yatakayopatikana kiasi hiki ni kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Ubungo Makoka Wilaya ya Kinondoni Mkoa wa Dar es Salaam linapita bomba kubwa la maji ya Ruvu juu. Pia upo mradi wa maji maarufu kama mradi wa Wachina. Eneo hili mara nyngi halipati maji ya kutosha pamoja na bomba kuu kupita maeneo haya. Ni vyema Serikali ikawaangalia wananchi wa maeneo haya. Sambamba na hili, watu wengi wamejenga karibu au juu ya bomba kuu la maji na wengine wanaendelea kujenga tu bila ya Serikali kuingilia kati. Nashauri Serikali ifanye ukaguzi wa kukomesha tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa maji wa Benki ya Dunia wa vijiji kumi Wilayani karagwe, wakati Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe inaandaa bajeti kwa ajili ya miradi ya maji ya vijiji vitatu.

Serikali iliagiza Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe kufanya makisio yao yasiyozidi bilioni mbili. Fedha hizi ilikuwa ni kwa ajili ya miundombinu tu bila kuhusisha shughuli nyngine. Tenda na *evaluation* vilishafanyika tayari na Jumatatu ijayo tenda zitafunguliwa na kuwa *awarded* lakini jambo la kusikitisha, Julai, 2011 Serikali imeleta agizo lingine na kusema kuwa bajeti iwe ndani ya "Ceiling" isiyozidi shilingi bilioni 1.1. Sasa katika mazingira haya: Je, miradi hii itatekelezeka? Naomba Serikali iliangularie jambo hili kwa umakini sana isije ikaleta kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya vifaa vya maji ni ghali sana kutokana na gharama za usafirishaji kutoka Dar es Salaam hadi Karagwe yapata Kilomita 1,500. Hivyo, nashauri kuwe na bajeti ya vifaa vya maji kwa Wilaya za pembezoni hasa za Mkoa wa Kagera ikiwemo Wilaya ya Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni hali ya jiografia ya Karagwe. Siyo rahisi kuchimba na kupata maji ya visima, hivyo wilaya ya Karagwe inahitaji maji ya kusukuma kwa mashine. Kwa kuwa Wilaya ya Karagwe inavyo vyanzo vya maji vingi ikiwemo na maziwa (*water bodies*) ni wazi kuwa Serikali inatakiwa itenye fedha za uhakika kwa ajili ya kusukuma maji kutoka Ziwa Kajunju na kwingineko ili yawafikie wananchi kwa matumizi yao, mifugo, mashamba na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji ya Kayanga na Omurushaka ndiyo miji mikubwa ya Wilaya ya Karagwe. Kila mji una wakazi zaidi ya 29,000. Mji wa Omurushaka watu wapatao 20,000, Mji wa Omurushaka hauna maji hata kidogo. Ni asilimia sifuri inayopata maji. Hii ni tangu miaka ya sabini mji huu hauna maji. Ombi langu kwa Mji wa Omurushaka ni kama ifuatavyo:-

- (1) Kukarabati kitekeo cha maji na kujenga ukuta wa kuzuia taka Sh. 45,000,000/=;
- (2) Kununua na kusimika mtambo wa kusukuma maji mnyanyuko wa Mita 360 umbali wa mita 3,300 Sh. 115,000, 000/=;
- (3) Kukarabati njia ya bomba kuu yenyeye urefu wa mita 3,300 Iliyojengwa tangu mwaka 1974 (*six inch diameter steel pipe*) Sh.196,000/=; na
- (4) Kukarabati tanki la ujazo wa lita 220,000 na kufunga uzio wa mzunguko Sh.45,000/=

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya mahitaji ni Sh. 1,302,000,000/=, lakini kwa kuanzia awamu kwa awamu angalau tuanze na namba 1, 2, 3, 4 kama nilivyoorodhesha juu. Baada ya hapo, mwaka kesho 2012 tutengewe Sh. 333,000,000/= kwa ajili ya kujenga njia ya mabomba ya usambazaji maji kwa eneo la Nyakahanga, Omurushaka, Bugene na Kishao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sipendi kujibiwa eti Serikali haina fedha. Zitafutwe fedha Sh. 1,302,000,000/= tu ili wananchi wa miji ya Omurushaka na Kayanga wapate maji. Ni haki yao. Mradi huu tangu usimame ni mwaka 1970. Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe haina uwezo hata kidogo kumudu mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusoma hotuba hii ya Maji. Aidha, nampongeza Naibu Waziri Lwenge kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, lakini vilevile kwa kazi nzuri, ngumu na kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Katibu Mkuu aliyeuwepo na aliyeopo na Wakurugenzi wote pamoja na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kipekee nawapongeza sana Bwana Washington Mutayoba ambaye ndiye *encyclopedia* ya raslimali za maji, mshkilieni sana hata kama amestaafu. Pili, Bwana Sailie amekuwa msaada mkubwa, pamoja na Bwana Daluti, bila kumsahau mdogo wangu Bwana Matemu mwenye uwezo na uzoefu wa sekta mbalimbali zaidi hii ya maji. Hayupo kwa makosa kwenye hiyo Idara, mpeni nguvu. Mama Kivyo, dDada Mrema wa Mipango na kwa umuhimu mkubwa Bwana Mkumwa. Misaada yake haielezeki kwa Wilaya ya Kilindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maji ni tatizo kubwa ndani ya Wilaya yetu. Awali tulikuwa na miradi mitano ya Benki ya Dunia, ni mmoja tu uliofanikiwa. Awamu ya pilii ile miradi iliongezewa na kuwa 15. Ushawishi na hamasa kubwa zilifanyika kuhakikisha wananchi wanachangia asilimia 20, jambo ambalo liliakamilika. Ghafla tukaambiwa kuwa fedha zimekuja. Cha kushangaza, badala ya miradi 15 ikawa miradi itakayopatiwa fedha kwa sasa ni mitano. Hivyo, pamoja na jitihada za wananchi hadi leo hakuna liliofanyika. Naomba Waziri aseme wananchi wa Kilindi wasikie, kwani mimi na Watendaji tunaonekana kuwa wababaishaji. Vilevile atamke wazi kuhusu fedha zilizokusanywa, tuwarudishie wananchi. Hili jibu ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia ya Wizara kuhakikisha Maji safi na salama kwa wananchi, Kilindi hakuna hata sehemu moja ambapo maji yanahakikiwa ubora wake, ukiacha pale Mjini Songea ambapo mara maji huwa na viwango na mara nyingine hayana. Nimeshuhudia maji yakiwa na viluwiluwi na uchafu wa aina mbalimbali. Magonjwa ya mlipuko yanazidi. Sasa sijui ni hatua gani au utaalamu gani unaotumika kusafisha maji kwenye visima au mabwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Kwamaligwa liliengwa mwaka 1954 na limekuwa likitoa huduma ya maji kwa vijiji zaidi ya kumi na mifugo 12,725 likiwa na samaki, migomba, miti ya matunda na vivuli mbalimbali. Bwawa hili liliunyika na kuleta hasara kubwa sana ikiwemo kilio kikubwa kwa hao watumiaji maji. Tathmini ilifanyika na wataalamu wa Wizara ya Maji, TAMISEMI, Mkoa na Halmashauri. Jumla ya gharama imekuwa Shilingi milioni 600. Naomba sana tupewe kipaumbele, kwani tunaweza kukamilisha na kuwahi mvua za vuli. Wananchi wa Kilindi hususan kijiji cha Kwamaligwa, Kibirashi, Lektingi, Kwediswati, Balanga, Jungu, Mgera watafurahia kusikia. Wananchi wa vijiji husika wamechangia Sh. 5,000,000/= na mfuko wa Jimbo Sh. 5,000,000/= jumla ni Shilingi milioni kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba *ni-declare interest* kuwa nimekuwa mjumbe wa Bodi ya Mto Pangani kwa miaka sita hadi sheria mpya ilipoanza. Hivi karibuni nashukuru kwa kuchaguliwa na ushirikiano mkubwa nilioupata kipindi chote ndani ya Bodi. Aidha, namshukuru Mzee Nnko - Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi, kwa uongozi wake imara na Wajumbe wote wa Bodi, pamoja na Watendaji mahiri K/bonde Hamza na Ofisi yake yote.

Naomba nikumbushe masuala muhimu. Mabonde ni muhimu sana, hivyo yawezeshwe kwa wakati ili yatekeleze majukumu yake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwango vya malipo ya *Water-right* yaangaliwe upya, yako chini sana. Walikuwa wanasubiri utafiti wa nchi nzima, lakini naomba nishauri kuwa, kwa vile Bonde la Pangani lipo tayari kwa zoezi hilo na wateja wenyewe wanaona viwango hivyo ni vidogo kwavile wamekwishahamasika, basi waruhusiwe kuanza viwango vipyta.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wilaya ya Kilindi inashughulikiwa na mabonde mawili. Bonde la mto Pangani ambalo liko *active* na tunawaona na nusu ya Wilaya ni bonde la Mto Wami ambao kimsingi hatujapata kabisa huduma zao. Kwa utekelezaji mzuri, niombe basi Wilaya yote iwe chini ya Bonde la Pangani. Hadi leo hakina hata *water-permit* moja pamoja na kwamba kuna mito inayotiririsha maji mfululizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naombe tupewe msukumo zaidi wa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya maji. Itasaidia kufanya miradi kuwa endelevu na yenye mafanikio. Tunaomba kwa vile tuko pembezoni, mtutupie jicho la huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Stephen Wasira kwa hotuba nzuri aliyoitoa juzi. Aidha, nampongeza Naibu Waziri wa Maji - Mheshimiwa Gerson Lwenge kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika Wizara na hivyo kuleta ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuikumbusha wizara kuhusu ombi maalum la Shilingi milioni 500 ambalo tuliliandikia barua na andiko tukiomba Wizara itusaidie fedha hizo kwa ajili ya kukamilisha mradi wa maji wa *North West Kilimanjaro* katika Wilaya ya Siha. Aidha, tuliomba Wizara ituondolee urasimu usio wa lazima ili tuweze kumalizia mradi huo kama ilivyopangwa. Mradi unategemewa kukamilika Aprili, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zilizofanyika za kuchimba visima vitano kila Halmashauri ziongezwe. Kazi ikamilike sehemu nyngi, visima vilichimbwa na maji yalipatikana, lakini tumeishia hapo, mwishowe vitaziba. Jitihada zifanyike visima hivi vikamilishwe haraka. Wananchi wanapata shida kubwa sana kutokana na ukosefu wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia visima hivi havitoshi. Pale Bukoba viliainishwa vijiji kumi ambavyo vingechimbiwa visima, lakini vimechimbwa katika vijiji vitano tu. Jitihada zifanyike hata hivi vitano navyo vipate visima. Tatizo la maji ni kubwa na ni vizuri Serikali ikalifanya kazi kwa uzito unaostahili.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa Sekta ya Maji ni uhai wa Wananchi na sehemu muhimu ya uchumi wa nchi, Wizara ya Maji haijapewa kipaumbele kwa kutengewa fedha zinazolingana na mahitaji; hivyo, siungi mkono hoja mpaka Serikali iongoze fedha za Bajeti ya Wizara husika. Aidha, siungi mkono hoja mpaka Serikali itoe maeleo na majibu ya kina kwenye masuala yaliyoibuliwa na Kambi rasmi ya Upinzani pamoja na mchango wangu wa maandishi kuhusu ufanisi wa Wizara na Taasisi zake. Sekta ya Maji iwe ni ya matumizi majumbani, viwandani kwenye uzalishaji au ya umwagiliaji katika kilimo; ni bomu la wakati kama Serikali isipolichukua kwa unyeti na uzito unaostahili. Hatari ya baadaye kwa Taifa letu ni migogoro inayotokana na uhaba wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maji (*Vol. IV*), fungu 49, kifungu 3001, kasma 3306, 3437, 3438, 3439 na 6275 ni kidogo; hivyo, kiwango cha fedha kiongezwe kulingana na Mpango wa Taifa wa miaka mitano, kipengele A.1.1.4 ukurasa wa 116 mpaka 118 kwa mwaka 2011/12. Mathalani, wakati mpango umeelekeza 2011/2012 Bwawa la Kidunda litengewe shilingi bilioni 26.8, bajeti hii inatenga shilingi bilioni 6.5 tu. Ruvu juu ilipaswa mwaka 2011/2012 itengewe shilingi bilioni 52.5 imetengewa shilingi bilioni 42 tu. Hivyo, Serikali irejee mchango wangu Bungeni nilioutoa mwezi Juni, 2011 kuhusu mpango wa miaka mitano na kufanya marekebisho yanayostahili wakati wa mapitio ya mpango wa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba ya Waziri, aya ya 24, ukurasa wa 19; hali ya utoaji wa huduma ya maji ya asilimia 55 kwa wastani wa saa tisa; haitoi picha halisi ya matatizo ya maji Dar es salaam na Jimbo la Ubongo. Ukitanya kwa saa 24, huduma ya maji ni chini ya asilimia 25.

Hivyo, pamoja na kusubiri Miradi Mikubwa ya Bwawa la Kidunda, Visima ya Kimbiji, Mpera na upanuzi wa Ruvu Juu na Chini ni lazima kama hatua ya dharura kupunguza upotevu wa maji katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12 toka asilimia 48 mpaka asilimia 30. Hivyo, ukaguzi maalum ufanyike toka Kibamba, Kwembe, Mbezi, Msigani, Saranga, Kimara, Ubungo, Makuburi, Sinza, Manzese, Makurumula na Mabibo, kudhibiti wizi wa maji na maji kutiririka ovyo. Hatua hii iende sambamba na kuharakisha ujenzi wa Mradi wa Visima Kumi Manispaa ya Kinondoni (Mradi wa Benki ya Dunia) na uzinduzi wa visima ambavyo vilikuwa vya ahadi ya Rais Kikwete - Mei, 2010; Mavurunza, Kilungule, King'ong'o na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya maji Mkoa wa Dar es Salaam na Jimbo la Ubungo hayawesi kushughulikiwa kwa haraka ikiwa udhaifu wa Kiuongozi, Menejimenti na Kiutendaji katika DAWASA na DAWASCO hayatashughulikiwa. DAWASA imeshindwa kusimamia ipasavyo Mkatuba wake na DAWASCO. Hii inadhihirika kutokana na maagizo ya EWURA ya mwaka 2009, ambayo hayajafanyiwa kazi kwa ukamilifu mpaka sasa 2011.

Aidha, mapendekezo ya CAG kuhusu DAWASA na DAWASCO ya 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010, nayo hayajashughulikiwa ipasavyo. Hivyo, Serikali irejee swali langu Bungeni la April 2011 na kufanya ukaguzi maalum wa kifedha, kiufanisi, wa DAWASA na DAWASCO pamoja na kufanya ukaguzi wa miundombinu ya mabomba. Wakati hatua hizo zikisubiriwa, Wizara kwa kutumia Mradi wa Maji Dar es Salaam pembezoni (BT na BTC) na Mradi wa Visima Kumi (Benki ya Dunia), ipeleke Miradi haraka maeneo ya Mpiji, Magohe, Makabe, Msakusi, Kibwegere, Hondogo, Galani, Bumla, Makola, Msigwa, Malambamawili na Goba, kama nilivyoeleza kwenye barua zangu za mwezi Machi na Juni, 2011. Aidha, uzinduzi wa visima vya DAWASCO Kilungule, Mavurunza na King'ong'o uharakishwe.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri na uwasilishaji mzuri wa Bajeti ya Mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu ya kushauri:-

Uvunaji wa maji ya mvua ni jambo muhimu sana. Kuna umuhimu wa dhati wa kutengeneza malambo na madimbwi madogo madogo (Ndiba), ambayo Wananchi watayatumia maji hayo kipindi cha kiangazi. Serikali isaidie juhudzi za Wananchi kwa kutoa vifaa kama saruji, nondo na kadhalika pamoja na utaalami.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaleta maombi yangu mara kwa mara kuhusu Miradi ifuatayo katika Jimbo la Lushoto:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Mji wa Lushoto umechukua muda mrefu na utekelezaji wake unasuasua sana. Naomba Wizara itembelee na kuhakiki utekelezaji wa Mradi huo. Matenki ambayo yamesemwa kwamba yamejengwa ni *Tank* moja tu ndilo liliojengwa. *Tank* kubwa ambalo lingepokea maji kutoka Kibohelo na kuyasambaza kwenda *Tank* la Kwembago na Kwesimo ni muhimu sana lijengwe haraka kuondoa uhaba wa maji Mjini Lushoto. Naiomba Serikali ilisukume swala hili kwa nguvu zaidi; Watendaji wanahitaji kusimamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipongeza juhudzi za Wananchi kubuni Mradi wa Maji ya Kata za Kwekanga, Kilole, Makole na Malibwi. Katika kujibu swali Bungeni, kipindi cha Mkutano wa Tatoo wa Bunge la Kumi, Serikali iliahidi kusaidia juhudzi za kukamilisha andiko la Mradi huo na kutafuta fedha za utekelezaji katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Naibu Spika, ramani zimepelekwa Tanga kwa ajili ya usanifu na michoro ya mwisho kwa ajili ya utekelezaji. Naomba Wizara ifuatilie na kuisukuma Halmshauri kuweka Mradi huo kwenye utekelezaji wa Miradi ya 2011/12. Naishukuru sana Wizara kwa usikivu wake na juhudzi zake katika kutekeleza Miradi ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Lushoto, Kijiji cha Lwandai kilichopo Kata ya Mlola, kilichaguliwa kupata Mradi wa Benki ya Dunia Vijiji Kumi kila Wilaya. Kwa bahati mbaya, utekelezaji wa Mradi huo umekuwa wa kusuasua sana. Wataalam wa kuchimba visima walikwenda Kijiji Lwandai kuchimba kisima mita 39 na wakaondoka Kijiji nayo bila taarifa na maji hayajapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Kijiji hicho na mimi mwakilishi wao, tuna wasiwasi sana wa utekelezaji wa Mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itoe kauli kwani Mhandisi wa Wilaya baada ya kuulizwa naye ameshindwa kutoa maelezo ya kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Wananchi watapewa maelezo ya kutosha ili wasipoteze imani kwa Serikali yao tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kero kubwa katika Wizara hasa Vijiji kunakuwa na Miradi ya Maji isiyokwisha. Tarafa ya Bungu, kuna chanzo cha Msitu wa Sakare, maji yamesambazwa kwa muda sasa lakini Mradi hauishi haieleweki kwa nini mpaka leo Wananchi hawana maji salama na lini Mradi huo utakamilika wananchi wapate maji.

Mji wa Mombo ni Mamlaka ya Mji Mdogo; ni lini maji yatakuwepo katika Mji Mdogo hasa Kijiji cha Jitengeni, Nduru na Mwisho wa Shamba hasa ukizingatia ni Mamlaka ya Mji Mdogo?

Je; ni lini Wananchi wa Mkomazi na Buiko watapata maji?

Naomba Serikali iviangalie Vijiji vya Kwashemshi na Vingo Kerenge, maji yallyopo ni machafu na yanapatikana kwa shida visimani. Vinahitajika visima virefu kwenye Jimbo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Maendeleo ya Wizara hii inategemea sana Wahisani. Uzoefu umeonesha kuwa, fedha hizi hazitoki. Toka nimeingia Bungeni mwaka 2005, nimekuwa nikiambiwa juu ya Vijiji Kumi lakini hakuna kijiji hata kimoja kilichopata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Mbanga una shida kubwa ya maji. Chanzo kizuri kipo na kina maji mengi (Ndengu), tatizo ni mabomba ya maji kutoka nayo Ndengu kwenda mjini. Majibu ninayopewa ni kwamba, mji huu upo chini ya ufadhilli wa Benki ya Dunia. Mpaka sasa hakuna kinachoendelea. Katika swali langu hapa Bungeni, Bunge la Tisa, aliyekuwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Chiza, aliahidi kutuma wataalam wake pale Mbanga Mjini, Kigonsera, Mkako, Litumba, Ndyosi, Kingole na Luhogara, lakini mpaka sasa hakuna maendeleo ya kuridhisha. Hivyo, ahadi hiyo haijatekelezwa mpaka sasa. Naomba majibu; ikiwa ni pamoja na mpaka lini yale maji yanayomwagika msituni pale Mbanga kwa Tizani yanashindwa kuja Mbanga Mjini kwa sababu hakuna fedha.

Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili maji hayo yaje mjini ili Wananchi wanywe? Hali ni mbaya na ni matumizi mabaya ya fedha, kuleta maji na kuyaacha porini yamwagike tu. Kama waandishi watapiga picha na kutoa kwenye vyombo vya habari, haitaleta tasnia nzuri kwa Serikali. Naomba fedha za haraka zipelekwe kumaliza kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya 2009/2010, Serikali illahidi kupeleka gari, pikipiki na *computer* kwa Mamlaka ya Maji Mbanga; mpaka sasa gari hilo halijapatikana mpaka. Gari hili

liko wapi? Kwa nini pia Miradi ya Maji Mbanga bado haijatangazwa; na ni lini Miradi hiyo itaanza kutekelezwa?

MHE. BENEDICT N. OLE NANGORO: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pole kwa Wizara, kwa kuuguliwa na Waziri wake, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandsosya. Ninamwombea na kumtakia apate nafuu mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, kwa kuandaa Hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara isukume mipango ya upatikanaji na usambazaji wa maji katika Mji wa Kibaya, mipango ilibaki kwa muda mrefu bila ya utekelezaji.

Miradi ya *World Bank* ya Visima Virefu itathminiwe na vijiji visivyo kuwa na maji wachimbiwe visima na kwa maeneo ambayo hakuna miundombinu ya usambazaji maji; basi visima mbadala vichimbwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti na usimamizi wa Miradi ya Maji uimarishwe ili *value for money* ionekane.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ifanye mawasiliano na Serikali Mpya ya Misri ili kuanza uchimbaji wa visima virefu uliokuwa ufanyike katika Wilaya mbalimbali ikiwemo Wilaya ya Kiteto

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni tatizo kubwa katika nchi yetu, ingawa ni kipaumbele cha kwanza cha Wananchi lakini kama Taifa hatujawekeza vya kutosha katika eneo hili, ndiyo maana maji bado ni kero kubwa.

Napenda kuishukuru Serikali kwa jitiahda inazofanya angalau kupunguza kero hii hususan katika Mji wa Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imesaidia katika hatua za awali za ujenzi wa *tank* la maji Mpanda Mjini na ujenzi umekwama kutokana na ukosefu wa fedha na dhamira ya kupunguza tatizo la maji kutokamilika. Naiomba Serikali ikamilishe Mradi huu ili Wananchi waweze kupata maji kwa urahisi zaidi, lakini pia ujenzi wa chujio katika chanzo cha Milala ili tupate maji safi na salama. Hivi sasa maji yanayotumika Mpanda Mjini yanatoka kwenye vyanzo moja kwa moja bila kusafishwa, bila kuchunjwa na bila kuweka dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa maji tunayotumia siyo salama, maradhi yatokanayo na maji yamekuwa yakijirudia mara kwa mara na kuigharimu Serikali pesa nyngi kwa tiba na madawa; hivyo, mahitaji ya visima virefu bado ni lazima kwa Mji wa Mpanda na vitongoji vyake vyote na tatizo hili lipo katika Kata zote za Jimbo langu. Tatizo ni kubwa zaidi katika Kata ya Kakese; vijiji vyote vitano havina maji. Aidha, nimekuwa kila mara naiarifu Serikali juu ya tatizo hili katika Kata za Misunkumilo, Ilembo, Shanwe, Kawajense, Nsemlwa, Mpanda Hoteli, Makanyagio na pia Kata ya Kashaulili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ikolongo, kwa takriban miaka mitano, nimekuwa nikiusemea, angalau sasa lipo tumaini la kuanza kwa Mradi huu. Naiomba Serikali iwekeze katika Mradi huu muhimu kwa ustawi wa Mji wa Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Mamlaka ya Maji ya Mji wa Mpanda haina uwezo wa kufikisha maji kwa walaji na wahitajio wa huduma hii, kwa kujenga mtandao wa mabomba kutokana na kasi ya kupanuka kwa Mji wa Mpanda; ni vyema na busara kusaidia mamlaka hii kusambaza njia za maji ili Mamlaka iweze kuongeza wateja na kuongeza mapato kwa Mamlaka ili iweze kujidesha kwa ufanisi. Naomba sana Wizara itusaidie katika azma hii njema na kuwapunguzia shida ya maji Wananchi na kuondosha kero hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuunga mkono hoja, naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nimpongeze Waziri wa Maliasili, kwa jitihada zake za kuweza kutembelea maporomoko ya Mto Kalambo yaliyoko Jimbo na Wilaya Mpya ya Kalambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, maporomoko hayo ambayo ni ya pili kwa ukubwa baada ya yale ya Victoria; pamoja na kuwa ni chanzo cha uhakika cha kufua umeme kama Serikali ikiwekeza lakini pia ni chanzo cha uhakika cha maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelazimika kuanza na chanzo hiki cha uhakika nikiwa na lengo la kuishauri Serikali ione ni jinsi gani Wizara hizi tatu zinavyoweza kufanya kazi kwa kushirikiana na hivyo kupunguza baadhi ya gharama na huku zikisaidia taifa na kufikisha huduma kwa Wananchi wa vijiji vingi vilivyo Mwambao wa Ziwa Tanganyika, lakini vikiwa na shida kubwa ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo hiki cha maji ni kivutio cha utalii na chanzo cha uhakika cha nishati ya umeme, kimetelelezwa kabisa huku upande wa pili jirani, yaani Zambia, wakitumia kama kivutio vya utalii japo kivutio hiki kinaonekana vizuri zaidi kwa upande wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya Halmashauri zilizo na hali mbaya kabisa katika jukumu kupelekea huduma ya maji basi ni pamoja na Halmashauri ya Sumbawanga. Hali hii imejidhihirisha katika hotuba iliyowasilishwa na Wizara, kwani hakuna uwiano hata kidogo kati ya Halmashauri nyininge ukilingalisha na Halmashauri ya Sumbawanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara ijihusishe kwa kikamilifu katika kulinda vyanzo vya maji badala ya kuziachia Halmashauri na Wizara nyininge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji inaonekana kama vile ime-relax kwa kupitia Miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, licha ya Miradi hii kuchukua muda mrefu bila ya kuleta matunda yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara ifanye juhudzi za makusudi kujiridhisha juu ya Halmashauri ambazo hazijapanga vizuri kwani baadhi ya sababu zipo nje ya uwezo wa Halmashauri kama vile ukosefu wa Mhandisi, hali inayoikabili Halmashauri ya Sumbawanga.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia Bajeti ya Wizara ya Maji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Misungwi ndipo kilipo chanzo cha maji yaendayo Shinyanga na Kahama. Vilevile mwaka huu kuna mpango wa kupeleka maji Nzega na Tabora. Inasikitisha kusema kwamba, Wilaya ya Misungwi idadi ya watu wanaopata maji safi ni asilimia 37 tu. Chakusikitisha zaidi, tangu mwaka 2008, Mheshimiwa Rais aliahidi kukipatia maji Kijiji cha Nyanhomango (Ihelele), mahali zilipo mashine za kusukuma maji kwenye Mradi huu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hali hii, pamoja na Mradi wa Nyahiti unaopeleka maji katika Mji wa Misungwi, naomba Wizara ilitazame suala la maji katika Wilaya ya Misungwi kwa umakini zaidi lisigeuke kuwa la kisiasa kwa kuwachochera Wananchi kukichukia Chama Tawala au kuhujumu Mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewasilisha mapendekezo yangu kwa Naibu Waziri wa Maji, nikieleza namna ambavyo tunaweza kutatua matatizo ya maji katika vijiji vilivyo karibu na maeneo yanayopitia bomba la maji liendalo Shinyanga na Kahama katika Wilaya ya Misungwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendeleko hayo ni pamoja na kuvipatia maji Vijiji vya Mbarika, Nyamhomango, Isesa, Mbalama, Nyamayinza, Seke, Buhingo, Misasi, Busongo, Mwagiligili, Buhunda, Gukwa, Mwagimagi, Mahando, Ikungumhulu, Mwamboku, Mwamazengo, Mwamagili na Kifune. Kwa kufanya hivi, tutakuwa tumewatendea haki Wananchi wa Misungwi ambaeo leo hii wanachunga ng'ombe lakini maziwa na nyama wanafaidi watu wengine, japokuwa hata kijiji kimoja hakijatajwa kwenye Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuishukuru Serikali, kwa mambo yafuatayo katika Jimbo la Mvomero:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Miradi ya Maji katika Miji ya Mvomero na Turiani umeanza na kwa ahadi ya Serikali Mradi huu utakamilika Juni, 2012. Ombi langu ni kuomba ujenzi wa Miradi hii miwili uendelee kwa kasi zaidi na ikamilike kama iliyopangwa. Aidha, miundombinu ya kusambaza maji ya vijiji vyote jirani ifanywe kwa haraka mara ujenzi wa Mradi ukikamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanza kwa utekelezaji wa Mradi wa Vijiji Kumi katika Halmashauri chini ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini; hadi kufikia tarehe 15 Agosti, 2011, kazi ya uchimbaji wa visima katika Vijiji Kumi ilishaanza. Naishukuru Serikali na Benki ya Dunia. Naomba kujua jina la Mkandarasi aliyepewa kazi Kijiji cha Kipera, Bumu na Mlumbilo. Kazi imefanyika Salawe (Kibati), vijiji vingine sijaona kazi hii. Naomba Waziri itoe taarifa ya wakandarasi waliopewa kazi katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi 689,089,000 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira 2011/2012. Naishukuru Serikali kwa kutenga fedha hizi kwa ajili ya miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchimbiwa visima katika Vijiji vya Misengele, Maharaka, Difinga, Msolokelo, Homboza, Pemba Masimba, Ndole, Kinda, Luale, Langali, Maguruwe, Bunduki, Nyandika, Ngungulu, Masarawe, Tchenzema, Makuyu, Mziha, Bwege, Dihinda, Kanga, Mafuru, Tangeni, Vikonge, Kata ya Melela, Shule za Sekondari 21 za Kata Jimbo la Mvomero. Maeneo nilyoyataja yanakabiliwa na tatizo la maji; naomba Wizara iangalie katika bajeti ijayo, ipange fedha kusaidia vijiji niliyovitaja. Aidha, maeneo ya wafugaji Masimba, Kambala, Wami Sokoni na Kibaoni (Melela), yapewe vipaumbele vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya za kuendeleza Sekta hii muhimu. Pamoja na pongezi hizo, nina changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya kwanza ni namna Mradi wa Vijiji Kumi unavyokwenda taratibu wakati Wananchi kwenye vijiji hivyo wakiwa tayari wamechangia. Nashauri badala ya Mradi huu kuendelea kutegemea ufadhilli toka Benki ya Dunia; ni vizuri Serikali ikawekeza kwa kiasi kikubwa Mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuiomba Serikali izingatie umuhimu wa kukamilisha miundombinu ya kuleta maji katika Mji wa Sikonge, kwa kuwa usanifu umekwishakamilika. Naomba Serikali ikamilishe Mradi huo kutoka kwenye bwawa lilokwisha chimbwa na sasa lina maji ya kutosha la Ulyanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mradi huu wa kutoa Maji Ulyanyama kuyaleta Sikonge Mjini utakuwa ukiendelea, napendekeza miundombinu iliyopo kwa sasa Sikonge Mjini, ambayo ni chakavu, itengewe fedha ili iweze kusaidia kutoa maji kuwasaidia kwa muda Wananchi wa Mji wa Sikonge, ambaeo kwa sasa wana dhiki kubwa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ushauri huo, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi una matatizo makubwa ya maji. Pamoja na jitihada za Serikali za kuanzisha Miradi ya Maji (*Quick Wins*), CTZ, World Bank, TASAF na Mbwiji, lakini hali bado ni tete, Mji wa Nachingwea ni jangwa unahitaji Mradi Mkubwa Mbwiji umeanza; lakini umechukua muda mrefu hadi leo bado umechukua. Nachingwea bado kuna tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lindi Mjini imezungukwa na bahari, inahitaji pia Mradi Mkubwa, Mradi uliopo wa World Bank unasuasua bado haujakwisha. Mashine zilizopo za maji ziliikuwa kwa ajili ya mashamba ya mkonge ya mkoloni, sasa watu wamezidi kuwa wengi maji hayo hayatoshi. Mtu anauza ndoo shilingi 1,000; ni mtu binafsi anayaiza pale mjini anachukua Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka msaada wa haraka Lindi Mjini na Nachingwea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikutano ya Wizara ya Maji kila mwaka ni mingi mno; ni gharama na inapoteza muda, waipunguze.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. CLARA D. MWAITUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuzungumzia juu ya suala la maji. Mara nydingi Serikali hutoa taarifa za kuwatumanishaa Wananchi juu ya upatikanaji wa maji. Matokeo yake ni kwamba, mafanikio yake huwa hayakamiliki ipasavyo. Mafundi wa kupima ramani huwa wanapita wakiweka alama za kuitisha mitaro ya maji/mabomba. Alama hizo huwekwa hata kwenye miti, lakini ni miaka nenda rudi hakuna matokeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wa visima hawa huweza kuchangisha michango (vijiji), lakini wao hufika na kuweka alama za kuchimba visima hivyo na pengine hata kujaribu kuchimba. Hata hivyo, sehemu nydingi huelewa ya kuwa maji yaliyopo katika sehemu hizo hayafai kwa matumizi ya wanadamu. Kutokana na hali hiyo, wanawenza kudai ya kuwa watarudi baadaye. Matokeo huwa hawarudi mapema na kupelekeea fedha zinazochangwa na Wananchi kupotea bila mafaniko yaliyokusudiwa kufikiwa. Mahali pengine visima huchimbwa mbali na wanakijji, wakidai watasambaza mabomba ili yapatikane kwa urahisi kijijini, lakini utaratibu huo haukamiliki. Kwa hali hii napenda kuishauri Serikali ya kuwa ikiamua kuanzisha Mradi fulani ni bora ufuatiliwe ili kufikia malengo yanayokusudiwa.

MHE. KASSIM M. MAJALIWA: Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ruangwa kwa sasa imekabilisha na tatizo kubwa la maji, ambapo vijiji vyetu havijafikiwa na huduma hii. Visima vidogo haijasambazwa au havijachimbwa kwenye maeneo mengi na hivyo Wananchi bado wanahangaika. Wilaya ilikuwa na Mradi wa Visima Virefu chini ya Mpango wa World Bank, lakini hadi leo hakuna utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtandao wa mabomba wa Mnacho, Mbekenyera na Mandawa, unahitaji ukarabati mpya ili kumudu kutoa huduma ya maji kwa vijiji vingi. Maeneo yote mitandao hiyo imeharibika, inahitaji kukarabatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Wilaya ya Nachingwea unapitisha mabomba kwenye Vijiji vya Wilaya ya Ruangwa, ambavyo vina hali mbaya sana ya maji. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka mabomba kwenye vijiji hivyo ili Wananchi wapate maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AGNESS E. HOKORORO: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpa pole nydingi Waziri wa Maji, Mheshimiwa Profesa Mwандосыа, Mwenyezi Mungu, ampe nafuu ya haraka. Aidha, nampongeza sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Lwenge, kwa kazi nzuri katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu na kukubali kuwa, maji ni uhai na kama hivyo ndivyo, yanatakiwa yapewe kipaumbele kwa kuhakikisha kuwa, huduma hiyo inawafikia Wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa maji Mkoani Mtwara ni tatizo sugu ambalo dawa yake hakuna matumaini ya kutatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna na hali yoyote ile, kwa bajeti iliyopo na kwa ukubwa wa tatizo la maji, haitoshi na haikidhi haja ya kuliondoa tatizo hilo nchi nzima kwa kuwa mikoa mingi haina maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Wataalam wa Maji hawavitambui vyanzo vya maji badala yake wamekuwa wanachimba visima kwenye maeneo yasiyo na maji? Visima vinachimbwa na maji hayapatikani kabisa. Hapa inashangaza sana, unakuta katika Halmashauri za Wilaya wanunu mitambo ya kuchimbia visima wakati katika maeneo hayo hakuna maji! Huo ni upotezaji wa rasilimali au matumizi mabaya ya rasilimali. Kama Wataalam wa Maji wapo na Serikali imewasomesha, inakuwaje hawana uwezo wa kutambua vyanzo vya maji vya asili?

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni Wilaya ya Masasi; katika maeneo ya Miyesi na Chiwambo, yana maji ya kutosha; kwa nini Serikali isivii marishe? Tangu mwaka 1955 katika maeneo hayo kuna maji, lakini Serikali haijawahi kuwa *serious* kuona namna gani vyanzo hivyo vinaweza kutumika kuwapatia maji Wananchi wake wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Makonde; inasikitisha na inashangaza, kwa miongo kadhaa sasa Newala inatambulika kana kwamba ni eneo kame kuliko yote Tanzania, kwa sababu tangu miaka ya 1970, 1980 na 1990 hadi sasa Wananchi wa Newala, Tandahimba, hawana maji. Wanawake wanazimika kutegesha maji ya mvua ya chini na kuyahifadhi kwenye visima; kwa kipindi chote hicho wanawake wanatabika kumbe tatizo si upungufu wa maji. Maji yapo, chanzo cha Maji cha Makonde kina uwezo mkubwa wa kuwapatia maji Wanawala, Tandahimba, tatizo ni bomba/chujio la kutolea maji kutoka chanzo hicho. Ninashindwa kuelewa; hivi hawa wataalam wa maji hawakuweza kuliona tatizo hilo?

Mara nyingi inaripotiwa uchakavu wa miundombinu, suala la ongezeko la watu na kuongezeka kwa matumizi ya maji lipo dhahiri na wazi; inasikitisha Wizara ya Maji imeacha Wananchi wanapata shida kwa kipindi kirefu sana mpaka sasa ndiyo inasema tatizo hilo litatatuliwa kwa kuongezwa uwezo wa kusambaza maji na kuongeza tanki la kuhifadhia maji. Serikali ili kuwa inasubiri nini kwa miaka yote hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upotevu wa maji njiani katika maeneo mengi ambayo yanapatikana bado maji hayo yanavuja ovyo ovyo, unaweza ukakuta visima bubu (mashimo yaliyoja maji yaliyovuja), ambayo yasingevuja njiani yangewafikia watumiaji ambao wanayakosa. Kama ilivyo umeme na maji mengi yanapotea hivyo hivyo. Tatizo kubwa ni uchakavu wa miundombunu, lakini pia kutokana na wataalam kutojali kazi zao au mafundi kutowajibika ama kutokuwa na uchungu na maji yanayopotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara mbali ya kutafuta vyanzo vingine, wangeimarisha vilivyopo na kuzuia maji kupotea bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Maji inatarajiwa kupunguza umaskini wa Watanzania lakini kwa sasa inaongeza zaidi umaskini kwa kuwa wanawake ambao ni wengi, asilimia 53 ya Watanzania hawashiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Serikali haioni kwamba inachangia kurudisha nyuma kipato cha Wanawake wa Mtwara ambao kwa miaka mingi wanatumia muda mwingi kutafuta maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. UMMY A. MWALIMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja na kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara, kwa juhudini kubwa wanazofanya katika kuhakikisha upatikanaji wa maji mjini na vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji yana uhusiano wa karibu sana na uboreshaji wa maisha ya Watanzania wote. Upatikanaji wa maji (safi na salama) ni muhimu katika kupigana/kupambana na umaskini na matatizo ya afya. Faida za uchumi zinaweza kupatikana siyo kwa njia moja tu, bali kwa kuwa na afya bora na kuokoa muda unaotumika kuhangaika na kazi za kuchosha za kubeba maji kwa umbali mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wengi wa kike wanapoteza muda mwingu kutafuta maji badala ya kuwa madarasani. Upatikanji wa maji utachochea kufikia kwa malengo ya usawa wa kijinsia kati ya watoto wa kike na watoto wa kiume katika elimu ya msingi, sekondari na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanawake wengi ndiyo wana jukumu la kutafuta maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na matumizi ya afya. Hivyo, badala ya kupoteza muda kutafuta maji, upatikanaji wa maji hasa vijijini, utatoa nafasi kwa Wanawake kushiriki katika shughuli za maendeleo na malezi bora ya watoto na hivyo kuiwezesha Tanzania kufikia Malengo ya Milenia Namba Nne na Namba Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu Wizara ikaweka mikakati endelevu ya kuhakikisha upatikanaji wa maji vijijini na mijini ili kuboresha maisha ya Wananchi hasa Wanawake na Wasichana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Wilaya za Muheza, Handeni, Korogwe na Lushoto, wamekuwa wakikumbana na kero kubwa sana ya kukosekana kwa maji. Mfano, katika Wilaya ya Muheza, upatikanaji wa maji wakati wa kiangazi ni asilimia 30 tu ya Wananchi wanaopata maji. Natambua kuwa, Serikali inalijua tatizo hili na hivyo imeandaa mipango ya muda mfupi na muda mrefu ya kutatua kero ya maji; ni muhimu sasa mipango hii kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutanguliza shukrani kwa nafasi hii. Pia naomba nitoe pole nyingi kwa Mheshimiwa Profesa Mwandoza, kwa maradhi yanayomsumbuwa. Namwombea uponyaji wa haraka kwa Mungu wetu ili aje tuungane katika shughuli za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Hotuba hii iliyotolewa hapa Bungeni na pia nampongeza Naibu Waziri, ambaye amekuwa akiisimamia Wizara hii, Katibu Mkuu na Watendaji wote. Ukweli ni kwamba, bado Wizara hii haijapewa kipaumbele kwani hata bajeti yake tu inaonesha ni ndogo, haiwezi kutatua matatizo makubwa ya uhaba wa maji Nchini Tanzania. Inaonesha Serikali bado inategemea bajeti za kutoka nje (msaada). Mimi nashauri Serikali iache kutegemea msaada toka kwa wafadhili, ipange utaratibu wa kutatua tatizo la maji yenye kama suala la dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze pia kutoa shukrani kwa mfanyabiashara maarufu, Mr. Sabodo, ambaye kuptitia Wizara hii tulipata barua za kututaka Wabunge tuombe visima kwake naye atasaidia. Nampongeza kwa moyo wake wa kujitolea na Mungu ambariki. Napenda kujua Wizara inashirkiana naye vipi katika kutimiza azma yake kwenye maeneo husika? Je, Wizara inajua ni Wabunge wangapi wameomba visima kwake? Je, Wabunge wangapi wameshapata msaada na ni kwenye maeneo yepi? Tafadhalii, naomba nipatiwe majibu na Watanzania wajue.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwa Programu ya Maji katika Mkoa wa Singida. Ninaomba nitoe ushauri kwamba, Programu hii iendane na mipango ya matumizi bora ya ardhi, ikiwa ni pamoja na mijii/makazi; kwa mfano, kama Programu inatekelezwa kwa kuzingatia wafugaji na wafugaji wengine wanapokuja kuonekana eti wanakaa eneo ambalo

hawapaswi kukaa wakahamishwa, tayari miundombinu itakayokuwa imewekwa kwa wafugaji hao lazima itatelekezwa. Hivyo, kutokuwepo kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi na hata mipango ya makazi, kumesababisha Wananchi kuishi vijiji kwa kusambaa sana kufuatana na ukubwa wa eneo/mashamba yao; hivyo miradi ya maji inayobuniwa inakuwa ni mikubwa sana kwa sababu ya kuwafuata Wananchi waliosambaa; na gharama inakuwa kubwa sana na baadhi ya Miradi hukataliwa kupatiwa fedha. Kwenye Mkoa wetu wa Singida, ilitarajiwa kuwa Programu ingefaidisha vijiji 53 katika Halmashauri tatu za Iramba, Manyoni na Singida, kwa sababu ya ukubwa wa Mradi. Kwa sasa ni jumla ya vijiji 11 vitakavyonufaika katika Halmashauri zote tatu. Wananchi katika vijiji 22 pamoja na hamasa na matumaini yao makubwa, wanaambiwa wasubiri awamu nyingine, haijulikani hadi lini; jamani inauma sana, mimi natembelea Mkoa wote ule kama Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wote ni maeneo yangu ya kazi, naona hata aibu, hasa wanawake wenzangu wanavyoumia, wakiniona wanapata tumaini. Jamani nakosa majibu kwao, wengi wamebakia katika harakati za kutafuta maji, watoto wa kike nao tabu tupu. Jamani tunaomba Serikali timizeni wajibu wenu wa kutatua tatizo hili la maji. Shule za Kata zenyen hosteli nazo ni balaa, wanatumia muda mwingi kutafuta maji badala ya kujisomea. *Please!*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokuwepo kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi, kunasababisha miundombinu ya maji ipitishwe kwenye maeneo ya miundombinu mingine au makazi ya watu na kuzua suala la fidia kubwa kwa wale watakaoathiriwa na miundombinu hiyo ya maji. Kwa mfano, Mradi wa Mwankoku Singida, umepita kwenye mashamba ya watu. Natambua kuwa jukumu la kuwa na mipango ya makazi na matumizi bora ya ardhi ni la Halmashauri, lakini Wizara ya Maji inapaswa kuweka utaratibu huu na maelekezo yenye msisitizo mapema ili utekelezaji wa Programu utanguliwe na mpango wa makazi na matumizi ya ardhi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu iliyotolewa katika vijiji kuwa na Kamati na Mifuko ya Maji kwa ajili ya uchangiaji, bado uelewa ni mdogo, wengi hudhani huduma hiyo ni ya bure; hivyo, Serikali itoe tamko na msisitizo kupitia Wizara hii ili kunusuru Miradi ambayo ipo tayari isishindwe kuendeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maji inayojengwa vijiji inahitaji uangalizi wa kitaalam hasa ile yenye injini na pia spea. Halmashauri zetu hazina mafundi wala spea za kuwezesha matengenezo ya Miradi hii. Je, Serikali itakuwa imejitayarisha vipi kutatua tatizo hili? Mimi nashauri kuwe na mpango wa kutoa mafunzo kwa mafundi na kutoa ajira ili kutatua tatizo hili. Kama hakuna mpango huo, Serikali ijue tutatekeleza programu na kutumia fedha nyngi kwa Miradi itakayokufa mapema; ni sawa na kuondoa ngoma juani, kwani Miradi ikikamilika baada ya kuharibika haitengenezeki!

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kuwezesha utekelezaji wa Miradi Mikubwa ya Maji katika Wilaya za Singida, Manyoni na Kiomboi Mjini katika miji ya Kiomboi na Manyoni. Wananchi pamoja na upungufu mdogo mdogo katika Miradi yao, angalau wanasherehekea, maana awamu za awali za Miradi hiyo zimekamilishwa. Mradi wa Maji Singida Mjini umekwama kutohana na kukosekana na fedha za kulipa fidia kwa wanaotarajiwa kuathiriwa na miundombinu ya maji ya Mradi huo. Katika udadisi wangu, nimearifiwa kuwa, zinahitajika kama shilingi 90,000,000.00 kwa ajili ya kulipa fidia. Hivi kwa Mardi wa US\$ 18,000,000.00, TSh. 90,000,000.00 ni kitu gani? Ukiachia Mamlaka ya SUWASA haitaweza, haina uwezo wa kulipa, kwani haina maji ya kuuza ili kuweza kulipa fedha hizo. Hivyo, naiomba Serikali iikopeshe SUWASA ama ilipe kabisa ili tuweze kuondokana na adha ya msururu wa ndoo za maji Mjini Singida. Hii ni aibu na adha kweli kwa waliowezesha US\$ 18,000, 000.00 kuelekeza SUWASA kukopa benki ni kuendelea kuchelewesha Mradi. Miaka michache iliyopita fidia kama hii kwa walioathiriwa na miundombinu ya maji hata hapa Dodoma ililipwa kutohana na Bajeti ya Serikali. Mbona kuna ubaguzi au tulichelewesha kwa makusudi ili tunyanyasike? Tafadhali sana, naomba hili nipatiwe jibu, nisingependa nisimame kwenye vifungu na kuanza kutoa shilingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kutoa shukrani zangu kwa Serikali, kwa kutuwezesha kutekeleza Mradi Mkubwa wa Maji Mjini Singida, ila nasikitika kuwa pale utakapokamilishwa na uzalishaji wa maji taka ukaongezeka, basi itabidi tuukimbie mji! Manispaa ya Singida inalo gari moja tu la maji taka ambalo kila mhitaji wake inabidi angojee juma moja au

zaidi kulipata gari ili kuondoa maji taka katika nyumba yake. Sasa uzalishaji wa maji taka ukiongezeki sijui itakuwaje kwani maji taka yataongezeka kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naipongeza Wizara ya Maji, kwa kazi kubwa inayofanya ya kusambaza huduma ya maji safi na salama katika maeneo yetu ya vijiji ni mijini, yenye idadi kubwa ya wakazi. Nampongeza vilevile Waziri wa Maji, Mheshimiwa Profesa Mark James Mandosya na Naibu wake, Mheshimiwa Eng. Gerson Hosea Lwenge, kwa kuandaa taarifa nzuri (iliyokwenda shule) ya Mpango wa Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika sana kwa taarifa ya kuanza kwa utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Bonde la Mto Songwe. Utekelezaji wa Mradi huu ni ukombozi kwa Wananchi wa Wilaya ya Kyela, ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakiathirika na tatizo la kuhamahama kwa Mto Songwe wakati wa mafuriko na hivyo mazao, mifugo na makazi ya Wananchi husombwa na maji. Programu hii itaidhibiti hali hiyo kwa kudhibiti kingo za Mto Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika vilevile kwa uamuzi wa Serikali za Malawi na Tanzania, kuuteua Mji wa Kyela kuwa Makao Makuu ya Programu hiyo. Tayari ofisi ya muda imepatikana Mjini Kyela. Ombi langu kwa Wizara ni kuwa, kwa kuwa Wizara inaanza ujenzi wa Ofisi ya Kudumu ya Programu katika mwaka mpya wa fedha, hakuna sababu hata kidogo ya kuibana bana Ofisi ya Programu hiyo ya Kimataifa Mjini Kyela wakati tunayo maeneo mengi mazuri sehemu za Kasumulu au Katumba Songwe (mpakani na Malawi), ambayo yangeweza kujengwa Makao Makuu hayo. Naihakikishia Wizara ushirikiano wangu na Uongozi mzima wa Wilaya ya Kyela kuitafutia Programu hii sehemu nzuri na mwafaka nje ya Mji wa Kyela.

Narudia tena kutamka kuwa, naunga mkono hoja.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia hoja hii kwa kuanzia na Sekta ya Maji. Naishukuru sana Serikali kwa kuanzisha Mradi Mkubwa wa Maji katika Mji ya Kibiti, Ikwiriri na Utete. Mradi wa Maji Utete umekamilika lakini Mradi wa Maji wa Mji ya Kibiti na Ikwiriri kama ilivyoinishwa katika ukurasa wa 76 wa Kitabu cha Hotuba ya Waziri imefikia asilimia 96. Nakubaliana na kauli ya Waziri hasa katika uchimbaji wa visima, ujengaji wa tangi kubwa la maji, kuweka mtandao wa maji na ujenzi wa ofisi pamoja na nyumba za watumishi umekamilika. Kazi inayoendelea kwa sasa ni uwekaji wa nguzo za umeme kuelekea kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi kubwa iliyofanyika, bado kuna kazi nyingine ya kutandaza mabomba kuelekea kwenye viosk na nyumba za Wananchi haijafanyika. Naomba Serikali iharakishe kukamilisha kazi hii kwani Wananchi wa Mji huu wanasubiri kwa hamu kukamilishwa kwa Mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri pia Serikali iuendeleze Mradi huu hadi kwenye Kijiji cha Mwangia, ambacho kipo kilomita mbili tu toka Kibiti. Kijiji hiki kina matatizo makubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mradi kukaribia kukamilika, tayari Mkandarasi ameanza kukabidhi kazi hiyo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji. Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, inatarajia kuunda Bodi ya Maji ya Mji Mdogo wa Kibiti. Kwa kuwa Mji wa Kibiti wenye sifa za kutosha kuwa Mji Mdogo bado haujatangazwa kuwa Mji Mdogo, naiomba Serikali itangaze rasmi kuwa Kibiti ni Mji Mdogo ili Bodi itakayoundwa iwe ni halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Miradi ya Benki ya Dunia ya Kuvipatia Maji Safi na Salama Vijiji Kumi kila mwaka katika Wilaya zote hapa nchini, Mradi huu unasuasua sana. Kuna sababu nyingi ambazo Wananchi wanakosa imani na Serikali yao kwa kutokeleza ahadi mbalimbali ilizoziahidi. Ahadi hii ilikuwa ikamilike na vijiji vingine viweze kutajwa ili Mradi uanz.

Hadi sasa visima vimechimbwa kwenye vijiji kumi vya Wilaya ya Rufiji, lakini katika Kijiji cha Mkenda maji hayakupatikana kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na visima kuchimbwa ni vijiji vitatu tu ambavyo mwaka huu vitapata pesa za kuweka mtandao wa maji. Vijiji hivyo ni Upondoa, Ngorongo na Kiwanga, vijiji saba vilivyobaki vitapata pesa kwenye bajeti ijayo; hii ni hatari. Naishauri Serikali kuwa kwa sasa ni vizuri kutenga fedha za kutosha kutohana na mapato yetu ya ndani kama tulivyofanya kwenye Mradi wa Maji toka Ziwa Victoria hadi Shinyanga. Hawa Wafadhili watatuangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Vijiji vya Delta ya Mto Rufiji, vingi kama siyo vyote, vina matatizo makubwa sana ya maji hasa wakati wa kiangazi. Naishauri Serikali kuwa ifanye kila linalowezekana ili kuhalikisha Wananchi hawa nao wanapata maji safi na salama na kwa umbali ulio karibu, kwa sababu Wananchi hawa wanapata maji baada ya kutembea kwa mitumbwi kwa zaidi ya saa sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji imeanza jitihada ya kuwapatia maji Wananchi hawa wa Delta kwa kujenga malambo ya kuhifadhi maji ya mvua. Kazi hii ni kubwa na hadi sasa wamefanikiwa kujenga lambo moja tu katika Kijiji cha Pombwe, Kata ya Kiongoroni. Ujenzi wa Lambo hili ni zaidi ya shilingi 100,000,000; fedha hizi ni nyingi kiasi cha Wilaya kushindwa kutekeleza katika vijiji vyote 20 vilivyo katika eneo la Delta.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, natanguliza shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya na kuweza kushika kalamu na kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa taarifa ya njaa kali sana Jimboni kwangu. Chakula cha msaada cha bure bado hakijafika na hasa cha bei ya shilingi 50 kwa kilo hakijafika. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura kuflikisha chakula hicho kwa haraka ili kuokoa uhai wa Wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Jimbo la Nyang'hwale limekumbwa na ukame mkubwa wa maji hasa kwenye Kata za Khalumwa, Izunya, Bukwimba, Busolwa, Nyijundu, Kakora, Kafita, Nyugwa, Nyashilanga, Shabaka, Nyang'hwale na Nyaburanda. Maji imekuwa tishio na kusababisha mimba na kuvunjika ndoa nyingi sana na ugomvi kwa akina mama visimani. Wanafunzi wa bweni wanachukua muda mrefu sana kufuutilia maji umbali mrefu na kupitwa na vipindi vya masomo. Naiomba Serikali iliangularie hili ikiwa ni pamoja na afya za watumiaji wa maji ambayo siyo safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo nayo inayohitaji maji salama, kwani inapata tabu sana kwa kukosekana kwa maji ya kunywa na kuogeshwa kwenye majosho. Ili mifugo iwe na afya nzuri ni lazima ipate maji ya kunywa na kuogeshwa ili iwe na siha nzuri. Naiomba Serikali iboreshe mabwawa yaliyopo katika Kata za Shabaka, Nyang'hwale, Nyijundu, Kakora, Nyugwa, Khalumwa, Bukwimba na Busolwa na kuchimba malambo mengine katika maeneo ya Kata za Nyashilanga, Nyabulanda na Kafita.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai kwa binadamu na mifugo; naiomba Serikali ituangularie kwa huruma Wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale, tuna shida kubwa sana ya maji, njaa na ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MADEYE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Prof. Mark Mwandoza (Mb), Waziri, kwa kazi nzuri aliyoifanya toka akabidhiwe Uongozi wa Wizara hii muhimu. Namwomba Mwenyezi, ambariki ili apone haraka na kurejea kuendelea kuiongoza Sekta hii. Nampongeza pia Mheshimiwa Eng. Gerson Lwenge (Mb), Naibu Waziri, kwa juhudhi anazofanya hivi sasa kusimamia

Sekta wakati Mheshimiwa Waziri akiendelea na matibabu. Nampongeza pia Ndugu Sayi, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri wanayofanya kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria zinazoongoza Sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarehe 17 Septemba, 2010, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipofanya mukutano wa hadhara eneo la Emasi Arusha, alipokea kilio cha Wananchi wa Hamashauri hiyo kuwa tokea Uhuru wa nchi yetu bado Serikali hajatafuta ufumbuzi wa kero ya maji inayowakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais aliagiza kuwa, Uongozi wa Wilaya na Mkoa, utayariske *Master Plan* ya Maji ya Wilaya haraka iwezekanavyo na kuwasilisha Serikalini ili Serikali itenye fedha za kutekeleza Mradi utakaomiliza kero ya maji kwenye Wilaya hiyo kabla ya 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikifutilia kwa Uongozi wa Wizara (Mawaziri), utekelezaji wa agizo hili. Awali, nilijulishwa chini ya Mradi wa Benki ya Dunia ataandaa *Master Plan* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iwajulishe Wananchi wa Wilaya hiyo kuitia Bunge ikiwa agizo hilo la Mheshimiwa Rais limetelekezwa. Naomba jibu kwenye majumuisho/hitimisho la hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefuatilia utekelezaji wa Miradi ya Vijiji Kumi kila Halmashauri, ilioanza mwaka 2007. Kwanza, naipongeza Serikali kwa kuanzisha mpango huu ambaa utatoa suluhisho la muda kwa tatizo la maji kwenye Wilaya mbalimbali nchini. Hata hivyo, kwa maoni yangu, utekelezaji wa Programu hii, umechukua muda mrefu sana kwa sababu ya usimamizi hafifu; mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuwa:-

- (a) Serikali iimarishe usimamizi wa utekelezaji wa Programu hii kuliko ilivyo sasa ambapo Mhandisi wa Maji ameachwa kufanya aonavyo yeye.
- (b) Uteuzi wa Mtaalam Mwelekezi uangalie uwezo wake. Karibu Halmashauri zote Mkoani Arusha zinatumia kampuni moja, jambo ambalo huchelewesha utekelezaji kwa kampuni ku-overstretch kuliko uwezo wake.
- (c) Wizara ihamishe Watumishi wa Sekta waliokaa kwenye kituo kimoja miaka mitano na kuendelea wahamishwe ili kuboresha utendaji kazi na kuongeza tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, natoa pole zangu na kwa niaba ya Wakazi wa Manispaa ya Tabora, kwa matatizo ya kiafya aliyoyapata Mheshimiwa Prof. Mwandsoya. Nachukua nafasi hii, kumwombea Mwenyezi Mungu, amjalie afya njema na arudi salama salimini toka huko India. Sisi Wananchi wa Tabora, tunamkumbuka sana na tunampenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tabora Manispaa ni moja kati ya Wilaya ambazo zimo katika ukanda wa hali ya ukame (*Semi Arid Zone*), ambayo husababisha uhaba wa vyanzo vya maji. Maji ya Tabora tunategemea sana mabwawa wawili; Bwawa la Kazima, ambalo kabla ya kukauka mwaka 2010 uwezo wake ulikuwa lita milioni mbili tu. Kutokana na matatizo ya ukame, kwa hivi sasa Bwawa la Kazima limekauka kabisa na kwa mujibu wa watafiti wa hali ya hewa, tunategemea mvua kidogo mwaka huu. Bwawa la Igombe ndiyo roho ya Watu wa Tabora, lenye uwezo wake ni kutoa lita milioni 15 tu. Kutokana na matatizo ya pampu ya maji na hali mbaya ya mitambo yake, uwezo wao kwa sasa ni lita milioni kumi na moja tu. Kwa maana hiyo basi, tunaomba Wizara itusaidie kufutilia madeni yetu sugu katika Wizara ya Ndani na Wizara ya Ulinzi, kwani *TUWASA* wakilipwa zaidi ya milioni 400, wanaweza kuleta pampu mbili na hivyo kutoa maji kwa wakazi wake wa Manispaa angalau lita milioni 14 mpaka lita milioni kumi na tatu na nusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji ya Visima wa Benki ya Dunia, sina imani nao hata kidogo kwani katika vijiji 12 vilivyo chimbwa vizima ni viwili tu ndiyo vimeonesha hali nzuri ya kuwepo maji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wataalam wa Maji wanajua matatizo ya ukame wa Tabora ni bora Wizara ikaelekeza nguvu zake katika kutoa elimu ya kukinga maji ya mvua (uvunaji wa maji).

Mheshimiwa Naibu Spika, kutengeneza mabwawa kwani katika hali hii ya ukame ni rahisi kupata maji juu ya ardhi kuliko chini ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kuhusu Maji ya *Lake Victoria*, nina imani kubwa Mradi huu amba ni ahadi ya Rais Kikwete, Wizara itautekeleza bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Maji mia kwa mia.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, sisi sote tunafahamu kuwa, Maji ni Uhai, Maji ni Afya, Maji ni Uzima. Kwa maana hiyo, binadamu ye yeyote anategemea sana maji ili aweze kuishi japo kuwa hata wanyama, ndege na viumbe vingine vyote vinategemea maji. Binadamu ni tofauti na viumbe vingine kwa kuwa anatakiwa apate maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, inashangaza sana huduma muhimu kama maji, tangu nchi yetu imepata Uhuru, takriban miaka hamsini, huduma ya maji inakuwa bado ni tatizo kubwa. Kwa kweli ni aibu yetu, ifanye kila linalowezekana kuondoa aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma muhimu kama hii kuitelekeza mikononi mwa wafadhili ni kujiaibisha na hata wafadhili wenyewe wameshindwa kuwaambia tu, lakini wanashangaa sana na ndiyo maana inachukua muda mrefu kushindwa kukamilika kwa Miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu nije kwenye Wilaya ya Sumbawanga; Wilaya ya Sumbawanga Vijiji ina zaidi ya vijiji mia mbili na hamsini na huduma ya maji katika Wilaya hiyo ni mbaya sana. Benki ya Dunia ilipanga kufadhili vijiji kumi toka mwaka 2004. Mwaka 2008 ni vijiji vinne tu vimefanyiwa upembizi yakinifu ambavyo ni Wanankanga, Kilyamatundu, Laela na Mpui. Hata hivyo, pamoja na kufanyiwa upembizi yakinifu, mpaka hivi sasa hakuna kinachoendelea. Naomba maelezo toka kwa Waziri, kwani Wananchi walichangishwa michango kwa muda mrefu sana, bado wamekuwa wakisubiri ni lini watapelekewa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga haina Mhandisi wa Maji, jambo ambalo linachangia kwa sehemu kubwa ukosefu wa mshauri mzuri wa kutoa utaalam. Tunao wasaidizi (*Technicians*) tu, pamoja na Wilaya kuwa kubwa kama hii; hivyo, Serikali ituletee Mhandisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maji iliyokamilishwa huko nyuma, inahitaji fedha nyingi ili ifanyiwe ukarabati, lakini Halmashauri zetu zinapewa fedha kidogo sana ambazo haziwezi kukidhi ukarabati wa Miradi hiyo. Mfano wa baadhi ya Miradi ya Maji ambayo miundombinu ilishaharibika na inahitaji ukarabati ni katika vijiji vifuatavyo; llemba, Mianganua, Mfinga, Kalembe na Mkombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Maji, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, alitoa ahadi ya kuwapatia Wananchi wa Kijiji cha Sakalilo, alipofanya ziara mwaka 2008, lakini ahadi hiyo hajitatekelezwa pamoja na kumkubusha mara kadhaa kwa mazungumzo na kwa maandishi, lakini hadi sasa hakuna majibu ya kuridhisha. Naomba leo awaambie Wananchi wa Kijiji cha Sakalilo ili wasikie wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya maji aliyoitoa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mji Mdogo wa Laela, naomba itekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo upendeleo mkubwa sana, baadhi ya mikoa imepata huduma kubwa ya maji kuliko mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni keki ya taifa, igawanywe sawa kwa mikoa yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja mpaka Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ahadi alioitoa Kijiji cha Sakaliboa ataitekeleza lini?

MHE. DKT. TEREZYA L. HUVISA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandonya na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri wanayofanya ili kuhakikisha kila Mwananchi anapata maji salama kwa afya na maendeleo ya Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyoju Maji ni Uhai; bila maji hakuna uhai wala maendeleo yoyote. Ili kuendeleza uhai ni lazima kuwa na vyanzo vya kutosha vya maji salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, uharibifu wa mazingira husababishwa na kilimo cha kuhamahama hasa kwenye vyanzo vya maji; kufuga mifugo holela hasa kwenye vyazo vya maji; uchafuzi wa maji unaosababishwa na uchimbaji mdogomdogo wa madini na matumizi holela ya zebaki (*mercury*) inayoharibu maji; na uchafuzi wa mazingira utokanao na taka ngumu, maji machafu na mabadiliko ya tabia nchi.

Ninaomba Wizara ijithidi kuelimisha Wananchi katika mambo yafuatayo: Kuacha kulima kwenye vyanzo vya maji; kuacha kulisha mifugo kwenye vyanzo vya maji; kuwaelimisha Wananchi hasa wachimbaji wadogowadogo kuwa na matumizi sahihi ya madini; kuwahamasisha Wananchi kupanda miti ya kutosha inayotunza maji; kuzingatia usafi wa mazingira hasa kwenye vyanzo vya maji ili kuondoa tatizo la magonjwa yanayosababishwa na maji machafu; na kuelimisha Wananchi kuhusu athari za mabadiliko ya tabia nchi na jitihada za kupambana na athari hizo hasa kupambana na tatizo la ukame na jangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na kuipongeza Serikali kwa umakini wake mkubwa na kukubali kuipatia Wizara jumla ya shilingi 446,094,636,000. Pamoja na pongezi hizi, napenda kutoa ombi maalum kwa Serikali yetu, kuona uwezekano wa kulipatia maji Jimbo la Mbogwe pamoja na Wilaya ya Bukombe, kutokea chanzo cha maji cha Ziwa Victoria, ambapo tayari imekwishafikisha huduma hii katika Mji wa Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa, Wilaya za Kahama, Bukombe na Mbogwe, ziliwahi kuwa Wilaya moja kabla ya kugawanywa.

Kwa kuwa Serikali illitambua tatizo la maji katika Wilaya Mama ya Kahama, tunaiomba sasa Serikali iendelee na jitihada hizo hizo ili huduma hii muhimu ya maji iweze kufikishwa katika Wilaya ya Bukombe na Jimbo la Mbogwe kutokea Ziwa Victoria, ambayo tayari yamekwishafikisha katika Wilaya jirani ya Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko pamoja na Wizara katika jitihada zake za kuwapatia Watanzania huduma hii muhimu kwa maisha ya watu wetu pamoja na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali kupitia Wizara ya Maji, iweze kusimamia ukamilishaji wa Miradi ya Visima inayofadhiliwa na Benki ya Dunia. Miradi hii ikikamilika, itatoa nafasi kwa vijiji vingine kumi kwa kila Wilaya ifikapo mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine, napenda niipongeze Serikali kupitia Wizara ya Maji, kwa kutoa kiwango kizuri cha fedha kwa Wizara hii ili iweze kufikishwa huduma ya maji kwa Watanzania wengi zaidi hasa vijiji ambako Wananchi wengi wanaishi bila upatikanaji wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Jimbo la Mbogwe na Wilaya ya Bukombe iweze kuwa na upatikanaji wa huduma ya maji wa kudumu; ni vyema maji yaliyofikishwa Mjini Kahama kutokea chanzo cha maji toka Ziwa Victoria yafikishwe Wilaya ya Bukombe na Jimbo la Mbogwe kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Waziri wa Maji.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Waziri, kwa hotuba yake nzuri na kazi nzuri aliyoifanya ya kupambana na changamoto kubwa zinazomkabili katika Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Vijihi Kumi chini ya Ufadhilli wa *World Bank* ni mzuri sana iwapo ungetekelawa kwa wakati mwafaka, kwani kumekuwa na urasimu mkubwa wa kuusimamia Mradi huu. Mpanda tuna vijihi vitapatavyo kumi na mbili ambavyo hatua za awali walishafanya lakini mpaka sasa bado Miradi hiyo haijakamilika. Vijihi hivyo ni Karema, Ikola na Ngomalusambo, ambavyo vipo katika Jimbo la Mpanda Vijihi. Katika Jimbo la Katavi, vipo Vijihi vya Usevya, Kibaoni, Mtakumbuka, Mwenge, Mamba, Majimoto, Mbede na Sungamilia. Maeneo haya bado Mradi haujakamilika kwa sababu zisizojulikana na kufanya dhiki kubwa katika maeneo hayo wanayoishi Wananchi wengi wanaohitaji huduma hiyo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Mpanda unakua kwa kasi kubwa na una idadi kubwa ya watu na hivyo, kufanya Mji huu uwe na matumizi makubwa ya maji. Miundombinu ya maji ni ile ile ya zamani, ambayo inashindwa kuhimili kuwapatia huduma Wananchi hao wa Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kupitia Wizara ya Maji, iongeze miundombinu katika Mji wa Mpanda na kuchimba visima vikubwa ambavyo vitahimili idadi ya watumiaji wa Halmashauri ya Mji wa Mpanda. Hali iliyoko Wilaya ya mpanda inatisha sana; tunaomba Wizara iangalie sana huduma hiyo katika Halmashauri ya Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na uhaba mkubwa sana wa madawa ya kutibu maji, kiasi cha kuwafanya Wananchi watumie maji yasiyo salama na kusababisha magonjwa ya matumbo na kuhara. Naiomba Wizara ilete madawa hayo kwa wingi na ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mpanda Vijihi lina matizo makubwa ya ukosefu wa maji katika Kata ya Mpandandogo hasa Vijihi vya Igagala, Ngomalusambo, Ifukutwa, Mchamcha, Igalula, Vikunge, Bungwe na Majalila; kijiji ninachotoka mimi. Kata zingine ni Kata ya Kabungu, Karema, Ikola, Katuma, Sibwesa, Mwese na Mishamo. Maeneo haya yana matatizo makubwa na kuathiri shughuli za uzalishaji kwa Wananchi, kwani muda mwingi wanautumia kutafuta maji ambayo yapo mbali sana na maeneo wanayoishi na maji yenye siyo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji wanayotumia Wananchi wa Jimbo la Mpanda Vijihi ukiyaona huwezi kuamini kwamba, yanatumiwa na binadamu. Tunaiomba Serikali iweke msukumo mkubwa katika maeneo ya vijihi vifuatavyo: Igagala, Ngomalusambo, Ifukutwa, Majalila, Vikunge, Bugwe, Kasekese, Milala, Iloba, Mnyagala, kabage, Kapalambsenga, Mwese, Bujombe, Mpembe, Igalula, Isengule na Kasangatonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya yanatisha sana, tunaiomba Wizara ihakikishe inaandaa mazingira ya kupeleka huduma hiyo kwa Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bonde la Ziwa Tanganyika, lipewe umuhimu wa pekee, kwa kuwa linapungua maji mara kwa mara. Ukiangalia liliyokuwa miaka kumi huko nyuma, hatua za dharura zichukuliwe kunusuru Ziwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji ishirikiane na Wizara ya Mifugo, kuhakikisha wanaandaa mipango ya kuhifadhi mazingira pamoja na kuwawezesha wafugaji wa eneo la Mpanda kuwachimbia mabwawa ya kunyweshea mifugo. Mazingira mengi yanaharibiwa na mifugo kukosa maeneo ya kunyweshea mifugo, inayosababisha kuharibu vyanzo vya maji. Sasa

hivi mifugo na binadamu wanagombania sehemu za kunyweshea mifugo na matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo yatakekelezwa kama nilivyoshauri, nitaunga mkono.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Namanyere katika Wilaya ya Nkasi una wakazi wasiopungua 15,000; una Hospitali ya Wilaya; Chuo cha Manesi; Sekondari tatu; Shule za Msingi sita; kuna *High School* moja; na pia kuna Kituo cha Afya lakini hakuna huduma ya maji. Vipo visima vichache tu na ifikapo mwezi wa saba mpaka Novemba huwa hakuna maji hata ya kununua. Miaka ya themanini maji yalikuwa yanapatikana; cha ajabu leo hii eti tunaendelea au tunarudi nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia maji katika miji ambayo ipo kandokando ya Ziwa Tanganyika, miaka ya themanini Miji ya Kirando na Kabwe, walikuwa wanapata maji ya bomba toka chanzo cha Ziwa Tanganyika. Ziwa lipo nusu kilometra tu toka Miji hiyo, lakini leo hii hawana maji; matanki yapo kama mapambo tu na Serikali iligharimia sana hayo matanki; lakini hakuna cha msaada wala chochote kile na huku visima kadhaa vilivyochimbwa miaka ya themanini leo hii vyote havifanyi kazi kabisa na Wizara haina mpango wowote wa kuvikarabati. Wizara nyingine zote zinaangalia na kuendeleza Miradi yake tofauti na Wizara ya Maji, Miradi ya Idara ya Maji inarudi nyuma hasa katika Vijiji vya Wilaya ya Nkasi Kaskazini kila kijiji hakina maji kabisa. Ninata pia kujua kuhusu visima 700 alivyosaidia Sabodo.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Stephen Wasira (Mb), kwa kuwasilisha Hotuba vizuri. Mchango wangu katika Wizara hii upo katika maeneo muhimu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi mingi ya Maji ya Wilaya haifanyiwi utafiti wa kutosha na hivyo kutoa mwanya kwa wakandarasi kuitekeleza kwa gharama kubwa kuliko gharama halisi za Miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi Mikubwa ya Maji hainufaishi Wananchi wa vijiji vinavyopitipa na mabomba, bali kwa kiasi kikubwa Wananchi wa mijini peke yao. Mfano ni Mradi wa Maji ya kutoka Misungwi kwenda Shinyanga na Kahama. Vijiji jirani vingi havijanufaika kabisa na Mradi huu, hata Mji wa Misungwi hauna maji ya uhakika. Mifano ya namna hii ipo mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri nyingi za Wilaya hazina Wataalam wa Maji, wenye ujuzi wa kutosha kusimamia na kutoa ushauri kwa Miradi inayoibuliwa na Wananchi. Aidha, vyanzo vingi vya maji havisimamiwi vizuri na wala hawatoki kwenda vijijini kushirikiana na Wananchi kulinda vyanzo hivyo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, umwagiliaji haujapewa kipaumbele cha kutosha, hasa katika maeneo ambayo hali ya hewa na jiografia inaruhusu. Jimboni Buchosa, yapo maeneo ambayo skimu za umwagiliaji zikiibuliwa, Wananchi wanao uwezo wa kuzalisha chakula kingi kwa ajili yao na kwa biashara. Naomba Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake, anithibitishie kwamba, maeneo yafuatayo yatapewa kipaumbele katika Miradi itakayofadhiliwa na Mfuko wa Umwagiliaji wa Wilaya (*DIDF*) na Mfuko wa Umwagiliaji wa Taifa (*NIDF*): Nyakasungwa Mtaroni; Nyaabano; Liteli Bukokwa; Katempisi; Luhorongoma; na Luharanyonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Wizara ndiyo isimamie mgawanyo huu wa fedha za umwagiliaji, badala ya kuziachia Halmashauri ziandae zenyewe andiko. Kwa kufanya hivyo, Wakurugenzi hawachagamkii kwani yako mahitaji ya Halmashauri kuchangia gharama za Mradi. Kwa hiyo, wengi wao hugoma kuweka *commitment* hiyo ya Halmashauri ili Wizara ipitishe Miradi inayopendekezwa.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mungu, kwa uhai alionipa. Pia napenda kumshanga sana Naibu Waziri, kwa kauli zake hapa Bungeni hasa alipokuwa akijibu swali langu kuhusu maji Musoma Mjini, ambalo majibu yake yanapatikana katika *Hansard*. Alisema Mradi wa Maji Musoma Mjini unaofadhiliwa na *AFD* ya Ufaransa, kwa gharama

ya Shilingi za Kitanzania bilioni 50, ambao umeanza tarehe 15 Mei, 2011 na kukamilika Desemba, 2013; majibu yasiyo na uhalisia hasa kwa kuwapa matumaini hewa Watanzania ni kosa na lazima uwajibikaji uwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi leo ninapoandika mchango wangu, hakuna dalili yoyote ya Mradi huo kuanza, japo tayari tarehe iliyotangazwa na Waziri imepita.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo tu tarehe kupita, bali sasa hali ya maji Musoma ni mbaya sana na hakuna mtu yelete anayeumiza kichwa kutatua kabisa tatizo hilli. Bunge lako Tukufu lilidanganya hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kwa Mji kama Musoma kuchimbiwa visima huku maji ya Ziwa Victoria yakienda Misri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosekanaji wa maji, umeleta hali mbaya sana kiafya na magonjwa ya milipuko yamekuwa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ya watu kuliwa na mamba kwa kufuata maji Ziwanu, sasa tungeomba yawe mwisho. Maji yamekuwa yakiwaliza sana Wananchi hasa akina mama na watoto, ambao hata shughuli nyingine hazifanyiki na kuwalettea umaskini, kwa kuwa muda wa uzalishaji wanautumia kwa kutafuta maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaumiza kuona Miradi ya Maji inangoja uchaguzi ukaribie ndiyo itekelezwe. Tunaomba maji yasitumike kama rushwa wakati wa Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni haki ya Wananchi, bila kujali itikadi. Tunaitaka Serikali isitafsirike vibaya katika usambazaji maji kiitikadi kwa kuweka kipaumble hata miji isiyokuwa chini ya Chama Tawala.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mark Mwандосыа (Mb), Waziri wa Maji, kwa kazi nzuri iliyotukuka na Hotuba nzuri ya Bajeti iliyowasilishwa leo. Aidha, nampa pole na kumwombea apone haraka ili arudi kazini na kuendolea na ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Eng. Gerson Lwenge (Mb), kwa kazi nzuri sana ya kuendeleza Wizara na Sekta ya Maji. Nawapongeza sana Katibu Mkuu, Eng. Chris Sayi na Naibu Katibu Mkuu, Eng. Mrindoko na Wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa kufanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanga ni Wilaya kame sana; kuna shida kubwa sana katika Ukanda wote wa Tambarare ya Magharibi inayojumuisha Vijiji vya Kileo, Kivulini, Kituri, Kifaru, Mwanga Mjini, Kiruru, Ibwe, Ijewa, Kisangara, Lembeni, Kiverenge, Mgagao, Mbambua, pamoja na vijiji katika Ukanda wa Bwawa la Nyumba ya Mungu, Nyabinda, Kagongo, Lang'ata Bora na Handeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya Mwaka 2010/2011, tulitaraja kuwa usanifu wa Miradi utakamilika na mkandarasi atapatikana. Naiomba Wizara iongeze msukumo katika utekelezaji wa Mradi huu ili tuweze kuondoa hofu ya Wananchi labda Mradi huu hautatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Vijiji Kumi kila Wilaya umekuwa ni tatizo kubwa kwa Wananchi. Mradi huu ultiangazwa katika Bajeti ya Wizara ya Mwaka 2003/04 na Bajeti ya Mwaka 2004/05, hadi sasa Wananchi wanangojea. Kwa sababu ya tatizo kubwa la ukame, naiomba Wizara itoe upendeleo maalum kwa Wilaya ya Mwanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji katika Kijiji cha Mgagao ni shida sana. Hiki ni moja ya vijiji kumi vya Mradi wa *World Bank*. Tumechimba visima virefu sita vya Mradi huo, tumepata maji katika kisima kimoja. Nguvu za kufunga pampu, jenereta na kusambaza maji kijijini hatuna.

Ninaomba Wizara itusaidie kama *special case*. Wananchi wanunua ndoo moja toka Same kwa shilingi 600 kwa ndoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Lomwe kina tatizo kubwa sana la maji pamoja na Vuagha. Naomba sana Vijiji hivi Lomwe, Vuagha na Mgagao, viwekewe msisitizo maalum sana. Matatizo ya maji ya Wananchi wa Mwanga ni makubwa sana, tutapata faraja mkiipa Wilaya kipaumbele kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, maji ni kila kitu. Tukitaka kupika lazima tutumie maji. Kuzuia magonjwa ya mlipuko lazima maji, kupata mazao mashambani lazima maji. Tukiugua lazima tupate maji. Hata kwa wenye bahati, wakitangulia mbele za haki lazima maji yawepo kuwasafisha na walio hai ili waweze kuishi vizuri, kwa usafi, wanahitaji maji kwa kufulia na kuoga. Hivyo, tunaona jinsi maji yalivo na umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji letu la Dar es Salaam ndiyo kioo cha nchi yetu, lakini ni kitu cha kusikitisha jinsi mifumo ya maji taka illivo; mvua zinaponyesha ni rahisi sana maji taka kuchanganyika na maji safi. Sasa ni wakati baadhi ya mabomba yake yabadilishwe; la sivyo, magonjwa ya mlipuko kama *Typhoid* na *Cholera* itakuwa ni hadithi katika Jiji letu na haliwezi kwisha. Je; ni lini Dar es Salaam watapata maji safi na salama ya kunywa? Kuna matatizo ya maji sehemu nyingi licha ya kuzungukwa na bahari. Je, hakuna jinsi ya ku-treat maji ya bahari yakawa mazuri kwa matumizi ya binadamu? Ni hatari sana kwa vijana wanaochota maji baharini kwa ndoo na kuwauzia watu majumbani na ukizingatia uchafu wote unaelekezwa baharini. Ningependa kujua Serikali ina mikakati gani ya muda wa kat, muda mfupi na mrefu, kwa sababu yaliyokuwa yanaitwa mabomba ya Wachina yamefeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 70s maji yaliokuwa yanatoka kutokea Maporomoko ya Mlima Kilimanjaro lakini sasa hivi mifereji ile inakauka kabisa, vyanzo vya maji vinakauka. Wakulima wengi ambaio ni zaidi ya asilimia 80, wanaoishi vijiji, walikuwa wakifanya kilimo cha umwagiliaji sasa hivi kahawa, migomba inakufa moshi kule Tela, Uru, Kibosho, Mahoma, Kidia na Mbokomu. Kibaya zaidi, katika Kata ya Mabogini, Wajapani wallanzisha kilimo cha umwagiliaji, kilimo cha mpunga, lakini baada ya Wajapani kukambidhi Mradi ule sasa umekufa na maji hayapo. Je, tatizo ni nini? Serikali ina mikakati gani kufufua kilimo hiki cha umwagiliaji kule Mabogini?

Sambamba na hilo, Kata ya Mbokomu Kusini ina shida sana ya maji. Unakuta mama anatoka zaidi ya kilomita sita kwenda kuchota maji ndoo moja na saa nyingine wanatoka nyumbani usiku sana ambapo ni hatari kwa maisha yao. Watoto kwenda kuchota maji kwa ajili ya kufanya usafi wa madarasa ikiwa ni pamoja na kumwagilia maua. Hili siyo jambo zuri; shule hiyo ilikuwa ikiitia *Mwanambeni Primary School* sasa hivi inaitwa *Mbokomu Primary School*. Sisi tulisoma pale, palikuwa hakuna shida ya maji, hivi sasa wanafunzi badala ya kukaa darasani na kusoma inabidi wakachote maji. Hivi kwa mtindo huu tunalalamika wanafunzi wanafeli; watafanyaje vizuri ikiwa muda mrefu wanakwenda kutafuta maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali ifanye mashindano ya Kimko na Kiwilaya na RC na DC wawe ndiyo Viongozi wa kuhakikisha vyanzo vya maji vinafufuliwa na miti inapandawa kwa wingi ili hali ya maji irudi kuwa ya kawaida.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni kubwa sana na muhimu sana. Ina kazi nyingi sana kusimamia maji nchi kisera na kicutendaji. Kwa mfano, Mamlaka za Maji za Majiji, Manispaa na Halmashauri, zote zinasimamiwa na Wizara. Programu zingine za maji kama Mabonde ya Mito Nile, Zambezi, Ruvuma, Songwe na kadhalika, husimamiwa na Wizara. Pia maji ya Ziwa Victoria na Tanganyika husimamiwa na Wizara. Sasa huu mzigo mkubwa sana wa Wizara, ukiongeza na Mradi mpya wa Maji Vijiji, unaifanya Wizara kulemewa.

Mpango wa Maji umeanza mwaka 2008, lakini mpaka sasa maendeleo halisi ni kidogo sana. Mipango yake ni mizuri sana. Mipango ya visima kumi kila Wilaya kwa kuanzia ni mizuri sana. Kinachofanya Mradi huu usianze ni kuelemewa kwa Wizara. Naomba tuchukue uzoefu ambao nchi imepata kwa kuanzisha *TRA* na *TANROADS*. Taasisi hizi zimefanya kazi vizuri sana. Kwa misingi hiyo, Serikali inaweza kuanzisha Mamlaka ya Maji Vijiji ikaitwa *TANWATER*. Mamlaka hii ikiundwa, itasaidia sana kusukuma Mradi huu ambao ni wa muda mrefu sana. Wahandisi wapo wa kutosha na mipango mizuri ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu katika Wilaya ya Chunya upo kwenye Vijiji vya Kiwanja, Mapogoro, Makongoro, Makongorosi, Mkolla, Lupa, Mwiji, Lualaje, Mtawila, Isangawana na Matwiga. Katika vijiji hivi, bado tupo kwenye uchimbaji visima tu toka mwaka 2008; kama kutakuwa na Mamlaka ya Maji, Miradi hii itaanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Mradi wa Bwawa la Matwiga; Bwawa hili litasaidia Kata za Matwiga, Mtanila, Lupa na Mamba. Utekelezaji wa Mradi huu unasuasua mno, naiomba Wizara iharakishe umalizaji wa Mradi huu kwa faida ya Wananchi wa Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MESHACK J. OPULKWA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa jitihada zake za kuipatia Wilaya ya Meatu angalau Bwawa la Mwanjolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuishauri Serikali kuwa, angalau mabwawa mengine mawili katika Kata ya Bukundi na Mwabuzo yaongezwe ili kuondoa kero ya maji ya mifugo Wilayani Meatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara, kwa kazi kubwa inayofanya katika kukabiliana na tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kisarawe ina tatizo kubwa sana la maji. Katika Kata ya Chole, Kibuta, Marumbo, Maneromango, Mzenga na Vhingo, hali ni mbaya sana. Naiomba Serikali ifanye kila liwezekanalo kuisaidia Wilaya ya Kisarawe ili Wananchi waweze kupata fursa ya kushiriki katika uchumi, badala ya kutafuta maji muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ijitahidi Mradi wa Maji wa *World Bank* ukamilike haraka iwezekanavyo ili kupunguza tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa fedha za maendeleo za kugharimia Miradi ya Maji uwe wa haraka ili kuwezesha Miradi ya Maji kukamilika ndani ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inachelewesha vibali vya uchimbaji wa visima. Sioni kwa nini vibali vichelewe sana ambapo inaleta usumbufu na ucheleweshaji wa utekelezaji wa Miradi ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali isimamie kwa karibu rasilimali za maji, zikiwemo magari na mitambo ya maji. Naiomba Serikali iangalie na kujianaa na mipango mikubwa ya baadaye ya kuliwezesha Jiji la Dar es Salaam na Mkao wa Pwani, kwa kubuni Mradi Mkubwa wa Maji kutoka Mto Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kutumia mpango mkubwa wa kulisa Jiji la Dar es Salaam, kwa kuwapatia maji Wakazi wa Tarafa ya Mzenga Wilayani Kisarawe, kwani Mzenga kuna tatizo kubwa sana la maji wakati eneo (Kata hiyo), ipo karibu sana na Mlandizi, chini ya kilometra 30. Naiomba sana Serikali katika Mradi wa Maji wa Upanuzi wa Vyanzo vya Ruvu Juu na ujenzi wa Bwawa la Kidunda, isaidie kuwapatia maji Wananchi wa Mzenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali isitoze VAT madawa ya maji, kwani yanaogeza sana ghamama za maji kwa mlaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. ALIKO A. KIBONA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu wake, pamoja na Watendaji wote, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, natoa pole kwa Waziri, kwa kuugua na naomba Mwenyezi Mungu, ampatie heri na amrudishie afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji ni Wizara mtambuka; kwa sababu hiyo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazotengwa ni kidogo na kuathiri upatikanaji Miradi mingi mipyä na hata ile iliyopo kutopewa fedha ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria za nchi na maagizo yanayotolewa na Viongozi hayafuatwi. Mfano; Marehemu Dokta Omar Ali Juma, alikuwa mkereketwa wa Mazingira pamona na wafiasi wake, sasa wamekata tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliwhi kukataza matumizi ya mifuko ya plastiki nchini, lakini mpaka hivi sasa inatukima na TBS wanaruhusu na kuipa chapa ya TBS. Mifuko hii inaharibu ardhi na inaua mifugo na pia inaharibu vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo na shughuli za kibinadamu; Mamlaka zinashindwa kusimamia vyanzo vya maji na kuruhusu watu kufanya shughuli kwenye vyanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya lleje ina upungufu wa maji katika maeneo ya Miji ya Itumba na Isongole, Kata ya Ibaba, Kata ya Itale na maeneo ya Chabu, Malangali, Ikinga, Ngulunguhi na Lubanda. Kwa niaba ya Watu wa lleje, naomba kupatiwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika maeneo yalijotajwa; ni vizuri utueleze lini tutapata maji maeneo hayo.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kina cha maji katika Ziwa Tanganyika kinashuka sana. Sababu mojawapo kubwa ni kuharibika kwa mlango wa kuruhusu maji katika eneo la Bukavu nchini DR Congo, ambapo maji ya Ziwa Tanganyika huingia katika Mto Kongo. Rais Jakaya Kikwete, alimtumia salamu Rais Joseph Kabila kuitia Waziri wa Maji, Mheshimiwa Profesa Mark Mwандосya kwamba, mlango ule katika Mto Lukuga ambaao ni sehemu ya Mto Kongo, unafanyiwa ukarabati na hivyo kuokoa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata maelezo ya Serikali juu ya suala hili kwani kuna hatari Bandari ya Kigoma ikajaa mchanga kutokana na kupungua kwa kina cha maji.

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Maji na nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Mwандосya na Naibu Waziri, Mheshimiwa Lwenge, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nampongeza Katibu Mkuu, Eng. Sayi na Wataalam wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara isaidie ujenzi wa Bwawa la Msange Singida kaskazini kwa ajili ya umwagiliaji, kazi kbuwa sasa ni kulifanyia upanuzi na *dragging* kuongeza kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara isaidie uchimbaji wa visima virefu katika Vijiji vya Nduamganga na Sokoine, ikiwa ni pamoja na kukamilisha ahadi ya Serikali ya Vijiji Kumi vya *World Bank Project*. Tunaomba Wizara isaidie kusambaza maji kutoka Kisima cha Ilonga hadi Chuo kitakachojengwa cha VETA Ilongero na pia katika vijiji kumi vinavyozunguka Kisima cha Ilongero.

Kuna sekondari tatu katika Kata ya Ilongero ambazo pia pamoja na shule za msingi zote na za kata jirani wasambaziwa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kubwa na Uongozi wa Wizara hii na kama Mbunge wa Jimbo, tutaendelea kutoa ushirikiano wote ili kusaidia jitihada za Serikali katika kuondoa kero ya maji katika Jimbo la Singida Kaskazini.

MHE. ASSUPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa pole sana Mheshimiwa Waziri kwa ugonjwa uliomposta na tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu, amponye haraka na Mungu wetu mwema atamponya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Nkenge ni Jimbo liliopo mpakani mwa Tanzania na Uganda na limezungukwa na Mto Kagera, wenye maji mengi na una uwezo wa kuhudumia Wilaya yote ya Misenyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya Misenyi haina Mamlaka ya Maji na matokeo yake hakuna huduma ya maji. Watu wanatumia maji ya visima, jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Misenyi ni mpya, sasa ni wakati mwafaka wa kuweka miundombinu ya maji wakati inajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Kagera ukifungiwa mashine kubwa ya maji kama inavyofanya Kampuni ya Sukari, yaani Kagera Sugar, wao wamefunga *pump* kubwa na wananyeshea mashamba yao; je watu na mashamba ni kipi bora? Vyema vyote viende pamoja, watu wapate maji na miwa ipate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kubwa, tunaomba Wizara ya Maji itufungie mitambo ya maji, ivute maji Mto Kagera na yasambazwe Wilaya nzima. Siyo vyema watu wapate shida huku wamezungukwa na maji. Mkoa wa Shinyanga wamevuta maji kutoka Ziwa Victoria, lakini Misenyi inashindwa kuwa na maji safi na salama wakati wamezungukwa na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwasilishwa kwako, mchango wangu katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji kuhusu Makadrio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara yake kama ilivyowasilishwa Bungeni kwa niaba yake na Mheshimiwa Masatu Stephen Wasira (Mb).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya (Waziri), kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili, nampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana katika utendaji wake wa kila siku. Pia nampa pole kwa maradhi yanayomkibili na tunamwombea Mungu apate ahueni haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uwasilishaji wa Hotuba, tumeona kuwa Wananchi wanasisitizwa kutunza vyanzo ya maji, rasilimali za maji na matumizi bora ya rasilimali za maji, lakini kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Wizara ya Mazingira, kuweka mkakati wa kuwashirikisha Wananchi kulinda na kuelimishwa umuhimu wa uhifadhi. Ifike wakati sasa miti na rasilimali zote ziingizwe kuwa ni mali ya Taifa na ziwe zinakabidhi kwa Uongozi wa Vijiji kama (*assets*) ambazo zinafanyiwa *inventory* kila mwaka au kila baada ya muda fulani ambao utapangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi inayohusu *World Bank* hakika ni kero kwa maana kila eneo lina tatizo la aina yake. Katika Wilaya ya Kilwa tatizo kubwa lipo katika uchangiaji wa asilimia kumi; naiomba Serikali kwa maeneo ambayo yana hali duni kimaisha, basi yenewe ibebe

jurukumu la kuchangia kwa niaba ya Wananchi. Licha ya kuchangia, pia Serikali iweke jitihada katika usimamizi wa Miradi maana yapo maeneo mengi ambayo Miradi imefanyika lakini hakuna mafanikio kwa maana ya maji hayakupatikana na wakandarasi wameshalipwa stahili zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa mgawanyo wa fedha za maji uangaliwe upya, maana maeneo ya mijini yanapangiwa pesa nyingi bila sababu za msingi na mara zote wao ndiyo wamekuwa chanzo cha matatizo kwa maana walishindwa kulipia *bills* za maji katika mamlaka husika hadi kupelekea mamlaka hizo kufilisika.

Pia ukataji wa miti au uharibifu wa mazingira, unachangiwa sana na mahitaji ya mijini. Napendekeza katika mgawanyo wa Miradi, licha ya kubuniwa na Halmashauri au Wizara, tuweke mfumo ambaao Viongozi kama Wabunge na Madiwani, washiriki katika usimamizi wa Miradi au mingine ipitie katika Mifuko ya Jimbo. Hali ya Wananchi kutokubaliana na vigezo vinavyotumika sasa kwa maana ya idadi ya watu, Wananchi wa Vijijini kama Kilwa, wana mazingira hatarishi zaidi kuliko mijini. Izingatiwe pia kuwa, ukubwa wa eneo la Kilwa kama Wilaya ni sawa na Mkoa mzima wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Kitabu cha Hotuba (kundi la nne) katika utekelezaji wa Miradi ya Maji, Mheshimiwa Waziri ameainisha kuwa, Wilaya ya Kilwa ina Miradi kadhaa, ambayo inasubiri usanifu. Ifike wakati tuone umuhimu wa kutekeleza Miradi hii kwa haraka ili kuwaondolea Wananchi adha kubwa katika maisha yao. Kwa kiasi gani tumesahau kaulimbiu ya "Maji ni Uhai"?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia ibara ya 32 katika Kitabu cha Hotuba, imezungumziwa Wakala wa Uchimbaji Visima na Mabwawa. Sielewi Wakala huu unafanya kazi gani huku tukipoteza pesa nyingi mno kwa kuwapa wakandarasi binafsi kazi ambazo pia huzifanya kwa kiwango cha chini, lakini kwa gharama kubwa mno. Hatua madhubuti zichukuliwe ili kuimarisha ujenzi wa mabwawa ili kuhifadhi maji ambayo ni mengi, yanapotea bila ya kutumika huku ikifika wakati wa kiangazi kunakuwa na upungufu mkubwa sana wa maji katika maeneo yote nchini hasa vijijini. Kama inavyoilewega, Tanzania haina tatizo la maji kwa maana vyanzo ni vingi mno, tatizo ni *management* ya maji haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa sana katika maeneo mengi hasa mijini, ambapo Wananchi kwa nguvu zao wameamua kuchimba visima. Matokeo yake wanalazimishwa kulipia kila mwezi, hali ya kuwa wanatumia vyanzo vya fedha kuanzisha visima hivyo na wanatumia kwa matumizi yao binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza pia sasa kubuni mbinu mpya za mapato ili kuweza kuimarisha huduma za maji vijijini hasa kwa kutumia Mamlaka za Maji Mijini kama DAWASCO, DUWASA, MUWASA na kadhalika, ziwe zinatoa gawio kwa Mfuko Maalumu utakaoanzishwa ili kumaliza tatizo la maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba nikushukuru kwa kunipokelea maoni yangu, kwa kuamini kuwa yatafanyiwa kazi stahiki na utekelezaji hasa ukizingatia umahiri wa Mawaziri na Watendaji wa Wizara hii. Nawatakia kila la kheri, namwomba Mungu atulinde sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naipongeza Serikali kwa kuipa Kipaumbele Sekta ya Maji kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012. Naipongeza pia kwa mafanikio yaliyopatikana tangu 2005 hadi 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yote, llani ya Uchanguzi ya CCM 2010, ibara ya 87, bado imeonesha dhamira njema ya kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kufikia asilimia 75 vijijini na asilimia 95 mijini ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina wasiwasi na lengo hili kwa upande wa mijini, kwani kwa kipindi cha miaka mitano (2005 – 2010), upatikanaji wa huduma hii uliongezeka kwa asilimia nane

na kufikia asilimia 86. Hii ina maana kwamba, ili kufikia asilimia 95 kunahitajika ongezeko la asilimia tisa tu ndani ya miaka mitano; hili linawezekana kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nina mashaka kuhusu kasi ya ongezeko la upatikanaji wa maji safi na salama vijiji, kwani mwaka 2005 – 2010, ongezeko lilikuwa asilimia 4.1 na kufikia asilimia 57.8. Sasa tunapokuwa na lengo la kufikia asilimia 75 ya upatikanaji wa huduma hii, tutahitaji ongezeko la asilimia 17.2. Nina wasiwasi kama lengo hili litafikiwa ifikapo mwaka 2015. Naiomba Serikali ilieleze Bunge, itatumia mkakati gani mahususi kwa ajili ya kutimiza lengo la Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 kwa upande wa vijiji. Ninashauri Bajeti ya Vijiji iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, bomba la maji kutoka Shinyanga – Nzega – Tabora litapita Kijiji cha Mayombo, ambacho kipo km 15 kufikia Kijiji cha Kigwa, kilichopo Barabara ya Tabora – Kigwa – Tura – Itigi – Manyoni. Wananchi wa Kigwa wamenituma wanataka Tawi lake liwaletee maji ya Ziwa Victoria ili kero sugu ya maji iishe. Wakazi ni takriban 15,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Uyui kwenye Mpango wa JICA visima 12 vimechimbwa na kukamilika mwezi Desemba, 2011. Hali ya maji Majimbo ya Igala na Tabora Kaskazini ni tatizo kubwa; ni dhahiri kila jumbo litapata visima sita. Visima sita vya Igala ni vijiji vipi kwani Igala ina vijiji 48? Nipate majina ya vijiji ili nikakague maendeleo ya Mradi huu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia taarifa nzuri kuhusu hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa Vijiji Kumi vya kila Halmashauri ya Wilaya chini ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji hadi kufikia tarehe 15 Agosti, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa sita na w asana; Tabora/Uyui kundi la nane; hili ni kundi la Halmashauri ambazo zimetangaza zabuni za kupata wakandarasi watakaochimba visima vya maji. Halmashauri nne zimetajwa ikiwemo Tabora/Uyui. Hii taarifa ilitolewa Februari, 2011. Je, bado zabuni hazijachagua wakandarasi na kuanza kuchimba visima? Naomba turekebishe hii taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Maji la Goweko kwa ajili ya maji ya kumwagilia, kunyeshe mifugo na matumizi ya binadamu baada ya kuchinjwa litakamilika lini? Mwezi Desemba, 2010 mtaalam aliahidi kuwa usanifu ungekamilika; je, Mradi umefikia wapi? Kwenye taarifa haionekani Wilayani Uyui!

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za *Geophysical and Hydrogeological Surveys* zinaonesha wapi maji yanaweza kupatikana. Inakuwaje ukurasa wa 23 na 24 visima 12 vilivyocheimbwa Urambo visima vyenye maji ni vitatu tu (25%); Sikonge vimechimbwa visima 12, vyenye maji vinne(33%); na Manispaa ya Tabora vilivyocheimbwa ni 16, vyenye maji 8 (50%). Teknolojia ya utambuzi ipo; je, tunaitumia au tunabahatisha kwa gharama kubwa? Imani ya Wananchi kwa Wataalam wetu itakuwa hali gani? Tufanye *well testing* kabla ya kuingia gharama kubwa ya uchimbaji.

MHE. DKT. MILTON M. MAHANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampa pole Mheshimiwa Waziri, kwa maradhi yanayomsumbu na namwombea kwa Mwenyezi Mungu, apone haraka arudi kushirikiana nasi katika ujenzi wa Taifa. Pili, naipongeza Wizara nzima kwa kazi nzuri na nitamke kwamba, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ningependa kuchangia kwenye Hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi mkubwa wa Maji katika Jiji la Dar es Salaam kama ilivyochezwa na Waziri, naomba Serikali iwe makini katika kuutekeliza ili isije ikatoa tena visingizo vya kutokamilisha Mradi huo ndani ya miaka mitatu ijayo kama ilivyoahidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Mradi wa Mabomba ya Wachina kukamilika, Mradi huu umeleta kero zaidi kwenye maeneo kadhaa ya Segerea, Tabata na Kisukuru, kwani hata maji kidogo yaliyokuwa yanatoka kabla sasa hayatoki maeneo hayo; tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ielewé kwamba, Mradi huu wa Maji wa Songas katika Kata ya Kinyerezi, ambapo tanki kubwa la lita 1,000,000 na ujenzi wa pampu kubwa na miundombinu mingine ilikamilika, lakini Mradi huu unategemea maji toka DAWASCO. Sasa ni miaka mitatu hakuna kitu! Naomba Wizara iweke Mradi huu wa Kinyerezi kwenye mipango yake ili ikamilishe Mradi.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa fursa hili, nami niweze kuchangia Hoja ya Bajeti ya Wizara ya Maji ya Mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunatambua kwamba, bila maji hakuna uhai, kwani viumbwe wote duniani hawawezi kuishi bila maji. Maji haya pia yanaweza kuwa na madhara kama binadamu akiamua kuyaharibu au kuharibu mikondo yake kama kumwaga maji yenye sumu kutoka viwandani na migodini katika mito, maziwa na hata bandarini, hivyo hivyo kuharibu vyanzo vya maji kama kulima na kukata miti kandokando ya vijito, mito na maziwa.

Mwisho, kuharibu mazingira kwa kuchoma misitu, kukata miti ovyo na kulisha wanyama wengi kwenye vyanzo vya maji. Vitendo hivi vya kuharibu mazingira (*environmental and water pollution*), husababisha kukosekana kwa mvua na kuleta ukame ambao unafanya mazao na mimea kukauka kwa kukosa maji pia mifugo hufa kwa wingi na kuleta baa la njaa na vifo kwa wanadamu.

Kutokana na kutojali kutunza vyanzo vya maji na vitendo vinavyosababisha mmomonyoko wa ardhi, sehemu nyingi kandokando ya mito, maziwa na bahari, zimekuwa zikikumbwa na mafuriko. Madhara yake yamekuwa makubwa kwa sababu mafuriko yanakumba mazao, mifugo na malisho kwa kuwa maji hukosa mwelekeo wa kufuata mkondo wake. Kuna tabia ya watu pia kuchafua vyanzo vya maji na kusababisha milipuko ya magonjwa kama kipindupindu na hata malaria kwa sababu uchafu hukuza mazalia ya mbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa maji, naomba nitoe kilio cha Wananchi wangu wa Jimbo la Kibaha Vijiji, ambao kila kukicha wanahakikisha wanatunza maji ya Mto Ruvu, kuhakikisha kwamba yanaendelea kuwepo kwa manufaa ya Wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha sana kuona Maji ya Mto Ruvu licha ya kwamba, chanzo chake kipo katika Jimbo la Kibaha Vijiji, lakini Wananchi wake wanaotunza mazingira ya Mto ule, wana matatizo ya maji. Maji ya Mto Ruvu yamepita Mlandizi kwenda kutumiwa na watu wanaoishi Kibaha Mjini na maeneo ya jirani na yanatumwa kwa wingi na Wananchi wanaoishi Dar es Salaam. Wananchi wa Kibaha Vijiji hawana tatizo na hilo kwani maji hayanyimwi mtu; tatizo lao kubwa ni wao kutopewa kipaumbele katika matumizi ya maji haya. Wananchi wa Kibaha Vijiji na hasa wale wanaoishi katika Kata za Mlandizi, Vijiji vya Vikuruti, Mande na Ruvu kwa Dosa, Kata ya Magindu, Ruvu, Kwala, Soga, Kikongo, Dutumi, Boko, Janga na Kilangalanga, wanakabiliwa na tatizo kubwa la maji safi na salama kwa matumizi yao ya kila siku. Wananchi hawa wamekuwa wakitegemea maji ya visima vya kuchimba kwa mkono, ambavyo ni vifupi, kwa hali hiyo maji yake siyo salama lakini wanatumia kwa kuwa hawana namna nyingine ya kuishi bila maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio hiki cha Wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijiji ni tatizo la muda mrefu; hivyo basi, naomba Mheshimiwa Waziri katika Bajeti hii awe muungwana na apange mipango mzuri ya kuhakikisha Wananchi wale ambao wamevumilia kwa muda mrefu, wameyatunza maji yale na kuyaweka mazingira mazuri, wakihakikishe mto ule uenaendelea kuwepo kutoa maji kwa Wananchi wa Kibaha na Dar es Salaam na maeneo mengine ya jirani,

wao wakunywa maji yasiyo bora na kutembea umbali mrefu kutafuta maji safi, nao sasa wanafaidika na maji ya Mto Ruvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mtovu wa skukrani kama sitatoa shukrani za dhati na kutambua juhudzi za Mheshimiwa Waziri wa Maji, kwa juhudzi zake za kutembelea vyazo mbalimbali vya maji, kuhakiksha Wananchi wanapata maji. Nimpongeze pia kwa kutembelea Jimbo la Kibaha Vijijini mapema mwaka huu, kwa madhumuni ya kuangalia maji ya Mto Ruvu na uhifadhi wake. Naamini kilio cha Wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini alikisikia na kwamba, bajeti yake ya mwaka huu, itawatatulia tatizo la kupatiwa maji ya bomba kama Wananchi wa sehemu nyingine. Natoa pia pongezi kwa Wizara yake, kwa kufanya Maonesho ya Juma la Maji Duniani, yaliyofanyika katika Viwanja vya Saba Saba, vilivyoko Wilaya ya Illemela, Mkoa wa Mwanza, kuanzia tarehe 16 hadi 23 Machi, 2011. Kaulimbiu ya Maonesho haya ilikuwa "Water: for cities: Responding to Urban Challenges, growing Urban water and sanitation demand, increased pollution from Municipal and industrial discharges, climate change and its foreseen risks and challengers, Overexploitation of available water resources and better targetting of urban poor." Natumaini pia walikumbuka Wananchi wanaoishi vijijini, kwani wao ndiyo hasa wanaotunza vyanzo vya maji haya waliyokuwa wakiyajadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe ombi kwa Serikali iware motisha Wananchi wanaojitolea kulinda vyanzo vya maji. Sambamba na hili, sheria ziimashwe ili ye yeyote anayefanya vitendo vya kuharibu mazingira au kuvuruga vyanzo vya maji au kuchafua maji kwa taka za aina yoyote ile; iwe sumu ya viwandani, taka za nyumbani na hata kutumia vibaya kwa mito, maziwa na bahari, basi watu hao wakikamatwa wafikishwe mahakamani na adhabu kali itolewe au iwekwe faini ya papo kwa papo. Faini hii inaweza kutumika kuwapa motisha Wananchi wa maeneo husika au kwa kufanya mambo ya Ustawi wa Jamii yatakayofaidisha sehemu husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kidogo pia matatizo ya usambazaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam. Ni jambo la kusikitisha kuwa mara kwa mara tumeona makampuni mengi ya kigeni yakifunga mabomba ya maji ili Wananchi wapate maji safi na salama ya bomba, lakini mara tu wamalizapo Mradi, mabomba yote ama mtandao wote hufeli na tatizo la maji linaendelea kuwepo pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, si adha tu ya kukosa maji, bali pia Wananchi wanakerwa na kupelekewa an kra za madai ya kulisipia maji wakati maji yenye wana yasikia kwa jina. Ningependa nifahamishwe hatua gani zinachukuliwa kwa wakandarasi hawa nawaopewa kazi na mara wanapomaliza kazi ile inakuwa hajakidhi haja. Mfano; mtandao wa mabomba ya Mchima ambao haufanyi kazi. Naamini uligharimu fedha nyingi, lakini matokeo yake Wananchi hawapati maji kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze sana kampuni inayosambaza maji katika Mji wa Moshi, Mkoani Kilimanjaro. Mara nyingi nimefika Moshi kila nyumba inabomba na mita ya kuonesha matumizi ya maji na mwisho wa mwezi kila nyumba inapokea ankara kufuatana na matumizi yaliyokuwa mwezi huo. Kama kukiwepo tatizo la maji au matengenezo yatakayoathiri mtandao wa maji, Wananchi wa sehemu husika wanapewa taarifa ya kuhifadhi maji ya akiba kwa matumizi ya siku hizo zenye matatizo; siku mbili kabla na baada ya tatizo kwisha huombwa radhi kwa usumbu uliokuwepo. Nashauri Mheshimiwa Waziri apange Programu ya kuwapeleka Wataalam na Mameneja wanaotoa huduma za maji katika mikoa mingine, wakatembelee Mji wa Moshi, Mkoani Kilimanjaro ili wakaone wenzao wanaotoa huduma ya maji kule wanafanya maajabu gani, kwani wenzetu kule hawazungumzii tatizo la upatikanaji wa maji ya bomba mjini wala vijijini na katika vitongoji kwani maji ya bomba yapo katika kaya nyingi hata kule vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kusema kwamba, kwa umuhuimu wa maji ni vyema basi Wizara ya Maji ikaweka mipango mizuri ya kutoa elimu kuhusu uvunaji wa maji ya mvua kwa Wananchi walio kati ka maeneo yanayokabiliwa na ukame mara kwa mara, kwani maji mengi ya mvua yamekuwa yanapotea na baada ya msimu wa mvua kwisha, Wananchi wamekuwa wakikumbwa na matatizo ya maji. Kwa hali ya duni ilivyo sasa hivi, kila tone la maji ni mali na halitakiwi lipotee bure; hivyo, Mheshimiwa Waziri ahakikishe Wananchi wanahamasishwa

kutunza kila tone la maji na kuelekezwa vifaa nafuu vya kuvunia na vinavyoweza kuhifadhia maji haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kuwa, bajeti hii imelenga kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi na kwamba, imelenga kutatua kero ya maji safi na salama kwa Wananchi bila kusahau wale wa Jimbo la Kibaha Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru na kuipongeza Wizara ya Maji kwa kutambua ukame wa Mji wa Dodoma na kusaidia kusambaza huduma za maji pande zote za mji na vijiji pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya maji katika Mji wa Dodoma, kwa sasa inatosha, lakini upatikanaji wa maji unakabiliwa na matatizo haya yafuatayo:-

Kwanza, ni miundombinu mibovu. Mabomba mengi ya maji yaliyopo yalijengwa tangu enzi za mkoloni, sasa yamechoka, yameoza na hupasuka daima pale nguvu ya maji (*water pressure*) inapozidi. Jambo hili husababisha upungufu mkubwa wa maji kwa kipindi ambacho Mamlaka ya Maji (*DUWASA*) wanapokuwa bado wanakarabati mabomba. Napendekeza kuwa mabomba yote ya Mkoloni, kwa vile yameoza, yang'olewe na kuwekwa mabomba mapya na imara zaidi kutoka chanzo cha maji cha Mzakwe hadi hapa Dodoma Mjini, ili mji uendelee kupata maji ya uhakika.

Pili, chanzo cha maji ya Mzakwe kina mwelekeo wa kuendelea kutoa maji hadi mwaka 2020. Baada ya hapa, visima vya Mzakwe havitakuwa na uwezo wa kutoa maji ya kutosha kwa matumizi ya Mji wa Dodoma na kumbe mji unaendelea kukua na idadi ya watu kuongezeka. Hapo barabara za Dodoma – Iringa, Dodoma – Babati na uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Msalato vitakapokuwa vimekamilika, idadi ya wakazi wa Dodoma itaongezeka maradufu. Ni vema Serikali ikafanya jitihada za haraka za kupata vyando vingine vya maji ili kuongeza wingi wa maji katika Mji wa Dodoma. Upanuzi wa haraka wa Bwawa la Farkwa (Kondoa) na utafiti mwingine wa maji katika nyika za Sulungai (Dodoma Magharibi), ungeweza kutoa jibu la haraka la kuuongezea Mji wa Dodoma maji ya kutosha. Lakini ni vizuri pia Serikali ikawa na mpango wa muda mrefu wa kuvuta maji ya Ziwa Victoria ambayo yangeweza kushuka kiurahisi kwa njia ya mteremko (*Gravity*) hadi Mkao wa Singida na baadaye Dodoma.

Tatu, pamoja na jitihada za Serikali kuchimba maji vijiji, Serikali imekuwa haifuatilii uhai wa visima hivyo. Hapa Dodoma Mjini kuna visima 18 ambavyo havifanyi kazi maeneo ya vijiji. Hii ni sawa na kusema kuwa hakuna maji safi na salama kwenye vijiji hivyo, kwa vile wananchi hawanufaiki na maji ya visima hivyo. Napendekeza Serikali itenye fedha ya kutosha katika bajeti yake ya kila mwaka, ili visima vipate kukarabatiwa na kutoa maji wakati wote.

Nne, maeneo mengine imeshindikana kuchimba visima kwa sababu wananchi ni maskini na hawana uwezo wa kuchangia mamilioni ya fedha ili Serikali ipate kuwachimbia visima. Napendekeza maeneo yote yenye hali mbaya ya uchumi vijiji, wananchi wachimbiwe visima vya maji. Baadaye watozwe pesa kidogo sana kwa kila ndoo ya maji kwa muda mfupi tu ili mchango wao upate kuonekana katika huduma ya maji, vinginevyo wananchi hao maskini watabaki miaka mingi bila huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja baada ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa hotuba yao yenye mwelekeo wa kutatua matatizo ya wananchi hasa wanawake katika tatizo la upatikanaji wa maji katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia yafuatayo:-

Kwanza, matumizi ya maji ya Bahari. Kwa kuwa Tanzania inakabiliwa na tatizo la maji katika maeneo mbalimbali na bahari huwa haikauki milele. Naishauri Serikali yetu iweze kutafuta fedha za kutosha na pia utaalalm wa kutumia maji ya bahari kwa matumizi ya kawaida kama kunywa, kilimo na kadhalika kama nchi nyiningine zilizoendelea zinavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ni gharama kubwa lakini Serikali lazima ione umuhimu wake maana maji ni uhai. Serikali iachane na miradi midogo midogo ya utafutaji maji na badala yake iamue kutumia utaalalm wa kubadilisha maji ya bahari (maji ya chumvi) na kuyaweka katika hali ya matumizi ya kawaida, hapo ndiyo Serikali itakuwa imemaliza tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali yetu ione umuhimu wa suala hili. Nchi yetu iepukane na ukame wa maji kama ilivyo sasa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri na yenye mwelekeo wa matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda kueleza matatizo makubwa yanayowapata wananchi vijiji kuhusu upatikanaji wa maji. Mradi wa vijiji kumi kila Halmashauri unaofadhiliwa na Benki ya Dunia unasuasua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wake hauridhishi ukizingatia ya kwamba mradi huu ulianza siku nyangi sana (2001) wakati gharama ziliwa nafuu na kwamba watu walikwischachangia mradi hii. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutafuta chanzo kingine cha fedha ili kukamilisha mradi huu?

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa hii ili niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia juu ya tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama vijiji na hasa katika Mkoa wa Singida. Mkoa wa Singida ni moja kati ya mikoa mikame katika nchi hii, Mkoa huu hupata mvua za msimu moja tu kwa mwaka na tena ambazo hazitabiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida una tatizo kubwa la maji kwa ajili ya binadamu na mifugo yao na hasa vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mji Mdogo wa Ikungi ambayo pia ni Wilaya mpya, kulichimbwa visima kwa msaada wa Japan lakini hivi sasa visima hivyo karibu vyote havitoi maji na hakuna jitihada zinazoonekana kuvifufua.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha vijiji karibu vyote vya Singida Vijiini vinakabiliwa na tatizo kubwa la maji mfano, katika Kijiji cha Mahambe wananchi wote wanategemea kisima kimoja tu. Hali hii inafanana karibu katika vijiji vyote vya Singida Vijiini, wanawake na watoto wanatumia muda mwingi kutafuta maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitaka Serikali ichukue jitihada za makusudi kuwaondolea wananchi wa Singida kero hii ya maji ukizingatia kuwa Mkoa huu ni mkame na haupati maji ya kutosha hata wakati wa masika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa tatizo la maji ni kubwa nchi nzima, lakini naitaka Serikali iweze kutoa vipaumbele katika maeneo ambayo yana tatizo kubwa la maji katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. BAHATI A. ABEID: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na wataalam wake kwa kuandaa mipango mizuri ambayo inawaletea wananchi maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai na ni afya, yakikosekana ni madhara makubwa sana kwani haiwezekani kiumbe yejote kukosa maji safi na akaishi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania walio wengi wa vijiji hawana maji safi hasa wale wa kipato cha chini na wakati mwingine visima vikichimbwa huwa havitoi maji. Hivi Serikali haioni sasa ipo haja ya kuanzisha Kampeni ya makusudi kuendeleza ujengaji wa matenki ya kuvuna maji ya mvua ili Watanzania hasa wale wa vijiji waweze kupunguza ukali wa upatikanaji wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itakubali ushauri huu wanawake wengi watapokea wito huo kwani wao ni waathirika wakuu wa tatizo hili la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi zinazoshughulikia maji zifanye ukarabati wa mabomba ili maji yasimwagike na yawafikie wananchi wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri kwa kuwasilisha vizuri hotuba yake ya bajeti, lakini katika majumuisho yake naomba mambo yafuatayo yapate majibu ya kina.

Kwanza, kwa nini Halmashauri ya Wilaya ya Lindi hajapewa kibali ili kusambaza miundombinu ya maji katika miradi ya *World Bank*, wakati uchimbaji umekamilika kwa zaidi ya miaka miwili.

Pili, je, Serikali ipo tayari kutoa kibali na kuielekeza Halmashauri kufunga pampu katika visima vya mradi wa *World Bank* katika vyanzo vilivyopatikana maji ili kufanya visima hivyo kuanza kutumika kwa muda?

Tatu, mradi wa majoribio wa uvunaji maji nashauri upelekwe kwenye shule ya Sekondari Mipingo na Milola.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Aidha, namshukuru Mungu mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha kuwepo katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze Waziri wa Maji na Umwagiliaji Profesa Mark Mwandoza kwa umahiri wake wa pekee katika kuiongoza Wizara hii. Aidha, nampongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Mhandisi Gerson Hosea Lwenge kwa umahiri wake wa kujibu maswali yahusuyo Wizara ya Maji. Naibu Katibu Mkuu kwa kazi nzuri ya utendaji pamoja na wataalam wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba naunga mkono hoja hii, lakini nina mambo kadhaa ambayo nahitaji kuchangia:-

Kwanza, katika Mji Mdogo wa Mbalizi mahali ambapo wakazi wake walio wengi ni wakulima na wafanyabiashara wachache, bei ya maji ni kubwa mno kiasi ambacho wananchi walio wengi hawana uwezo wa kulpia *Bill za maji*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwananchi hulipia maji kwa sh. 7500/= kwa mwezi, hiki ni kiwango kikubwa sana cha malipo, kumbuka kwamba mwananchi huyo ndiye ambaye anachangia ujenzi wa shule za Sekondari, Msingi, Zahanati na kituo cha afya. Naomba Serikali iangalie kwa upya gharama za maji katika Mji Mdogo wa Mbalizi.

Pili, Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alipofanya ziara yake mwaka 2009 Mbeya Vijiji aliwaahidi wananchi wa Kijiji cha Kikondo, Igoma, Santilya, Jojo, Illembu na Isuto kwamba watapewa maji ya Bomba. Aidha alipokuwa katika ziara yake ya kampeni mwaka jana pia alitoa ahadi ya kupewa maji wananchi wa Vijiji vya Kata ya Mshwewe hususan Njerenge, Mapogoro, Mjele na Chang'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kutekeleza ahadi ambayo Mheshimiwa Dokta Jakaya Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwaahidi wananchi wa vijiji nilivoyitaja.

Tatu, Mheshimiwa Naibu Spika, Mji Mdogo wa Mbalizi, Rais pia aliahidi kwamba Mji huo utapewa maji ifikapo mwezi wa Juni – Julai, 2011. Aidha, ahadi hiyo ilitolewa na Waziri wa Maji kwa niaba ya Rais. Naiomba Serikali kukamilisha ahadi ambayo ilikuwa *specific*.

Nne, Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa mwisho katika Wizara hii ni kuhusu mradi wa muda mrefu wa Igale – Iwindi.

Mradi huu alianza kuufuatilia Mheshimiwa Mwalyego ambaye kwa sasa hivi ni marehemu na hatimaye Marehemu Nyaulawa pia aliufuatilia kwa bidii zote lakini mradi hadi leo haujatekelezwa. Je, ni lini Serikali itautekeleza mradi huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri na mipango mizuri tulyoolezwa katika hotuba hii ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji, bado naiomba Serikali kufuatilia kwa karibu kazi hii muhimu ambayo inamgusa kila mwananchi. Miradi na ahadi za Rais zitekelezwe kwa haraka. Tusiwaachie wataalam wa Halmashauri tu bali tuwe karibu nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kwa kukubaliana na rai kwamba maji ni muhimu sana katika maisha ya watu na wanyama na ni rasilimali kuu katika kuendeleza sekta zote za maendeleo. Mchango wangu utahusu mambo yafuatayo:-

- (1) Matatizo ya kijumla.
- (2) Matatizo ya maji Jimbo la Bukombe

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na matatizo ya kijumla. Umuhimu wa maji katika maisha kwa jumla hauzingatii katika utekelezaji wa miradi ya maji. Tatizo kuu ni utovu wa umakini katika utekelezaji wa miradi na kutokamilika kwa miradi. Mfano mzuri, ni ule Mradi wa Wachina ambao ulitekelezwa katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam. Kazi iliyofanywa na Wachina hawa haikuwa makini na haijatimia. Ukamilishwaji wa mradi huu imegeuka ndoto na matumaini ya wananchi kupata maji yameshapotea.

Kutotimia kwa mradi huu kumewafanya baadhi ya watu kuanza kuwa na hisia kuwa mradi huu ulikuwa harufu ya rushwa. Tatizo ni kwamba kucheleweshwa kukamilika kwa mradi kumefanya miundombinu iliyowekwa imeanza kuharibika. Swali kwa Waziri, Mradi wa Wachina katika Jiji la Dar es Salaam utakamilika lini ili wananchi wapate maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niente katika matatizo ya Maji Jimbo la Bukombe. Jimbo la Bukombe linakabiliwa na tatizo sugu la maji. Kata zote 13 zina matatizo makubwa ya maji hasa wakati huu wa ukame mkubwa, ambapo karibu visima vyote vya asili/kawaida vimekauka. Nimepigwa simu na wananchi mbalimbali katika Kata zaidi ya 10 wakilalamikia tatizo hili. Wananchi wanahangaika sana kutafuta maji na shughuli nydingine muhimu zinaathirika kutokana na shughuli hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nitasemea mradi wa Benki ya Dunia na Mradi wa Maji katika Mji Mdogo wa Ushirombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Miradi ya Benki ya Dunia. Miradi hii ilianza kwa kuchimbwa visima 10 na visima nane ndio vilikutwa vina maji, visima viwili havikukutwa na maji. Miradi ilipoanza watu walipewa matumaini kuwa watapata maji muda si mrefu. Lakini kinyume chake kimetokea. Miradi hii imetelekezwa na matumaini ya wananchi hayapo tena. Swali kwa Waziri, Miradi ya Maji ya Benki ya Dunia itakamilika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Maji Mji Mdogo wa Ushirombo. Huu ni mradi wa Wizara toka mwaka 2008. Mradi huu ulikuwa ni sehemu ya mradi wa majisafi na majitaka wa Manispaa ya Shinyanga na Mji ya Maswa, Kishapu na Kahama. Mradi ulihiusisha shughuli ya upembuzi yakinifu, usanifu na usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za Zabuni. Kwa mujibu wa Waraka wa Wizara wa 2008, Kampuni zifuatazo ndizo zilipaswa kuhusika na mradi huu *GIBB Africa Limited, Natural Resources Consulting Engineers (Marekani) na Service plan Limited (Tanzania)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mujibu wa taarifa zilizopo, hatua za awali za upembuzi yakinifu, usanifu na usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni zimekamilika. Swali kwa Waziri, je, hatua za kukamilisha mradi huu zitatekelezwa lini?

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, katika tatizo la maji Jimbo la Kwimba, Jimbo ninalotoka si tatizo la kufanya mzaha kwani linatakiwa kuchukuliwa kama ni dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakazi wa Ngudu Mjini kununua lita 20 za maji kwa Sh. 500/= yanapopatikana. Wananchi wa Hungumalwa wanununa dumu moja la maji kwa Sh. 300/= mpaka 400=/. Wakazi wa Kata ya Ilula hasa wale wa Kijiji cha Manai hawana kabisa maji hata kwa kununua kwa bei yoyote. Wananchi wa Kijiji cha Manai wamekuwa wakichimba mabwawa bila utaalam wowote ilihali wapate maji ya aina yoyote hata kama yanakuwa na rangi kama ile ya chai ya maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri alichukulie tatizo la maji Jimboni kwamba kama dharura. Hivyo basi, namwomba Waziri wa Maji atembelee Jimbo la Kwimba afanye ukaguzi na ashughulikie dharura hii haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri aliyowasilisha leo. Namtakia uponyaji wa haraka ili aendelee na majukumu yake. Pongezi nyingine zimwendee Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji ni roho kwa maendeleo ya mwanadamu. Shughuli zozote zile ziwe za kilimo, ufugaji, uchimbaji wa madini zinahitaji maji. Ni kweli kwamba maji ni uhai. Katika mchango wangu nitajikita katika maeneo matatu yafuatayo:-

- (1) Hali halisi ya upatikanaji maji vijijini.
- (2) Ahadi ya Rais katika Mji wa Geita, Mji wa Katoro na Mji wa Nyarugusu.
- (3) Mradi wa *World Bank* wa vijiji 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na kipengele cha kwanza, upatikanaji wa maji safi na salama vijijini bado uko chini sana kulingana na Ripoti ya utekelezaji ya 2008 ya malengo ya *Millenia* ni asilimia 57.1 ya wananchi walioko vijijini wanapata maji safi na salama. Utekelezaji wa malengo haya bado yako chini sana ukizingatia kwamba mpaka mwaka 2015 utekelezaji unatakiwa kufikia asilimia 74. Ili tuweze kufikia malengo ya *millennia*, naishauri Serikali ielekeze nguvu kubwa miradi ya maji vijijini. Hii itasaidia wananchi wengi kuepukana na usumbufu mkubwa walionao sasa. Mfano, katika Jimbo la Busanda lenye Vijiji 76 ni Vijiji vitano tu ambavyo viko katika

mpango wa JICA na vijiji 70 kubaki bila huduma yoyote vijiji vitano vimechimbiwa jumla ya visima 15. Hivyo, mahitaji ya maji ni makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha pili kinahusu ahadi za Rais za mwaka 2010, aliahidi kuleta maji katika Mji wa Nyarugusu, katoro na Mji wa Geita. Ndani ya hotuba suaona mpango wowote wa kuleta maji Nyarugusu na Katoro. Mji hii ina idadi kubwa sana ya watu na miji hii haina vyanzo maalum vya maji. Watu wanahangaika sana kupata maji, wakati mwingine wanunua maji jambo ambalo linaweza kuleta athari kwa kutokea kwa magonjwa ya mlipuko. Hivyo, naomba Serikali iangalle namna itakayofanya ili kutekeleza ahadi ya Rais. Tunashukuru Mji wa Geita upo katika mpango. Naomba fedha zilizoahidiwa zipelekwe mapema ili mradi uanze kutekelezwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha tatu na cha mwisho ni mpango wa vijiji kumi wa maji unaofadhiliwa na *World Bank*. Mradi huu umekuwa wa muda mrefu sana bila utekelezaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Naomba Serikali katika bajeti ya mwaka huu ufanyike utekelezaji wa mradi huu ili wananchi wanufaikie kwa maji safi na salama kwa hayo machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Watendaji wote wa Wizara kwa hotuba yao nzuri pia inayotia moyo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa Maji asimamie vizuri vyanzo vya maji ambavyo vinaharibiwa na wananchi aidha kwa ujenzi wa nyumba au kilimo jambo ambalo nchi yetu inakuwa na tatizo la maji, baadhi ya sehemu ambazo wananchi wanatumia maji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubwa ya Dar es Salaam bado kabisa hawajafaidika na upataji wa maji kwa sababu wananchi wengi huwa wanunua maji kwa watu binafsi ambao wana visima vyao vya maji, maji ambayo yanauzwa dumu moja sh.200/= na baadhi ya sehemu yanazidi bei hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji yanauzwa kwa wananchi hao, wanayaita maji ya mwamba. Ni dhahiri kabisa bado wananchi hawajafaidika na matunda ya uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri achukue hatua za makusudi kufanya ziara ili ajue matatizo ya maji ambayo yanawapata wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Mark Mwandosya Waziri wa Maji, pamoja na Naibu wake *Engineer Lwenge* kwa kazi nzuri na kubwa katika kuhakikisha kuwa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri. Pole kwa maafa yaliyomfika Mheshimiwa Mussa Silima kwa kufiwa na Mke wake Mama Mwanakheri na Mungu amjalie kupona. Pia nampa pole Mheshimiwa Mwandosya, Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lwenge, Naibu Waziri nazidi tu kumkumbusha kuhusu lile suala la *billing system* ya maji mradi wa Mango, mradi uliofadhliliwa na *DANIDA*. *Support* hiyo ikipatikana, itakuwa chachu ya kuufanya mradi huo uwe endelevu. Wafadhili

wanatushangaa, kwa nini wanatupa miradi mizuri kwa pesa ya walipa kodi wao halafu mradi huo unakufa. Kwa ajili tu ya *poor management*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ni juu ya kero ya maji kwenye miradi mikubwa, hususan katika Jimbo la Peramiko. Mimi mwenyewe niliwahi kuhuduria kikao cha uhamasishwaji Peramiko njia ya kwenda Litisha. Tukaelimishwa kwenye mkutano wa umma na tukaelezwa na njia ya kusambaza maji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza ni kuwa kila siku mradi huu unaleta *Consultants* na Wataalam mbalimbali kutoka Dar es Salaam na nje ya nchi na hakuna kinachoendelea. Watu wamechangia karibu Sh.78,000,000/= mpaka leo hali ndiyo hiyo, kwa kweli hilo ni tatizo kubwa. Ni vema mradi huu uweze kutekelezwa kwa wakati. Lakini pia hivi hii miradi ya *World Bank* ni nini? Mbona imekuwa na usumbufu mwingu kuliko kawaalda?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, jambo linalofanana na hilo katika Mkoa wa Lindi, kuna matatizo makubwa ya maji. Bahati nzuri nimeishi sana katika maeneo hayo. Maji ya Lindi ni chumvi sana kiasi tu hata ukipikia maharage mpaka uweke magadi. Maji hayo hayafai hata kupikia wala kuoga katika hali ya kawaalda. Lakini katika eneo la Chikonji Manispaa ya Lindi, utakuta karibu kila familia ina shimo lake la maji, ni hatari kubwa. Maji ambayo yamekuwa *contaminated* na *other activities* kama vyoo. Lakini pia kuna hiyo miradi ya *World Bank* katika eneo la Namkongo, Likwanja, Kilomambwani na Lihimilo vilivypopo Lindi Vijiijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hizi zisipofanyika ni sawa na hujuma kwa Chama cha Mapinduzi, kama haiwezekani, basi wananchi wakaelimishwe haraka juu ya tatizo liliopo na sio kuacha mateso makubwa kwa wagombea uchaguzi wakati watu wa *executive* wamepumzika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa maji ni uhai na kwa kuwa miradi mingi ya maji vijiijini inayofadhiliwa na Benki ya Dunia imesimama, tena kuna vijiijini visima vimechimbwa, je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia kazi zilizobaki ili wananchi wapate huduma hiyo muhimu sana kwa maisha ya watu? Mashine nydingi za maji zimekuwa, naomba ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ina mpango gani wa kuzifufua au kununua mpya? Ni miradi gani ya maji itatekelezwa mwaka huu kwa Jimbo la Mtera?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna nchi iliyojaliwa na Mwenyezi Mungu kuwa na vyanzo vingi vya maji ya Bahari, Maziwa, Mabwawa, Mito na maporomoko ni Tanzania. Lakini pamoja na neema yote hiyo, bado kuna matatizo makubwa ya upatikanaji maji ya kunyweshea mifugo, umwagiliaji na matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ione haja ya kuweka mipango madhubuti ambayo itamaliza matatizo hayo kwa kutumia fursa zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie tatizo kubwa la maji liliopo Wilaya ya Kilombero licha ya Wilaya hiyo kuwa na vyanzo vingi vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji Mdogo wa Ifakara na viunga vyake una tatizo kubwa la maji. Kwa taarifa za hivi karibuni mji huo una ongezeko kubwa la watu sio chini ya 70,000 ambapo mahitaji ya maji yanapaswa kuwa lita 2.5 milioni kwa siku. Na kwa sasa visima sita (6) vilivypopo vinatoa lita 600,000 (laki sita) tu kwa siku ambapo hayatoshi kabisa na kutishia afya na maendeleo ya wananchi, kwa nini sasa Serikali ikaharakisha kumalizia mradi mkubwa wa maji ulioanza mwaka 2004, uliotumia bilioni moja kwa upembuzi na mwaka 2009 ulipata 2.2 bilioni ambazo ziliendeleza mradi huo hadi kujenga matanki matatu (3).

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo wa Mto Lumemo ambapo chanzo toka Kiburubutu pamoja na kutokilika mwaka huu wa fedha umetengewa Sh. 500.2 milioni ambazo ni za uhuishaji tu, Serikali haioni umuhimu wa kutenga fedha za kutosha ili kumalizia mradi huo ambao ulitolewa ahadi na Rais mwaka 2010 kuwa atamaliza tatizo hilo haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji Wilayani Kilombero ni kubwa si kwa Mji Mdogo wa Ifakara tu, zipo Kata na Vijiji vingi ndani ya Kata 23 ambazo maji kwao ni mafuriko na kuharibu miundombinu, makazi na mazao lakini mafuriko yakipita ni kero kubwa kwao kupata maji salama. Hivyo, Serikali haina budi kumaliza matatizo hayo kwa kutenga bajeti toshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Maji kwa kazi ngumu lakini nzuri ambayo Wizara inafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo napenda kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Kwanza, tatizo la maji katika Jimbo la Rombo. : Jimbo la Rombo lina tatizo kubwa sana la maji, jambo ambalo nadhani ndilo tatizo la msingi na kero kubwa kwa wananchi. Awali chanzo pekee cha maji kilikuwa ni Mto Itona ambacho kiko Marangu.

Hivi sasa chanzo hiki sio cha hakika kwani ujazo wa maji unaoingia katika tanki kubwa la Amboni kimepungua sana. Baada ya kutafiti tumegundua kwamba Kampuni ya Maji *Kilwater* iliweka *pump* katika bomba na kwa sababu *pump* hizo zina machujio ya uchafu mara nyingi huziba na kusababisha maji kupita kwa shida.

Kwa kuwa mimi binafsi nilitembelea bomba hilo na kutoa ushauri kwa Wahandisi na Halmashauri, naiomba sana Wizara itoe ushauri na au kuchukua hatua ili kurekebisha tatizo hili.

Pili, Kampuni ya Maji *Kilwater* Kampuni hii ilikuwa ikidhaminiwa na GTZ. Baada ya wahisani hawa kuondoka kampuni sasa inasusua na haitimizi malengo yake kwa sababu zifuatazo:-

(a) Haina mtaji wa kutosha kwa ajili ya kurekebisha miundombinu yake na hivyo kutegemea miundombinu ya zamani ambayo mtandao wake ni mdogo sana.

(b) Watumishi ambaio sio waaminifu. Mara kwa mara watumishi hawa wamekuwa wakifunga na au kugawa maji kwa upendeleo. Yapo maeneo ambayo hugawiwa maji kidogo yaliyopo mara kwa mara na yapo maeneo ambayo hayapati maji hata baada ya miezi mitatu. Naandika haya kwani malalamiko haya ni ya mara kwa mara na hatua hazichukuliwi. Ni matumaini yangu kwamba, Wizara itachukua hatua za kutoa maelekezo au hata karipio ili kero hii ikome.

Tatu, ni kuhusu Bwawa la Ikuini. Bwawa hili ambalo limejengwa katika ardhi yenyewe eneo la ekari 2.5, mali ya Halmashauri limeingia katika mgogoro wa kifisadi. Mwananchi mmoja Damas Tesha amejenga nyumba ya kuishi karibu na bwawa umbali usiozidi mita kumi. Madai yake ni kwamba eneo hilo ni mali yake alilobadilishana na Serikali ya Kijiji. Vipi kijiji kibadilishane na raia eneo la Halmashauri! Vipi Halmashauri inakaa kimya eneo lenye maslahi ya wananchi kama hili linapochezewa na je, sheria zinasemaje kuhusu umbali wa kujenga kati ya chanzo cha maji na makazi. Naomba jambo hili lishughulikiwe kwani imefikia hatua hata tajiri huyo hutumia silaha kuwatisha wananchi.

Nne, Mradi wa visima vya *World Bank*. Taarifa zimekuwa zikitolewa kwamba mradi huu umeanza na kwamba visima kumi na tano vitachimbwa. Naomba mradi huu uharakishwe kwani maeneo ambayo yamekusudiwa yana shida kiasi kwamba sasa maji yanatafutwa nchi jirani usiku na katika hatari ya wanyama wakali. Kimsingi katika ukanda wa chini Jimbo la Rombo hali ya upatikanaji wa maji na ukame ni ngumu sana.

Tano, maombi ya ujenzi wa malambo. Suluhisho la maji katika ukanda wa chini Rombo ni ujenzi wa malambo ili kutunza maji ya mvua ili yatumike wakati wa kiangazi. Kwa kuwa utafiti wa ujenzi wa malambo hayo umeshafanyika, tungeomba kujua ni lini hasa ujenzi huo utaanza na kukamilika.

Sita, matumizi ya maji ya Ziwa Chala. Maji haya yanatumika na wenzetu wa Kenya kwani ni ya pamoja. Katika majibu ya Serikali hapa Bungeni tuliambiwa kwamba utafiti unafanywa na mamlaka ya bonde la Pangani. Tungependa kujua utafiti huu utakamilika lini ili wananchi wa lambo wawe na matumaini ya kutumia maji hayo badala ya kuyaangalia tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja nikitumaini kupewa matumaini ya utatuzi wa baadhi ya yale ambayo yamewasilishwa.

MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchukua fursa hii kuchangia maoni yangu katika Wizara hii muhimu sana hasa kwa akinamama wa Kitanzania wanaoendelea kuteseka kwa adha kubwa ya kutafuta maji umbali mrefu mijini na vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunatambua kuwa "maji ni uhai" kama ilivyoainishwa katika hotuba ya Mheshima Waziri wa Maji ukurasa wa 112. Lakini hadi sasa Watanzania wengi tunaendelea kutumia maji yasiyo safi na salama kutoka kwenye visima vingi vifupi ambavyo vimechimbwa katika maeneo yenye msongamano mkubwa wa makazi. Kutokana na hali hii ugonjwa wa kipindupindu umekuwa ni wa kudumu hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya asilimia sita ya eneo lote la nchi yetu ni maji lakini hadi sasa Serikali imeshindwa kutumia vyando vyetu vikubwa vya maji vizuri kama Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa na mito kama Mto Ruvuma, Rufiji, Ruu na mengineyo na hivyo kuendelea kubuni miradi ya uchimbaji maji ardhini. Kama mradi wa vijiji kumi ambaao unafadhiliwa na *World Bank* ambaao umekuwa kero kwa Watanzania wengi hasa wanaoishi vijiji kwani miradi mingi imeshindwa kutekelezwa kwa wakati na kuwaacha wananchi wakiendelea kuteseka na adha ya kukosa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Maji wa Vijiji Kumi. Katika ukurasa wa 76 wa kitabu cha hotuba kinaonesha kuwa katika Wilaya niliyotoka ya Rufiji kuwa ujenzi wa miradi ya maji katika Mji wa Ikwiriri na Kibiti umefikia asilimia 96%. Sijui ni vigezo gani vimetumika kupima kiwango cha utekelezaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakazi wa Ikwiriri na Kibiti waliahidiwa na Waziri wa Maji Profesa Mwandosya toka mwezi Julai, 2010, kuwa miradi ingekuwa imekamilika na maji yangesambazwa kwa watumajji lakini hadi leo mradi haujakamilika na hatimaye tunaelezwa kuwa umefikia asilimia 96 hali ya kuwa hata hiyo miundombinu ya kusambazwa maji hajajengwa. Je, huu mradi kweli unaotaka kumkomboa mkazi myonyo wa Kibiti na Ikwiriri kuondokana na adha ya kutumia maji yasiyo safi na salama?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Miradi ya Maji inayoendeshwa na Mifuko ya *TASAF*, *SIROP* na *QUICKWIN*. Tunatambua juhudini zinazofanywa na Serikali kuendelea kutafuta wafadhili mbalimbali ili tuweze kuboresha hali ya upatikanaji wa maji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na ubadhirifu mkubwa katika pesa ama fedha za miradi ya maji zinazopelekwa katika Halmashauri zetu hapa nchini kutokana na masharti ya pesa hizo zinazopelekwa katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kutokana na masharti hayo magumu kuna baadhi ya fedha za miradi kama ya *QUICKWIN* zimekuwa hazitumiki kwa wakati, hivyo, kutowanufaisha wananchi kama tunavyotarajia. Fedha nyingi pia zimekuwa zikifujwa kwa kulipana posho kwa watumishi hasa Wahandisi wa Maji na mafuta ya magari badala ya kuingia katika utekelezaji ili Watanzania wanyonyo waweze kupata huduma hii muhimu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri au mapendekezo yafuatayo:-

- Kuendelea kutekeleza mipango endelevu ya ujenzi wa mabwawa ya kuvuna na kuhifadhi maji.
- Huduma za usambazaji maji zibin afsishwe kwa kupewa kampuni zenyne uwezo, utaalam na uzoefu wa kutoa huduma bora kwa wananchi.
- Serikali (Wizara) iendelee kufanya juhudzi za makusudi na za uhakika kuboresha miundombinu ya kusambazia maji ambayo mingi tumeirithi toka kwa wakoloni ili tuweze kupanua huduma ya maji kulingana na ongezeko la watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, namwombea kwa Mwenyezi Mungu Mheshimiwa Waziri Profesa Mark Mwандосya apate nafuu ama apone haraka ili tuweze kujumuika nae katika Bunge lako hili Tukufu. Ahsante.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza Waziri na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri na jitihada zao katika kutekeleza majukumu ya kuwapatia maji Watanzania hasa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ulanga Magharibi hasa wa Kata ya Ngoheranga ambao wamepewa bahati ya kupata mradi wa maji kuitia ufadhilli wa *World Bank*, lakini wataalam walipokuja kuchimba visima hawakufanikiwa kupata maji. Je, nini mbadala wa visima hivyo? Kata hiyo ina tatizo kubwa sana na huduma za maji. Wananchi wanaomba waelezwe na Serikali kuitia Wizara ya Maji hatima ya suala la upatikanaji wa maji baada ya mradi huu wa *World Bank* kushindwa kuchimba kisima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai, bila maji viumbe vilivyomo katika ulimwengu si rahisi kuishi. Binadamu anahitaji maji kwa asilimia 75% hata Madaktari husema kila siku mtu anywe maji kiasi cha lita moja na nusu tena yawe safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekte ya maji ni rasilimali muhimu katika maisha ya mwanadamu. Serikali inahitaji kuweka nguvu kubwa zaidi sehemu hiyo ili kuhakikisha kero ya maji inapungua kwa wananchi wake hususan waliopo vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania Mungu kajalia mabonde, mito, mabwawa na bahari, lakini cha kushangaza wananchi wanakosa maji safi na salama. Sehemu ambazo watu wanapata maji hasa vijijini, hayastahii hata kunywa mnyama sembuse binadamu. Maji ni machafu utadhani jivu lillotiwa maji wa kukorogwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingi za Tanzania maji ni mashaka kuyapata. Wanawake ni watu wanaoathirika, hutoka usiku au asubuhi, wapo kwenye foleni ya maji na wala hawayapati.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kubakwa limeshika kasi kwa kuwaharibu wanawake, watoto na vijana. Je, Serikali hamlioni hilo? Wenye nguvu huwapinga wanawake na kukinga au kuchota maji na kutia kwenye madumu ambalo dumu moja ni kati ya shilingi 500 hadi 700. Je, ni familia ngapi zenyne uwezo wa kununua maji hayo wakati wengi wao ni masikini, hata fedha ya mlo mmoja ni shida?

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwaka wa 50 tangu Tanganyika kupata uhuru, lakini hadi hii leo Tanzania haina maji ya kuwawezesha Watanzania kustarehe katika nchi yao. Maji yanatekwa kwenye vidimbwi, maji machafu, maji yallyotuwama ambayo si salama. Tanzania ina maporomoko ya maji ambayo yanapatikana katika Mikoa ya Iringa, Rukwa, Ruvuma, Mbeya, Kagera na Tanga ambavyo vyanzo hivi vingeweza kusaidia maji katika baadhi ya mikoa ya karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka za Maji zimeweza kutoa huduma za maji kwa watu 3,523,335 kati ya watu 3,962,650. Je, Serikali inazungumza nini juu ya watu 439,315 katika mamlaka 19 za Miji Mikuu ya Mikoa ambayo hawapati maji? Huu ni uonevu, ni vema Serikali ikajitahidi kuwapatia wananchi maji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi inakosa uchumi kwa sababu haina maji, umeme hakuna, mazao yanapungua. Ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia, kilimo kinakuwa kizuri kwa umwagiliaji wa maji, kama hakuna mvua na maendeleo ya nchi hayapatikani. Ni vema Serikali ikajenga mabwawa ya kutosha ya kuhifadhi maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mikataba. Kutokana na ripoti ya CAG ya mwaka ulioishia 30 Juni, 2010 inazungumzia juu ya mikataba mibaya inayoingiwa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mkataba ulioingiwa baina ya Wizara na M/S Nyakirangani *Construction Limited* kwa ajili ya ujenzi wa bwawa katika Kijiji cha Kawa, Wilaya ya Nkasi, ambao Mkandarasi kalipwa jumla ya Sh. 721,971,009/= kati ya sh. 1,092,868,644 ambayo kazi aliyopewa haikukamilika na kazi hii ilitakiwa ikamilike tarehe 9/5/2009 lakini hadi Novemba 2010 Mkandarasi hajakabidhi. Je, Wizara hamwoni kwamba fedha ya walalahoi ambao wanashinda na njaa, mnaowakata *tax* leo anaila mtu mmoja na wala hana huruma wala tija ya kupeleka nchi mbele? Namwomba Waziri atapokuja fanya majumuisho alieze Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iweke mikakati ya kuhakikisha kuwa rasilimali hiyo inaendelea kuwepo na kuwafikia watu kwa urahisi zaidi. Serikali iweze kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza na kusambaza rasilimali hiyo ya maji kwa wananchi kwa lengo la kuendelea kutatua kero zao pia kurahisisha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazojitokeza katika sekta ya maji ni:-

- Ukusanyaji hafifu wa Mifuko ya Maji katika vijiji vyenye miradi ya maji na vijiji ambavyo vimeomba kujengewa miradi ya maji.
- Ukosefu wa fedha za kutosha za ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji.
- Ukosefu wa fedha za usimamizi na ufuatiliaji miradi ya maji.
- Ukosefu wa vitendea kazi vya kisasa kama mashine za kuchimbia visima na vifaa vya upimaji (*survey*).
- Ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wa idara ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri ufuatao:-

- Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa miradi mipy ya maji.
- Serikali iwashirikishe wadau mbalimbali wajitokeze kusaidia ujenzi wa miradi ya maji vijijini.
- Serikali ijitahidi kwa nguvu zote juu ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama angalau kufikia asilimia 75% ifikapo mwaka 2015.

MHE. SALOME D. MWAMBU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja ya Wizara ya Maji. Naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya pamoja na ukubwa wa nchi yetu. Naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *World Bank* wa maji umekuwa ni kero kwa wananchi:-

(a) Wananchi wamechangia na kufungua *Account Bank*. Wanaona hawapati maji na tayari wameshajenga dhana kuwa fedha yao imeliwa.

(b) Wizara na Serikali haloni kuwa tunachelewesha maendeleo ya wananchi? Je, kama tuliweza kusimamia mradi wa maji mkubwa kutoka Ziwa Victoria na kuvuta hadi Kahama na kwa fedha zetu wenyewe kwa nini Serikali isitafute fedha popote na kuendeleza mradi huu wa *World Bank*? Naomba majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Iramba Mashariki, kuna Kata ya Matongo na Nkinto ambayo ina mwamba ambao huwezi kuchimba visima vifupi. Pia kuna mabwawa ya asili ambayo yamefukiwa na matope. Je, Serikali lini itafufua mabwawa hayo ili wananchi na mifugo wapate maji? Pia yatasaidia kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inapoteza maji mengi ya mvua wakati wa masika. Wizara inatakiwa itengeneze miundombinu ambayo itakuwa ya kudumu ambayo itakinga maji ya mvua na kuelekeza kwenye mabwawa mfano Mtera. Bado nchi yetu pamoja na mabadiliko ya hali ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, na nawasilisha.

MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutangaza awali kuwa naunga mkono hoja. Aidha, napenda kuipongeza na kuishukuru Serikali yetu kwa hatua inazozichukua kupunguza tatizo la maji Wilayani Newala. Moja kati ya matatizo yaliyosababisha kuwepo uhaba mkubwa wa maji Wilayani Newala ilikuwa ni ukosefu wa umeme wa kusukuma maji. Mwaka jana Serikali imeunganisha umeme toka Naliendele Mtwara (umeme wa gesi toka Msimbati) hadi vyanzo vya maji vya Milema, Mkunya na Mji wa Newala. Hali ya upatikanaji umeme ni nzuri maana hakuna mgao tena. Aidha, napenda kuipongeza Serikali kwa kufunga mitambo mipywa ya umeme kule Mkunya na mitemba. Pamoja na pongezi na shukrani hizo naomba ishughulikie masuala yafuatayo:-

Kwanza, naomba Wizara ikamilishe kufunga mitambo ya *booster station* unaojengwa kati ya Mkunya Bondeni na Makote. Sasa ni karibu miaka mitano tangu kuanza kwa mradi huu. Jengo na nyumba ya mtumishi imekamilika lakini mitambo bado kufungwa na kila ukiulizia unaambiwa mara mitambo iko bandarini au inaletwa.

Pili, baada ya umeme wa gesi kufika Newala, siku zingine tunaambiwa umeme umekuwa mwingi kiasi kuwa wanashindwa kusukuma maji. Kwa raia wa kawaida ni jambo ambalo haliingii akilini. Ni vizuri Wizara na Shirika la Umeme Tanzania wakalimaliza tatizo hili mara moja.

Tatu, pamoja na kuwa maji hayatoshi kuna upotevu mkubwa wa maji katika maeneo ya Mtopwa na Ngongo kwenye chanzo cha maji cha Mitema. Maji kumwagika ovyo lakini Mji Mdogo wa Kitangari haupati maji. Haya ya Wizara kurekebisha hitilafu zilizopo ili maji yote yanayozalishwa yawafikie watumiaji wa maji.

Nne, kuna maeneo mengi ambayo wakati Mradi wa Maji Makonde ulipoanza katika miaka ya hamsini ilikuwa inapata maji. Hivi sasa maeneo mengine kama vile Makukwe, Makonga, Naguruwe hayapati maji. Jitihada zifanyike kuhakikisha wanapata maji kama zamani.

Mwisho, wakazi wa Mji wa Newala wanaomba waunganishwe na chanzo cha maji cha Mitema ambako kuna maji mengi na ya uhakika kuliko chanzo cha maji cha Mkunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji kwa Vijiji Kumi katika kila Wilaya uliodhaminiwa na Benki ya Dunia hautekelezeki kwa kiasi kinachotakiwa. Hii ni kwa sababu muda mrefu sasa tumekuwa tukisikia habari za mradi huu, lakini pia bajeti zimekuwa zikipitishwa bila kutekelezwa hali inayopelekea wananchi wasiwe na imani kwa Serikali yao juu ya miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sababu hii muhimu na ya kukatisha tamaa namwomba Waziri atoe tamko juu ya mradi huu wa vijiji kumi na aeleze kwa ufasaha kwa nini kasi ya utekelezaji ni ndogo sana na nini ufumbuzi wa tatizo hili, kama haliwezi kutekelezeka ni kwa nini mradi huu usifutwe kabisa ili kuepuka kupitisha bajeti ambazo hazitekelezwi kila mwaka na wananchi wajue kama mradi upo au haupo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kwamba Tanzania tumebarikiwa kuwa na bahari, maziwa na mito mikubwa, bado kwa muda mrefu Watanzania wamekuwa wakipata usumbu mkubwa, hii ni kwa sababu tumekuwa tukitegemea Mataifa au Taasisi za nje kututekelezea mradi ya maji hali inayopelekea mradi ya maji isitekelezeke kwa wakati kwani hutoa pesa kwa muda waupendao wao licha ya kwamba tumekuwa tukipitisha bajeti kila kukicha.

Kwa mfano, mradi wa vijiji kumi kwa kila Wilaya unaodhaminiwa na Benki ya Dunia kwa Wilaya ya Kasulu, bajeti yake ilipitishwa mara kadhaa mwaka 2009/2010, 2010/2011 na 2011/2012, lakini mpaka sasa hakuna kijiji hata kimoja kilichotekeliza hali inayopelekea wananchi wasiwe na imani kwa miradi inayodhaminiwa na Mataifa ya nje. Namwomba Waziri atueleze ni lini Serikali itaamua kwa dhati kutenga bajeti kubwa ya ndani ili kutumia fursa tulizonazo kwa lengo la kuondoa kabisa tatizo la ukosefu wa maji kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule za Kata zimekuwa kimbilio kwa vijana wengi wa Kitanzania lakini upatikanaji wa maji kwa matumizi mbalimbali umebakili kuwa kitendawili kisicho julikana kitajibika lini, hali hii inahatarisha afya za watoto wetu na kuathiri kiwango cha ufaulu kwani kuna uwezekano wa kutokea kwa magonjwa ya mlipuko yanayoweza kurudisha nyuma juhudzi za walimu na wanafunzi katika elimu. Kwa hiyo, namwomba Waziri atueleze ni lini Serikali itahakikisha upatikanaji wa maji kwa shule zote za Kata hasa ukizingatia shule zingine zipo kwenye vijiji ambavyo havina maji, kwa mfano, vijiji vingi vya Jimbo langu la Kasulu vijijini.

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kupata wasaa wa kuchangia kwa maandishi hotuba iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba nimpongeze Waziri wa Maji na nimtakie afya njema, nimpe pole na maumivu yanayompata. Mungu ni mwema atampa heri na kurudi salama ili aje tuungane naye tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu maji Mkoa wa Geita. Mkoa wa Geita na Wilaya zake Nyang'hwale, Bukombe, Chato, Mbogwe kuna shida kubwa sana ya maji. Akinamama wanateseka sana kutafuta maji wanaamka usiku saa kumi kwenda kutafuta maji, wakitoka huku wanakuwa wamechoka hawawezi hata kufanya kazi nyininge.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali ituangalie kwa jicho la huruma tuweze kupata maji safi na salama katika Mkoa wa Geita, watu hawa kwa kweli wanateseka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Nyang'hwale tulikuwa na mradi ambaa ulituwekeea mabomba kutoka Ziwa Victoria. Katika Kijiji cha Nyamtokuza mabomba hayo yalitusaidia sana. Lakini bahati mbaya yalipoharibika yakatelekezwa na hakuna mtu aliyefuatilia mpaka yakawa mabovu yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali iweze kuyakarabati mabomba hayo ili yaweze kutoa maji wananchi waweze kupumzika na adha hiyo ya maji inayowapata wananchi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja.

MHE. ABDUL R. MTEKETA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpa pole ndugu yangu Profesa Mwandosya. Baada ya pole hiyo, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilombero ni Jimbo ambalo lina mito mingi na mabwawa mengi lakini kwa ajabu kubwa Jimbo hilo lina matatizo ya maji. Ukitaka kujua jiografia ya Jimbo hilo ni kwamba, lilikuwa na mito isiyokauka 79 hapo zamani lakini hivi sasa imebaki mito kati ya 39 au 40, yote hayo ni kutokana na uharibifu mkubwa unaofanywa katika vyanzo vya maji. Uharibifu huo unatokana na ukataji wa miti ovyo na mifugo ambayo imekuwa kero kubwa katika Jimbo hilo.

Katika Mji wa Ifakara ambaa umepata sifa ya kuwa Mji Mdogo na kwa sababu hiyo ni dhahiri idadi ya watu imeongezeka, shida ya maji imekuwa kero kubwa sana kwa wakazi hao. Naomba Serikali ilione hilo. Pamoja na juhudhi zilizofanywa na Halmashauri na nchi ya Swiss kwa kutaka kuleta maji kutoka Mto wa Kibuluguti, mradi wa maji ya kukinga umeshindikana, mradi huo mpaka hivi sasa unagharimu sh. 2.2 bilioni. Mradi huo ni mkubwa mno kufanywa na Halmashauri. Suala hilo pia linahusu Mlimba, Uchindile na Tanganyika Masagati. Kwa kuwa Jimbo letu ni oevu maji hupatikana siyo kina kirefu, naomba Serikali ituchimbie visima katika sehemu zote ambazo zina matatizo ya maji.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu nami nichangie bajeti hii ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumtakia Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya *a quick recovery* huko hospitalini ili arudi nyumbani kujumuika nasi katika ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kushukuru Serikali kwa kusikia kilio cha wananchi wangu na kupeleka chakula kingi Jimboni kwangu ili kuwanusuru wananchi katika njaa iliyowakumba. Ni matarajio yangu kwamba pamoja na njama za mafisadi kutaka kutorosha chakula hicho na kukipeleka Kenya, tumefanikiwa kwa kiasi fulani kudhibiti njama hizo na nashukuru kuona chakula kimeanza kuwafikia wa njaa Jimboni mwangu. Ahsanteni sana kwa hatua hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kusema siungi mkono bajeti hii. Wananchi wangu hususan wa Muhoji (Kata ya Bugwema), Sugiti, Mugango, Tageruka (eneo la Mayani, Lyamisanga, Buswahili (Wegero) Sironi Simba, Buhemba, Butuguri Shule ya Oswald Mang'ombe, Busegwe Shule ya Chief Ihunyo Butiama hususan kwa Mama Maria Shule ya Wasichana ya Chief Wanzagi, Kyabakari, Kata nzima watanishangaa sana wakisikia eti naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika maji ni uhai, wananchi wangu waishio katika maeneo yote haya niliyoyataja hawana maji. Wamekuwa wakililia bajeti hadi bajeti bila mafanikio yoyote. Kwa nini kila mwaka niendelee kuunga mkono bajeti kama hii ambayo haina tija kwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bwawa la Wagero nataka Serikali inisikie. Wananchi wangu wamenituma niyaseme haya. Wamechoka kusubiri ahadi zisizotekelzeza. Wamechoka na ujisadi katika Halmashauri ya Musoma. Wki iliyopita ilibidi niende Kiagata, Kata ya Buswahili, Kijiji cha Wegero. Nilichukua waandishi wa Habari ili wawaoneshe Watanzania wote waone ujisadi uliotendeka kwenye ujenzi wa Bwawa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nasema Musoma Vijijini haiko, itakuaje kama Bwawa kubwa kama hilo libomoke wakati bado likijengwa bila Idara ya Maji wala *DED, DC* au *RC* kujua?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Buswahili ndiko anakotoka Mheshimiwa Jaji Werema, Mwanasheria Mkuu. Ndiko anakotoka pia dada yangu Mheshimiwa Kabaka, Waziri wa Kazi. Hawa viongozi hawawezi kulisemea jambo bayo na la aibu kama hili. Ni lazima mimi Mbunge wao nilisemee. Sasa nimelisema. Watanzania mnasikia, wakazi wa Wegero mnasikia. Je, kweli Serikali iko Wilaya ya Musoma? Kwa nini Halmashauri isivunjwe kuundwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja hii. Pia nitatoa Shilingi moja kutoka kwa mshahara wa Waziri kwa uzembe uliofanyika Wegero.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vipindi vyote viwili vya Ubunge wangu nimekuwa nalia na Meremeta Buhemba bila mafanikio. Wakati Mheshimiwa Edward Lowassa akiwa Waziri Mkuu kwa kutambua uzito wa suala la Buhemba, alinipa Mawaziri watatu waende Buhemba kujiona wenye. Mawaziri waliofuatana nami walikuwa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandomsy, Waziri wa Mazingira; Mheshimiwa Steven Masato Wasira, Waziri wa Maji na Mheshimiwa Ibrahim Msabaha aliyekuwa Waziri wa Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri hawa watatu wakiwakilisha Serikali, bila shaka waliripoti kwa Rais. Matokeo *nothing doing*. Wakati tunakwenda kuona Buhemba, kila kitu kilikuwa *intact*, umeme ulikuwa unawaka, nyumba walimokuwa wakiishi wale Makaburu ziliikuwa kweli zinameremeta. Katika ziara hiyo Serikali iliniahidi mbele ya wananchi kwamba watalishughulikia suala la mazingira haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Buhemba imebaki hame. Vyanzo vyote vya maji vimejaa sumu (*Mercury*). Buhemba sasa ni *Time Bomb*. Serikali imekaa kimya. Hata Waziri Mkuu wa sasa wala Rais wanaona aibu kwenda Buhemba. Wananchi wangu wanalia. Serikali kimya, eti sasa wanasema wanaleta *STAMICO*. Eti sasa *STAMICO* imefufuka upya. Je, wananchi wafurahi? Kweli wana Buhemba watanufaika? Kwa lipi? Maji hakuna, barabara hakuna, Zahanati hakuna, Shule hakuna, Bajeti iliyotengwa na Wizara ya Maji kuhusu Buhemba hakuna, bajeti ya Wizara ya Mazingira inayohusu Buhemba hakuna chochote, kwa nini basi niunge mkono bajeti hii? Siungi mkono bajeti hii kata kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Maji Mugango, Kyabakari *Trunk Route Four (4)*. Tangu mwaka 2000 hadi sasa nimekuwa nikiomba Serikali ielekeze nguvu kubwa kwenye mradi huu. Mradi huu ni mionganoni mwa miradi mikubwa ya Kitaifa iliyobuniwa na Serikali ya awamu ya kwanza. Ndugu yangu Mheshimiwa Dokta Abdalla Kigoda amekwishesasemea umuhimu wa miradi hii ya Kitaifa. Sitaki kurudia rudia yaliyokwishesasemwa na mwenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuongeza kusema ni kwamba, mwaka huu Tanzania Bara inatimiza miaka 50 ya Uhuru tena eti Sherehe za kutimiza miaka 50 ya Uhuru zitafanyiwa Butiama alikozaliwa Baba wa Taifa, alipolazwa Baba wa Taifa. Nataka kuwaambia Watanzania wote wanaoniskiliza kwamba sherehe hii inayotarajiwa kufanyika Butiama ni usanii mtupu, Serikali hii haiko *serious* kuhusu Butiama. Vile aliyoyoviacha Baba wa Taifa Butiama (hususan Mwitongo) ni vile vile vilivypopo hadi leo isipokuwa uchakavu. Mazingira ya anakoishi mjane Mama Maria ni ya kusikitisha, Mradi wa Maji Mgango Kiabakari Butiama hadi Tringati yaani *Trunk Route Four (4)* ulishakufa. Mama Maria na wajukuu wake wote aliotuachia wanaishi kwenye hali mbaya na ya kutisha. Hawana maji, Hospitali aliyoiacha haina maji wala umeme. Mashamba aliyotuachia yamekatiwa umeme, zizi lake limetoweke. Tangi la maji aliloliacha pamoja na joshoa la kuoshea ng'ombe lilioko karibu na iliyokuwa Butiama *Artificial Insemination Centre (BAIC)* limeoza. Kwa miaka 10 ya Ubunge wangu sijawahi kuona *Veterinary* yoyote anatembelea joshoa hilo. Hii ndiyo hali halisi ya Butiama.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijisenti vyangu ninavyopata kutohana na posho za Ubunge ndivyo vilivyonisaidia kuchimba visima viwili, kimoja kwa ajili ya Mama Maria na cha pili kwa manufaa ya Kijiji cha Butiama. Ni kichekesho. Nasubiri kuona Sherehe za miaka 50 tangu tupate Uhuru zina manufaa gani kwa wana Butiama isipokuwa kuongeza huzuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri kwamba, ili kutunza historia ya Butiama nashauri Serikali ifanye sehemu yote ya Mwitongo hifadhi ya Taifa kama vile ilivyofanywa Olduvai Gorge au Ngorongoro Crater au Mlima Kilimanjaro. Kwa kufanya hivyo, fedha zinaweza kupatikana kuhifadhi mambo yote aliyoyaacha Baba wa Taifa kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali ilifikirie jambo hili kwa haraka iwezekanavyo ili mashamba ya Mwalimu, Bwawa la Kiarano, Mwitongo kwa Chief Wanzagi na Mwitongo alikolazwa Baba yetu Mwalimu zibaki *permanent record* ya Watanzania, Afrika na

ulimwengu mzima. Sioni kwa nini tusiige mfano wa watu wa India kuhusu Mahatma Ghandi au Mozambique kuhusu Machel.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, siungi mkono hoja hii.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa kazi nzuri ya kuwapatia Watanzania maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoonekana kuwepo sio maji bali ni juhudhi na mipango ya kutafuta maji, bado Serikali ina kazi kubwa ya kuhakikisha kuwa inawapatia Watanzania maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usalama wa maji. Hata kama maji yanayotoka Ruvu Juu na Ruvu Chini kuelekea Dar es Salaam yanapitia taratibu zote za usafirishaji yanapofika Dar es Salaam yanakuwa yamechafuka na hivyo sio salama kwa matumizi ya binadamu. Je, Serikali inachukua hatua gani kulinda afya za wana Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na shida ya maji Dar es Salaam. Dar es Salaam ni kioo cha nchi. Ili kupunguza tatizo la maji Dar es Salaam wananchi wameamua kuchimba visima vifupi. Tatizo liliopo hapa haijulikani maji haya ni safi na salama kiasi gani. Serikali inapaswa kwanza kuwashukuru wananchi wa Dar es Salaam kwa kuisaidia Serikali katika suala zima la maji, lakini vilevile lazima iandae mpango mkakati wa kufuatilia visima vyote vilivyochimbwa ili kuona kuwa ni salama kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusumfumo wa maji taka. Pamoja na kukamilika kwa ukarabati wa mabomba ya maji taka Dar es Salaam lakini bado maeneo mengi ya Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na Mbezi Beach, Magomeni, Manzese, Kijitonyama, Kinondoni, Sinza, Ubungo, Ilala, Temeke na Kurasini katika maeneo haya mfumo wa maji taka bado haujaunganishwa na hii ni hatari kwa afya ya wananchi. Je, Serikali inafanya jike katika muda mfupi ujao kuona kuwa majitaka yanadhibitiwa lakini hata yale yenye mfumo wa maji taka yanayoelekea baharini yanahatarisha maisha ya viumbe hai wa bahari. Je, Serikali inalishughulikiae tatizo hili ndani ya muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti iliyofadhiliwa na Benki ya Dunia 2008 inaonesha kuwa 70% ya nyumba za vijiji bado zinatumia vyoo vya asili ambavyo havina huduma za maji na 83% hawana huduma za maji hata ya kunawa mikono kwenye vyoo vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mpango wa Taifa wa kusambaza huduma za maji vijiji (*NWSSP*) tathmini ilikuwa ni kwamba mpaka kufikia 2010 huduma za maji vijiji itakuwa imepatikana kwa 65% na itakapofika 2015 huduma hiyo itakuwa inapatikana kwa 74%. Ni kwa nini malengo hayo hayakufikiwa kwa 7.2% ya lengo la mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tafiti zilizofanywa na Tamizne na Perez Fogmet zinavyosema, hakuna haja ya kuwa na makadirio ya kuimariika kwa huduma ya maji ukilinganishwa na kuongezeka kwa kutokutenda kazi kwa miradi mingi ya maji (*high rate of non-functionality*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima iondoe urasimu katika utekelezaji wa miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu wengi kupongeza Wizara kwa kazi nzuri mnayoifanya. Mungu awabariki sana. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ila naomba mziangalie hoja mbili za Wilaya ya Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kilombero katika Mji wa Ifakara, miundombinu iliyowekwa ya Mamlaka ya Maji ni ya watu 7,000 katika miaka ya 1980.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi Mji wa Ifakara una wakazi zaidi ya 100,000! Kuna vyuo kama nane (8), kuna shule nyingi, hospitali na mifugo mingi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya Mamlaka ya Maji Ifakara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali mbaya sana katika mji huo inaweza ikasababisha mlipuko wa magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Kilombero imepeleka maombi maalum ya kuboresha miundombinu hii chakavu Hazina na TAMISEMI lakini majibu bado hayajapatikana. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atuonee huruma tupate pesa za mradi wa Kiburubutu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilombero tulipewa visima 14 vya mradi wa *World Bank* kwa Vijiji vya Mlimba A, Mlimba B, Karuwere, Naawawahe, Idete na vingine vya Mbwa, maji yapo bado miundombinu tu. Tunaomba miundombinu iwekwe ili visije vikajifukia.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nianze mchango wangu kwa kumpa pole Mheshimiwa Waziri Profesa Mark Mwandosya kwa maradhi aliyoyapata. Tunamwombea kheri. Pia niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri *Engineer Lwenge*, Katibu Mkuu, *Engineer Say* pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa hotuba yao waliyoiwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai, bila maji hakuna jambo linaweza kufanikiwa lakini maji limekuwa tatizo lisilotatulika kwa urahisi hasa katika vijiji vyetu hapa nchini. Akinamama wengi sana wamekuwa wakipata matatizo makubwa sana kuhangaika huku na huko mpaka kusababisha kushindwa kufanya kazi za maendeleo. Inasikitisha maji yameshatishia mpaka ndoa za akinamama wengi kuwa hatarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, yametokea maradhi mbalimbali ya mlipuko sababu ya maji. Naiomba Serikali itoe kipaumbele kama ilivyotoa kwa Wizara ya Nishati na Madini kwa suala la umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyanzo vya maji. Vyanzo Vingi vya maji vinaharibiwa ovo. Serikali haijasema lolote kuhusu motisha kwa wananchi wanaotunza ili visiharibiwe. Naomba Waziri atakapokuwa anajibu atueleze kuhusu mkakati wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Serikali haijasema lolote kuhusu motisha kwa wananchi wanaovituma ili visiharibiwe na kuhakikisha vyanzo hivyo vinatunzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, urasimu wa miradi ya maji. Kumekuwepo na urasimu mkubwa sana katika miradi hii ya maji katika Halmashauri nyingi hapa nchini mpaka kusababisha pesa nyingi kutumika katika kufanya utafiti, kwa kuwa upo utaratibu wa kuwalipa wataalam wa kufanya utafiti kabla ya uchimbaji wa visiwa hivyo. Lakini visiwa vingi pamoja na kufanyiwa utafiti na kulipa pesa nyingi hakuna maji yanayotoka na mtaalam huyo analipwa pesa zote je, huo sio uharibifu wa pesa za miradi hiyo ya maji. Kwa nini wataalam hao wasilipwe nusu ya malipo kwanza ili maji yakiwepo ndio amaliziwe malipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji taka. Mifumo ya maji taka hasa kwa Mkoa wa Dar es Salaam mingi ni mibovu sana mpaka kusababisha mji kutapakaa kwa maji barabarani na kutoa harufu mbaya wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshashuhudia mabomba ya maji taka yakiunganishwa na mabomba ya maji safi (Kata ya Buguruni), hii ni hatari sana kwa maisha ya binadamu. Ningeomba pia Serikali ichukue hatua kali kwa wananchi wanaojiunganisha maji bila kibali cha DAWASCO.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia *bills* zote ziangaliwe, kunakuwa na malalamiko ya kupewa *bill* kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naiomba Serikali itenye Fungu kubwa kwa ajili ya miradi ya maji ili tusitegemee sana pesa za wafadhili kwani zinasababisha kuchelewa kwa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na nichukue fursa hii kumpongeza sana Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii kwa hotuba yake nzuri pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote waliohusika kwa njia moja au nyine katika uandaaji wa hotuba hii ya bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna kero kubwa Wilayani Nanyumbu ni uhaba mkubwa wa maji. Karibu kila kitongoji, kila Kijiji Wilayani Nanyumbu, tatizo kubwa ni la maji. Wananchi hawana maji. Wananchi Wilayani Nanyumbu wanahahaha huku na huko kutafuta angalau ndoo moja ya maji. Akinamama wanatembea kutwa nzima kutafuta maji. Wanaamka alfajiri ya saa tisa (9) hata saa kumi (10) alfajiri kutafuta maji. Wananchi wa Nanyumbu tuna tabu kubwa ya kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri atakapofanya majumuisho atueleze Wananyumbu, Serikali ina mpango gani mkakati wa kututua au kumaliza kero ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Kikwete alifanya ziara Wilayani Nanyumbu tarehe 28/07/2011 na kilio kikubwa kilikuwa ni maji na kuagiza Serikali itafute ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Ruvuma wenyewe kutiririsha maji mengi unapita Wilayani Nanyumbu. Ni mto pekee unaokuwa na maji muda wote. Naiomba Wizara ipeleke nguvu zake kwenye Mto Ruvuma kama suluhisho la tatizo ya maji Wilayani Nanyumbu kwa kujenga mradi mkubwa wa maji kama ule wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Kata za Mikangaula, Maratani na Nandete nisngeshauri pajengwe malambo makubwa yatakayotunza maji mengi, hiyo kupunguza tatizo la maji katika Kata hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ya Mto Ruvuma, ambayo yanatiririsha maji baharini yangeweza pia kutumika katika miradi ya umwagiliaji kwenye vijiji vilivyopo kandokando ya mto, hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Lakini maji hayo ya Mto Ruvuma yanaishia baharini tu bila tija yoyote. Naiomba Wizara ianzishe miradi ya umwagiliaji katika bonde la Mto Ruvuma, Wilayani Nanyumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma tumekuwa na Baraka ya Ziwa Tanganyika, Ziwa ambalo ni la pili kuwa na kina kirefu duniani ambalo linatoa 17 percent ya maji baridi yote duniani. Lakini la kusikitisha ni kwamba, wakazi wa Mkoa wa Kigoma hawapati maji kwa kiwango cha kuridhisha. Je, Waziri anatwambia ni sababu gani zinapelekea adha hii hasa kwa wakazi wa Ujiji, wakazi ambao Ziwa lipo takriban mita mia mpaka mia mbili kutoka maeneo yao. Je, tatizo ni nini Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni kitu muhimu sana katika mahitaji yote ya mwanadamu, pia maji ni uhai. Lakini ni uhai kama yatakuwa safi na salama kwa matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mpango wa maendeleo wa mwaka 2010/2011 wa utekelezaji wa miradi ya maji safi na maji taka katika vijiji kumi kwa kila Wilaya lakini bado hali ni mbaya hasa Vijiini na Mijini pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa na Katavi kuna vijiji ambavyo wananchi wanaishi utadhani sio Watanzania kwa jinsi walivyosahaulika kwa kila kitu. Nikianza na Mpanda Vijiini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpanda Vijiini kuna vijiji ambavyo Serikali ilijaribu kujenga visima lakini vinahitaji marekebisho kutokana na kubomoka au kutitia. Vijiji hivyo naomba nivitaje, ambavyo ni Igalula, Itunya, Kapalamsenga, Katuma, Illebula Majalila, Mpembe, Kabungu na Mishamo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna vijiji ambavyo havina maji wala visima kabisa, ni vijiji ambavyo Serikali imevisahau na wanaopata shida kubwa ni akinamama wanaohangaika kufuata maji kwa umbali mrefu vijiini kutafuta maji. Naomba nivitaje vijiji hivi, ni pamoja na Sibwesa, Kagunga, Kamsanga, Ngoma Lusambo, Kafisha, Mnyagara, Kakese, Fikonge, Kambanga, Kapanga Mchakamekaka, Igagara, Ikaka na Sijonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ndiyo vijiji hasa ambavyo havina kabisa maji wala visima na wananchi wake wanaishi ili mradi tu waliumbwu. Wananchi hawa ndiyo wazalishaji wa chakula wakiwemo vijana ambao ndiyo tegemeo la Taifa. Sasa je wasipopata maji safi na salama tunawajenga au tunawaua?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naiomba Serikali kuitia Wizara hii, iweke mikakati ya kazi, hawa wote maafisa wa idara za maji, kazi yao sio kukaa tu ofisini kusaini *cheque* au kufuatilia *bill* za maji, hapana! Wajitahidi kutoka kufuatilia kuona shida za maji wanazopata wananchi mijini na vijiji, walipa kodi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu sana miaka hamsini ya uhuru bado wananchi wanahangaika na ndoo mikononi kuhanganya kutwa kutafuta maji kwa matumizi ya kawaida. Je, mashamba ya umwagilaji yatawezekana?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata kuhoji pesa za miradi ya maji, baada ya kukuta wananchi wa Kijji cha Chamalendi kilichopo Tarafa ya Mpimbwe wanafukua mchanga kwa jembe la mkono ili wapate maji ya kutumia kwa ukosefu wa visima, wakipata maji hayo ambayo yana rangi kama maziwa, hayo hayo wanachangia kunywa na ng'ombe. Huu siyo uhai tena, bali ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mpanda Mjini na Vijiini tumechoka kuumwa *typhoid* kila kukicha. Tunaua nguvu kazi ya Taifa. Vijana wanashindwa kufanya shughuli za uzalishaji mali kama kilimo cha umwagilaji kwa kukosa maji na hapa ndiyo mwanzo wa vijana kukosa mwelekeo na badala yake kukata tamaa na kushawishiana kuijunga na vikundi visivyo na maana kama uvutaji bangi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema naomba majibu kutoka kwa Waziri. Ni lini sasa wananchi wa vijiji nilivovitaja watajengewa visima ili na wao wapate unafuu wa maisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji limekuwa kubwa sana nchi nzima, kuanzia Dar es Salaam hadi mikoani na inaonesha Serikali imeshindwa kutatua suala hili. Wingi wa watu unazidi nchini lakini kila siku zinavyokwenda maji yanazidi kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitazungumzia Jiji la Dar es Salaam, kila sehemu watu wamejenga visima na sijui hawa watu wamepewa vibali au wamechimba tu hivi visima na pia wamepewa elimu ya kutosha ambayo ni ile kila muda fulani maji haya yanatakiwa kutiwa dawa. Licha ya hayo, hivi visima kuwa vingi vinaharibu mazingira na uwezekano wa kupata mmomonyoko wa ardhi Dar es Salaam unaweza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule vijiji maji wanayopata mengi ni machafu si ya kutumia binadamu, lakini wafanye nini inabidi watumie hayo hayo maji machafu na hii inawafanya wasiwe na afya nzuri na kupata matumbo ya kuhashira kila mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huku vijiji naishauri Serikali kuchimba visima vidogo kwa kuwataka wananchi wachangie nusu ya thamani na Serikali itoe nusu ya thamani. Halmashauri za vijiji zikusanye hizi fedha kwa kila nyumba 100 au nyumba 150 kwa kila mkaazi atoe elfu tano (5,000/=). Naamini zikikusanya pesa hizo na Serikali ikisaidia basi kwa kiasi kikubwa shida ya maji itapungua vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bajeti iliyotengwa ni kidogo mno hizo fedha zisimamiwe vizuri kwenye miradi ya maji na mamlaka ya maji jijhushe zaidi kwenye usambazaji wa maji kuliko kuwekeza katika uzalishaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitaka Serikali iwe na mikakati madhubuti ya maji ili bajeti inayokuja angalau tupike asilimia 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ni siku, naamini huu ushauri ulioutoa wa kujenga visima vidogo vidogo vijiji utauzingatia na nakuomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho ueleze kwamba ushauri huu umeupokea.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tatizo la maji Kibondo. Napenda kupata majibu kutoka kwa Waziri, ni lini Kibondo kutakuwa na maji? Ni aibu kwa Wilaya kama hii ya hata kabla ya uhuru kuwa na tatizo sugu la maji. Pili, kwa nini wananchi watozwe Sh. 20/= kwenye kila lita 20 za maji na matumizi ya pesa hizo hawajafahamu wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kibondo kuna tatizo la maji Kata ya Mabamba, Kibondo, Misezero, Murungu, Kizasi, Busagara, Kumsenga na kadhalika. Hivyo, ni lini tatizo hili litakwisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tatizo la maji nchini na miradi mikubwa ya kutatua kero ya maji nchini. Napenda kupata majibu ni lini Serikali itakuja na mipango mikubwa kama ule wa Rais Mstaafu Benjamini William Mkapa wa kutoa maji Mwanza hadi Kahama. Je, lini tutakuwa na miradi mikubwa kama hii ya kutoa maji Ziwa Tanganyika kusambaza Mikoa ya Magharibi, Ziwa Nyasa Kusini, Victoria Kanda ya Ziwa, na Bahari ya Hindi Mashariki?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Miradi ya Maji Vijiini. Napenda kupata majibu kwa nini miradi ya vijiji kumi kwenye kila Wilaya haikamiliki. Je, sababu ni nini na kwa nini Serikali (Wizara) imeachia zoezi hili Halmashauri na ikifahamu kwamba kuna Halmashauri nyingi zinakwamisha zoezi hili? Kwa nini jambo hili lisimamiwe na Wizara moja kwa moja?

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, napenda kupata majibu, kwa kuwa Wilaya ya Kibondo ina tatizo la maji na Rais anafahamu hivyo na Idara ya Maji ya Wilaya hiyo imekuwa ikipata hati chafu. Je, ni fedha kiasi gani zimepotea, kukusanya na hatua gani zimechukuliwa?

MHE. MARYAM S. MSABAHA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mradi wa maji vijiji. Miradi ya maji 4,134 iliyopo vijiji mpaka sasa bado ni kidogo sana ikilinganishwa na mahitaji ya wananchi wote walio vijiji vyote 13,000 nchi nzima. Wanawake wengi ndiyo wanaoathirika na tatizo hili la maji kwa kuwa wanatumia muda mwangi kwenda kutafuta maji. Asilimia 75 ya wanawake ndio wanaohangaika kuhusu suala hili la utafutaji wa maji na wamekuwa wakikumbana na matatizo mbalimbali kama kubakwa kwa sababu wanawake hawa wanaamka mapema sana asubuhi kwenda kutafuta maji

na tatizo hili la maji linachangia hata baadhi ya ndoa kuvunjika kwa sababu wanatumia muda mrefu sana na waume zao wanakuwa hawaamini, hivyo, inasababisha ndoa kuvunjika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vyanzo vingi nya maji huko vijiji ni salama. Wananchi hawa wanatumia maji hayo ambayo si salama kwa matumizi mbalimbali kama kupikia, kunywa, kuogea na maji haya haya ndio wanyama wanayatumia kwa kunywa. Hivyo basi, maji haya ambayo si salama yanababisha wananchi hawa kupata maradhi mbalimbali kama homa za matumbo, *typhoid* na malaria kwa sababu ya mazalia ya mbu yaliyoko kwenye maji hayo. Kwa kuwa suala hili la maji limekuwa ni tatizo sugu na wananchi wamekuwa wakiliulizia sana na hatimaye kuishia kwenye makaratasii ili wananchi wawe na imani na Serikali yao. Je, Serikali ina mpango gani kuhusu kutatua suala hili la maji kwa vitendo huko vijiji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la maji katika Mji wa Dar es Salaam. Kwa kuwa Mji huu wa Dar es Salaam umekuwa na ongezeko kubwa la watu na msongamano wa nyumba. Hivyo basi, katika mji huu kumekuwa na tatizo la upatikanaji wa maji safi. Matajiri wengi katika Mji huu wa Dar es Salaam wamekuwa wakimiliki vyanzo nya maji na kujichimbia visima vyao wenywewe katika nyumba zao. Hii inachangia tatizo la upatikanaji wa maji safi katika Mji huu wa Dar es Salaam. Ukubwa wa shida hii unatokana na ukweli kuwa mahitaji ya maji katika Mji wa Dar es Salaam ni kiasi cha mita za ujazo 450,000 kwa siku lakini mpaka sasa kiasi cha maji kinachopatikana ni mita za ujazo 300,000 ikiwa ni upungufu wa mita za ujazo 150,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 50 ya maji yanayozalishwa hupotea kwa sababu ya uchakavu wa miundombinu na wizi wa makusudi wa maji unaofanywa na baadhi ya watu wanaojunganishia maji kinyume cha taratibu kwa maslahi yao binafsi. Je? Serikali sasa haioni kama kuna umuhimu wa kutenga fedha za kutosha katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kuharakisha uchimbaji wa visima kwenye maeneo mengi yenye shida kubwa ya maji katika Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza hili tatizo na huku miradi mikubwa kukamilika? Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu kwa kuchunguza na kudhibiti wizi na upotevu mkubwa wa maji katika Mji wa Dar es Salaam kwa kuhakikisha inakarabati kwa haraka miundombinu chakavu na kuwachukulia hatua wale wote walioingilia mfumo wa bomba kwa kujunganishia maji kiubin afsi hata kusababisha wakazi wengi wakose maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko mengi ya wananchi kuhusu *DAWASA* na *EWURA* idhibiti matumizi ya bei ya maji kwenye miradi iliyopo chini ya Jumuia za wananchi kwani tafiti zinaonesha kuwa inadumu hulipia mara 15 zaidi kuliko Yule anayehudumia maji ya bomba. Serikali ihakikishe kampuni ya usambazaji maji Dar es Salaam (*DAWASCO*) inatekeleza kikamilifu mapendekezo yote yaliyotolewa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali toka mwaka wa fedha 2007/2008. Naishauri Serikali kuhusu viongozi na watendaji wote waliosababishia *DAWASCO* hasara ya shilingi bilioni 12.6 wasimamishwe mara moja na kuchukuliwa hatua kali za kinidhamu na kisheria. Wizara ishirikiane na mamlaka za Serikali za Mitaa, Asasi Zisizo za Kiserikali na vyombo vya dola ili kudhibiti biashara ya vyuma chakavu na kuelimisha wananchi kulinda miundombinu ya maji isihujumiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huu mradi wa maji na Benki ya Dunia. Mradi huu umekuwa ukilalamikiwa na wananchi hasa wa vijiji. Wananchi wengi wameuchangia mradi huu hadi sasa hawajanufaika nao na hawajui fedha zao walizozichangia zipo wapi, ulikuwa ukilalamikiwa na wananchi hasa wa vijiji. Wananchi wengi wanauchangia mradi huu lakini hadi sasa hawajanufaika nao na hawajui fedha zao walizozichangia ziko wapi. Namwomba Waziri atakapokuja kutoa majumuisho aniambie mradi huu uliishia wapi na fedha za wananchi walizochangia katika mradi huu ziko wapi na ni kwa nini mpaka sasa hivi vijiji hivyo havijapata maji? Mfano mzuri ni Wilaya ya Hanang ambapo kwenye Viji ya Katesh, Gihandu, Mng'enyi na Mirongori kwa mwaka 2007/2008, ruzuku ya maendeleo (*Capital Development Grants CDG*) na fedha za program ya maji kwenye vijiji 10 (*WSDP*). Zimekuwa zikitengwa kwa ajili ya maji kwenye maeneo hayo takriban kila mwaka lakini bado maji ni shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa Mifuko ya *TASAF*, *SIROP*, *QUICKWIN* na wafadhili wa ADRA walishatekeleza miradi kwenye maeneo hayo. Jambo la kujuliza ni je, fedha zilizotengwa na Serikali kuu, Halmashauri pamoja na wafadhili hao zilikwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hoja endapo nitapatiwa majibu kwa haya yote niliyoyachangia kwa maandishi hapo juu.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii kwa maandishi. Nampongeza Waziri wa Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yao ya watendaji kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii. Natamka kuwa naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kauli mbiu ya Wizara hii ya Maji inavyosema, "Maji ni uhai na usafi wa mazingira ni utu". Naipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanya ya kuwapatia wananchi wake (wa Mjini na Vijijini) maji safi na salama kupitia miradi na program mbalimbali. Hata hivyo, mahitaji ya maji kwa matumizi ya binadamu, mifugo, kilimo na viwanda ni makubwa kuliko uwezo uliopo wa rasilimali pesa. Ndio maana hatuna budi kama nchi kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wetu, kuongeza pato la Taifa na hivyo kuiwezesha Serikali kutoa huduma hii muhimu kwa wananchi, hasa ikizingatiwa kuwa miradi ya maji ina gharama kubwa za uwekezaji na uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua jiolojia na haidrolojia hasa kwenye maeneo kame, ikiwemo Wilaya ya Bariadi nashauri Wizara ya Maji ije na mpango kamambe wa uchimbaji wa visima virefu na uchimbaji wa visima hivyo utee kipaumbele cha kwanza kwenye maeneo kama ya vijijini yaliyo na idadi kubwa ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila kilio kina wenyewe. Kilio changu kinahusu mahitaji ya maji katika Mji Mdogo wa Bariadi. Mji Mdogo wa Bariadi ni mionganini mwa Mji inayokua haraka sana na kwa sasa una wakazi wanaokadiriwa kuwa elfu sitini (60,000). Idadi hii ya watu ni kubwa kuliko uwezo wa vyanzo vya maji vilivyopo. Tegemeo la mji mdogo wa Bariadi ni Bwawa la Mto Bariadi ambalo sasa limejaa tope na hivyo uwezo wa kutunza maji umepungua sana. Kuna mradi wa Chujio, ujenzi wa matenki ya kuhifadhi maji na miundombinu ya kutiririsha na kusambaza maji ambaa unakaribia kutimiza miaka kumi bila kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wakati anahitimisha hoja yake awaeleze wananchi wa Mji Mdogo wa Bariadi, mradi huo utakamilika lini na gharama ya mradi wote ni shilingi ngapi? Wananchi wamechoshwa na maelezo ya kila siku kuwa Halmashauri ya Bariadi iangalie uwezekano wa kutumia fedha za DADPS, wanataka maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kutohana na hali hiyo tete ya upatikanaji wa maji Mjini Bariadi iliyowafanya wananchi kumwomba Rais Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa kampeni mwaka jana, Serikali yake iangalie kwa haraka uwezekano wa kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria na kuyaleta Bariadi (kilometra 65) ili kuhudumia mji na viunga vya mji huo na pia kutoa huduma ya maji kwa vijiji vya karibu na bomba hilo la maji. Mheshimiwa Rais alilipokea ombi hilo na aliahidi kuwa Serikali yake italfanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako na kupitia Bunge hili wananchi wa Bariadi kuhusu *status* ya ahadi hiyo ya Rais.

Eneo la mwisho ambalo napenda nilichangie ni kuhusu malambo ya maji katika Jimbo langu ambayo mengi yalijengwa mwazoni mwa miaka ya sitini. Malambo hayo ndio yanategemewa na wananchi wa Jimbo langu kwa matumizi ya nyumbani na mifugo. Nimesema mara nyingi hapa Bungeni kwamba malambo hayo yamejaa tope, yameshambuliwa na magugu maji na hivyo kupunguza uwezo wa kutunza maji mengi. Hali inaendelea kuwa mbaya zaidi kutohana na ongezeko kubwa la watu (Bariadi Magharibi ina watu zaidi ya 400,000). Majibu ya Wizara yamekuwa yale yale kuwa kutoa tope ni kazi yenye gharama kubwa na hivyo ni afadhali kujenga malambo mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na idadi kubwa ya watu, Bariadi hatuna maeneo mapya ya kuhamisha (*re-settle*) watu ili kupisha ujenzi wa malambo au mabwawa. Namwomba Mheshimiwa Waziri atupatie majibu yanayoendana na hali halisi ya Wilaya ya Bariadi yenye watu takriban laki nane (800,000).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipaye majibu.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuchangia bajeti hii kama ifuatavyo. Wilaya ya Masasi hususan katika Jimbo langu la Masasi lina matatizo makubwa sana ya maji. Naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kuanza kutekeleza mradi wa maji Mbwinji ambaa utasaidia kutatua tatizo sugu la maji katika Mji wa Masasi.

Mheshimiwa Spika, kwa Mji wa Masasi kulikuwa na bwawa la Mchema ambalo ndiyo lilikuwa mkombozi, kwa miaka mingi bwawa hili lilipasuka, hivyo kushindwa kutunza maji, lakini Serikali ilishaweka ahadi ya kukarabati bwawa hilo na kuchimba bwawa lingine katika Mto Myesi. Naomba kuja kazi hii ya kukarabati Bwawa la Mchema na kuchimba bwawa la Myesi itaanza lini? Je, katika bajeti hii zimetengwa fedha kiasi gani kwa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006 ulianza Mradi wa Maji wa Vijiji Kumi kupitia fedha toka *World Bank* na kwa Wilaya ya Masasi ulikuwa unatekelezwa katika Vijiji vya Mtranshi, Mtakujia, Nambawala, Lilala, Mihima, Sindano, Mkaliwata, Nanganga, Mpindimbi na Shaurimoyo. Katika mradi huu Mshauri ambaye ni *Don Consultant* alilipwa fedha Shilingi milioni 20 kwa ajili ya kutoa ushauri wa maeneo ya kuchimba visima hivyo na kila kisima kiligharimu Shilingi milioni nne na wananchi walipaswa kutoa mchango wao wa Sh. 2/= kwa kila kijiji kilichokuwa na mradi huo na mshauri alitakiwa asimamie mradi huo hadi kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana visima hivi vimechimbwa lakini kisima kitakachokuwa na uwezo wa kutoa maji ni kimoja tu cha Sindano, visima tisa havitawezwa kusambaza maji kwa sababu havina maji na kimoja cha Mkaliwata kina chumvi nyangi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, lengo la Serikali lilikuwa ni kuondoa tatizo la maji katika vijiji hivyo na mshauri alishalipwa pesa kwa kazi hiyo, ambayo kwa hivi sasa ni kama Serikali imepata hasara kubwa sana? Je, Serikali itachukua hatua gani kwa huyu mshauri ambaye hakutoa ushauri wake kitaalam hivyo kusababisha kupoteza muda mrefu bila mafanikio yoyote. Kwa hivi sasa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi inatarajia kupokea Shilingi 967 milioni kwa taarifa toka Halmashauri ya Masasi. Naomba nitoe ombi maalum kwa Serikali kwa kuwa Jimbo la Masasi katika vijiji viliviyotarajiwa kupata mradi huu havina vyanzo vya aina yoyote ambavyo wananchi wanaweza kupata huduma hii ya maji na kwa kuwa njia pekee ya kuwakomboa wananchi hawa ni kuchimba mabwawa, kwa nini Serikali isifanye mazungumzo na wafadhili wetu fedha iliyotarajiwa kujenga mradi huu yakachimbwa mabwawa katika vijiji husika kwani hiyo ndiyo itakuwa njia pekee ya kutatua tatizo sugu la maji. Tafadhalii Serikali izingatie ombi hili kwani fedha zipo na maeneo yanayofaa kwa kuchimba mabwawa hayo hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mradi huu lakini bado katika Kata ya Lukuledi, Kijiji cha Lukuledi B kuna bwawa ambalo liliichimbwa mwaka 1956 na Wamisionari na maji zaidi ya vijiji vitano vinavyozunguka kijiji hiki na vijiji jirani vya Wilaya ya Nachingwea, lakini kwa hivi sasa bwawa hili linashindwa kutunza maji ya kutosha kutokana na kupungua kina cha maji kwa sababu toka lijengwe halijawahi kufanyiwa ukarabati wa kupunguza tope, na kwa kuwa bajeti ya Halmashauri inashindwa kutekeleza kazi hii. Je, Serikali inaweza kuleta wataalam ili kuona bwawa hili na kufanya makadirio ya ukarabati ili Serikali ifanye kazi hii kwa haraka ili huduma hii iendelee kwa vizazi vijayvo? Tafadhalii naomba hiki ni kilio cha wananchi wa Lukuledi na vijiji jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika mradi wa maji Mbwinji Serikali illahidi kutoa fedha kwa wananchi ambaa waliridhia maeneo yao kupisha utekelezaji wa mradi huu, kuna wananchi wanadai fidia ya mazao yao yaliyofekwa, nyumba, mikorosho na kadhalika lakini hadi hivi sasa hawajalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua wazi Serikali ilifanya tathmini ya madai haya na inajua ni fedha kiasi gani wananchi wanadai, ni kwa nini hadi leo wananchi hawa hawajalipwa? Kwa kuwa tathmini ilifanyika mapema kwa nini wananchi hawakulipwa kabla ya kuanza mradi ili kuondoa kero kwa wananchi? Tafadhalii naiomba Serikali ilipe haraka fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Maji wa Vijiji Kumi. Huu ni mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia katika vijiji 10 kila Wilaya. Mradi huu umekuwa kitendawili, hautekelezwi, matumaini ya wananchi yamekwishaondoka katika mipango ya maji ya Serikali na umewafanya Wabunge waonekane waongo kwa wananchi. Haya ndiyo madhara ya kutegemea fedha za wahisani kupita kiasi! Nashauri Serikali itenye fedha ya kutosha kwa miradi mikubwa yenye athari kwa wananchi kwa mfano, maji, umeme, nishati ya mafuta, afya na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miji Midogo ya Wasso na Liliondo (Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro) hayana maji. Miji hii sasa inakuwa kwa kasi kwa sababu ya kupata umeme na barabara ya Mto wa Mbu-Loliondo itaanza kujengwa hivi punde. Naomba fedha za visima virefu Loliondo, Sakala na Wasso.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu aliényevezesha leo kuchangia katika Bunge lako Tukufu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumtakia Mheshimiwa Profesa Mark J. Mwandsoya, Waziri wa Maji, apone haraka na kuendelea na gurudumu hili la maendeleo ya maji nchini. Pongezi namtakia Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na watendaji wote wa Wizara ya Maji, kwa kazi nzuri na nzito wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni hitaji muhimu kwa maisha ya binadamu, wanyama, ndege, mimea na kila kitu chenye uhai hapa duniani kinahitaji maji kwa maisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ni vizuri ihakikishe upatikanaji wa maji safi na salama, kwa asilimia kubwa yanawafikia wananchi. Kama kweli tunaitakia Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi na ushindi wa kuendelea na dola kwa kishindo mwaka 2015, ni lazima mikakati, uadilifu na uajibikaji kwa kutenda kazi, kwa kila mfanyakazi wa Wizara ya Maji utiliwe maanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango na miradi yote Serikali inayopanga, ni vizuri kujitahidi kuitimiza. Ahadi zote zilizotolewa kuhusu upatikanaji wa maji kwa wananchi, ni vizuri zitimizwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanahitaji maji na kwa kuwatimizia hitaji hili kwa asilimia kubwa tunaweza, Mheshimwa Waziri, tufanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunajua kuwa kuna tatizo la fedha. Bajeti yetu ya maji inayohusudha za maendeleo Sh. 41,565,045,00/= ni fedha za ndani na sh. 387,073,918,000/= ni fedha kutoka nje. Jambo hili ni zuri ila nina wasiwasi kwa maana bajeti kubwa inabebwa na fedha za kutoka nje. Ukweli ni kwamba ni tatizo mojawapo ambalo limepelekea miradi mingi, inayotegemea fedha za nje, kususua kwa sababu ya fedha hizi. Fedha hizi, wakati mwingine hazifiki kabisa. Kwa hiyo, jambo hili ningeomba liangaliwe hasa wakati tunavyopanga na kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la uhifadhi wa vyanzo vya maji, ni muhimu sana. Kwa hiyo, tukitaka mito ya nchi yetu, iendelee, ni vizuri kutunza vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvunaji wa maji, ni jambo muhimu sana, kwa wananchi na upatikanaji wa maji. Kwa hiyo, elimu izidi kutolewa na kuhamisha wananchi kukinga maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Maji ni muhimu sana, kwa hiyo, mambo mazuri yaliyofanyika kwenye Wizara hii yaendeleee. Miradi yote, Wizara ijitahidi kuimaliza. Kwa hiyo, watalaaam wa maji wazidi kujitahidi kufanya kazi kwa moyo mmoja ili asilimia kubwa ya Watanzania wapate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa Mbunge kutoka Morogoro, natoa pongezi kwa miradi, kwanza ya Benki ya Dunia, mabwawa na miradi mingine inayoendeshwa Mkoani humo. Lakini

Morogoro ikiwa sehemu ndogo ya nchi ya Tanzania, Wizara, ijitahidi kwa njia yoyote ile, Watanzania wapate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa mmojawapo wa Kamati ya Kudumu, inayoshughulikia masuala ya maji, mengi tumeyasema kwenye Kamati. VAT kwenye dawa ya maji (ili maji yawe safi na salama) iondolewe. Maji ni muhimu kwa binadamu, kadri tunavyoweka VAT, bei ya madawa inakuwa juu na hiki ni chanzo cha matatizo ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema kuwa Serikali imefanya mambo mengi mazuri, lakini Wizara izidi kuangalia upatikanaji wa maji kwa wananchi, kama tulivyoahidi kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010. Ili kuhakikisha kuwapunguzia umaskini wananchi, ni kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kufikia asilimia 75 vijiji na mijini, asilimia 95 ifikapo mwaka 2015. Mipango ikiwa mizuri kama ilivyo, na uwajibikaji tutatimiza wito wangu. Naomba watendaji wa Wizara wajipange na wafanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linaloisibu Wizara hii ni bajeti ndogo iliyopata au inayotengewa bajeti sh. 446,194,636,000/= ikiwa ni sh. 428,638,963,000/=, ni fedha za maendeleo ni kidogo kwani kila Mkoa, Wilaya, Tarafa, Kata, Kijiji na Kaya za kila mmoja au kiumbe chenye uhai na (mimba pia) wanahitaji maji. Bajeti zinazokuja au zitakazopitishwa miaka ijayo ziwe kubwa au iongozeke kwani binadamu huwezi kuishi bila ya maji.

Naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri kwa kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji kwa niaba ya Waziri wa Maji. Pongezi kwa kazi nzuri na ngumu, Wizara inayofanya ili kutatua tatizo la maji kwa wananchi. Wananchi wote hasa wanaojenga nyumba za bati, washauriwe kukinga maji au kujenga matanki ya kuhifadhi maji wanayovuna wakati wa mvua. Miradi ya uchimbaji wa malambo na mabwawa ipewe kipaumbele. Pia uvutaji wa maji kwa wananchi, ujenzi wa kisima uende kwa kasi mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kumshukuru Mungu kwa nafasi hii na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na wataalam wake kwa kuandaa mipango mizuri ambayo inawaletea wananchi maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai, ni afya, yakikosekana ni madhila makubwa sana kwani haiwezekani kiumbe yeoyote kukosa maji safi na akaishi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania walio wengi wa vijiji hawana maji safi hasa wale wa kipato cha chini na hasa wa vijiji na wakati mwininge visima vikichimbwa huwa havitoi maji, hivi Serikali haionti sasa ipo haja ya kuanzisha kampeni ya makusudi kuendeleza ujengaji wa matenki ya kuvuna maji ya mvua ili Watanzania hasa wale wa vijiji waweze kupunguza ukali wa upatikanaji wa maji safi na salama?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itakubali ushauri huu wanawake wengi watapokea wito huo kwani wao ni waathirika wakuu wa tatizo hili la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi zinazoshughulikia maji zifanye ukarabati wa mabomba ili maji yasimwagike na yawafikie wananchi wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika maeneo haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Tanzania ni nchi ya 11 kwa mito mingi duniani ikiwa na maziwa makubwa kama Tanganyika na Victoria. Ni aibu leo miaka 50 ya Uhuru bado Serikali inashindwa kufikisha maji ya kutosha kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Miradi ya Benki ya Dunia kwenye maji vijiji bado ni usumbufu mkubwa kiasi cha kuitwa miradi ya kitapeli kwa sababu utekelezaji wake unasuasua mno kiasi cha kukatisha tamaa. Ningependa kujua katika Mkoa wa Kigoma hususan Wilaya ya Kigoma ni asilimia ngapi za miradi hii imetekelezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Wilaya ya Kigoma hususan Jimbo la Kigoma Kusini kuna tatizo sugu la miradi ya maji. Kuna Kata kama Mganza ulipelekwa mradi wa maji miaka ya 2006 mpaka leo hakuna kinachoendelea. Kuna Kata ya Uvinza ina miundombinu yote ya maji iliyojengwa tangu miaka ya 1980 lakini mpaka leo Kata hii haina maji tangu *pump* za kusukuma maji kutoka Mto Malagarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Ukanda wa Kusini mwa Ziwa Tanganyika yenyе Kata za Ilagala, Simbo, Sunuka, Sigunga, Igalula, Buhingu na Kalya zipo ufukweni mwa Ziwa Tanganyika umbali wa mita 100 lakini hakuna huduma ya maji. Hali ya namna hii ningependa Wizara yako itazame kwa namna yake maana inashangaza Serikali kusafirisha maji kutoka Ziwa Victoria mpaka Shinyanga lakini waliopo mita 100 kutoka usawa wa Ziwa hawana maji.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Maji kwa maandalizi ya hotuba nzuri ya Mapato na Matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda sasa kuchangia maeneo machache na kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa maji wa Kakonko, Kakonko ni moja katи ya Wilaya mpya ambazo zitaanzishwa hivi karibuni. Nilipokuwa Naibu Waziri Maji na Umwagililaji nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu aliiagiza Wizara kutoa kipaumbele kwa kupeleka huduma ya maji katika Makao Makuu ya Wilaya mpya. Kwa bahati nzuri mradi wa maji wa Kakonko unachangiwa pia na Shirika la *CARITAS*. Wizara ya Maji ilikwishatoa shilingi 50,000,000/= kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Tuliamua kuwa mradi huo utekelezwe kwa awamu kutokana na gharama yake kuwa kubwa Wizara ya Maji, katika mwaka 2009/2010 ilitenga shilingi milioni 300 kwa lengo la kuanza utekelezaji.

Naomba Wizara iendelee kutenga fedha ili fedha zilizokwishatumika ziwe na manufaa na kazi iwe endelevu. Kwa bahati nzuri, hivi sasa Wilaya ya Kibondo ina Mhandisi wa Maji ambaye ana uzoefu na ni *very practical* kiasi kwamba akipata fedha mradi wa Kakonko utatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kusitiza kwamba mradi wa maji wa Kakonko ni wa mtiririko (*gravity*) na chanzo chake ni mto wenye maji mengi na ya kudumu. Hapa ndipo pa kupata *mileage* badala ya kung'ang'ania miradi ya visima ambayo kwanza haina uhakika wa kupata maji na pili ina gharama kubwa za uendeshaji. Tafadhalii tekelezeni mradi wa Kakonko.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa na shukrani, nilifanikiwa kupata fedha shilingi 132,000,000/= kwa ajili ya mradi wa maji wa vijiji vya Kabingo na Kiyobera katika Wilaya ya Kibondo. Kwa kushirikiana na Ofisi ya Bonde ya Ziwa Tanganyika na Mhandisi wa Maji wa Wilaya wa sasa (ambaye ana uwezo mkubwa wa kazi) tumetumia Sheria ya Rasilimali za Maji Na.11/2009 kufufua na kulinda chanzo cha maji ya vijiji vya Kabingo na Kiyobera (*gravity*) na sasa vijiji hivyo vimepata maji tena baada ya kukosa maji kwa zaidi ya miaka 15. Hii pia ni *mileage* kwa Wizara katika kutekeleza mradi wa vijiji kumi!

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Wizara ya Maji iliendelea kujenga mabwawa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika nayo inajenga mabwawa ya umwagililaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kuna ugumu gani Wizara hizi mbili kupanga kwa pamoja ujenzi wa baadhi ya mabwawa? Kwa kuunganisha mipango ya ujenzi wa mabwawa tutapata faida zifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kupunguza gharama za ujenzi, hivyo kuipunguzia Serikali mzigoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuweka miundombinu ya matumizi ya maji ya kunywa, kilimo, mifugo, uvuvi na kadhalika kutoka kwenye chanzo kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila sekta ikijenga bwawa lake ardhi inayotumika ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa poongezi, kwani inatia moyo kuona kwamba sasa karibu kila Halmashauri ya Wilaya ina wataalamu washauri chini ya mradi wa vijiji kumi. Hivi sasa Waheshimiwa Wabunge wanachotarajia kusikia ni ujenzi wa miradi ya maji kuliko kusikia lugha ya mchakato wa kumpata mtaalamu mshauri, nashauri sasa majibu yenu yote yalenge kujenga imani ya ujenzi wa miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na kumwombea Mheshimiwa Profesa Mwandosya apone haraka.

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote natoa pole kwa Waziri Mheshimiwa Mwandosya kwa kuugua na vilevile natoa salaam za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Mussa Khamis Silima, kwa kuondokewa na wazazi wao wote wawili (baba na mama).

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji ni tatizo kubwa sana hapa nchini, kuna maeneo mengi bado yanapata shida ya maji kutokana na kutokuwa na aidha, maji ya kisima au ya bomba, hili ni tatizo kubwa na hasa ukizingatia wanawake ndio waathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vipi Serikali imejipanga katika kueneza/kusambaza maji maeneo mbalimbali ikiwemo kwenye vituo/zahanati/hospitali, shule na hata kwenye vyuo mbalimbali. Ni vyema nipatiwe majibu japo Serikali imejipanga kwa kodi kuchimba visima kwa vijiji kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna baadhi ya maeneo ambayo ardhi yake haina maji (*water table*) au yapo chini sana, kama maeneo ya Wilaya ya Kisarawe, ni vipi Serikali imejipanga kutoa elimu na vifaa kwa wananchi kwa vipi watavuna maji ya mvua ili kupeukana na tatizo la maji na kuweza kuyapata kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya maji vya asili vipo hatarini kutoweka na kwa kweli baadhi ya vyanzo vinaanza kufa kutokana na ufye kaji wa misitu katika maeneo husika. Licha ya kuwa suala la mazingira lipo Ofisi ya Makamu wa Rais lakini kwa vile suala la mazingira ni mtambuka ipo haja Wizara ya Maji pia iweke juhudhi za waziwazi wa kupambana na wanaochafua mazingira katika maeneo yenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa nyumba unafanyika karibu na Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria. Kuendelea kuwaachia wananchi kujenga karibu na maziwa hayo matokeo yake hapo baadae ubora wa maji wa vyanzo hivyo vya maji utakuwa haupo. Je, Wizara inachukua hatua gani au imejipanga vipi katika kulikibili suala hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, ilipotokezea janga la uvujaji wa kemikali katika Mgodi wa *North Mara* ilidhihirika Ofisi ya Bonde la Ziwa Victoria ilikuwa na uwezo mdogo wa kupima ubora wa maji kwenye Mto Tigithe ambaa ilidhihirika baada ya operesheni kuwa mto huo maji yake yamechafuliwa na kemikali. Ipo haja ya Wizara kuwezesha ofisi hiyo pamoja na ofisi nyingine za mabonde ili wawewe hutekeleza kazi zinazowahu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hotuba ya Waziri ukarasa 82 aya 145 Wizara inataka kuondoa tatizo la upotevu wa maji Dar es Salaam. Katika hilo kunafanyika na kumefanyika utafiti juu upotevu huo wa maji, kwa aya hiyo baada ya Wizara kufanya utafiti hakuna mpango wa namna gani upotevu huo wa maji utaondolewa. Ni vyema Wizara ikanieleza vipi upotevu huo utaondoshwa. Utafiti ni kujua tatizo na sio kuondoa tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina vyanzo vingi sana vya maji, mito, maziwa chini ya ardhi mabwawa na kadhalika, licha ya utajiri huo wa vyanzo vya maji bado nchi yetu ina tatizo kubwa la upatikanaji wa maji. Ipo haja Wizara huondoa aibu hii kwa kuwapatia wananchi maji yaliyo safi na salama. Ahsante.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji. Miradi ya maji ni mionganoni mwa miradi ya kihandisi (*Engineering Projects*) ambayo utekelezaji wake unataka/unahitaji utaalamu stahili katika kipindi chote cha uhai wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaalam stahiki katika miradi ya kihandisi chini ya Sheria Na.15 ya mwaka 1997 huthibitishwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi nchini yaani *ERB*. Uthibitisho huu ni kwa Wahandisi na Makampuni ya ushauri na kufanywa kupitia usajili ambao ndiyo sifa pekee ya uwezo wa mhandisi ama kampuni kutekeleza kazi za uhandisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi ya maji inayotekelvezwa kwenye Halmashauri zote kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia, jumla ya Kampuni 26 hazijasajiliwa na *ERB* hivyo uwezo wao kitaalam kuwa wa mashaka licha ya kukosa sifa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ni hatari, Serikali haina wataalam washauri katika miradi ambayo imekabidhiwa kwa makampuni haya 26 yasiyokuwa na sifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa kwamba Bodi ya Usajili wa Wahandisi kupitia kaguzi zake na taarifa zinazowafikia wamebaini utekelezaji mbovu wa miradi hii katika baadhi ya maeneo na kwamba hali ikiachwa hivyo wananchi hawatapata kile wanachokisubiri kwa hamu na Serikali itakuwa imepoteza muda na fedha (*no value for money*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Serikali ikachukua hatua sasa ili kuepusha aibu na fedheha siku za usoni. Tumekuwa tukishuhudia baadhi ya miradi kuamuwa kurudiwa hii sio njia nzuri kwa Serikali, ni vema kuhakikisha kila kitu kipo sawa katika hatua hizi za awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jicho la Serikali katika miradi hii ni wataalam washauri hivyo ni bora wawe wenye sifa na uwepo wao uwe wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, makampuni yote 26 (orodha inapatikana Bodi ya Usajili wa Wahandisi (*ERB*) yanaamuriwe kutekeleza hitaji la kisheria la kujisajili. Wakienda huko kupeleka mambo watatakiwa watimize vigezo ambavyo ndivyo vitakuwa uthibitisho wa uwezo wao kitaalamu kumudu kufanya kazi walizopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Sheria Na.15 ya mwaka 1997 hakuna mtu au kampuni inayoruhusiwa kufanya kazi za kihandisi bila kusajiliwa na bodi. Serikali haiwezi kuwa mstari wa mbele kuvunja sheria zake yenye (sheria za nchi).

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja ya Wizara hii kwa kuzingatia kuwa Wizara hii ni moja kati ya Wizara nyeti sana ambazo Taifa kwa maana ya Serikali inatakiwa kutoa kipaumbele cha hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiojichika kuwa maji ni uhai kwani bila maji viumbi hai vyote tukiwemo sisi binadamu, mimea na wanyama wengine wasingeishi. Kwa dhima pana kabisa ni kwamba uhai wa nchi na uchumi wake kwa kiasi kikubwa vinategeremea maji. Mfano mzuri ni sisi wenye sisi binadamu, hebu tuijulize tukikosa maji ya kunywa tutakufa kwani zaidi ya asilimia 70 mwilini ni maji, tusipooga tutambue tutapata magonjwa nyemelezi ya ngozi, chawa na mengine mengi kama ukurutu, tusipofua nguo zetu tutapata magonjwa nyemelezi, tusipotumia maji kusafisha mazingira yetu tutapata magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu na zaidi kabisa maji hutumika kwa shughuli za nyumbani kama kuandaa milo, pia viwandani pia kwa kiasi kikubwa kutumia maji kwa shughuli viwandani, na hii inaifanya sekta ya maji kuwa ni kitovu cha uchumi wa nchi yoyote ile duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii hali ya huduma za maji nchini inasikitisha sana licha ya kuwa na utajiri mkubwa wa vyanzo vya maji kuanzia mito, maziwa na bahari lakini bado wananchi wanaoteseka na shida za maji mjini na vijijini kitu ambacho kinatia fedheha sana na uchungu kwa kuona kwa nini Serikali inakuwa kipofu kwa kuona hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana kuona ndugu zetu wanateseka kwa maji hasa wananchi waishio vijijini, na ukizingatia uhalisia wa mambo, hawa watu wa vijijini ndio wanaoteseka kwa kutembea kilomita zaidi ya kumi wakitafuta maji kuanzia alfajiri hadi saa tano hadi saa saba mchana wakirudi wanapata vipigo au mtafaruku kwa wanandoa wenzao. Hivyo ningetaraja Serikali kwa maana ya Bajeti ya mwaka huu ingetoa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Serikali iweze kuendana na kaulimbiu yao ya Kilimo Kwanza. Kiuhalsia kabisa Serikali ingeweka kaulimbiu ya maji kwanza *then* kilimo kitatekelezeka pasipo na matatizo yoyote yale. Wakati ukweli ukibaki kuwa pale pale kwamba watumiaji wengi wapo vijijini na maji haya hutumika kwa kiasi kikubwa kwenye shughuli mbalimbali ikiwa ni kilimo, ufugaji na matumizi mbalimblai ya maji ya nyumbani, na kwa taarifa zilizopo ni chini ya asilimia moja tu ya wakulima wote nchini wametumia kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ni vyema Serikali ingeweka maji kuwa kipaumbele cha hali ya juu ili hata tuwe na kilimo cha umwagiliaji chenyehuleta tija na maarifa kwa wananchi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti zinazotengwa katika Wizara ni ndogo sana, na kiasi kikubwa cha fedha za maendeleo kwenye sekta ya maji yaani kwa vijijini (maendeleo ya maji na usafi wa mazingira) na mijini (maendeleo ya maji safi na maji taka). Na mbaya zaidi hii Bajeti ndogo lakini bado inategemea wahisani kwa zaidi ya asilimia 75. Na izingatiwe kuwa hawa wahisani mara nyingi hawatimizi ahadi na ikitokea wakatimiza basi kwa wakati kitu ambacho hakina afya kwa maslahi ya Taifa letu hili. Hizi fedha ndogo zilizotengwa kwenye miradi ya maji vijijini ni kiasi cha shilingi bilioni 50.7 ilhali tukijua kabisa kwamba kijijini ndiko kwenye uhitaji mkubwa wa maji na ndiko kuna watu wengi kuliko mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Bajeti ya 2011/2012 mgawanyo ule umedhihirisha kuwa Serikali haina dhamira ya dharti/mkakati madhubuti wa kuhakikisha wanawapa maji wananchi wa vijijini kwa kasi ya ajabu yaani ndani ya mwaka/miaka miwili wawe wamepata maji safi na salama. Nimepitia randama na kuona kuwa programu ya maji na usafi mazingira ni asilimia 26.8 tu wakati ile ya mijini yaani maendeleo ya maji na maji taka ni zaidi ya asilimia 73 ambayo ni bilioni za Kitanzania 313.5. Hivyo Bajeti hii inaathiri zaidi vijijini kuliko mjini na ikizangatiwa kuwa kwa taarifa zilizopo ni zaidi ya 86% ya wakazi mijini wana maji sasa kwani wamepewa fungu kubwa zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, inabidi Serikali ifanye kila linalowezekana ili liweze kuongeza fungu kwenye programu ya maji vijijini mathalani Wizara ya Ujenzi bado inaziada ya zaidi ya shilingi bilioni 213 hizi zinaweza kuchukuliwa kama vile walivyofanya kwa Wizara ya Uchukuzi.

Vilevile ni muda muafaka sasa Serikali inabidi iwe na *monitoring* ya hali ya juu kwenye miradi ya maji pote mijini na vijijini ambapo tumeshuhudia vitendo vya kifisadi kwenye miradi mingi ambapo fedha nyingi kutumika lakini hatuoni kazi zikimalizika kwa ubora uliokusudiwa au inaishia bila kuhakikisha maji yanapatikana. Mfano Bwawa la Wegero ambalo limetumia zaidi ya shilingi bilioni 1.2 lakini ukiliona utaona ni upakuaji tu umefanyika na cha ajabu Serikali inakiri kuwa bwawa hili limekamilika kwa asilimia 77. Hii hali ipo hivyo kwa maeneo mengi na hasa katika miradi hii ya Benki ya Dunia. Ni aibu kwa kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu nyingine ni kuhusu mradi wa awamu wa maji katika Vijiji 10 kwenye kila Halmashauri. Mradi huu haujafanikiwa kama ilivyotaarifiwa, ni takribani miaka minne sasa tangu uanzishwe lakini hatujaona Halmashauri zikipata visima vyenye uhakika wa kutoa maji kwa taarifa zilizotolewa Bungeni 14 Feburari na Waziri ni kuwa hadi Disemba, 2011 ni jumla ya maji takribani 4,314 tu, umewanufaisha watu milioni 2.7 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukibaki katika hili haya siyo mafanikio kwa Serikali kabisa kwani idadi ya wafanyakazi ni ndogo sana, na kwa mpango huu wa vijiji kumi kwenye kila Halmashauri licha ya kuwa unasuasua lakini pia inawanufaisha watu wachache sana kwa maana ya visima 1,320 kwa kila awamu ambavyo ni asilimia kumi tu, ukumbukwe kuwa tuna vijiji 13,000 Tanzania. Hii ina maana hawa Watanzania zaidi ya 11,680 wataendelea kutaabika kwa kipindi kisicho julikana hadi awamu zao zitakapofikia, hii ni dhambi isiyokubalika kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mtindo kwa watu/mamlaka zisizo na uadilifu zinajivekeea fedha ambazo hazielekezeki kwenye mikataba kama ongezeko la bei ambayo kwa taarifa zilizopo kwenye mkataba, hili ongezeko la bei huwa ni kati ya asilimia 28 hadi 212 ya bei halisi ya mkataba. Huu ni wizi wa wazi kabisa na ambao unachangia kuzorota kwa kumaliza tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tatizo la maji taka kwenye miji ni kubwa sana hasa kwenye mitaa ambayo haijapimwa, inabidi Serikali kupitia mamlaka zao husika kuhakikisha miundombinu imara na bila haya wanaunganisha na njia halali ya kutoa maji taka, na siyo kungoja mvua zinyeshe ndio wafungulie maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzungumzia matatizo sugu ya maji katika Jiji la Dar es Salaam. Pamoja na kuwa Jiji la Dar es Salaam lina idadi kubwa ya watu kuliko majiji mengine Tanzania na pia shughuli nyingi za uzalishaji ambazo zinatumia kwa kiasi kikubwa maji. Na hili Jiji nalo lenye kuchangia pato kubwa kwa uchumi wa nchi yetu lakini cha ajabu hadi leo Serikali imeshindwa kabisa kutatua tatizo la maji pamoja na kwamba baadhi ya wakazi was Dar es Salaam wameunganishwa na huduma ya maji safi na salama. Ingawa pamoja na kuunganishiwa maji lakini wanakuwa hawapati maji muda wote unaweza shangaa maji yanatoka mara moja kwa wiki au hata mara mbili kwa mwezi. Hivi tunaenda wapi kama Taifa? Hii inalazimu mtu awe na *storage tank*. Hili linawezafanikiwa kwa wale wenye uwezo tu. Hebu tuangalie wanachi wenye kipato cha chini ambao hawezi kuweka matanki ya kuhifadhi maji kwani nyumba zenyewe za kupanga na kipato chenyewe ndio hivyo hata kutoa shilingi 500/= kununua maji au 70,000/= kununua lita 6,000 ama 10,000 za maji hana, inabaki kuteseka tu. Kwa hili hatuwatendea haki Watanzania na ndio maana nashauri tusipitishe Bajeti hii. Leo hii tunaambwiwa *demand* ya maji Dar es Salaam ni $450,000M^3$ lakini hawazipati zote. Wanapata kwa wastani $300,000M^3$ kwa siku. Hii sio haki, maji ni uhai!

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na tatizo la maji kujaribiwa kutatuliwa lakini pia tumeshuhudia mapungufu mengi ikiwemo uchakavu wa miundombinu ambao unasababisha upotevu maji, kwani zaidi ya 50% ya maji yanayozalishwa hypotea, na hii hutokana na wachache kutokana na watendaji watiifu ambao hushirikiana na wananchi wasio waaminifu kujunganishia maji kinyemela, pia tumeona mradi wa mabomba ya Wachina kushindwa kuonesha adha ya maji kwani hayatoi maji, yamebaki kama pambo. Mfano mwingine ni hizi *Water User Association* kama *Goba Water User Association* pamoja ya kuwachangisha wananchi ili waunganishiwe maji lakini hayatoi maji, unaweza kwa zaidi ya wiki mbili bila moja hii sio haki. Upotevu huu hypoteza mabilioni ya fedha, na hivyo Serikali ichukue hatua mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa masikitiko makubwa kuona Serikali haijatoa kipaumbele cha kuchimba visima kwenye vijiji vinavyozunguka Mgodi wa *North Mara*, na ukizingatia maeneo yale yamepata athari kwenye vyano vya maji licha ya taarifa ya uongo iliyotolewa na Waziri wa Mazingira alisema visima zaidi ya saba vimechimbwa. Baada ya kugundulika havijachimbwa, nataka Wizara katika kujumuisha wanieleze kama visima vimechimbwa au wana mpango gani kuvichimba? Pia hatujapewa mradi wa kuchimbiwa bwawa katika Jimbo la Tarime ukiangalia Mkoa wa Mara ni Tarime tu, ndio hawajapata fursa ya kuchimbiwa bwawa licha ya mifugo na binadamu kwenda muda mrefu ili waweze kupata maji. Na hata pale Tarime Mjini maji hayapo sehemu zote. Tunaomba maelezo juu ya vigezo vya kupeleka maji maana vijiji vingi havina maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nashauri Wizara ichukue hatua za haraka kuchimba visima virefu kwenye maeneo ya vijiji vya mgodi na kwingineko. Vilevile vijiji vilivyopo katika Mgodi wa Buhemba maana hawana vyano vya maji safi na wananchi wanataabika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yangu ni Serikali kuipa sekta ya maji kipaumbele, kwa kuchimba visima virefu, mabwawa, kuimarisha miundombinu ya mabomba. Kusimamia kazi za maji ya vioski na madhumuni ili Mtanzania wa kawaida aweze kumudu kununua maji, kuzuia biashara ya vyuma chakavu ambavyo huwanafanya wakate mabomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuhakikisha Mamlaka za Maji zinafanya kazi kama inavyotakiwa na kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na siungi mkono hoja na Wabunge wote pia wawe wazalendo.

MHE. NASSIB S. OMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la maji Dar es Salaam, kuna wizi mkubwa wa maji katika Jiji la Dar es Salaam. Maji haya huwa yanatumika ovyo ovyo kwa sababu yanapatikana bila malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inahitaji kujipanga vizuri ili kuwagundua wale wote wanaoshiriki katika maovu haya. Patolewe motisha kwa wale wote watakaotoa taarifa ya wale wanaoiba maji. Pia paundwe Idara itakayoshughulikia suala la wizi wa maji pamoja na wizi wa vifaa vinavyotumika katika miundombinu ya maji. Vifaa hivi huuzwa kwa wanunuvi wa chuma chakavu hivyo kuna umuhimu pia wa kudhibiti biashara ya vyuma chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvunaji wa maji ya mvua, inasemekana kuwa Tanzania Bara inapata maji kutokana na mvua yenye mita za ujazo zifiziazo milioni 921,032. Inasemekana pia kiasi cha asilimia 90 ya maji hayo hypotea kwa kwenda baharini na mitoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa nchi nyingi huyavuna maji haya kwa kuyakusanya katika mabwawa ili kuyatumia wakati wa msimu wa kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kiwekwe kitengo maalum cha kushughulikia suala hili, hasa katika maeneo ambayo hayapati mvua za kutosha.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwombea afya njema Waziri Mheshimiwa Profesa Mark Mwandoza wakati huu akiendelea na matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nawapongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kuendeleza kazi nzuri Wizarani na katika sekta za maji mikano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo napenda kutoa ushauri kuomba ufanuzi na maombi maalum katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu hali mbaya ya uhaba wa maji – Muheza. Chanzo cha mradi wa maji kwa Jiji la Tanga, ni Mto Ziggi uliopo Tarafa ya Amani Wilaya ya Muheza. Hivyo Jiji la Tanga linapata maji tena ya ziada kutoka Muheza wakati Wanamuheza wenywewe hawana maji!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Muheza unakuwa kwa kasi hivyo chanzo kilichokuwepo cha Magoroto kinakidhi 30% ya mahitaji na wakati wa kiangazi 20% ya mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu ahadi za Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kuondoa matatizo ya maji Muheza. Mradi wa maji kwa mji wa Muheza kutoka chanzo cha Mto Ziggi (muda mrefu). Mwaka 2005 na Agosti, 2010, Mheshimiwa Rais ametoa ahadi ya utekelezaji wa mradi wa maji kutoka chanzo cha Mto Ziggi kwa Mji Mdogo wa Muheza. Tathmini za mradi wa muda mrefu zimekamilika kwa ufadhili wa Benki ya Dunia na usimamizi wa maji Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, nini maendeleo ya utekelezaji wa mradi huu kama sehemu ya ahadi ya Mheshimiwa Rais?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu mkakati wa muda mfupi wa uchimbaji wa visima virefu na miundombinu ya usambazaji. Uchimbaji wa visima virefu maeneo ya Mji Mdogo wa Muheza unalenga kuanza kupunguza makali ya tatizo kuu kabla ya utekelezaji wa mradi wa Ziggi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi 16 Agosti, 2011 mradi huu haujaanza kutekelezwa na hiyo hali ya Muheza bado ni mbaya sana. Je, nini maendeleo ya utekelezaji wa mradi huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, miradi ya vijiji kumi wa Benki ya Dunia, hatua iliyofikiwa hadi Julai, 2011 ni uchimbaji wa visima katika vijiji hivyo kumi. Hata hivyo pampu hazijafungwa wala miundombinu ya usambazaji haujafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini hatma ya ukamilishaji wa miradi hiyo? Je, fedha za kuweka pampu na ujenzi wa miundombinu zimetengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tano ni kuhusu ahadi ya pili ya Mheshimiwa Rais kwa mradi wa maji wa Mbarambara Muheza Vijiji. Mwaka 2008/2009 wakati Mheshimiwa Rais akifungua rasmi Shule ya Sekondari ya Kata Mtindiro, mbele ya viongozi mbalimbali akiwepo pia Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji (wakati huo) aliahidi kutekeleza mradi wa maji wa Mbarambara ili kuwezesha shule hiyo kupata maji na Kata za Songa, Mhamba na Mtindiro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alipendekeza Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuunganisha mradi huo na mradi uliokuwepo wa Benki ya Dunia kwa Kijiji cha Kilongo. Licha ya Halmashauri kutekeleza hatua zote za ushauri huo, utendaji ndani ya Wizara yenyewe ya Maji na Umwagiliaji haukuridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo ahadi ya Mheshimiwa Rais bado haijatekelezwa na Shule ya Sekondari ya Mtindiro bado haijapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri naomba uyapitie maelezo haya na kunipatia ushauri elekezi kwa ajili ya wananchi wa Wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakutakia kazi njema na naunga mkono hoja.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu Waziri, Wenyeviti wa Kamati na Katibu Mkoo. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Wizara hii nitachangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza miradi ya maji ambayo itasaidia wananchi wa Mikoa wa Dar es Salaam kupata maji safi, pili, usimamizi katika sekta ya maji na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya maji, naipongeza Serikali yangu kwa kuandaa miradi mbalimbali ya maji kusaidia wananchi wa Mikoa wa Dar es Salaam wapate maji safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi hiyo ni pamoja na ule wa Kisarawe II, Wilayani Temeke na Kidunda Mikoa wa Morogoro. Napongeza Serikali ule mradi wa Kidunda nimeona kazi imeanza. Lakini ule wa Kisarawe II, Kigamboni mbona bado hauleweki?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote bado Serikali imeonesha nia ya kutaka kuchukua eneo kubwa zaidi kiasi cha kuzuia wananchi wasifanye maendeleo japo hawajalipwa. Je, bado Serikali ina nia hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri kwa Serikali yangu Kisarawe II, Kigamboni ni jirani sana na Mji wa Dar es Salaam kuliko Kidunda. Hivyo basi ni vyema tukaupa kipaumbele mradi huu kwa maslahi ya wananchi wa Mikoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, *EWURA* inasimamia zaidi mafuta kuliko maji, maji yanauzwa ovyo ovyo sehemu nyingine dumu kwa shilingi 300 hadi 500. Lakini mikoa mingine yanafika mpaka shilingi 1,000 wakati wa Kiangazi. Je, mamlaka ya usimamizi inakuwa wapi na imejipanga vipi katika kukabiliana na hali hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa tukae tuangalie hali hii, pia maeneo ya Oysterbay na Masaki wanununa katika magari. Je, Serikali inatoa bei ya maji hayo? Maisha ya Oysterbay na Masaki yanakuwa magumu kwa gharama za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengineyo ni kuwa mipango ya Serikali ni mizuri tatizo ni utekelezaji wake, changamoto zipo tukabiliane nazo kwa maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja 100%. Ahsante.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kwa kunipa afya ya kutosha na kuweza kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa mimi siungi mkono hoja hii mpaka Waziri anipe jibu ambalo ni sahihi na siyo la kunifanya kila siku niendelee kuuliza swali hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni nilluliza swali kuhusu mradi wa maji Ziwa Victoria unaokwenda Nzega, Tabora. Majibu niliyopewa yalisema kazi ya tathmini itaanza mwezi wa Oktoba, 2011 na kazi itaanza mapema mwakani na alitaja maeneo yatakayopitiwa na mradi huu mkubwa wa maji ikiwemo Kagongwa, Isaka na Mji Mdogo wa Tinde. Lakini kwenye Bajeti hii inaonekana mradi wa maji ya Ziwa Victoria kwenda Tabora unategemewa kuanza usanifu mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili limenifanya nisiunge mkono hoja hii kwa kuwa Mji Mdogo wa Tinde ulikuwemo kwenye mradi wa Benki ya Dunia wa vijiji kumi ambapo kisima kilichimbwa na maji hayakupatikana, je, fedha iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya ujenzi wa matenki wa kisima hicho imepelekwa wapi? Ni kwa nini sasa matenki hayo yasijengwe na kuweza kuvuna maji ya mvua katika Kituo cha Afya cha Tinde ambapo hawana maji kabisa na kusababisha manesi na wanaohudumia wagonjwa kuhangaika kutafuta maji ya kununua na kama hivyo haiwezekani ni kwa nini sasa matenki hayo yasijengwe hata kwenye shule za msingi zilizopo hapo kijijini ni mbili ambazo zina wanafunzi zaidi ya 1,000 kwa kila shule?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu sahihi yasiyojichanganya ni nini hatma ya wananchi wa Tinde kuhusu maji ukizingatia Mji Mdogo wa Tinde ni njiapanda ya kwenda Burundi – Mwanza – Dar es Salaam na Tabora, na mji huu una mkusanyiko mkubwa wa wafanyabiashara wa mchele, una kituo cha mzani, kituo cha afya, shule mbili za msingi, kituo cha polisi na shule moja ya sekondari pia mnada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri haoni kama kuna umuhimu mkubwa wa wananchi hawa kupata maji ya uhakika safi na salama kwa haraka zaidi ili kuepusha maradhi ya kuhara kwa kutumia maji yasiyo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, swala la pili ni kuhusu vijiji kumi vilivyochimbwa na maji kupatikana na hakuna chochote kinachoendelea kwa sasa. Naomba nipewe majibu ukizingatia Mkoa wa Shinyanga tatizo la maji ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja naomba sana Waziri anipe majibu yaliyo ya kweli wakati anahitimisha hotuba yake. Ahsante.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa mchango wangu kuhusu hotuba ya Waziri wa Maji Mheshimiwa Profesa Mark Mwandsoya, iliyowasilishwa Bungeni ya Mpango na Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara iweze kufanikisha na kutekeleza majukumu yake Wizara imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 446,094,636,000/=, kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Kati ya fedha hizo, kiasi cha fedha za ndani kwa ajili ya maendeleo ni shilingi 41,565,045,000/= ni fedha za ndani na shilingi 387,073,918,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashindwa kuelewa ni kwa nini Wizara inaomba kiasi kidogo sana cha fedha shilingi 41,565,045,000/= za ndani kwa ajili ya kushughulikia tatizo la maji ambalo limekuwa kero kwa Watanzania wengi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Wizara ya Maji kutenga kiasi kikubwa zaidi kutoka nje, (shilingi 387,073,918,000/=), ni kutokuwa makini, ni kutowafikiria wananchi wanaoteseka siku hadi siku kwa taabu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inapoomba kiasi kikubwa cha fedha za maendeleo endapo fedha hizo hazitapatikana kwa vile ni fedha zinazotegemewa kutoka kwa wafadhili, je, ina maana miradi ya maendeleo ya maji haitafanyika? Je, Wizara imeliona hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka Wizara ya Maji huadhimisha Wiki ya Maji kuanzia tarehe 16 hadi 22 Machi. Kwa kiasi kikubwa maadhimisho hayo yamekuwa ni kero kwani Serikali hutumia fedha nyangi kwa ajili ya shamrashamra za maadhimisho hayo, kwa mfano mavazi (sare) fedha kwa ajili ya safari kwani hufanyikia nje ya Dar es Salaam. Fedha hizo zinazotumika zingeweza kabisa kukarabati au kununua mabomba mapya ili kubadili mabomba chakavu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufanya maadhimisho wakati maji hakuna ni kukosa *vision* (maono). Wizara itafute mbinu mpya ya kuhakikisha wananchi wanapata maji. Endapo maji yatakuwepo basi maadhimisho ya wiki ya maji yaendelee, lakini kama maji hakuna basi maadhimisho yasitishwe kwani kwa Wizara huu umekuwa mradi wao wa kutumia fedha za Serikali bila *vision* (maono) wakati maadhimisho yanabakia kuwa ya mabomba yasiyo na maji na visima vilivvyokauka, hii ni kuwakejeli wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji katika ukurasa wa 129 wa kitabu cha hotuba kuna visima vilivyochimbwa Meru. Ningependa kufahamishwa vipo maeneo gani ya Meru? Kwa sababu visima vingi vilivyochimbwa vimekauka havina maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri, ni nini maamuzi au msimamo wa Tanzania kwa nchi ambazo hazijasaini mkataba wa ushirikino wa nchi wanachama wa Bonde la Mto Nile kuhusu Misri na Sudan, kwa kutaka mkataba utambue matumizi ya maji ya Mto Nile na haki kama zilivyo katika mikataba ya kikoloni na mkataba huo wa kikoloni unasemaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache naomba kuwalilisha.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kwa nafasi hi, nikushukuru na kumpongeza Waziri mwenye dhamana kwa jitihada wanazofanya na hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa pamoja na kuwa na mito, maziwa na maporomoko ya Kalambo na pale kijiji cha Kate lakini Wilaya ya Sumbawanga Vijijini, Kalambo na Nkasi nya Kate, Kipande, Kirando, Isale na vijiji vingine vimeathirika kwa ukosefu wa maji. Hii inapelekea hata akinamama washindwe kushiriki katika shughuli za ujenzi wa Taifa na shughuli za kutunza familia na kushiriki katika shughuli za vikundi nya akinamama nya uzalishaji mali kuinua uchumi wao na kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji liangaliwe sana, akinamama wanashinda visimani ambako maji yakishachotwa na wanawake watatu au wanne yanakuwa yameisha. Wasaidieni wananchi wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ufinyu wa Bajeti ya Wizara ya Maji, Serikali inastahili kuwa siku na kukubali maoni ya Wabunge kwa kuwa fedha zilizotolewa tangu mwaka 2007 – 2011 kwa kiwango kikubwa hazikufanya kazi nzuri kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa takwimu sahihi na taarifa za utekelezaji kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kupata taarifa sahihi za matumizi ya fedha ngazi za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu mbovu za manunuzi na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 hazitumiwi kwa manunuzi ya Kitaifa. Mfano Wilaya ya Hanang, taarifa iliyotolewa katika Kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kilichofanyika tarehe 25/02/2011 ni miradi ya maji na usafi wa mazingira (*RWSSP*) katika vijiji kumi. Kazi zilizotekelawa ni usanifu wa mitandao ya maji na uandaaji wa nyaraka za zabuni za miradi ya maji ya vijiji vya Gidagharbu, Getasamu, Ng'alda, Simbay, Ishponga, Garawja, Galangala na Wandela. Fedha zilizotumika ni shilingi 41,527,081.04.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za utekelezaji kutokutimia au kufanyika ni nyaraka zimerudishwa kwa Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho kutokana na dosari zilizobainika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kauli ya Serikali kuhusu utekelezaji wa programu ya maji na usafi wa mazingira vijiji iliyowasilishwa Bungeni na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandomsya na Waziri wa Maji tarehe 14/02/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Wilaya ya Hanang, visima vilivyochimbwa 15, visima vyenye maji 8. Je, kwa taarifa hizi mbili ipi ni sahihi iliyotolewa na Wizara au iliyotolewa katika kikao cha wanaoidhinisha fedha katika Halmashauri amba ni Kamati ya Fedha? Hizo ndizo sababu za kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mabovu ya fedha za umma, ununuzi wa vifaa visivyo na ubora, ujisadi uliokithiri katika Halmashauri. Uchangiaji wa mifuko mingi kwenye mradi mmoja kwa kazi hiyo hiyo nayo husababisha mianya ya *Engineer* wa Maji kutumia fedha kwa matumizi yake. Mfano ujenzi wa mradi wa maji kuanzia mwaka 2006 – 2011. Gehandu/Mirongoro/Min'genyi.

(1) Tarehe ya taarifa kikao cha halmashauri 11/04/2007; utekelezaji ni ununuzi wa *pump* kwa kiasi cha shilingi 20,000,000 na mchangiaji ni *CDG*;

(2) Tarehe ya taarifa kikao cha halmashauri 22/05/2007; utekelezaji ni ukarabati wa Kisima kwa kiasi cha shilingi 18,510,000 na mchangiaji *CDG*;

(3) Tarehe ya taarifa kikao cha halmashauri 29/06/2007; utekelezaji ni kununua mabomba ujenzi wa viosiki vitano Belhande, kutandaza mabomba kwa kiasi cha shilingi 57,490,000 mchangiaji ni Program Ndogo na Usafi wa Mazingira (*RWSSP*);

(4) Tarehe ya taarifa kikao cha halmashauri 29/06/2007; utekelezaji ni kujenga vioski viwili Mirongori na kutandaza mabomba kwa kiasi cha shilingi 25,000,000 na mchangiaji (*RWSSP*);

(5) Tarehe ya taarifa kikao cha halmashauri 17/08/2007; utekelezaji ni usafishaji kisima (Gehundu, Mingenyi, Mirongori) kwa kiasi cha shilingi 29,900,000 na mchangiaji *CDG*;

(6) Tarehe ya taarifa kikao cha halmashauri 08/02/2008; utekelezaji ni ujenzi wa uzio, kutandaza mabomba, kununua *pump*, kujenga nyumba ya *pump* (Gehundu, Mingenyi, Mirongori) kwa kiasi cha shilingi 95,412,612 na 25,383,00; mchangiaji ni *RWSSP*;

(7) Tarehe ya taarifa kikao cha halmashauri Juni 2005/2006 (6/6/2006); utekelezaji ni kukarabati kisima Gehundu kwa kiasi cha shilingi 10,000,000 na Mingenyi kiasi cha shilingi 10,000,000 na mchangiaji *CDG*;

(8) Tarehe ya taarifa kikao cha halmashauri Machi, 2009; utekelezaji wa ujenzi wa vioski nane vyta kuchotea maji, utandazaji wa mabomba katika vijiji nya Gehandu, Ming'enyi, Mirongori kununua mabomba kwa kiasi cha shilingi 36,000,000 mchangiaji *TASAF*; na jumla yote ni shilingi 327,695,612.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii hesabu haieleweki ipo kwenye kabrasha za Halmashauri, kama ni ushahidi ninao na pia naomba sasa Serikali ikubali iwe sikivu kwa kwenda kufanya *auditing* Wilaya ya Hanang kwa kuhakikisha na kuona vitabu vyote, *value for money* kuona visima vyenyewe. Nina uhakika na hili na nipo tayari kuwa shahidi na siyo hapa tu bali katika miradi yote ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa vyoo kwa fedha za *quick win*, usafi wa mazingira. Mfano choo cha Gelangala, choo kimechimbwa na wananchi, ujenzi toka shimonim pa usawa wa *slab* wamefanya wananchi, kuna kiasi cha matofali, kuna kiasi cha mchanga na kokoto, fedha za *quick win* shilingi 5,000,000 ilifanya yafuatayo; kupauwa kwa batini, mbaa za kupauwa mbili, *fisier board* mbili, jaba mbili, milango mibovu miwili, vitasa vibovu viwili na kupiga ripu *cement* na *slab* kwa vyumba vidogo viwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni kweli ilitumika kiasi cha shilingi 5,000,000/=?

Mheshimiwa Naibu Spika, ubadhirifu ni mkubwa sana kazi ibaki majibu yenyе kuridhisha toka kwani Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini miradi iliyojengwa na wafadhili yote yana maji na kwa gharama ndogo sana.

MHE. AMINA ANDREW CLEMENT: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji ni suala sugu hapa nchini kwetu, lakini vijijini suala hili limekithiri, hakuna vijiji ambavyo tunaweza kujisilia walau vina visima vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali imeandaa mkakati gani wa kupeleka maji vijijini? Naiomba Wizara ifanye utafiti wa kina kutafuta sehemu zenyе maji ardhini na kuchimba visima, mbona wananchi wenye uwezo wanachimba visima vyao na wanapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iandae mikakati ya kutoa mafunzo pia kuwapatia vifaa katika vijiji mbalimbali kwa kuvuna maji ya mvua hii pia itasaidia japo kidogo kupungua uhaba wa maji kwa wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msemo unasemwa maji ni uhai. Je, huu uhai uko wapi na maji hakuna?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono. Ahsante.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza hotuba nzuri ya Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kuunga mkono hoja na napenda kuchangia hotuba hii kwa maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji vijijini katika Jimbo la Manyovu, linaomba ukamilishaji wa maji katika vijiji sita vya mradi wa *World Bank*. Vlijiji hivyo ni Muzeze, Mubanga, Kitelema na Nyamugani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyo vijiji vya Mnana, Mkatanga, Kitambuka Kibwigwa, Kibande na Mwayaya, tunayo matatizo ya maji kwa kiwango kikubwa sana na tunaomba Serikali itunusuru kwa tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti iliyotengwa Kasulu ni ndogo na haitaweza kutatua matatizo ya maji tunaomba Serikali ilete fedha hizo kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba uwezeshaji wa Halmashauri katika kufanya ukarabati wa pampu za visima vilivyoaribika na kusababisha kero kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi na ushauri, Wizara iwajibike zaidi.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu wake na wataalam wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkao wa Tabora na Wilaya zake hususan Wilaya ya Urambo na Igunga kuna tatizo kubwa sana la maji. Hatua zinazochukuliwa na Serikali kushughulikia kero ya maji katika Mkao huu hazioneshi matumaini kwa wakazi wake hasa akinamama na watoto wanaoathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na adha ya kukosekana kwa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alipota ahadi Mkoani Tabora ya kuonda tatizo sugu la maji haraka iwezekanavyo tulipata matumaini wananchi wa Tabora. Lakini muda unaotumika kutekeleza ahadi hiyo ni mrefu sana. Kweli mateso yale kwa wananchi yaendeleee hadi mwaka 2014? Ni muda mrefu sana. Tunaiomba Serikali ilipe suala la kuunganisha maji mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Kahama, Shinyanga kipaumbele cha pekee ili fedha itengwe mapema mradi huu utekekezwe haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa uchimbaji wa maji ya visima kwa vijiji 10 – 15 kila wilaya unakwenda taratibu sana na kwa maeneo mengi umekosa tija kwa walengwa. Kunakosekana umakini mkubwa kwa wataalum wahandisi wa maji kwenye Wilaya kuteua makandarasi wa kutekeleza miradi hii ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya 70% ya visima inayochimbwa inakosa maji. Ina maana wanakuwa hawapimi kwanza uwepo wa maji kabla ya kuanza uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ghamama kubwa zinatumika bure bila tija na matokeo yake migogoro inaanza kati ya Halmashauri na makandarasi na pesa imekwishachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Urambo – vijiji vitatu vya Ushokola, Utindi na Songambale vilionekana vina maji na visima hivyo vimekamilika ila maji hayajasambazwa kufikia kwa walaji. Ni lini maji hayo yatasambazwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nini hatma ya visima 12 ambavyo bado havijachimbwa na mkandarasi ameshalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ghamama za maji zimekuwa kubwa sana kwa mikoa mingi ikiwapo Morogoro hapa Dodoma. Kupandisha *unit* moja ya maji kutoka shilingi 665/= hadi 762/= ni juu sana! Tunaomba Serikali ileze ni kwa nini ghamama imepanda kwa kiasi hicho wakati maji yanapatikana *once a day* tena kwa saa mbili tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Dodoma tuna huduma ya maji taka ambayo wateja wanalipia kila mwezi. Miundombinu ya majitaka ni mibovu sana na ni ya muda mrefu, imechakaa na hakuna marekebisho yanayofanywa. *System* zimechoka na kila leo zinaziba, huku tunalipa ghamama kubwa ya huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ileze ghamama za maji taka zinazotolewa/pesa tunazolipa zinafanya nini? Ni kwa nini tuendeleee kuteseka? Utaendeleaje kuvuna pasipo kuwekeza ili huduma iwe endelevu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itambue kwamba idadi ya watu imeongezeka, familia zinaponuka na huduma za maji taka pia inatakiwa kupanuliwa. Miundombinu ya maji taka eneo la Mtaa wa Makongoro – Arusha Road imechoka, Serikali ifanye mabadilisho sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya maji vimeharibika kwa kiasi kikubwa kutokana na kukosekana kwa usimamizi wa maeneo na elimu kwa wananchi wanoishi jirani na eneo hilo. Mwaka 2007/2008 hapa Bungeni tulipitisha Sheria ya Kulinda Vyanzo vya Maji maeneo yote yenye vyanzo vya maji yaanishwe na kupimwa, kiwekewe mipaka yake ili yatambulike kisheria na yahifadhiwe kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ieleteze Bunge mpaka leo 2011 ni maeneo mangapi na wapi yanapimwa na kuwekewa mipaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu kubwa la kulindwa vyanzo vya maji limebaki kwa wananchi, idadi ya watu inaongezeka kwa kasi kubwa na matumizi ya ardhi yanaongezeka kila leo. Bila kuwepo na utaratibu endelevu kwa kuhakikisha kila anayetumia maji anawajibika kulinda vyanzo vya maji vyanzo vyote vitakuwa na ukame unatunyemelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa jinsi gani watumiaji wakubwa wa maji mfano viwanda, mashamba makubwa, mitambo mbalimbali wanashirikishwa kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inashiriki kuruhusu uwekezaji wa miradi mbalimbali mfano, uchimbaji wa madini, ukataji wa magogo na mbao kwenye vyanzo vya maji na hata kilimo kwenye ardhi bora. Vipi leseni na vibali vinatolewa na watendaji wa Serikali hii. Hili ni tatizo kubwa, Serikali iwjajibike.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Mikumi Wilaya ya Kilosa Mkoa wa Morogoro kuna tatizo kubwa sana na sugu la upatikanaji wa maji safi na salama. Kabla ya kuwepo mamlaka ya Mji Mdogo wa Mikumi kuna kampuni ya mwananchi aliyejitelea kuanzisha kampeni ya maji kwa kushirikisha Kamati ya Maji ya Mikumi kwa kushirikisha Kamati ya Maji ya Mikumi ili kusambaza maji kwenye eneo hilo. Kampuni hiyo ipo kisheria na kwa muda mrefu imesaidia wananchi kupata maji kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miezi miwili iliyopita Mbunge wa eneo hilo ameunda akishirikiana na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo Mikumi wameikataza kampuni hiyo kuendelea na utoaji wa maji na kuvunja Bodi ya Maji iliyokuwepo. Aliitisha mkutano na kuwateua watu wake ye ye mwenyewe kuunda Bodi Mpya ya Maji bila kufuata utaratibu. Akaagiza watumie ofisi yake kuendesha shughuli za maji wakati ofisi ya maji ipo. Aliagiza wananchi waende kuvunja ofisi ya kampuni ya maji (kutoa makufuili) ili bodi aliyounda ye ye iweze kuendesha utoaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji limeongezeka Bodi ya Mbunge huyo inauza maji ndoo shilingi 700/= wakati kampuni walikuwa wanaiza shilingi 200/= hadi 300=/. Pili maji yanafunguliwa mchana tu ili waweze kukusanya hela vizuri, maji yanafika maeneo machache sana na jioni wanafunga, usiku hakuna maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wameajiri wakusanyaji wa pesa mmoja kila kituo na mgambo kila kituo jambo linaliongeza gharama na machungu kwa wananchi maskini pato la maji ndilo linalolipa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubiniasi wa Mbunge na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo umekuwa ni mateso kwa wananchi wa Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge amepeleka majina aliyooyachagua ye ye kwa Waziri wa Maji na kusema kuwa ndio bodi ya wananchi siyo kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ieleteze Bunge, nchi hii inaendeshwa kwa sheria na taratibu. Ni sheria gani inaruhusu ofisi ya kampuni iliyosajiliwa kisheria kuvunjwa na wananchi kwa shinikizo la Mbunge na Mwenyekiti wa Mji?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, utaratibu gani ultakiwa kufuatwa pale mamlaka ya Mji Mdogo ingetaka kupokonya mradi wa maji kutoka kwenye kampuni iliyopo kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, majina yaliyoletwa kwa Waziri ambayo yameteuliwa na Mbunge kwa maslahi yake na watu wake kwamba Serikali imeunda Bodi ya Maji pale Mikumi na Mbunge tayari anatangaza kwamba ni Waziri ameunda bodi hiyo. Huku siyo kwenda kinyume na Sheria na Sera ya Maji ya Taifa? Je, bodi hiyo kweli itakuwepo kisheria katika Mji huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wakazi wa Mji wa Mikumi wanapata maji ya uhakika na endelevu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itoe ufanuzi imeshiriki vipi kuunda Bodi ya Maji ya Mji Mdogo wa Mikumi bila wananchi kushirikishwa?

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai, suala la maji ni muhimu sana, Wilaya ya Ludewa kati ya vijiji 10 vya mradi wa maji kutoka *World Bank* wao wamepewa vijiji viwili tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Manda imepewa mradi wa *Irrigation* shilingi milioni 400 lakini mradi huu bado haujaanza kutoka kwa watu wa Kanda Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza kwa nini Wilaya ya Ludewa Kata ya Manda na Wilaya nzima haina kabisa mradi wa *irrigation?* Swali Wilaya ya Ludewa ilitengewa shilingi milioni 39 tu maji nikauliza swali maana zilikuwa ndogo sana! Baada ya swali Wilaya ikapewa milioni 336 za maji yaani kutoka milioni 39 to milioni 336.

Mheshimiwa Naibu Spika, au walitaka kutuchakachua? Mto Ruaha tubuni bwawa zuri Iringa Manispaa na tusiache Ruaha kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya *Irrigation* Wilaya ya Makete/Njombe ipo michache sana *why?*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, *but* kwa nini Dar es Salaam kuna Bahari bado kuna shida ya maji? Wataalamu wabuni mbinu *please!*

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo sugu ya maji katika Mji wa Tunduma Tarafa za Kamsamba, Msangano na Ndalambo. Kwa miaka 50 sasa ya Uhuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) imeshindwa kabisa kutatua kero ya maji katika Jimbo la Mbozi Magharibi ambayo sasa ni Wilaya mpya ya Momba japo wamekuwa watiifu sana katika kuipigia kura CCM kwa miaka yote hiyo, wakati wa uchaguzi na kuifanya CCM iendelee kutawala lakini baada ya uchaguzi Serikali ya CCM imekuwa ikiwatelekeza wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wananchi wa Mji wa Tunduma, kwanza Tarafa ya Kamsamba yenye Kata tano za Kamsamba, Mkonko, Usoche, Senga na Muuyu pamoja na Kata za Ivuna, Mpapa, Kamsamba, Mkulwa na Chikulumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Tarafa ya Ndalambo (yenye kata tano za Ndalambo, Mkanzamo, Nyunga, Nzoto na Kapele) pamoja Tarafa za Msangano (yenye kata mbili za Msangano na Chitete). Hivyo basi wananchi wa Mbozi Magharibi wanataka wafahamu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lini tatizo la maji litakwisha? Lini ahadi ya Serikali ya CCM zisizotekelzeza za maji zitakamilika? Je, kero ya maji ndio imekuwa kigezo/sababu za kujipatia kura wakati wa uchaguzi? Je, Serikali itaacha lini kuwadanganya Wanambozi na Watanzania juu ya kumaliza kero ya maji nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba kupatiwa majibu ya mwisho juu hatua yetu ya kutatua kero ya maji katika Jimbo la Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naompongeza Mheshimiwa Waziri Mwandosya na Naibu wake Mheshimiwa Lwenge kwa maandalizi na hotuba nzuri ya Bajeti yao. Napenda pia kumpa pole Mheshimiwa Mwandosya kwa matatizo ya afya yanayomsibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa masikitiko yangu kuhusu kasi ndogo ya mradi wa maji unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kwani tokea mradi huu umeanza mwaka 2003 hadi sasa ni visima 14 tu ndio vimechimbwa. Sasa najiuliza kama katika kipindi cha miaka tisa ni visima 14 tu ndio vimechimbwa hii ni kasi mbaya ya huu mradi na kwa kweli hauwasaidi wananchi. Ni hadi lini vijiji zaidi ya 100 vya Jimbo langu vitapata maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vipi llani ya Uchaguzi ya kuwapatia maji wananchi wa vijiji kwa 75% ifikapo mwaka 2015? Nashauri tutafutiwe *alternative* mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lowassa alipokuwa Waziri wa Maji, alitembelea Singida mwaka 2003 na kuwaahidi wananchi wa kijiji cha Mlandala, Tarafa ya Sepuka visima viwli kuwa kitachimbwa kwa fedha za Wizara na kimoja au cha pili kitajengwa na Halmashauri ya Wilaya hadi leo hakuna hata kisima kimoja kilichochimbwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ina maanisha nini? Kama ahadi ya Waziri haitekelezwi Waziri ambaye aliteuliwa kuwa Waziri Mkuu sasa ahadi ya nani itaheshimika? Sitaunga mkono hoja mpaka nipate maelezo ya kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria katika awamu ya pili usiishie Shinyanga, ufile hadi Singida ili kutuokoa na hasa kwa kuzingatia kuna mradi wa Benki ya Dunia haufai!

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida inayoendelea kujengwa inakabiliwa na upungufu wa maji, naomba tusaidiwe kuchimbwa visima virefu walau viwili, vinginevyo hduma za hospitali zitakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua Wilaya mpya ya Ikungi na Halmashauri yake imezingatiwa katika Bajeti hii? Fedha za maendeleo shilingi bilioni 387 zinatoka nje. Je, uhakika wa kupatikana upo?

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukuaji wa miji na ongezeko la hitaji la maji, kumekuwepo na hitaji kubwa la maji kutokana na ongezeko la idadi ya watu na ukuaji wa miji mipyä hivyo kusababisha kero ya maji kuendelea kuwa kubwa na kuwa tatizo sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu Serikali ijipange ifanye tathmini ya kina kujuu mahitaji halisi ya maji na kujuu gharama halisi inayotakiwa ili Serikali kuelekeza nguvu zake kutatua kero ya maji na wananchi, kuweza kuchangia gharama kutokana na gharama halisi za uendeshaji wa kupata huduma za maji ikiwemo kupandisha bei ya malipo ya bili za maji ili kuweza kukidhi mahitaji halisi na wananchi wote kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri huo kwa sababu kumekuwa hakuna usawa katika ugawaji wa huduma ya maji kwani wakazi wanaopata maji ya bomba wanauziwa ndoo moja ya maji kwa shilingi 500 hadi 1,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii siyo sawa kabisa tena maeneo ambayo hayana maji ya bomba asilimia kubwa ni wale wenye kipato cha chini huku wanafaidi kodi za wananchi ni wale wenye kipato cha juu amba ni watumishi katika sekta mbalimbali na wanasiwa na viongozi wakubwa halafu bado ndio wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba sana Wizara iangalie upya mgawanyo wa rasilimali ya maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu limeingia kwenye ushirikiano na Benki ya Dunia katika kuondoa kero ya maji tangu mradi huu umeanza, Serikali haijafanya thathmini ya kina ya kujua mafanikio ya mradi huu. Tumekuwa tukiletewa ripoti mbalimbali toka Wilayani kuwa visima kadhaa vimechimbwa, lakini ukienda kwenye *field* huvikuti visima hivyo au unavikuta havina kiwango. Napendekeza Wizara ifanye thathmini ya mradi huu wa maji wa *World Bank* nchi nzima na kuleta taarifa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado sielewi dhana ya wananchi kusubiri miaka zaidi ya mmoja kwa mradi kuanza eti kwa kigezo kuwa wanapaswa kuchangia asilimia kumi ya gharama za mradi. Wakati wananchi wakiwa wanasubiri 90% ya fedha za mradi zinakuwa zipo benki ambapo fedha au shilingi inashuka thamani na vitu vinapanda bei kadri siku zinavyozidi kwenda mbele. Nashauri Serikali iliangular suala hili kwa mapana yake. Tutafute njia mbadala katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za maji zimepanda sana hivi sasa, maji ni bidhaa ya muhimu na ya lazima, hivyo Serikali inapaswa kuangalia upya suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pampu nyangi za visima vya maji hapa nchini zinaharibika kabla ya kufikisha miaka mitatu. Inavyoelekea kuna tatizo kubwa la uadilifu katika ununuzi wa vifaa hivi vya maji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilombero imebarikiwa kuwa na vyanzo vingi vya maji, ina mito mikubwa na midogo, mabwawa, lakini bado Wilaya hii ina matatizo ya maji. Napendekeza Serikali iweke mkazo wa ziada katika Wilaya hii ili tatizo la maji liondoke. Ni aibu kwa Serikali Wilaya ya Kilombero kukosa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Singida mjini wana hali mbaya sana na tatizo la maji. Wizara iwaangular wananchi hawa.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naendelea kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema inayoniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya Kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kwanza kuwatakia kheri Waziri wa Maji Mheshimiwa Profesa Mark Mwandsosya apone haraka na kurejea kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kutekeleza mpango kazi wa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajielekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa mradi wa maji wa Chalinze, naomba niipongeze Wizara ya Maji kwa kuanza utekelezaji wa awamu ya pili ya Mradi wa Maji Chalinze unaojumuisha usambazaji wa maji safi katika vijiji 48.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vyote vilivyotajwa katika awamu hii vina matatizo makubwa sana ya maji. Hali ni mbaya katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yaliyotajwa kwenye *lot 2* na *lot 3* (Kiwangwa/Mwavi, Fukayosi, Makurunge, Mkenge, Kidomole, Masuguru/Mwetemo, Msinune, Pongwe, Msungura, Madesa, Kisanga, Malivundo, Mindukeni, Kinzangu, Makombe, Msigi, Talawanda) yana shida kubwa sana ya maji, hivyo naiomba Wizara isimamie kwa karibu utekelezaji wa mradi huu ili kuzuia ucheleweshaji wa aina yoyote ambayo italeta madhara zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji katika Miji ya Ikwiriri na Kibiti. Kwa niaba ya wanawake Wilaya ya Rufiji naipongeza sana Wizara ya Maji kwa kutekeleza miradi hiyo kwa asilimia 75 na 96. Kimsingi tunafarrijika kuona kero ya maji katika maeneo hayo inakaribia kupitia ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo maeneo ya visiwani (Salale, Kiongoroni Mbuchi na Maparoni) vina shida kubwa ya maji, licha ya kuzungukwa na visiwa, hakuna miundombinu yoyote ya kusaidia usambazaji wa maji safi na salama. Je, ni lini Serikali itakuja na mpango wa kusaidia maeneo hayo kupata huduma ya maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma ya maji safi Dar es Salaam, Kibaha na Bagamoyo, upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam, Kibaha na Bagamoyo una matatizo makubwa sana. Inajielekeza tatizo hilo katika Miji ya Kibaha na Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha utoaji wa huduma ya maji safi asilimia 55 kinachosambazwa na DAWASCO hakitoshelezi mahitaji ya wananchi wa maeneo ya Mji wa Kibaha na Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza maeneo ya Mji wa Kibaha na Bagamoyo ndio maeneo ambayo vyanzo vikuu vya maji vya Ruvu Juu, Ruvu, Chini vipo katika Miji ya Kibaha na Bagamoyo na hata mitambo imejengwa katika maeneo hayo. Jambo la kushangaza maeneo kama Kibaha Mjini, Kibaha kwa Mathias, Kongowe, Visiga na Mlandizi yana matatizo makubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mipango ya kuboresha utoaji wa huduma ya maji kuainishwa katika ukurasa wa 78 - 83 wa kitabu cha hotuba ya Waziri, lakini kutokana na urasimu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji napata mashaka na mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kisarawe Mkao wa Pwani ina tatizo kubwa sana la maji na Wilaya hii ipo karibu na Jiji la Dar es Salaam, je, Serikali haioni kuna haja sasa Wilaya hii ya Kisarawe kuhudumiwa na mamlaka ya maji safi na maji taka Dar es Salaam (DAWASA) kama zinavyohudumiwa Miji ya Kibaha, Bagamoyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa uchimbaji visima virefu vya Kimbiji na Mpera maeneo ambayo yapo karibu na Wilaya ya Kisarawe, Serikali haioni sasa Wilaya ya Kisarawe isambaziwe maji kupitia visima hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upotevu wa maji kwenye Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka, nimesikitishwa sana na kiwango kikubwa cha upotevu wa maji wa asilimia 36 kwa mwaka 2009/2010 ambao umepungua hadi asilimia 33.5. Tatizo la upotevu wa maji unasababisha Mamlaka ya Maji kukosa mapato na hivyo kufanya mamlaka hizo kushindwa kutoa huduma za usambazaji maji kadri inavyostashili. Nimesikitishwa zaidi na lengo la kupunguza kiwango cha upotevu huo hadi asilimia 30 ifikapo mwaka 2015. Ni jambo la kushangaza sana kuona mipango ya Wizara hii ni kupunguza upotevu wa maji kutoka asilimia 33 – 30 kiasi cha asilimia tatu tu, pamoja na Wizara kufahamu athari kubwa ya tatizo la poteve wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Jiji la Dar es Salaam pekee, upotevu wa maji ni zaidi ya asilimia 48. Upotevu huu umesababisha hasara kubwa sana na kukosekana kwa mapato kwa mamlaka hizo ambayo hupelekea mamlaka hizo za DAWASA, DAWASCO kushindwa kuboresha upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam. Bagamoyo, Kibaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. JAJI FREDERICK M. WEREMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaiunga mkono hoja na ninamtakia Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya kila la kheri katika matibabu yake na Mwenyezi Mungu amjalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada kubwa za kutosha katika sekta ya maji zinafanywa. Ninampongeza Waziri na wataalam mahiri katika kufanikisha miradi ya maji. Hata hivyo, nimeona Wizara imefungua maeneo mapya ambayo kwa muda mrefu hayakuwa na miradi ya maji. Maeneo hayo ni pamoja na Kongoto, Wegero, Buswahili na Kiagota, ingawa imeonyeshwa kwamba Wizara inaisaidia Halmashauri ya Musoma Vijiji, ninashauri kwamba Wizara isimamie miradi hiyo ambayo kushindwa kwake itakuwa ni kero na upotevu wa rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Mkono, Mbunge wa Musoma Vijiji amesema kwa hisia kali na nadhani mtu yejote anayeyafahamu maeneo hayo atasema hivyo hivyo. Halmashauri hiyo ilipewa mradi wa maji na Mbunge lakini imekuwa fedheha kubwa. Aidha, Bwawa la Wegero linahitaji utaalamu ambao unapita kimo cha wataalamu wa Halmashauri, nashauri Wizara iingilie kati. Maeneo hayo yanastahili kushirikishwa katika maendeleo ya maji.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa jitihada wanazofanya katika tatizo la maji katika maeneo mbalimbali, tunaomba jitihada hizi ziendelezwe. Kwa hali hii naunga mkono hoja. Pamoja na hayo, naomba kutoa maoni/maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Mji wa Manyoni Mjini, mradi huu ambaou natekeleza kwa ubia baina ya Halmashauri na Shirika la Kidini la *Precious Blood*, utekeleza jijini umefikia 70%, hapa tunatambua mchango wa Wizara yenu katika kutekeleza mradi huu. Kwa kuwa mradi huu haujakkiliwa tunaomba Wizara iendelee kutuunga mkono kazi zinazobaki na ujenzi wa tenki kubwa la ujazo wa lita milioni mbili pia gharama za ununuzi wa mabomba ya inchi nane na kuyasambaza. Mchango wa Wizara unahitajika katika kukamilisha mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa maji Kintinku/Lusilile, mradi huu upo chini ya fedha za *World Bank* ambapo mkandarasi amechimba visima lakini amekosa maji. Ushauri ni kwamba kwenye muinuko wa Mbwesa/Saranda kuna visima vya maji zaidi ya vinne vimifunika, hivyo maji hayo yavutwe katika Mbwesa hadi Kintinko/Lusilile na kwa kufanya hivyo vijiji vya njiani litakapopita bomba la maji navyo vipate maji, vijiji hivyo ni Chilejeho, Mweni na Mwimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bwawa la Mbwesa, katika eneo la Mbwesa kuna *site nzuri* ya kuziba mto ni kutengeneza bwawa, wataalamu wa maji wamekagua eneo hili (*gorge*) na kuridhika kwamba ni *site nzuri* ya bwawa kubwa litakalotumika kwa binadamu, mifugo na umwagiliaji. Tunaomba Wizara ituunge mkono kwa kuitia programu yenu ya kutengeneza mabwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchimbaji wa mabwawa madogo madogo, maeneo ya ukanda wa kati ni kame, yanapata mvua kidogo na kwa kipindi kifupi. Namna moja ya kusaidia upatikanaji wa maji ni uchimbaji wa mabwawa madogo madogo kuvuna maji ya mvua. Mabwawa hayo yana gharama ndogo na utaalamu mdogo. Wizara ikileta makatapila ya kuchimba mabwawa sisi tutachangia dizeli. Jambo hili linawezekana kwa kushirikiana na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. MATHIAS M. CHIKAWE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri ya Bajeti pamoja na kwamba hali yake ya kiafya si nzuri sana. Namwomba Mola ampe afya njema na nguvu ili arejee kuja kutekeleza majukumu yake ya ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri na Wizara yake kwa kuanza utekelezaji wa mradi wa maji wa Masasi/Nachingwea. Mradi huu wa Mbwinyi umeanza na tunategemea ifikapo mwezi Mei mwakani tatizo la maji Nachingwea Mjini litakwisha. Kwa hili nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa vijiji kumi wa Benki ya Dunia, taarifa ambazo Wizara imetoa si sahihi, mpaka sasa Nachingwea vimepatikana visima vinne tu na siyo saba kama inavyosema taarifa, naomba Wizara ifanye masahihisho hayo.

Aidha, hata hivyo vinne, bado havijakamilika uchimbaji tayari lakini usambazaji na utumiaji bado. Wizara ikamilishe visima hivyo ili vianze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja hii.

MHE. VICKY P. KAMATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Mungu kupata fursa ya kuchangia kwa maandishi katika Wizara hii muhimu ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuipongeza Serikali kwa mipango yake madhubuti ya kuondoa tatizo la maji katika Mkoa wangu mpya wa Geita. Naipongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo naomba Serikali kupitia Wizara husika itoe elimu ya kutosha kwa Madiwani wa Geita ili Madiwani hao waisambaze kwa wananchi. Nasema hivi kwa sababu moja kubwa, kumekuwa na maneno maneno yanasantazwa na baadhi ya Madiwani kwamba chanzo cha maji cha Nungwe si chanzo chenye maji safi na salama kwa wanadamu na hata wanyama.

Kwa imani yangu sitarajji Serikali kwa kushirikiana na *Geita Gold Mining* wanaweza kusambaza maji ambayo hayajafanyiwa utafiti na wataalam wakajiridhisha kwamba maji hayo ni salama kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali leo hii itoe tamko kwa wananchi wa Geita ili wawe radhi na mradi huo uweze kuanza mara moja kusudi tatizo la maji liwe historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni hayo naunga hoja mkono asilimia mia kwa mia.

MHE. SAIDI R. BWANAMDOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba nzuri ya Wizara naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya maji toka Benki ya Dunia, miradi hii inasusua sana takribani nchi nzima. Ni vizuri Serikali ikaona jinsi ya kuikamilisha miradi hii mapema zaidi kwani wananchi wengi sasa wameonesha kutokuwa na imani na Serikali yao juu ya miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Jimbo la Chalinze kuna miradi sita ya aina hii ambayo kwa muda mrefu sasa wananchi hawaoni kinachoendelea, ni vizuri kuingilia katili ili miradi hii ikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itoe fedha za miradi ya maji, katika Mradi wa Chalinze kuna ucheleweshaji mkubwa wa kutoa fedha za ujenzi wa miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ione haja ya kutoa fedha hizo ili mradi ukamilike kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuboresha maji Jijini Dar es Salaam, ni muda muafaka sasa kwa Serikali kuchukua hatua madhubuti ili kuhakikisha kuwa maji katika Jiji la Dar es Salaam yanapatikana kwa kiwango kikubwa.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi vijiji katika sehemu nyiningi nchini wanatumia maji yasiyo salama na hivyo kuhatarisha afya zao, je, Serikali ina mpango gani wa kunusuru afya za wananchi vijiji?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kwa taarifa iliyonayo Wizara kuna mikoa yoyote ambayo angalau nguvu kubwa ya Serikali ilielekezwa au mikoa yote ina matatizo sawa kutokana na kila mwaka fedha kidogo kidogo inapelekwa kila mahali?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matumaini ya kupunguza tatizo la maji nchini?

MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA: Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia Waziri Mheshimiwa Profesa Mwandosya apone haraka ili arejee nchini haraka na aendelee kuingoza Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kubuni utaratibu wa kuigawa nchi katika mabonde tisa ya maji. Ni jambo jema kwa kuzingatia kwamba nchi yetu ina eneo kubwa lakini vilevile matatizo yanatofautiana mahali na mahali.

Jukumu la taasisi hizi ni kubaini vyanzo vya maji kwamba maji ya kutosha yanapatikana na yanafuatiiliwa hadi yanapofikia mahali pa kutumiwa. Hivyo mabonde yanajihusisha na usalama wa vyanzo vya maji, mabadiliko ya tabianchi, matumizi ya maji kwa usafiri, matumizi ya maji katika viwanda, matumizi ya maji ya umwagiliaji, matumizi ya maji majumbani, uchafuzi wa maji unaoleta madhara ya afya, *internationally shared waters* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni kwamba shughuli nilizoorodhesha zinagusa Wizara nyingi na baadhi ya Wizara zina sheria na kanuni zinazoelekeza sehemu zinazozihu. Nataka kushauri kwamba kutokana na sura ya utambuka wa shughuli za mabonde, mabonde haya yangekuwa chini ya Wizara yenye dhamana ya Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na wasaidizi wake kwa kazi nzuri wanayofanya na kwa hotuba makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri.

MHE. JOHN M. SHIBUDA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa nasema ahadi za kutekelezwa, ahadi ya Mheshimiwa Rais za 2005 – 2010 hadi leo 2011 hazina mpango maalum wa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nakumbusha kwa barua na majadiliano na Waziri Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya nina maandishi mengi ya barua za kuahidiwa utekelzaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ahadi ni deni na ahadi hizo bado kutolewa utambulisho makini kwa hiyo sasa kuitia mchango huu wa maandishi naiomba Serikali itamke hapa Bungeni ni lini nitapatiwa majibu makini kwa hoja zote za madai ya huduma ya maji katika Wilaya ya Maswa?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inataka nifuutilie wapi ili mahitaji ya kuisimamia Serikali ya Kikatiba yaye nimeyafaulisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi za toka aliyekuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ndugu Edward Lowassa na ahadi za Mheshimiwa Rais Dkt. Kikwete hivi sasa zinaipaka matope Serikali. Naomba tamko la Serikali je, zipo hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Maswa wanashukuru kwa maneno ya matumaini. Sasa naomba kauli za Serikali kuhusu utekelezaji unaotegemewa na lini utaanza kutoka Serikalini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba majibu.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kupongeza Wizara hii kwa jitihada kubwa inayofanya. Pia natoa pole kwa Waziri Mheshimiwa Profesa Mwandosya, namwomba Mungu apone haraka ili kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji ni kero kwa wanawake na watoto wa Tanzania kwani inhabidi watumie muda mwingi kutafuta maji ikiwemo kutembea mwendo mrefu. Hivyo kutatua tatizo hili ni kuleta maendeleo ya mwanamke na mtoto kwa kuwapunguzia mzigo wa kazi hivyo kupunguza vifo nya mama wajawazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Manispaa ya Iringa hasa maeneo ya Kata ya Nduli ambayo ni kata mpya wanakabiliwa na tatizo kubwa la maji. Uwezo wa *IRUWASA* ni mdogo kuweza kutawanya maji kwa haraka, hivyo tunaomba Wizara isaidie hii bodi ili iweze kupata uwezo wa kusambaza maji kwa kasi inayolingana na ukuwasji wa kasi ya ongezeko la watu katika Manispaa ya Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia iangalie na isaidie Halmashauri ya Mji wa Njombe ili kutatua tatizo la maji katika Mji wa Njombe na Kata zake ikiwemo Kata ya Kifanya, Mji wa Njombe una tatizo kubwa la maji. Pia watu wanaongezeka kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iringa Vijijini ina tatizo la maji hasa Tarafa ya Isimani na maeneo ya Magulilwa. Hivyo Serikali ichimbe malambo ambayo yatasaidia kupata maji ya umwagiliaji na maji kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, VAT 20% iondolewa kwa malipo ya hiari. Nawasilisha.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja ya Wizara ya Maji kwa maandishi, na kabla ya kuanza kuchangia naomba kuwapongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji ni Wizara mtambuka hasa unapofikiria na kuona umuhimu wa maji katika uhai wa binadamu na viumbi vyote na hata mimea katika kukua na hata kustawi kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu huo katika uhai Wizara imekuwa inajitahidi sana katika kupunguza tatizo la maji ambalo ni kubwa sana katika baadhi ya maeneo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji limekuwa linasaidiwa na wadau mbalimbali wanachangia misaada katika baadhi ya maeneo ili kuisaidia Serikali na wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Serikali kuhakikisha maji yanapatikana inaonekana dhahiri kwamba fedha zinazotumika hasa katika uchimbaji wa visima ni nyngi. Tatizo ni kuwa miradi mingi inafanyika bila kushirikisha jamii katika maeneo husika, matokeo yake ni kwamba visima vingi ni vya gharama kubwa vinavyochimbwa havitou maji na vichache vinavyotoa maji vinakosa ulinzi na utunzaji na hivyo mara vinapoharibika au kushindwa kulipa bili za umeme wananchi hukosa maji kwa kipindi kirefu. Mimi nashauri Serikali kuwa wananchi washirikishwe kikamilifu katika *projects* za maji na wakabidhiwe kwa uendeshaji na utunzaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha nyngi za miradi ya maji zinapelekwa katika Halmashauri zote nchini. Lakini fedha hizi katika maeneo mengi hazitumiki vizuri laiti ingekuwa hivyo tatizo la maji lingekuwa limepungua kwa kiwango kikubwa. Nashauri Serikali kuitia Wizara isimamie kwa karibu fedha zote zinazopelekwa katika Halmashauri ili zitumike ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya katika Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *World Bank* wa vijiji kumi kila Wilaya, katika Wilaya ya Iringa upembuzi yakinifu ulifanyika na *NORPLAN*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NORPLAN* walieleza kwamba vijiji vya Lumuli, Isupilo na Itengulinji maji yanayopatikana maeneo hayo yalikuwa si salama kwa hiyo uchimbaji wa visima haukupendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la *NORPLAN* ni kuchukua maji kwa njia ya *gravitation* kutoka Mlima wa Maboga kwa gharama ya shilingi bilioni 5.5; je, mradi huu sasa utaanza lini?

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa jitihada zake za kufanya kazi nzuri katika mazingira magumu ya Bajeti ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ngara ina vijiji 73. Vijiji vyote hivyo havina maji safi, hakuna visima vilivyo chimbwa na hakuna mabwawa yaliyo chimbwa. Watu wanahangaika kuchota maji kilomita mbili au tatu kutoka mabondeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya Benki ya Dunia ya kuchimba visima katika vijiji 13 imeshindikana au haijatekelezwa wakati wananchi katika vijiji hivyo walishachanga fedha shilingi 3,000,000/= kila kijiji fedha hiyo inazidi kupungua kutoptaka na makato ya benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nydingine kwa Wizara ni kuhakikisha usambazaji wa maji safi uwe ni kwa nchi nzima hata kwa Wilaya za pembezoni kama Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, semina kwa wananchi kuhusu uvunaji wa maji ya mvua zifanyike nchi nzima. Sina hakika kama semina hizo zimefanyika Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ihakikishe vijiji 13 ambavyo tumekubaliwa kupata maji ya mradi wa Benki ya Dunia mwaka huu wa fedha (2011/2012) tuyapate maji hayo. Vijiji vinavyohusika ambavyo vinatakiwa kupata maji mwaka huu ni Rulenge, Mbuba na Ngundusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la wataalam wa maji, naiomba Wizara iwe makini katika kufuatilia kazi za wataalam wa maji katika Wilaya mbalimbali kufuatilia kazi wanazofanya ikiwa ni pamoja na uadilifu wao. Mara nyigi wataalamu wanaokuwa *posted* katika wilaya za pembezoni kama Wilaya ya Ngara wanajiona kama wapo likizo. Inawezekana fedha zinazotumwa kwa ajili ya uendelezaji wa maji zisitumike zote kwa madhumuni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ichunguze matumizi ya fedha za maji Wilayani Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule zote 22 za sekondari za Kata hazina maji kabisa, naiomba Wizara inisaidie kuzipatia shule hizi maji kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kila la heri.

MHE. AMINA N. MAKILLAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu juu ya hoja muhimu ya Bajeti ya Wizara ya Maji. Wizara ambayo ni muhimu kwa uhai wa wananchi wetu hasa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Waziri wa Maji Mheshimiwa Profesa Mark James Mwandoza, Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer Gerson Hosea Lwenge*, Katibu Mkuu Mheshimiwa Christopher Sayi, Naibu Katibu Mkuu Mheshimiwa Bashiri Mrindoko na wote walio tayarisha Bajeti hii. Pia naomba kumpa pole Waziri Mheshimiwa Profesa Mwandoza kwa kuumwa. Namtakia afya njema apone haraka na kurejea nyumbani kuendelea na majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nije katika kuchangia Bajeti hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono Bajeti hii kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Sekta hii, kwa mantiki hiyo mimi ni msimamizi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, pia naunga mkono Bajeti hii kwa kuwa randama ya Bajeti hii imetayarishwa vizuri na tatu, naomba kuzungumzia upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukrani nyingi sana kwa Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika chanzo cha Mto Ruvu, Kitunda, Mgezi na Mpiji ili kuwezesha dhamira ya Rais wetu shupavu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Ilani ya CCM iweze kutekelezwa ili itakapofika mwaka 2014 wananchi wa Dar es Salaam wawe wanapata maji safi na salama kwa kiwango cha 80%. Pamoja na shukrani naomba kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu, naomba kuishauri Serikali (Hazina) kutoa fedha kwa ajili ya chanzo cha Ruvu, Kimbiji, Mipera na Kitunda haraka kwa Mamlaka husika ili utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa miundombinu iweze kuanza mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa fedha iliyotengwa kwa ajili ya mradi huu ni matarajio ya fedha za nje. Naishauri Serikali longeze kasi ya kuwafuatilia wadau wetu wa mradi huu ili waweze kutuletea fedha kwa wakati ili fedha iliyokadiriwa iendane na malengo yetu na kututumika kuingia gharama za mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2012/2012, 2013/2014 Serikali ijitahidi kutenga fedha zaidi za ndani kwa ajili ya mradi huu ili pakitokea dharura ya wadau wetu kushindwa kutusaidia mradi huu uendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la maji vijijini, naomba niipongeze Serikali kwa kazi nzuri inayofanya kuhakikisha wananchi walio vijijini wanapata maji safi na salama kwa kutumia vyanzo vya maji yaliyo juu ya ardhi na chini ya ardhi na kuwawezesha Watanzania wanaoishi vijijini kupata huduma hii kwa kiwango kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakipongeza Chama cha Mapinduzi na Serikali yake kwa kutambua kwamba pamoja na mafanikio yaliyopatikana bado lipo tatizo kubwa sana la maji na hivyo kuititia Ilani yake ikatamka wazi tatizo hilo la kuweka dhamira ya kuhakikisha itakapofika mwaka 2015 wananchi wa vijijini wanapata maji safi na salama kwa kiwango cha juu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi, naomba kuishauri Serikali kuhakikisha fedha hiyo iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji vijijini inatolewa kwa wakati na inafika katika mamlaka husika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa miradi ya maji vijijini lazima isimamiwe kikamilifu ili kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuondoa kasoro za kuchimba visima kasha ukosa maji na kadhalika na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa vijiji kumi, mpango wa visima vya maji katika vijiji kumi katika kila Halmashauri unaofadhiliwa na Benki ya Dunia umekuwa ni mkombozi katika vijiji ambavyo mradi huu umekamilika. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana lipo tatizo la mradi huu kusuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ningependa Serikali iwaambie Watanzania hasa wanawake tatizo hasa ni nini la kusuasua kwa mpango huu wenye lengo la kuwakomboa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tatizo ni Serikali kutokuwa na wataalam wa kutosha tujue, pamoja na mipango iliyopo ya kuwapata wataalam hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tatizo ni wananchi kutokuwa tayari kuchangia ghamra za mradi tujue na pia mipango iliyopo ya kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuchangia mradi huo kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tatizo ni ushindani wetu katika Benki ya Dunia tujue. Na Benki ya Dunia wanasema nini juu ya kutekeleza dhamira yao hii njema ya kunusuru uhai wa Watanzania kwa kuwapatia wananchi wake maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bodi za Maji, naishukuru Serikali kwa mpango wake wa kuimarisha Bodi za Maji Mijini na vijijini ili ziweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iendelee na mkakati wake wa kuhakikisha bodi za maji zinakuwa na uwiano kwa hususan 50/50 kati ya wanawake na wanaume kwa sababu mahali ambapo bodi zimekuwa na uwiano ulio sawa kati ya wanawake na wanaume, bodi hizo zimefanya kazi nzuri sana katika mamlaka zao na kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kufikisha hoja kwa wananchi wanaozungukwa na vyanzo vya maji ya Ziwa na Mito na yaliyo chini ya ardhi Serikali ni lazima iweke mkakati wa makusudi kabisa kufikisha maji kwa wananchi walio karibu na vyanzo hivyo kama ilivyofanya katika Mto Wami. Bila kufanya hivyo matokeo yake ni miradi kufanyiwe hujuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa jitihada zifanyike ili maji ya vyanzo vya maji ya Ziwa Victoria yawafikie pia wananchi wa vijiji vya Mikoa ya Mwanza, Mara, Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kushauri haya, naunga mkono hoja.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali Mwaka 2011/2012 - Wizara ya Maji

(Majadiliano yanaendelea)

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mnyaa.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako, kuhusiana na matukio tofauti ambayo yametokea katika Bunge lako, pamoja na hili la leo la punde tu, kwamba, Bunge hili la Kumi katika kipindi hiki cha bajeti, limeshuhudia mambo ambayo yametokea na baadaye kupatiwa ufumbuzi katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili la Kumi katika kipindi hiki cha bajeti, limejitokeza suala la umeme wa dharura na baadaye Wizara ya Nishati na Madini ikaahirishwa, ikaja tena na baadaye Serikali ikaweza kuleta *package* ya *solution* ya tatizo la umeme. Vile vile, limetokea tatizo la baadhi ya miji kukosa umeme na baadaye ikatokea hoja hapa na Serikali ikaamriwa, baadaye Waziri akaleta maelezo binafsi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo kama hili ambalo tumelishuhudia sote, tatizo la muda la kubadilishwa Kanuni kiasi ambacho mijadala haiwezekani wakati mwingine kuhitimishwa ipasavyo na Mbunge kuweza kumhoji Waziri ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kutokana na hali hii yote, leo ndio tunashuhudia Mabunge kama ya Uingereza kuwa na *full time job*, siyo ya vipindi vinne kwa mwaka kama linavyofanya Bunge la Jamhuri ya Muungano. Tunashuhudia umuhimu wa Bunge la Kenya kuwa na muda mrefu wote na kuweza kufanya kazi na Mbunge akaweza kufanya kama hizi kazi ambazo zimefanywa mara hii za Kibunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako: Je, Serikali haijaona au hujaona umuhimu wa Bunge lako kuwa na *full time job*, ili tuweze kufanya kazi zetu kama ipasavyo? Kuliko siku zote kukosa muda na ikawa tunarukia mambo tu? Naomba Mwongozo wako. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mimi nakushukuru sana Mheshimiwa Mnyaa, umezungumza jambo ambalo ni la kweli kwamba, Bunge hili lina majukumu makubwa na mazito, lakini muda kwa kweli wa kushughulikia mambo hayo umekuwa hautoshi. Hii ni changamoto ya Waheshimiwa Wabunge wote, ni changamoto ya Kamati ya Uongozi, ni changamoto ya Tume ya Huduma za Bunge, ni changamoto ya Serikali, ni changamoto ya Kibajeti, ni jambo ambalo kwa kweli niwahakikishie Uongozi wa Bunge, tunalo, tunalitazama kwa mapana yake ili huko tuendako tuweze kutazama namna bora zaidi ya kulitendea haki Bunge letu katika uwakilishi wake kwa kazi zake ambazo linafanya. (*Makofii*)

Kwa hiyo, niseme ni hoja ambayo sisi tunaipokea, mtuachie tuendelee kuifanyia kazi kwa pamoja na tutafika mahali tutaelewana namna tutakavyokwenda. Kwa sasa naomba nimwite moja kwa moja Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Injinia Lwenge, karibu sana.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba niwasilishe salamu za rambirambi kutoka kwa Mheshimiwa Profesa Mwandosya, anaomba kutoa rambirambi kwa msiba ambao Bunge tumeupata, kwa kufiwa na Mheshimiwa Mussa Khamis Silima - Mwakilishi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Naomba sana kwa niaba ya Wizara ya Maji, pamoja na Viongozi wote, Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hii ni mara ya kwanza, naomba mnivumilie, niseme machache maana ndio nachangia kwa mara ya kwanza. Kwanza namshukuru Mungu kwa mengi aliyonitendea ikiwa ni pamoja na kunifikisha hapa Bungeni. Nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Njombe Magharibi, kwa kuniamini na kunipigia kura nyingi za kishindo. Naomba sana wananchi wote wa Tarafa ya Imalinyi, Mdandu na Wanging'ombe msiwasikilize kabisa walioshindwa kwenye uchaguzi, leo wanapita na kuwadanganya. Mbunge wenu niko Bungeni na niko imara na ninatekeleza ahadi nilizoahidi ndani ya llani ya CCM. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kunteua kuwa Naibu Waziri wa Maji. Nitaifanya kazi hii kwa uadilifu mkubwa. Nampongeza Mheshimiwa Naibu Spika, Spika, Wenyevitii wote wa Bunge pamoja na Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwenu kuwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, japo sio kwa umuhimu, nawashukuru sana familia yangu yote popote ilipo na ndugu wote katika Kristo ambao tuna imani moja, kwa kunivumilia na kuniombea mimi pamoja na Bunge lote kwa ujumla. Mungu awabariki wote, amina.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hoja hii, kwanza naomba nitoe taarifa kwamba Waziri wa Maji anaendelea vizuri hospitali na leo nimeongea naye. Naomba nitoe taarifa pia, habari zilizoandikwa na gazeti la dira juzi, kwamba Waziri wa Maji amejiuzulu, siyo za kweli. Hajawahi kuandika barua ya aina hiyo. Hayo ni mambo ambayo wanataka watu watafaruku tu katika kuchangia hoja hii ya Wizara ya Maji na Waziri Mwandosya, kila siku tunapigiana naye simu, anaendelea kutuelekeza namna ya kuboresha huduma ya maji. Ni Waziri ambaye anapenda uongozi wa pamoja, ni shupavu na ana upendo. Kwa hiyo, naomba tumwombee arudi haraka aweze kuendeleza uongozi wa Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hoja hii, kwanza naomba nielezee changamoto chache ambazo sekta hii imekuwa inazipata. Kwanza kumekuwa na tatizo kubwa la idadi ya ongezeko la watu. Tumekuwa na miradi ya maji karibu kila mahali, sasa miradi ile mingi ilijengwa miaka mingi, mingine ina miaka zaidi ya 40. Huwezi kutegemea mradi wa miaka 40 bado ukidhi kiwango cha kutoa huduma ya maji kwa hali ya sasa. Kwa hiyo, tunahitaji miradi ile tuiboreshe, tuikarabati ili iweze kukidhi mahitaji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili, mabadiliko ya tabia ya nchi; najua wananchi mnajua kwamba, hali ya maji inapungua siku hadi siku kwa sababu ya tabia ya nchi na pia kuna raslimali za maji zinapungua kwa sababu vyanzo vingi vya maji vimeendelea kuharibiwa kwa sababu ya majukumu mbalimbali. Viwanda vimetanuka, mambo ya kilimo, kwa hiyo, raslimali za maji kila siku zinapungua. Kwa hiyo, hizo ni changamoto ambazo tunazikabili na kupambana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utangulizi, naomba kwanza nijibu hoja za Kamati ya Bunge ya Kudumu ambayo inashughulika na Kilimo, Mifugo na Maji. Kwanza kulikuwa na hoja kwamba Serikali iangalie umuhimu wa maji kwa viumbe na kilimo hivyo kuongeza bajeti ya Wizara hii inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu ni kwamba, katika Mpango wa Miaka Mitano, bajeti ya miradi ya maendeleo ya fedha ilikuwa kama ifuatavyo: Shilingi bilioni 78 mwaka 2006/2007, Shilingi bilioni 75 mwaka 2007/2008, Shilingi bilioni 46 mwaka 2008/2009, Shilingi bilioni 50 mwaka 2009/2010 na Shilingi bilioni 30 mwaka 2010/2011. Kutokana na mwendendo huo, Serikali imekuwa ikifanya juhudui kuongeza mapato yake ili kuongeza bajeti ya Sekta ya Maji. Serikali imeongeza fedha ndani ya bajeti hii ya mwaka 2010 kufikisha Shilingi bilioni 41.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi kweli hazitoshii, lakini kutokana na mipango ambayo tunayo ya miaka mitano, Serikali imeweka Sekta ya Maji kama ni kipaumbele baada ya miundombinu ya umeme, tunasema kinachofuata ni maji. Tunataka tufikishe mahali Serikali iamue kwamba, Sekta ya Maji ipate kipaumbele kama tulivyofanya kwenye afya, kwenye elimu na kwenye barabara. Kwa hiyo, hii ni mipango ambayo Serikali imeahidi, Rais Kikwete mwenyewe ameahidi na ndani ya Bunge hili kwamba, Serikali itaongeza kiwango cha bajeti katika fedha za ndani katika huu mpango wa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine kuhusu suala la kupunguza utegemezi, nimeshalijibu. Hoja nyiningine ilikuwa Serikali ihakikishe kwamba, utafiti wa kina unafanyika kabla ya kuchimba visima ili kuepeuka upotevu wa fedha nyangi zinazotumika kuchimba visima vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu ni kwamba, Wizara inatambua adha wanayoipata wananchi kutokana na kukosa maji katika visima vinavyochimbwa. Pamoja na kuwa upatikanaji wa maji chini ya ardhi kwa Tanzania uko kati ya asilimia 50 mpaka asilimia 70, hali hiyo huchangiwa vilevile na tabia ya baadhi ya wahusika kutofuata taratibu zilizoainishwa na Sheria ya Maji, ambapo wachimbaji hupaswa kupata idhini kutoka kwa Afisa wa Bonde wa Maji, ambapo kisima hicho huchimbwa. Maafisa wa Maji wanao wataalamu ambao wanaweza kuhakiki taarifa za utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine ilikuwa, Serikali iweke mkakati wa kuvitazama upya visima vya asili ili viweze kupunguza tati zo la maji. Jibu ni kwamba Wizara inaendelea na zoezi la kuvitambua vyanzo vyote vya maji vikiwemo visima vya asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine ilikuwa visima vifupi vichimbwe wakati wa majira ya kiangazi ili kuhakikisha maji yanapatikana. Nakubaliana na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali kutoa elimu kwa wananchi juu ya athari za mabadiliko ya tabia ya nchi, pamoja na maelezo yaliyoleezwa katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maji, aya Na. 189 Wizara imemwajiri Mtaalamu Mshauri, anayetathmini athari za mabadiliko ya tabia nchi katika raslimali za maji na kupendekeza njia stahiki ya kukabiliana na athari hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine ni kwamba uchafuzi wa vyanzo vya maji kutokana na matumizi ya kemikali katika maeneo ya uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kuititia Ofisi za Mabonde, itashirikiana na *NEMC* kuimarisha kaguzi na kudhibiti uchafuzi unaotokana na uchimbaji wa madini kwa kufanya uperembaji kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya maji na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kwamba, Wizara ifanye uchunguzi wa kina katika maeneo mbalimbali kuchimba visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokea na Wizara itaendelea kufanya utafiti mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa, Serikali iendelee kuhimiza na kuhamasisha jamii kwa kutoa elimu ya utaratibu wa uvunaji wa maji ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu ni kwamba, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010 Serikali imehamasisha uvunaji wa maji ya mvua. Jumla ya matanki nane yamekarabatiwa, matanki 271 yamejengwa mwaka 2011/2012. Serikali kwa kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira, itatoa mafunzo kwa mafundi wawili kutoka kila Kijiji ya namna ya kujenga matanki yatakayohifadhi maji ya mvua. Aidha, matanki ya aina tatu tofauti yatajengwa wakati wa ujenzi wa miradi ya maji kwenye vijiji kumi, katika kila Halmashauri. Lengo ni kuwapa fursa wananchi kuona na kuiga teknolojia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nijibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Kambi ya Upinzani. Kwa sehemu kubwa, hoja yao ilikuwa ime-base kwenye hoja ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme tu kwamba, hoja ni jambo lingine na majibu ni jambo la pili. Taarifa ambayo ameitumia Mwakilishi wa Hoja ya Upinzani, ameitumia kama vile hoja ilivyotolewa. Lakini baada ya kutolewa hoja na zile fedha ambazo zimehojiwa, yeye amezichukulia kama ndiyo ubadhirifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili siyo kweli kwamba ukishatoa hoja yanatolewa maelezo. Mara nyingine inakuwa nyaraka hazionekani, lakini nyaraka zikishaletwa, Auditor anaridhika. Kwa ujumla ni kwamba, hoja hii baada ya kuletwa, Serikali imelifanyia kazi kwa ukamilifu, tumetoa majibu ya kila kipengele na Auditor ameridhika. Kwa hiyo, kama hajaridhika huwa ana-re-issue na kama kuna jambo, kuna mtu ye yote ambaye ndani ya hoja ile anaonekana amefanya ubadhirifu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, amepewa madaraka ya kumshughulikia huyu ambaye amefanya ubadhirifu na kumpeleka kwenye vyombo vya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo suala naomba niwahakikishie Wabunge wenzangu kwamba mpaka sasa halijathibitika kwamba kuna mtu ye yote katika hoja ile ambaye amefanya ubadhirifu. Sasa niseme tu baadhi ya vipengele ambavyo vimehojiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hoja inasema, matumizi ya Dola za Kimarekani milioni 39 sawasawa na Shilingi bilioni 63 kwenye mazingira ya utata bila kuzingatia miradi hiyo kwenye mpango kazi wa mwaka.

Mheshimiwa naibu Spika, majibu ni kwamba, haya ni matumizi ya ununuzi wa vifaa mbalimbali vya miradi ambayo ilikuwa vinunuliwe katika mwaka wa fedha 2007/2008, na vilikuwa kwenye mpango wa ununuzi wa mwaka huo, lakini kutokana na kutopatikana fedha kwa wakati, vilinunuliwa mwaka 2008/2009 na 2009/2010. Vifaa vilivyonunuliwa ni pamoja na jenereta lilioko Ofisi ya Maji Makao Makuu. Ukarabati wa majengo ya Ofisi ya Wizara, ununuzi wa vifaa vya kupimia, wingi wa maji chini ya ardhi, vifaa vya ramani, vifaa vya Maabara, vifaa vya Ofisi kama kompyuta na mashine za kudurufia na mashine za kiofisi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Waheshimiwa Wabunge mfahamu kwamba hii Programu ya Sekta ya Maji wanaoitekeleza ni wengi sana. Ni pamoja na Halmashauri za Wilaya zote. Kwa hiyo, inajumuisha watu wengi ambao wanaitekeleza. Kwa hiyo, hoja ili-cover maeneo mengi na hayo yote ndiyo tumeweza kuyatolea maelezo na kujibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni ununuzi wa mashangingi yapatayo 68 kwa jumla ya Yen 235.4 sawa na zaidi ya Shilingi bilioni tano bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ni kwamba magari yaliyonunuliwa siyo mashangingi. Mashangingi mara nyingi wanasema yale magari ambayo kwa mfano wanatumia Mawaziri. Magari yaliyonunuliwa ni *Hard Top - Land Cruiser*, ni yale magari ya kazi, sio mashangingi. Kwa hiyo, naomba wananchi wafahamu ni yale magari ya kawaida na kwamba, magari yaliyonunuliwa yalikuwa 82, siyo magari 68. Magari hayo yaligawiwa kwa Halmashauri za Wilaya na Miji nchi nzima, pamoja na Ofisi za Mabonde, kusaidia utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyine iliyotolewa ilihusu kutokuwa na ufuutiliaji wa karibu wa pesa za miradi ya maji zinazopelekwa nchi nzima kwenye miradi ya maji iliyoko katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kweli kwamba Wizara haifuutilii utekelezaji wa Miradi. Ufuutiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maji hufanywa kwa ngazi zote. Kwanza, ukaguzi wa pamoja kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo, *Joint Supervision Missions*, hufanyika kila baada ya miezi sita. Aidha, Wizara hushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kufanya ufuutiliaji katika Halmashauri, mara mbili kwa mwaka kwa nyakati tofauti na zile za ukaguzi wa pamoja na washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa nayo hupitia Ofisi za Washauri wa Maji wa Mikoa, kufanya ufuutiliaji wa utekelezaji wa mradi katika Halmashauri za Wilaya kila robo mwaka. Lengo la ufuutiliaji huu ni kuhakikisha kuwa matumizi ya fedha yanayofanyika yanazingatia sheria za nchi na Kanuni zake ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu wenye lengo la kuboresha matoeko ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyine ilikuwa ni matumizi makubwa katika miradi mbalimbali ya maji kuliko gharama kwenye Mkataba. Amezungumzia suala la ujenzi wa bwawa la matwiga, mkataba wa awali ulikuwa dola milioni 284 lakini zikatokea *variations* za milioni 129.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niwaelekeze Waheshimiwa Wabunge kwamba, katika mikataba, suala la kazi za nyongeza ni kitu cha kawaida. Kwa sababu unaweza ukawa na kazi ambayo viwango vya kazi vimeainishwa, lakini kwa sababu mbalimbali huwa kunakuwa na ongezeko la kazi. Kwa hiyo, kukitokea ongezeko la kazi ni lazima kunakuwa na *addendum* au *variation order*. Suala linalotakiwa hapa ni ile *addendum* ipite kwa wale wanaotakiwa kuidhinisha. Sasa haya masuala yote yallfanyika. Kwa hiyo, majibu hayo tulimpa *Auditor General* na aliridhika na majibu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la mradi wa Mpwapwa. Mkataba huu ulikuwa wa shilingi milioni 69, matumizi ya ziada yalikuwa Shilingi milioni 56. Maeleo yake yanafanana na hiyo ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba mwininge ambao umehojiwa ulikuwa ni wa Mamlaka ya Majitaka ya Moshi. Mkataba wa awali ulikuwa Shilingi milioni 485, lakini kazi ile iliongezeka mpaka ikafikia bilioni 1.5, sasa hapa kilichojitokeza ni kwamba, baada ya kumwajiri yule Mhandisi Mshauri, ulikuwa ni katika kufanya usanifu katika eneo dogo. Lakini baadaye ikaonekana kwamba, wale wafadhili ambao walikuwa wamefadhilli mradi huu, wakataka waendeleze kufanya kazi katika miji mingine ambayo ulikuwa ni miji ya Same, Mwanga na Korogwe.

Sasa kwa sababu huyu Mhandisi Mshauri alikidhi vigezo vya kuajiriwa na kwa sababu kazi ile ilikuwa inafanana, kuna utaratibu ambao hata *PPRA* inaruhusu kumwendeleza kazi Yule yule ambaye amejiriwa na ndicho kilichofanyika. Kwa hiyo, vile tulipeleka kwa *Auditor General* na ameridhika na maeleo ambayo tulyatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyine ambayo imezungumzwa ni suala la vijiji kumi. Naomba hili suala atalizungumza Mtoa Hoja, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Mahusiano na Uratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kulikuwa na hoja inahusu *DAWASA* na *EWURA* wadhibiti bei ya maji kwenye miradi ya jumuiya za wananchi. Jibu ni kwamba *DAWASA*, *DAWASCO* wameshatoa

utaratibu wa bei ya kila ndoo moja iliyochotwa kwenye miradi ya maji ilipiwe Sh. 20/=. Wasimamizi wa utaratibu huo pamoja na bei ni Serikali za Mitaa.

Hoja nyingine ilikuwa hasara ya shilingi bilioni 12.9 *DAWASCO*, hili naomba Waheshimiwa Wabunge kwamba hasara iliyotokea ni tofauti ya gharama za uendeshaji kuzidi jumla ya mapato yote kwa shilingi bilioni 12.9. Gharama zilizozidi ni pamoja na gharama za kihasibu, *financial cost*, madeni chakavu (*bad debts*), uchakavu na malipo ya kimkataba kwa *DAWASA*. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kipaumbele cha kampuni ya *DAWASCO* ni kutoa huduma siyo faida. Kwa hiyo, katika kuhoji zile *balance sheet*, kuna madeni ambayo hayawezekani kulipizwa kwa sababu zozote zile labda kampuni iliyokuwa inadaiwa kiwanda kimefungwa. Sasa haya huwa tunaita madeni chakavu. Kwa hiyo, sisi siyo hasara *in such* au kwamba ni ubadhirifu umefanywa ndani ya *DAWASCO*. Kwa hiyo, haya ni maelezo ambayo tumempelekea Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali na ameridhika na maelezo hayo.

Kulikuwa na maelezo ya matumizi mabaya ya Shilingi bilioni 12 kutoka mamlaka ya Mijini, jumla ya fedha kwenye jedwali ni shilingi bilioni 1.8. Hizi ni hundi. Zilikuwa ni hundi zilizokuwa zimeandaliwa kwa ajili ya malipo. Lakini hadi mwaka wa fedha ulipokwisha hazikuwa zimesainiwa na Afisa Masuuli, kwa hiyo, hazikuwahi kulipwa, na hadi sasa hundi hizo zipo kwa ajili ya kumbukumbu. Kwa hiyo, hundi hizi zote zimepelekwa kwa Mdhibiti. Kwa hiyo, zilionekana kama vile zililipwa, lakini zilikuwa hazijalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maelezo yote ambayo yamehojiwa na Kambi ya Upinzani, yanayohusiana na hoja hizi za ukaguzi, tumeyapeleka na kuyajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nijibu tu baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wameweza kuchangia. Nianze na hoja ya Mheshimiwa Zabein Mhita, yeeye alihoji kwamba katika mgawanyo wa vikundi, sehemu kubwa ya vijiji vimepelekwa kwenye Jimbo la Kondoa Kusini na kule Kondoa Kaskazini imebaki na vijiji viwili. Naomba nimwahidi kwamba, katika programu itakayofuata, Mheshimiwa Mhita amenifuatilia na tumezungumza na anapigania kweli kweli, tutaweka katika upande wa pili sasa utakuwa *considered zaidi* na Halmashauri kutoa vijiji vingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda hauniruhusu, naomba niseme naunga mkono hoja na naomba sana Waheshimiwa Wabunge muunge mkono hoja ya Wizara ya Maji. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mhandisi Lwenge - Naibu Waziri Maji. Nakushukuru sana kwa kupitia hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri, naomba niwatangaze wageni watatu wa Mheshimiwa Cynthia Hilder Ngoye, viongozi wa YWCA kutoka Mbeya, popote pale walipo msimame. Ahsante sana na karibuni sana akinamama. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Stephen Wasira -Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) ili kupitia hoja zake kama mtoa hoja kwa niaba ya Waziri wa Maji.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU) - (k.n.y WAZIRI WA MAJI): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kupitia hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ningependa kueleza masikitiko makubwa kutokana na msiba uliotokea wa Mheshimiwa Mbunge mwenzetu, Hayati Mussa Khamis Silima, pamoja na mke wake ambayo yote yametokea hapa Dodoma na Dar es Salaam katika muda mfupi sana. Tunasikitika sana kwa jambo hili, lakini hatuna uwezo nalo. Kwa hiyo, tunamwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho za Marehemu hawa mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliojadili, walioandika na hata walionyamaza, wote nawashukuru kwa sababu naamini hata walionyamaza wanakubaliana na waliosema kwamba tunalo tatizo kubwa la maji Tanzania. Mimi nadhani tunakubaliana. Huwezi kusimama hapa uka-*dispute* juu ya suala hili kutokuwepo maji ya kutosha. Hili ni tatizo kubwa na pamoja na kazi niliyopewa ya Uwaziri wa siku tatu wa maji, zimenitosha kabisa kuelewa uzito na ukubwa wa tatizo tulilonalo. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unahitaji tu kwenda Wizara ya Maji hata kwa siku mbili tu, ukauliza maswali, utapata majibu kwamba nchi hii ina *problem* kubwa sana ya maji. Kabla sijaingia kwa undani kueleza nilichojifunza na kilichopo, kwanza niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja hii kubwa nzito.

Kwanza kabla hata hoja hii haijaletwa, Waheshimiwa Wabunge 10 walichangia wakati nilipowasilisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, walizungumza maji. Kwa sababu muda siyo mrefu sana na kwa sababu walishatambuliwa na niliyewatambua nilikuwa mimi, kwa hiyo, naomba wanisamehe nisiwatambue tena. Lakini kwa bajeti ambayo iliwasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mkulo, Wabunge 35 walijadili na kutoa maoni yao juu ya maji. Hoja zao zote ziko pale Wizarani, zinafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, sasa Wabunge wapatao zaidi ya 150 wamechangia kwa maandishi. Hao nataka kuwatambua, maana ni wa leo hii na pengine hawajatambuliwa. Wa kwanza ni Mheshimiwa Ismail A. Rage, Mheshimiwa Augustino L. Mrema, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa Moshi S. Kakoso, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Vincent J. Nyerere, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Clara D. Mwatuka, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Jerome D. Bwanausi, Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mheshimiwa Selemani J. Zedi, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Juma S. Nkamia, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Albert O. Ntabaliba, Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla, Mheshimiwa Lucy P. Owanya, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Mwigulu L. Mcemba, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mheshimiwa Silvestry F. Koka, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Yusuph A. Nassir, Mheshimiwa Ally K. Mohamed, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Aliko N. Kibona, Mheshimiwa Eng. Christopher K. Chiza, Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro, Mheshimiwa Henry D. Shekifu, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mheshimiwa Charles M. Kitwanga na Mheshimiwa Amos G. Makalla. (*Makofii*)

Wengine ni Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Fatuma A. Mikidadi, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Goodluck J. Ole-Medeye, Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mheshimiwa Dkt. Terezya P. L. Huvisa, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mheshimiwa Dkt. Charles J. Tizeba, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Meshack J. Opulukwa, Mheshimiwa Selemani S. Jafo, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Assumper N. Mshama, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Eng. Athumani R. Mfutakamba, Mheshimiwa Dkt. Milton M. Mahanga, Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa, Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mheshimiwa Gregory G. Teu, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Abuu H. Jumaa, Mheshimiwa Charles J. Mwijage, Mheshimiwa Mendrad L. Kigola na Mheshimiwa Moses J. Machali. (*Makofii*)

Wengine ni Mheshimiwa Dkt. Augustino Lyatonga Mrema, wanajirudia, waliandika wakaandika tena, bado hii inaeleza uzito wa tatizo. Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimiwa Ally K. Mohamed, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Mheshimiwa Juma S. Nkamia, Mheshimiwa Jerome D. Bwanausi, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Stephen J. Masele, Mheshimiwa Deo K. Sanga, Mheshimiwa Innocent E. Kalogeris, Mheshimiwa Mary M. Nagu, Mheshimiwa Nyambari C. M. Nyangwine, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Naomi A. M. Kaihula, Mheshimiwa Dkt. John P. Magufuli, Mheshimiwa Modestus D. Kilufi, Mheshimiwa Philipa G. Mturano, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Dkt. Titus M. Kamani, Mheshimiwa Saleh A. Pamba, Mheshimiwa Ester L. Midimu, Mheshimiwa Dkt. Faustine E. Ndugulile, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Sylvester M. Kasulumbayi, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mheshimiwa Dkt. David M. Malole, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla, Mheshimiwa Saidi M. Mtanda,

Mheshimiwa Mch. Lackson N. Mwanjale, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Lolecia J. Bukwimba, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya na Mheshimiwa Livingstone J. Lusinde. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Eng. Ramo M. Makani, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Azza H. Hamad, Mheshimiwa Mariam N. Kisangi, Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Felix F. Mkosamali, Mheshimiwa Christina G. Ishengoma, Mheshimiwa David Z. Kafulila, Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhammed, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa AnnaMaryStella J. Mallac, Mheshimiwa Subreena H. Sungura, Mheshimiwa Susan L. A. Kiwanga, Mheshimiwa Joseph R. Selasini, Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mheshimiwa Salome D. Mwambu na Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Agripina Z. Buyogera, Mheshimiwa Josephine T. Chagulla, Mheshimiwa Abdul R. Mteketa, Mheshimiwa Mch. Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina, Mheshimiwa John S. Magalle, Mheshimiwa Albert O. Ntabaliba, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Dkt. Seif Selemay Rashidi, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Rose K. Sukum, Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila, Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo, Mheshimiwa Jaji Fredrick M. Werema, Mheshimiwa Subira K. Mgatu, Mheshimiwa Sara M. Ally, Mheshimiwa Capt. Johnn Z. Chiligati, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Margaret S. Sitta, Mheshimiwa Saidi R. Bwanamdogo, Mheshimiwa Vick P. Kamata, Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Agness E. Hokororo, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis na Mheshimiwa Beatrice M. Shelukindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hao niliwasoma, bado wengine waliongezeka, nao ni Mheshimiwa Christina L. Mughwai, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Dkt. Antony G. Mbassa, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Mheshimiwa Zaynab M. Vullu, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mheshimiwa Zarina S. Madabida, Mheshimiwa Pudenciana W. Kikwembe, Mheshimiwa Vincent J. Nyerere, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Salum K. Barwany, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda na Mheshimiwa Bahati Ali Abeid. Zaidi ya hapo, kulikuwa tena na ambao labda sikuwataja, lakini nikipata majina sahihi baadaye kabla sijamaliza nitawatambua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wafuatao 24 walisema hapa Bungeni, nao tulanza na Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ile, halafu akafuatiwa na Msemaji wa Upinzani, halafu akafuata Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Dkt. Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Abdul-Aziz M. Abood, Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Selemani J. Zedi, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Omari A. Badwel, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Munde T. Abdallah, Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Benardetha K. Mushashu, Mheshimiwa Selemani S. Bungara, Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Esther L. Midimu, Mheshimiwa Saidi M. Mtanda, Mheshimiwa Moshi S. Kakoso na Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangalla. Hao ndio waliosema na Mheshimiwa Amos G. Makalla namwongeza. (*Makofi*)

Sasa kabla sijaanza kujibu hoja, kwanza nilikuwa nimeanza kwa kukiri kwamba tunalo tatizo kubwa la maji nchini. Ningependa mjue kwanini nimelazimika kusema hivyo. Kwa sababu maji katika miji midogo ya Tanzania yanapatikana kwa wastani wa asilimia zinaanzia 30 mpaka 50, yaani hiyo ni Miji Mikuu yote ya Wilaya. Ukienda kwenye Miji Mikuu ya Mkoa, ndiyo unawenza ukaona nafuu. Lakini nafuu hiyo nayo haiko kwa miji yote. Kwa ujuzi wangu labda nianze na Miji Mikuu ya Mkoa. Miji Mikuu ya Mkoa ambayo *coverage* ya maji yake ni nafuu kabisa ni Arusha,

Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Mwanza, pamoja na kazi inayoendelea pale Mwanza Mjini na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika miji yote 19 ambayo wastani wa upatikanaji wa maji uko kwenye asilimia 75 mpaka kwenye 80 na kitu. Miji saba, maana takwimu za wastani haziwakilishi hali halisi wakati mwininge. Kwa hiyo, katika miji saba ya Makao Makuu ya Mkoo, bado tuna tatizo kubwa la maji. Miji hiyo ni Lindi, Sumbawanga, Kigoma, Babati, Musoma na Bukoba. Sijui kama imefika saba, nitakuwa nimeacha mmoja labda, lakini hiyo ndio miji ambayo kwa kweli kiwango chake cha upatikanaji wa maji kiko chini ukilinganisha na ile miji mingine ambayo hali yake ni nafuu.

Sasa jana, rafiki yangu Abood, alisema yeye haungi mkono. Sasa unajua ukienda hospitali ukakuta watu wote ni wagonjwa, wale walikoko *ICU* huwa wanahudumiwa kwanza, maana usipowahudumia watakuifa. Kwa hiyo, rafiki yangu Abood nilimwomba baada ya kuelewa hali ilivyo, sasa aunge mkono sasa maana Morogoro ina nafuu sana ukilinganisha na mji wowote wa Tanzania katika ile saba niliyoitaja. Pale *coverage* ya Morogoro Mjini ni asilimia 96, najua alikuwa anataja vijiji ambavyo vinazunguka mji wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mgawanyo wa Majimbo na vijiji vinaitwa Morogoro Mjini, wale mnaopita Morogoro ukifika Kingorwila, bado uko mjini, lakini kwa kweli Kingorwila ni Kijiji. Miaka ya zamani niliwahi kuishi pale, lakini hapabadilika sana, pako hivyo hivyo! Nilikuwa nasoma Mzumbe, nikaenda kufanya utafiti Kingorwila, nyumba nilizoiacha ni zilezile. Sasa yale ni mazingira ya vijijini.

Sasa mimi nakubaliana na Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood kwamba wale watu waliopo katika eneo lile nao wanastahili huduma, lakini ukichukua *Morogoro Urban* kama ilivyo 96% ya watu wa Morogoro Mjini wanapata maji. Kwa hiyo, mimi nilidhani Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood katika mazingira magumu ya upatikanaji wa maji Tanzania, nadhani angetuunga mkono katika hili na hasa ukizingatia kwamba kuna mradi unaotekelawa na *MCC* ambaao utaongeza zaidi upatikanaji wa maji katika Mji wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda alisema jambo ambalo lazima nikubaliane naye. Alisema sisi hatuna utamaduni wa ku-*maintain* mradi, yaani *maintenance* kwa ujumla kwa sababu ya kutokuwepo utamadumi. Mtu anaweza akadhani miaka 50 hakuna kilichofanyika, lakini ukweli ni kwamba miaka ya 1970 mpaka 1980 kulikuwa na miradi na kila Mkoo. Kulikuwa na kitu kinachoitwa *Regional Water Master Plan*. Miradi hii ambayo mnaisikia sasa, inaitwa *Handeni Truck Main*, Wanging'ombe, Mgango Butiama na miradi ya namna hiyo, ilikuwa inatekelezwa kila Mkoo. Lakini vilevile ni vizuri kujua kwamba mwaka 1961 tulipojitawala Watanzania walikuwa milioni tisa, lakini leo tupo zaidi ya milioni 40. Lakini miradi ile au haikuwa *maintained* au *investment* yetu haikwenda kasi kutohana na ongezeko la kukua kwa watu.

Kwa hiyo, ukienda Wanging'ombe unakuta watu wanaotumia ule mradi kwa sasa ni wengi kuliko waliokuwa wamekusudiwa wakati mradi ule unawekwa. Kwa hiyo, kwa namna yoyote ile lazima katika Mpango wetu wa Maendeleo wa Miaka Mitano tuweke *rehabilitation* ili miradi ile ianzo kutoa maji kwa watu wengi zaidi kuliko ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka Bunda. Mwaka 1970 na sisi tulikuwa na mradi ulioitwa *Guta Bunda Truck Main* katika hiyo *program* ya *Master Plan*. Lakini Bunda mjini kulikuwa na watu 7,000 wakati huo, leo kuna watu 83,000 na hao watu 83,000 wanakunywa maji ya watu 7,000 waliokuwa wamekusudiwa. Kwa hiyo, *obviously* patakuwa hakuna maji. Kwa hiyo, ukienda Bunda unakuta *coverage* ni 26%. Kwa sababu ni 26% ya watu 83,000, lakini ilikuwa 100% kwa watu 7,000 miaka 40 iliyopita.

Kwa hiyo, nilitaka niseme kwamba ni vizuri tuanze kutazama jambo hili, kwa miji ambayo nimeitaja kuwa ni miji ya Mkoo, lakini ina matatizo. Hiyo ndio tuna shughuli za kufanya kwa miji ya Mikoa. Kwanza Lindi, Sumbawanga, Mji wa Babati pamoja na Mji wa Kigoma imeingizwa katika mpango unaoitwa *Café W*, ndio wanaogharamia na kuanzia mwaka huu wa fedha ambaao tupo

sasa, miradi hii itaanza kusimamiwa na utekelezaji utaanza wa kupanua huduma za maji katika miji hii kwa kugharamiwa na *Café W*, Shilingi bilioni 11 zimetengwa kwa kazi hii. Kwa sababu huwezi kuweka miradi yote ikatekelezwa katika muda wa miezi 12, hata *capacity* nyenyewe ya kutekeleza haiwezekani. Lakini mategemeo yangu ni kwamba katika bajeti inayokuja ambayo ndio tunaanza mpango wa kwanza wa maendeleo ya miaka mitano, maana huu ni *zero year*, tutawekeza katika kusaidia na kuhakikisha kwamba miji hii saba ambayo ina matatizo makubwa ya maji, kwa sasa inapatiwa maji ya kutosha kama ilivyo kwa miji mingine ya Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mikoa mipya ambayo na yenyewe itahitaji maji kwa mfano tuna Mkoa wa Katavi ambao Makao Makuu yake yatakuwa Mpanda. Katika mwaka unaofuata itabidi tuanze kuweka taratibu ambazo zitawezesha kuweka huduma za maji katika miji ya Mpanda na Bariadi, Simiyu ambayo sasa itakuwa ni Makao Makuu ya Mikoa. Kwa hiyo, lazima tuweke *provision* ama sivyo, kutakuwa na *influx* kubwa ya watu na kile kilichopo sasa kitaonekana hakipo. Kwa hiyo, tunaanza tena *crisis*. Kwa hiyo, itabidi tuangalie na nitaeleza kidogo kwa Simiyu hatua ambazo tumeziamua.

Mheshimiwa Naibu Spik, kwenye Miji wa Musoma na Bukoba ambayo imezungumziwa hapa na wawakilishi akiwemo Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini na Mheshimiwa Vincent Joseph Nyerere. pale tunataka kutekeleza mpango huu kuanzia mwaka huu wa fedha na fedha zake zitaghamiwa na Ufaransa. Kwa hiyo, tunaanza utekelezaji mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema ni kwamba, kwenye Mikoa tuna Miji saba ambayo inahitaji *attention* ya haraka ili kuhakikisha kwamba wananchi wengi wanaoishi katika maeneo hayo wanapata maji safi na salama na mengi. Kwa hiyo, ni miji lakini ninacho-*argue* hapa ni jinsi hali ilivyo ngumu. Kwenye miji midogo, yaani kama nilivyosema *average* ya *coverage* katika miji midogo ni kati ya 30% na 50% na hiyo ni mingi kabisa, wala sidhani kama ninaweza kuitaja yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachowenza kusema ni kwamba Mamlaka za maji zilizopo kwenye Miji Mikuu ya Mikoa ambapo kila Mkoa una Mamlaka ya Maji, tumezipa kazi ya kusaidia kuanzisha *feasibility study* au upembuzi yakinifu na kutengeneza usanifu wa miradi kwa kuwaajiri Wahandishi wa kufanya kazi hiyo ili baadaye tunapoanza bajeti na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano kuanzia mwakani tuwe na miji ambayo tutaiweka katika *phase* ya kuanzia. Shabaha ni kuongeza kiwango cha maji katika miji yote ya Wilaya na miji midogo ili kiwango cha maji kiweze kulingana na mahitaji pamoja na ahadi zilizotolewa katika ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndio ilani inayotekelozwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kuna miji ambayo tayari wamekwishaanza kufanya usanifu na hiyo ikiwa tayari mwaka unaofuata ndio utakuwa unaingia kwenye *phase* ya kwanza ya utekelezaji kwa sababu miji hii ni mingi. Nchi hii ina miji 132 sasa ukianza kutaja mji mmoja mmoja katika miji 32 mtanipigia kengele kabla sijafika popote. Kwa hiyo, mnachotakiwa kujua ni kwamba ninajua na mimi kwamba liko tatizo la maji katika miji yetu.

Mheshimiwa William Augustao Mgimwa naye alichangia, nilikuwa nimem-*omit*, naomba aingizwe kwenye orodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hali ilivyo katika Miji ya Mikoa na Wilaya na ambayo kweli inatuhusu wote sana, sasa labda nitumie fursa hii kueleza kidogo tena kwa ufupi, kuna Mheshimiwa William Augustao Mgimwa wa Kalenga naye kumbe alichangia, unajua akina Mgimwa wako wengi kidogo humu ndani mtanisamehe.

Kwa hiyo, naomba sasa nitumie nafasi hii kusema kwamba nimezungumzia miji 19 lakini miji 12 iko katika hali nafuu lakini miji saba ina matatizo. Lakini mji mmoja wenye matatizo makubwa unaitwa Dar es Salaam, huu siwezi kuuzungumzia sana kwa sababu Dar es Salaam tumeiwekea mpango kabambe wa miaka mitano. Lazima tukiri kwamba Dar es Salaam ndio mahali ambapo watu wote wa nje wanafikia kabla hawajakwenda popote Tanzania na hapo ni lazima tukidhi mahitaji ya maji.

Tumeweka mpango kabambe ambao unahusisha uchimbaji wa visima vya Kimbiji na Mpera na tumeweka *program* kwamba nyaraka za Zabuni zinakamilishwa Septemba, 2011 kwa ajili ya uchimbaji. Zabuni inaitishwa Septemba, tunapokea Novemba na kuanza uchimbaji Januari, 2012. Matumaini yetu ya Dar es Salaam yanategemea sana uchimbaji wa visima katika eneo hili. Lakini vilevile tutafanya uchunguzi wa kina ili kuona kiwango gani cha maji na ubora wake kadri tunavyoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna bwawa la Kidunda ambalo uzuri wake ni kwamba mto wa Ruvu, *flow* ya maji yanayokwenda Dar es Salaam huwa inapungua hasa wakati wa kiangazi. Kwa hiyo, ukipungua ule mto, Dar es Salaam inakwenda bila maji. Kwa hiyo, tunajaribu kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba bwawa lile linajengwa kwa sababu itakuwa ni *reserve* ya maji ya Dar es Salaam. Maji yakipungua yata-*flow* kutoka Bwawa la Kidunda ambalo ni bwawa muhimu, lilikuwa limekusudiwa kujengwa miaka mingi iliyopita. Tumechelewa kulijenga lakini sasa tumeshatenga fedha na tumeanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani ukiwa na visima vya Kimbiji na Mpera, na ukiwa Bwawa la Kidunda uka-*improve* kama tunavyojaribu ku-*improve*, Ruvu Chini tunaijenga na maji mengi zaidi yatakuwa yanaweza kuchunjwa Ruvu Chini kabla ya kuja Dar es Salaam. Pamoja na kujenga bomba ambalo linaitwa *Parallel line* kutoka Ruvu Chini kuja kwenye *tank* la *University of Dar es Salaam* ambalo ndilo linalotumiwa Dar es Salaam katikati tukifika hapo na tukabadilisha na kutengeneza kama tulivyokusudia Ruvu juu na kuweka bomba linalokuja mpaka Kimara, sehemu nyingi za Dar es Salaam zitapata maji. Ndiyo maana tunaamini kwamba maji yatapatikana ifikapo mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema kwamba Rais alisema mwaka 2013 na ninyi mnasema 2014. Tunazungumza lugha ile ile, yaani tunazungumzia mwaka wa fedha na Rais alikuwa anazungumza *calendar year*, lakini mwaka ni ule ule wa 2013/2014 na Mheshimiwa Rais anasema mwaka 2013 Desemba, ni mwaka ule ule. Kwa hiyo, nataka wenzangu wa Dar es Salaam ambao na sisi tunaishi huko adha ile na sisi tunaipata, kwa hiyo, nataka kuwahakikisha kwamba ujenzi wa bwawa na kazi tunayoifanya ya kujenga Kidunda na kazi itakayofanyika Ruvu chini na kujenga *line* ya kutoka Ruvu chini kuja *tank* la *Dar es Salaam University*, itasaidia sana kupunguza adha.

Napenda wawakilishi wa Mkoa Dar es Salaam wajue kwamba tunaelewa vizuri maeneo ambayo yanapata maji na ambayo hayapati maji kabisa. Yapo! Kuna maeneo ambayo hayapati maji ya *DAWASA* kabisa, lakini kwa kazi tutakayofanya tunadhani kwa kipindi hicho tuta-*improve* hali ya maji katika Jiji la Dar es Salaam, tutajaribu kurekebisha kingo za mto Ruvu kwa ajili ya kuleta *flow* ya maji katika Jiji la Dar es Salaam. Upanuzi wa mtambo wa Ruvu Chini utafanyika, ulazaji wa bomba kutoka Ruvu Chini hadi Dar es Salaam utafanyika, upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu na ulazaji wa bomba upya kutoka Kibaha kwa Mathias hadi Kimara utafanyika katika kipindi hicho chini ya mpango huu. Kulaza mtandao wa mabomba Tegeta hadi Bagamoyo, kulaza mtandao wa mabomba Mbezi hadi Kiluvya, ujenzi wa mtandao wa mabomba utafanyika na hayo yote yatafanyika katika kipindi cha miaka mitatu kwa ajili ya ku-*improve* hali ya maji katika Jiji la Dar es Salaam.

Hiyo itatuwezesha kuwapa watu wa Dar es Salaam maji kwa 75% ifikapo mwaka 2013/2014, lakini mpango wetu wa maendeleo wa miaka mitano unasema ifikapo mwaka 2015/2016 tutakuwa tumefikia 90%. Maana yake ni kwamba, kumaliza mpango wa dharura hautakuwa mwisho wa uwekezaji kwa maji ya Dar es Salaam kwa maana ni lazima tuendelee. Labda niseme kwamba lazima tuwe na *program* kwa kweli tunayowekeza kulingana na ongezeko la watu. Tukiendelea hivi, unawekeza, kisha unaacha baada ya miaka 10, 15 au 20 tutaanza upya tena miradi katika maeneo hayo.

Hiki kitu ni lazima kinaendelea na kwa kweli kwa suala hili la maji wala tusiulizane tarehe ngapi tutamaliza, kwani hakuna kumaliza na wenzetu katika nchi nyingine wanakuwa na mradi, lakini wanakuwa wanajua *life time* ya huo mradi inakwisha lini. Hata barabara ukiengwa baada ya miaka 10 au 20 hiyo barabara inaweza ikawa haipo, kwa hiyo, kabla hajifika unakuwa na

mpango wa *re-surface*. Miradi ya maji lazima tufanye hivyo kwa sababu inakwenda kulingana na ongezeko la watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie suala kabambe ambalo limesemwa hapa, linalohusu vijiji 10. Sasa vijiji 10 imekuwa kama wimbo, hasa wimbo wa vijiji 10 amba hata mimi naujua, niliuimba. Naujua sana! Lakini ni lazima tukubali kwa kweli kwamba tunapotaka kufanya kazi na mashirika ya kimataifa, tunalazimika kufuata utamaduni wa Mmataifa hayo yanayotusaidia na hatuwezi kukataa kabisa hata kama gharama zake ni hizi tutakazozisema hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa Waziri wa Maji mwaka 2006 na mpango huu wa vijiji 10 ulianza mwaka 2005. Mwaka 2006 tulizungumza na *African Development Bank* na wakati ule nadhani tulizungumza vilevile na Benki ya Dunia kwamba kwa sababu miradi ya vijiji hivi kwanza ni mingi, halafu ni midogo midogo, lakini gharama zake kwa kuwa ni kidogo, tungelitumia Kanuni zilizopo katika Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004, yaani Sheria yetu wenyewe kwa sababu siyo mradi mkubwa kama ujenzi wa bandari au *airport* amba unatumia fedha nydingi.

Mwanzoni hapo tulikubaliana kwamba tufanye *procurement* ya Wahandisi Washauri, tufanye *locally* na kwa kweli tulifanya tena kwa niaba ya Halmashauri zote nchini tukawapata. Mimi mwenyewe nikiwa Waziri, niliwaomba nionane nao wote katika kikao kimoja, nikaonana nao na nikawaambia tuna shida kubwa sana ya maji, tunataka mfanye kazi yenu hii kwa haraka ili uwekezaji uanze mapema tuweze kulingana na mahitaji na uharaka tulionao katika kuwapatia wananchi maji. Hiyo ilikuwa ni mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007 wakati *delegation* yetu ipo Tunisia ina-negotiate kwenye *African Development Bank* amba wao kwa kweli walikuwa wanakubali tuendelee hata bila utaratibu wa Benki ya Dunia. Habari zikatoka Washington kwenda Tunisia kwamba hapana, *procurement* ni lazima ifuate Kanuni za Benki ya Dunia. Kwa hiyo, Wataalamu washauri amba tulikuwa tumewapata kupitia Sheria ya Manunuzi wote wakaondoka ikaamriwa warudi waombe upya. Hapo tukawa tumepoteza zaidi ya mwaka. Hapo ndipo tatizo lilipoanzia.

Sasa tumeanza, na wakasema wale wanao-*procure* ni walengwa, siyo Wizara ya Maji, wawe ni Halmashauri za Wilaya na sisi wote hapa tunatoka Wilayani, hatuna Wataalamu Wilayani huko wanaojua vizuri mambo hayo ya Benki ya Dunia. Kwa hiyo, Wizara ya Maji ikaanza kazi ya kuwafundisha sasa ili waelewe namna ya kujaza fomu na kufuata Kanuni za Benki ya Dunia, muda ukapita.

Sasa kuna kijitabu tulichotoa hapa ambacho kinaleza kila Halmashauri imefikia *stage* zipi, lakini mpaka sasa hivi kwa kweli Halmashauri 130 zimefikia mahali pazuri pa kuanza utekelezaji na Halmashauri mbili tu kati ya 132 nadhani ni Simanjiro amba ndiyo sasa wana-*procure*, Mhandisi mashauri pamoja na Morogoro, lakini Halmashauri 130 zimeshakamilisha hiyo kazi na washauri hao kwa hatua mbalimbali, wameshatekeleza wajibu wao.

Sasa kilichotuletea hapa mjadala mkali kabisa na mimi wala sina tatizo katika kukubali hicho, kwa sababu hata mimi mwenzenu nina Viji, yaani ukweli lazima uuseme tu. Hata mimi nina vijiji 12 katika Wilaya yangu ya Bunda lakini kwa bajeti hii wanatekeleza miradi ya vijiji viwili tu. Waziri Mustafa Mkulo anavyo vijiji kumi, yeye kwake wanatekeleza miradi ya vijiji viwili vinabaki vinane. Waziri Mkuu naye anavyo kumi kule Katavi. Hili ni tatizo na ndiyo maana wenzangu waliposema kwa jazba nilikuwa naelewa kwamba hawajisemei wao, bali wanatusemea wote maana nani hapa hana Jimbo au hana Viji? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tatizo liko wapi? Tatizo liko kwenye bajeti. Katika hotuba ya Waziri wa Maji ile niliyosoma kwa niaba yake, imeeleza fedha kiasi gani zinakwenda wapi, tena zina-vary lakini jumla ya zote ni shillingi billioni 86. Lazima nikiri kwamba Shillingi billioni 86 haziwezi kutekeleza miradi yote ambayo imesanifiwa. Kwa hiyo, kuna *deficit!* Tukubali tatizo. Unajua ukianza kubishana hapa ni sawasawa na kupingana na maji ambayo yanakwenda hivi, wewe unataka kuogolea unakwenda juu. Maji yatakurudisha na kukuelekeza kule yanakokwenda, ndiyo

nature ya gravity! Kwa hiyo, huo ndiyo ukweli. Sasa hali iko hivyo. Tunafanya nini? Tunaanza kutekeleza kwa kutumia fedha Shilingi bilioni 86.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kweli kama alivyosema Mbunge wa Mchinga - Mheshimiwa Saidi Mtanda, kama alivyosema Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama alivyosema Mheshimiwa Festus Limbu na wengine wengi kwamba tumewahimiza watu huko wamechanga fedha zao na wanangoja maji, sasa tunawaambia nini hao waliochanga? Hii ni *serious* na sisi ni *political organ*. Sisi ni *politicians* na kazi yetu ni *ku-deal* na matatizo ya wananchi, hatuwezi kukwepa kuwaambia tuna tatizo, lakini vilevile lazima tuwaambie *way forward*. Kwa hiyo, tatizo hili tumelzungumza na Waziri Mkuu na alikuwa ananinong'oneza hapa kwamba hata mkuu naye amemnong'oneza na mimi nafanya ofisini kwake pale, nitaendelea kumwambia, lakini mambo wala siyo rahisi. Maana ndiye alinituma kuja kufanya kazi ya Uwaziri hapa, lazima nirudi kwenda kumpa *feedback*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili tumelielewa lakini tunaweza kufanya yafuatayo:-

Moja, ni lazima tusimamie utekelezaji, lakini tutajaribu kushirikiana na Wizara ya Fedha kuona jinsi tunavyoweza kuongeza fedha kiasi kutokana na haya ambayo nitayasema hapa ili tuongeze kiwango cha vijiji vitakavyosimamiwa. Moja, tumesaini mkataba na *African Development Bank (ADB)* na wana fedha kiasi, sina hakika kama wanawenza kutupa zote, lakini wanazo Shilingi bilioni 56 ambazo tumesaini nao Mkataba.

Hilo ni suala la Waziri wa Fedha kuzungumza nao. Lakini pili kuna Waingereza kupitia shirika lao linaitwa *DIDF*, nao vilevile wameji-*commit* kutoa Shilingi bilioni 15 kwa ajili ya programu za maji. Hizi ni za maji tu, siyo za maeneo mengine. Vilevile kuna Wajerumani wameji-*commit* Shilingi bilioni 30, sasa Wizara ya Maji na Wizara ya Fedha tutakaa chini tutafute namna tutakavyoweza kusaidia ili itakapofika *mid year review*, tutazame namna tunavyoweza kusaidia miradi mingine ili kuongeza kasi ya utekelezaji. Sasa mengine mniachie, lakini mniamini kwamba hakuna kulala, nitahakikisha Mustafa Mkulo halali na Baraza zima la Mawaziri halilali ili tujibu hoja hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia, kwa sababu gani! Sisi, *we are a political government* na wale watu wa vijiji ndiyo wateja wetu, ndiyo maana hakuna kulala maana tunawahudumia wateja. Sitaki kusema zaidi, maana wote mnaelewa uteja wenyewe hasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo juu ya vijiji, sasa nitoe majibu kwa watu wengine ambaeo nao walisema. Nitatoa majibu kwa hoja za watu wachache kwa sababu sina uhakika kama kengele haitapigwa kuanzia sasa. Nimekwishajibu baadhi ya maelezo ya wale waliokuwa wamesema kwa uchungu sana.

Mheshimiwa Rosemary Kirigini, alisema kwa uchungu sana kwamba ni Kata nne tu za Musoma. Nimeshajibu kwamba mpango wa Wafaransa utasaidia kuongeza maji katika mji wa Musoma, na mimi ni mdau. Kwa hiyo, ningependa wananchi wa Musoma nao waelewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile alizungumzia sana mradi wa Mugango kwenda Butiama. Naujua mpango huu, nao vilevile una-*suffer problem* kama ile ya Handeni *Trunk Main*, Wanging'ombe na kadhalika. Kinachofanyika pale ni kwamba kupitia Mamlaka ya Maji ya Musoma Mjini, Mhandisi Mshauri alikwishapatikana, ametengeneza miradi yote ya Miji ya Wilaya za Mkoa wa Mara pamoja na huu wa Butiama. Yote imefanyiwa usanifu, sasa unakamilishwa na mimi nataka kuwashakikisha kwamba miji yote ile tutaiingiza katika mpango wa maendeleo kuanzia mwaka 2012/2013 maana usanifu ule pamoja na makabrasha ya tenda ndiyo yanakamilishwa na huyu mshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mradi wa Musoma – Kyabakari – Butiama umefanyiwa usanifu na unaendelea kukamilishwa. Tunachotaka kufanya pale wasanifu wale wameniambia kwamba kutoa maji Mugango mpaka Butiama na kuyasambaza kwenye vijiji vyote ambavyo Mheshimiwa Nimrod Mkono alikuwa anavisemea jana inawezekana isiwe na ufanisi mkubwa. Kwa hiyo, huenda wakafkiria kuigawa ili mingine ipate maji kutoka Bwawa la Butiama, kwani inakuwa rahisi zaidi kuliko kusubiri kutoka Mugango.

Hata hivyo, bado tunazungumza nao ili kama unaigawa basi ile ya Mugango ibaki kuwa ya Mugango, ihudumie walio karibu na Mugango, na hii ya Butiama ihudumiwe na bwawa la Butiama. Hizo ndizo ziliikuwa hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Rosemary Kirigini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omary Badwel alisema haungi mkono hoja. Mimi nataka kumshawishi katika hali hii ya mawimbi na taabu atuunge mkono, maana ukikuta mtu anaogelea na wewe humuungi mkono, sasa unafanyaje? Ooh, kama amezama, maana kuogelea ni raha zaidi. Tunaelewa tatizo la mji wa Bahi, alilokuwa analizungumza Mheshimiwa Mbunge. Mimi nimewahi kufika Bahi nikaweka jive la msingi kwenge Halmashauri ya Wilaya ya Bahi pale, lakini ni mahali panya. Kwa hiyo, ndugu yangu Badwel ana tatizo la kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya namna hiyo nimyaelezea katika miji mingine ambayo hata ni ya zamani kuliko Bahi. Kwa mfano, ule mji wa Tarime wa Mheshimiwa Nyambani Nyangwine ulikuwepo wakati wa ukoloni, tena tangu wakati wa Wajerumani, lakini bado haujapata maji na wenyewe uko kwenye programu hizi. Kwa hiyo, ndugu yangu Badwel tukubaliane kwamba tatizo lipi, lakini lishughulikiwe kulingana na vipaumbele na uwezo wetu wa kujibu hoja hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Munde naye alikuwa mkali mpaka ikanitisha. Mimi namjua sana, alikuwa mkali kweli! Lakini baadaye nikaenda kusoma nikasema, lakini nadhani yeje pamoja na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla hawakusoma vizuri mambo ya humu. Sisi tumesema humu mwezi Novemba ndiyo tunapata mhandisi mshauri wa kuanza kufanya kazi ya kutengeneza usanifu kutoka Shinyanga kuja katika miji ya Tabora, Nzega na Igunga mwaka huu.

Kwa hiyo, tulipokuwa tunazungumzia mwaka 2014/2015 maana ukianza kutengeneza ule mradi kutoka kule kuuleta Tabora, huwezi ukaweka tarehe. Ule nao ni mradi mkubwa kwa sababu ule wa kwanza ultiotoka Iherere kuja Kahama na Shinyanga umetuchukua muda mrefu sana, tofauti ya ule mradi na huu. Ni kwamba kule sasa hatujengi tena Iherere (*source*) nyingine. *Source* imeishajengwa na urahisi wake. Ni kwamba sasa tunayatoa maji hapo yalipokomea kama ni Shinyanga au Kahama, unayaleta kuja kwenye Miji ya Tabora, Nzega na Igunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kumwomba Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, halafu alikuwa analalamika anasema hataki usanifu huu. Lakini Dokta ni *scientist*, bwana huwezi kubeba mabomba hivi uende kuyapanga, maji hayaendi bwana! Lazima kwanza tuchore. Aah, sasa tuweke tu mabomba, tutawadanganya watu wa Tabora! Lazima tuchore vizuri, halafu tufike mahali ndiyo maji yaweze kufika.

Kwa hiyo, hili liko katika ilani ya Chama, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekwenda Tabora, amewahakikishia, na Wizara yake ya Maji inawahakikishia kupitia Bunge hili kwamba tuko *serious* na hii kazi itafanyika na tunataka wananchi wa Tabora, Igunga, Nzega; narudia na wa Igunga wasikie vizuri kwamba tutawapelekea maji kutoka Ziwa Victoria. Narudia, wananchi wa Igunga lazima wasikie vizuri, hiyo natia chumvi, lazima mchangamke msije mkasinzia. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Stephen Ngonyani wa Korogwe Vijijini alikuwa anazungumza juu ya Mombo. Mwaka 2008 tulipeleka kule fedha na sasa hivi tunaandaa taratibu za kupata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya usanifu ili tuje tuanze utekelezaji wa kuupa mji wa Mombo maji, kama ilivyo kwa miji mingine ya Wilaya na miji midogo ambayo ina watu wengi na ambayo yote tunai-target katika kazi hii.

Mheshimiwa Bernadetha Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum anazungumza juu ya matatizo ya maji shirikishi. Kwanza na hapa anazungumzia juu ya matatizo ya miji midogo katika Mkoa wa Kagera. Kwanza maji shirikishi, sera yetu ni wazi, tunashirikiana na nchi zote ambazo tunapakana nazo na ambazo vyanzo vyake vya maji vinaingiliana na sisi ili tuweze kushirikiana, maana maji haya hayawezi kuwa ya nchi moja.

Nilipokuwa Waziri wa Maji na hata baada ya kutoka akaja Dkt. Shukuru Kawambwa, na kabla yangu alikuwepo Mheshimiwa Edward Lowassa, tulikuwa tunahudhuria Mikutano mingi sana ambayo inahusiana na mambo ya maji shirikishi na hasa kuhusiana na Mkataba wa Mto Nile. Wako jamaa wengine wanafikiri maji haya yatakuwa ya kwao, na walikuwa wanadhani siyo haki sisi kuyatumia. Hata kama ungelikuwa umeajiri mtu kukulindia maji, kweli anayo maji pale halafu unatumia wewe, yeye hatumii! Utakuta ameyanywa hata kama ungekuwa umemwajiri kuyalinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haya maji shirikishi lazima tushirikiane. Tunashirikiana Kusini, kule bonde la Ruvuma, tunashirikiana sana, bonde la ...(*hapa simu ya Mheshimiwa Waziri illita*)

Hii simu, haina adabu. Ngoja nishughulike nayo kwanza. Huyu anayepiga naye, sijui haoni kama tunaongea humu! Basi, ataelewa tu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunasema maji shirikishi, tunashirikiana na mabonde, na mabonde tunayo mengi kwa sababu sisi tunazungukwa na nchi nyngi. Huku Rombo kuna lile Ziwa letu la Chara, tunashirikiana na Kenya. Nilikuwa naeleza mabonde yale ambayo Mheshimiwa Bernadetha Mushashu, ameyazungumza.

Mabonde yale tunashirikiana na nchi mbalimbali, kule Mara ule mto Mara unaanzia Kenya unaingia Ziwa Victoria. Sasa kule kwenye chanzo, jamaa wa Kenya waliwahi kuhamia kule, wengi kweli na wakawa wanakata miti. Ule mto ungelikauka baada ya muda tu, lakini tunawashukuru sana Waziri Mkuu wa Kenya baada ya kuona ile hali ikabidi wale watu wahamishwe. Sasa ule mto unaendelea kwa sababu kama tusingeshirikiana na Kenya ku-solve hiyo *problem*, ule mto ungekuwa umeshakauka. Lakini tuna ushirikiano mzuri sana na nchi zote tunazopakana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, rafiki yangu mmoja wa upinzani alikuwa amesema na gazeti likamnukuu kwamba: "Vita inanukia kati ya Malawi na Tanzania." Mimi ninakwambia hiyo harufu ya vita huko sjaisikia! Hakuna vita hapo! Sisi tumeunda Kamati ambayo inaunganisha nchi mbili hizi na tunazungumza kama nchi mbili rafiki na ndugu.

Sasa ukianza kutangaza vita, unaweza ukafanya yanayofanana na ile hadithi ya zamani ambayo zamani hizo walikuwa wanasema mwongo anaua kabla ya mchawi kwa sababu anakwenda anawaambia hawa, "wale wako tayari kwa mapambanao," halafu anarudi huku kwa wengine na kuwaambia, "wale nao wako tayari," halafu wakionana bila kujua sababu wanapigana. Hiyo haikubaliki! Tuache kutumia maneno hayo kwa sababu yanaweza yakapeleka *message* ambayo siyo sahihi katika nchi za wenzetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Betty Machangu, amezungumzia masuala ya msingi kuhusu Serikali kwamba irekebishe sheria ya umbali wa kulima karibu na vyanzo vya maji. Tunakubaliana naye kabisa, kwa sababu vinatuathiri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme habari ya Mheshimiwa Festus Limbu na na matumizi ya maji ya Ziwa Victoria. Nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunakubaliana naye katika jambo hili, kwa sababu hiyo hiyo kwa kweli. Maji yanaenda Tabora lakini walioko karibu nayo hawanywi. Itakuwa ni *theory* hiyo hiyo kama ya Misri na Tanzania.

Kwa hiyo, tunaelewa kuna Mkoa mpya wa Simiyu, sisi tumekubaliana na wataalamu kwamba tubuni mradi amba *source* ya maji itakuwa Nasa, tuyapandishe kwenda kwenye mlima, ukiyafikisha kwenye mlima ule yatatirika kwenda Bariadi, Meatu na Maswa kwa *gravity*. Kwa sababu Bariadi huku kutakuwa na Mkoa mpya, lazima tupate *source* ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Bariadi tulijaribu, lakini chanzo kinakauka, miundombinu ipo, hiyo ni *problem*. Kwa hiyo, tumekubaliana hilo na ninataka Mheshimiwa Festus Limbu ajue vilevile kwamba ule mradi amba una fanyiwa usanifu sasa pale kwake Magu, utaendelezwa mpaka Ngudu ili tuweze kujibu hoja ya Magu na Ngudu kwa pamoja. Haya sasa ni ya *long term* katika kujibu matatizo ya maeneo yaliyo karibu na ziwa, lakini hayana maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Stephen Masele, alizungumzia bei ya maji. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tatozo la watu wa Shinyanga tumelipata, tunalifanya kazi na tutashirikiana na *EWURA* kuangalia suala la bei ya maji katika Mji wa Shinyanga na tutakapomaliza kazi hiyo, basi tutaweza kutoa majibu, lakini kwa sasa tunaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshamjibu rafiki yangu Dkt. Kigwangalla na nimewaambia watu wa Tabora wakae mkao wa kula, maji yatakuja kutoka kule. (*Makofii*)

Namshukuru rafiki yangu John Momose Cheyo ambaye alieleza vizuri tu kwamba mambo ya *CAG* tusiwe tunayachukua kama yalivyo na kuyafanya ni ujisadi, maana kwa kweli hili nalo linaleta taabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* anakagua, anatoa maoni, anamwambia anayemkagua lete majibu, anampelekea majibu akiridhika ndio ameridhika. Sasa wewe tena unasema shilingi bilioni 63 sasa unawafanya watu wanakuwa matumbo moto, kumbe tumenunua magari, vifaa na kadhalika. (*Makofii*)

Naomba tuwe tunafanya utafiti kwanza halafu ukikuta kweli kuna ushahidi mzuri ndio unasema. Ehee!!! Hiyo nam-address rafiki yangu Mheshimiwa Highness Kiwia, lakini simlaumu maana ndio kazi yake iliyomleta huku. Tofauti yake na mimi ni kwamba mimi nasema halafu nafuatilia, yeeye unasema tu halafu anaenda kupumzika. Hiyo tu ndio tofauti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Michael Lekule Laizer alizungumza bwawa la Longido tumeshalionna na Waziri alishatembelea, nataka kumhakikishia kwamba totalifuatilia, wataalam tumewatuma hata lile Bwawa la Wegero tumewatuma wataalam waende watazame ili watuletee ushahidi ni kitu gani ambacho kipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nataka kutumia nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na nawaomba kabisa jambo hili ni letu sote, tupitishe tuanzie hapo halafu tupige hatua kwenda mbele. Baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA ARDHI, NYMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofii*)

(*Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kwa kuititia hoja hizi zinazohusiana na Wizara ya Maji na kwa kweli tunakushukuru sana kwa mengi ambayo umeyafafanua na hoja yako imeungwa mkono. (*Makofii*)

Kwa kifupi sana niseme neno moja kuhusiana na matumizi ya ripoti za *CAG* kama alivoyzungumza Mheshimiwa Waziri na nimekuwa nikiiona mara nyingi pamekuwa na matumizi yasiyokuwa sahihi. Kwa sababu ripoti ya *CAG* inapoletwa hapa Bungeni kuwekwa mezani huwa ni ripoti ambayo baada ya kuwekwa mezani inaenda katika Kamati zetu zile tatu, Kamati ya Mashirika ya Umma, Kamati ya Serikali za Mitaa na Kamati ya Hesabu ya Serikali Kuu, kwa hiyo, huwa ni ripoti ambayo haijawa kamili. (*Makofii*)

Kamati zile zinafanya kazi pamoja na wakaguzi wale kuititia ripoti ile na kuwaita wahusika mwisho wa siku Kamati zile za Bunge tatu zinaleta ripoti zao hapa mbele. Kwa hiyo, kama kuna wizi, ubadhirifu inatakiwa ripoti zile za Kamati za Bunge ndio iwe *reference*, sio ile ya Mkaguzi Mkuu ambayo imekuwa imewekwa mara ya kwanza pale. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaenda kwenye hatua inayofuata nitambue wageni wa Mheshimiwa Martha Mlata kwenye *gallery* Ndugu David Mnamka na wageni wako kutoka Uingereza David Dagley, Sunny Ahonsi and Benson Ossai. Ahsanteni sana mnakaribishwa.

I am told you, you are visiting Bunge, and you are also making arrangements for a master's programme that would link Tanzanians students and UK Universities. We wish all the best in that programme. (Makof)

KAMATI YA MATUMIZI

Fungu 49 – Wizara ya Maji

Matumizi ya Kawaida

Kifungu 1001 - Administration and GeneralSh. 2,473,406,000/=

MWENYEKITI: Tuanze na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwa kuwa vipaumbele vya Serikali baada ya umeme ni maji, na kwa kuwa tunayo maji mengi katika nchi hii, kwa bahati nzuri tuna mito mingi, maziwa makubwa, lakini Naibu Waziri amesema kuna *ground water* kati ya asilimia 50 mpaka 70, inakuwaje hasa hata yale malengo tuliyoyaweka hamyakamilishi? Kwa mfano maji vijijini mmeandika kufikia asilimia 65, lakini mmeshuka sana. Sababu nini, fedha, uongozi, uwajibikaji au nini? Ahsante. (Makof)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi kwa Mheshimiwa Salim kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli baadhi ya maeneo hatujafikia kama tuliyoweka kwenye llani na matatizo yaliyojiteza ni kwa sababu ya uwekezaji. Kama tulivosema changamoto tunayokabiliana nayo ni kuongezeka kwa watu kuliko ambavyo tulikuwa tumepanga. Kwa hiyo, lazima kidogo mtawanyo wa maji utapungua. Kwa hiyo, huo ndio uwekezaji, lakini kwa sasa tumejipanga kuongeza uwekezaji ili tuweze kufikia hivyo viwango ambavyo tumeviweka. (Makof)

MHE. ESTHER L. M. MIDIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Mradi wa Maji Wilayani Bariadi upo ndani ya ahadi za Rais wakati wa Kampeni mwaka 2010, je, ni lini mradi huo utaanza kutekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi swali la Mheshimiwa Esther Midimu kama ifuatavyo, kama nilivosema hata kwenye majibu hapa Bungeni kwamba ahadi za Rais sisi tunazipa kipaumbele na ahadi za Rais kwenye llani maana yake utekelezaji wake ni katika mwaka 2010 mpaka 2015. Kwa hiyo, tutahakikisha tuatekeleza katika kipindi hicho. (Makof)

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi nilichangia kwa maandishi ya kwamba Mji Mdogo wa Ifakara, Wilaya ya Kilombero sasa hivi una wakazi takriban laki moja na zaidi, vyuo ni vingi, shule zimeongezeka, hospitali na kadhalika, lakini miundombinu inayotumika ni ile ile ya miaka 1980 wakati huo wakazi walikuwa 7,000 tu. Sasa sikuona anagusia chochote Mheshimiwa Waziri, mtumishi wa Mungu Wasira, angalia Ifakara Kilombero. (Makof)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mama Askofu...

WABUNGE FULANI: Mama Mchungaji.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Wale wanaume wanaitwa Baba, huyo anaitwa Mama Askofu. Sikutaja miji yote, lakini nimesema kwamba miji ile ambayo ni ya Wilaya na Mji Midogo inapata maji kwa kiwango kidogo sana kiasilimia. Kwa hiyo, tunasema Mamlaka za Maji za Mikoa ile zimeagizwa zipate Wahandisi Washauri, watengeneze upembuzi yakinifu pamoja na usanifu ili kuanzia mwaka 2012 na kuendelea tuanze kuingiza miji ya Wilaya

kuipa kipaumbele ili tupate maji mengi katika maeneo yake, kwa hiyo, hata mji anaouzungumza Mchungaji Rwakatare itakuwa katika mfumo huo. Ahsante. (*Makof*)

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Nishukuru majibu ya Serikali kwa mpango wa muda mrefu kwa maeneo kama mkoa wa Simiyu. Lakini katika mchango wangu wa maandishi nililezea tatizo liliopo katika Mji Mdogo wa Bariadi kuhusiana na chujio ambalo limechukua takriban miaka 10 kujengwa na sasa hivi bwawa ambalo lilitegemea kuwa chanzo cha maji kimekauka. Je, nauliza katika mpango wa muda mfupi na muda wa kati haingelikuwa busara kwa Serikali ikaelekeza nguvu yake katika kuchimba visima ili angalau wananchi wa mji mdogo wa Bariadi ambaoina idadi kubwa sana ya watu na inaongezeka waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifafanue suala la Mheshimiwa Chenge kama ifuatavyo, naomba tukubali huu ushauri wake kwamba tutaongeza uchimbaji wa visima kama *solution* ya muda wa kati, wakati tunasubiri ule mpango mkubwa wa kupeleka maji Bariadi. (*Makof*)

MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani tulihoji kwamba *DAWASA* na *EWURA* walitoa tamko kuhusiana na kudhibiti bei ya maji na kwamba Mheshimiwa Waziri pia alivyojibu alisema kwamba maji yanatakiwa yauzwe kwa shilingi 20/=. Lakini ukiangalia mpaka sasa hivi wananchi wa maeneo mengine na wale ambaio wanachukua maji kwa malori hawauzi kwa bei hiyo. Je, tunataka kujua Waziri ni hatua gani itakayochukuliwa kuhakikisha kwamba wananchi wanununa maji kwa shilingi 20/= na si vinginevyo? Nashukuru. (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swalii la Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis kuhusu *DAWASA* na *EWURA*. Kwanza naomba tuelewe kwamba *EWURA* tumeiweka sisi kwa mujibu wa sheria isimamie suala la bei. Ni kwamba anatazama mlaji na yule anayezalisha. Sasa walivyopanga hizo shilingi 20/= ina maana inabidi tuisimame na hiyo shilingi 20/=. Sasa hili ni suala la utekelezaji kama kutakuwa na tatizo la hilo basi totalifuatilia. (*Makof*)

MHE. LOLEIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi nimezungumzia habari ya ahadi ya Rais ya kupeleka maji katika kijiji cha Nyarugusu na katika kijiji cha Katoro ambayo ni miji mikubwa yenye watu wengi sana. Lakini Makao Makuu ya Mji wetu wa Geita ahadi imekuwa ya siku nyingi lakini hakuna utekelezaji. Napenda kupata ufanuzi katika hayo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema, Mheshimiwa Rais akishatoa ahadi sisi tunafanya kazi. Kwa hiyo, kwa ahadi ya Rais lazima tutahakikisha kwamba maji yanakwenda Katoro na Nyarugusu pamoja na Makao Makuu ya Wilaya ya Geita. Nilishaeleza kwamba tunao mradi tayari na tumeshapata wafadhili wa kutoka Ziwa Victoria kupita kwenye Mgodi wa Geita mpaka kupeleka kwenye Mji wa Geita. Kwa hiyo, ni kitu ambacho tayari kipo kwenye process na hayo maeneo mengine tutaendelea kufuatilia kama Rais alivyoagiza. (*Makof*)

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Pamoja na kwamba wananchi wa Jiji la Mwanza na wananchi wa Mkoa wa Mwanza kwa ujumla, maji wanayaangalia kama jua baadhi yao na kuyashika hawawezi; na kwa kuwa tunaelewa kabisa tatizo la umeme katika nchi yetu linavyoendelea kwa kasi na umeme kuwa mdogo. Napenda kujua Wizara ya Maji wamejipangaje kununua jenereta ambayo inaweza ikasukuma maji ambapo pale umeme unapokosekana ili wananchi waweze kupata maji na kutoathirika kama ilivyotokea? (*Makof*).

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, hili analoliulizia tunakubali, lazima kuwe na jenerati na pale Jijini Mwanza lipo jenereta kubwa kweli la *standby* ambapo umeme ukipungua basi huwa linaweza kutumika. Lakini ku-*pump* maji ya

kunywa kwa kutumia jenereta kwa Jiji kubwa kama la Mwanza inaweza ikawa gharama kubwa sana, lakini tunalo *standby* jenereta Mwanza. (*Makofii*)

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwa kuwa maji ni janga la Kkitaifa na kila sehemu kuna tatizo la maji. Napenda kujua kwa nini Serikali isije na mkakati kama aliokuja nao Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa kutumia maji kwenye Maziwa kwa mfano watu wa Magharibi tutumie Ziwa Tanganyika ku-*supply* maji eneo lote la Magharibi, watu wa kwenye Ziwa Nyasa kule tuachane na haya mambo ya kwenye visima, watu wa kwenye Bahari ya Hindi tutumie bahari kusambaza. Sasa napenda kujua kama Serikali inaweza ikaja na mkakati hata kama si kwa mwaka huu ila kuonyesha ni namna gani tunaweza kutumia vyanzo hivi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkosamali na sisi wa Dodoma tutatumia...!! Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo ya Mheshimiwa Mkosamali ni makubwa na mazuri lakini utekelezaji wake unaweza ukawa usiwe rahisi kama anavyofikiri kwa sababu nchi yetu ni kubwa na vyanzo vya maji vipo vya kila aina. Hata unapotekeleza huu mpango ambao tunauzungumza wa *World Bank* tunaenda kwa wananchi tunawapa *option* wao wachague teknolojia gani wanawea kuigharamia. (*Makofii*)

Sasa wengine wanasema sisi ukituwekea kisima pamoja na umeme wa *solar* tutalipia gharama zaidi kuliko tukipata maji ya Ziwa Victoria. Sasa tukisema tuache visima tuwe tunatumia maji kutoka kwenye Maziwa gharama zake zitakuwa kubwa na inawezekana tukachukua muda mrefu kama ambavyo tungependa. Kwa hiyo, tutakwenda na yote. (*Makofii*)

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi nilielezea namna ambavyo Waziri wa Maji Mheshimiwa Mwandosya alitoa ahadi kwenye kijiji cha Sakalilo kwamba tutawapelekea maji kutoka tarehe 19/08/2008 na nimekuja kumkumbushia akaniambia nilete mchanganuo, nimeleta kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, napenda wananchi wapewe majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba kama Waziri wa Maji alikuja pale na akaahidi ni jambo ambalo alikuwa anajua kabisa kwamba tunaweza tukalitekeleza. Sasa naomba utupatie muda tutalitekeleza ahadi za Waziri Mheshimiwa Mwandosya. (*Makofii*)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Napenda nipate ufanuzi, katika kitabu chako cha hotuba Mheshimiwa Waziri kampuni ya *PNR* imepewa *tender* ya kuchimba visima katika Halmashauri 24 katika nchi hii, ni vigezo gani vimetumika kwa sababu kampuni hii inaonekana ina mashine nne tu. Nina wasiwasi kidogo na ufanisi huu na kuna mazingira fulani tatanishi. Napenda kujua ni vigezo gani vimetumika? Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namna ya huyu mkandarasi wa kuchimba visima anapatikana ni kwamba Halmashauri inatangaza *tender* kwa hiyo wale wanaotaka kazi ile wanaomba. Sasa *PNR* alikuwa mmojawapo wa aliyeomba na ndiye aliyeshindia ile *tender* sasa kama kuna matatizo ya utendaji kuna vitu ndani ya mkataba namna ya kusitisha mkataba wake kama hawezikutekeleza kwa jinsi walivyokubaliana. (*Makofii*)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwanza naomba nichukue fursa hii kumtakia kheri na afya njema Mheshimiwa Profesa Mwandosya, *get well soon Professor*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Mbeya ni tajiri wa vyanzo vya maji lakini Mbeya Mjini kumekuwa na matatizo makubwa ya maji kutokana na miundombinu. Naomba ninukuu kwenye hotuba ya Waziri ukurasa wa 71; "Katika Mji wa Mbeya ujenzi wa majengo kwa ajili ya mitambo ya kutiba maji maeneo ya Sisimba, Sawaya na Imeta umekamilika, ufungaji wa mitambo ya kutibu

maji umefikia asilimia 40, ujenzi wa matanki saba ya kuhifadhia maji yenyenye ujazo wa mita 6,900 umekamilika eneo la Forest, Iwambi, Iganzo, VETA na kadhalika."

Mipango ni mizuri kwa mradi huu ambaa kule Mbeya ni maarufu kama mradi wa *SOGEA* au *SOG*. Lakini pamoja na mikakati yote hii na asilimia zote hizi mimi napenda kujua kwa niaba ya Wanambeya ni lini mradi huu utakamilika kwa sababu nakumbuka niliongea na Profesa Mwandosya akaniahidi kwamba mwezi wa nane ungekamilika lakini humu sioni michakato yake? Ahante. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ni lini mradi unakamilika imeanishwa kwenye mkataba. Sasa kwenye utekelezaji kunaweza kukawa kumejitokeza matatizo madogo madogo na ule mradi wa Mbeya ni mkubwa sana na upo karibu kwenye asilimia 90 ya kukamilika. Kwa hiyo, itabidi tuutizame ule mkataba na tuone imewekwa mpaka tarehe ngapi. Kwa sasa hivi sina jibu la moja kwa moja lakini tutalifanya kazi na kuhakikisha mradi ule unaisha kulingana na mkataba. (*Makofi*)

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Wasira kwa majibu mazuri kuhusiana na upatikanaji wa maji Nzega. Lakini hoja yangu ya msingi hapa inahusiana haswa haswa na ukosekanaji wa maji kule Butiama kama nilivyochangia jana nilipochangia kwa kuzungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti na Wabunge wote mnaompenda na kumuenzi Baba wa Taifa naomba sasa nitumie fursa hii ili tulijadili suala hili kwa upana kutoa hoja ya kutoa shilingi kwa mujibu wa Kanuni ya 103(2). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja ya kuondoa shilingi ili tuweze kujadili kwa upana suala la upatikanaji wa maji katika Mji wa Butiama. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Hoja yako haijaungwa mkono, mmechelewa kusimama. Tunaendelea na Mheshimiwa Rosemary Kirigini. (*Makofi*)

MHE. ROSEMARY K. KIRINGINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nampongeza sana Waziri kwa kutambua tatizo kubwa la maji liliopo katika Mji wa Musoma na nina imani kwa kutambua tatizo hilo basi suluhu ya haraka itapatikana. (*Makofi*)

Kwa kuwa maabara ya maji katika Mji wa Musoma inalo tatizo kubwa sana la upungufu wa vifaa vya kupimia ubora na kufanya utafiti na kujua usalama mzima wa masuala ya maji. Je, Waziri na wataalam wapo tayari kwenda kufanya ziara katika maabara ile, kufanya ukaguzi wa kutosha na kuangalia ni kwa namna gani wanaweza kuongeza vifaa katika maabara ile ili tuweze kuwahakikisha wananchi wetu wa Mji wa Musoma maji safi na salama kama llani ya Chama cha Mapinduzi inavyotutaka? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye, tutakwenda Musoma na kuweza kuona vifaa vinavyohitajika ili tuweze kuboresha maabara ile. (*Makofi*)

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa tatizo la Butiama ni kubwa sana Kitaifa na kwa kutambua tutasheherekeea miaka 50 mwaka huu pale Butiama na Mama Maria Nyerere hana maji, naomba nitoe hoja ya kutoa shilingi moja kwa Mheshimiwa Waziri. Lakini kabla ya hapo naomba hoja hii ijadiliwe kuhusu tatizo la maji la Butiama. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkono amenichanganya. Hoja yake nimeikubali lakini katoa vitu viwili. Sasa sijui anataka kipi anatoa shilingi au anataka hoja ijadiliwe maana huwezi kutoa vyote viwili kwa wakati mmoja. (*Makofi*)

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka hoja ijadiliwe.

MWENYEKITI: Kwa kutumia Kanuni ipi? Waheshimiwa Wabunge naomba mkae ili tumpe nafasi Mheshimiwa Mkono. (*Makofi*)

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni 103(1); "Kwa kuzingatia utaratibu wa majadiliano uliowekwa na Kanuni hizi, Mbunge ye yeyote anaweza kuomba ufanuzi ama maelezo zaidi katika kifungu chochote cha Fungu linalohusika, wakati kifungu hicho kitakapofikiwa na Kamati ya Matumizi."

(2)"Vilevile Mbunge ye yeyote anaweza kutoa hoja ya kuondoa shilingi moja katika kifungo chochote cha Fungu hilo."

MWENYEKITI: Kwa hiyo, ninachokipokea na kilichoungwa mkono ni kutoa shilingi. Nadhani tuokoe muda tupate majibu tuone tunavyokwenda. Kwa sababu kwa Kanuni ulioitumia ni ya kutoa shilingi na mimi nakukubalia ili tuweze kuendelea. (*Makofi*)

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia kifungu kidogo cha pili kutoa shilingi kwa mshahara wa Waziri kuhusu maji ya Butiama. (*Makofi*)

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitoleta lamuliwe*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kumsihii Mheshimiwa Mkono arudishe hiyo shilingi haraka sana kwa sababu kwanza Waziri anayemtolea shilingi anaumwa, kwa hiyo, kibinadamu haitakuwa sahihi sana kumuondolea shilingi kwenye mshahara wa Waziri. (*Makofi*)

Lakini ukiondoa hilo nataka kusema mimi nafahamu sana tatizo la maji la Butiama. Nataka nilongee *with seriousness* na tuisilichanganye na matatizo ya Mama Maria Nyerere. Mama Maria ni mwanakijji mmojawapo kati ya wanakijji wa Butiama. Tukili-centre kwa Mama Maria tutakuwa tunafanya na nadhani Mama Maria hapendi vilevile watu wamtumie ye ye badala ya kuzungumza matatizo ya watu wa Butiama. Tunazungumza *issue* ya *community* ya Butiama na si *issue* ya familia ya Mwalimu. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Lakini la pili nimesema wakati najibu hapa kwamba ule mradi ni ule mradi uliotengeneza mwaka 1970 na *ime-run down*. Kwa hiyo, maji yanayotoka Mgango yanapita Kyakabari, yanakuja Butiama yanakwenda Bisali yanakwenda Bumangi mahala pengi sana yale maji hayafiki.

Kwa hiyo, mpango wetu tulionao ambaa umefanyiwa usanifu na wataalam tayari ni kuingiza katika mpango ili tuweze ku-rehabilitate ili maji yawewe kupatikana kwa uhakika kwa jamii ya wananchi wa Butiama. (*Makofi*)

Vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Mkono kwa sababu yeye anachangia sana katika kutengeneza visima vya kusaidia pale Butiama. Sasa juhudii zake hizo zitaungwa mkono na juhudii za Serikali na tatizo hili tutalipatia ufumbuzi. Kwa hiyo, namwomba aunge mkono hoja kwa kurudisha shilingi ya Mheshimiwa Waziri Mwandosya. (*Makofi*)

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nizungumzie suala la Butiama. Mradi ninaouzungumzia ni *trunk route four* ambayo umebuniwa tangu mwaka 1974. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkono, sasa hivi nilichokupa nafasi ni ama ya kurudisha kwa kukubaliana na Mheshimiwa Waziri au kutupa utaratibu mwingine ili niweze kuhoji. (*Makofi*)

MHE. NIMROD E. MKONO: Sikubaliani na Mheshimiwa Waziri natoa shilingi kuhusu suala la Butiama. (*Makofi*)

(*Hoja ilihamuliwa na Kukataliwa*)

MWENYEKITI: Waliokataa hoja ya Mheshimiwa Mkono wameshinda. Mheshimiwa Bura.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Unapozungumzia Mikoa yenye ukame huwezi kuuacha Mkao wa Dodoma kwa sababu Mkao wa Dodoma tunapata mvua kwa siku zisizozidi 20. Kwa hiyo, matatizo ya maji ni makubwa sana katika Mkao wetu. Wilaya ya Bahi ni Wilaya ambayo ina matatizo makubwa kutokana na kutokuwa na kisima hata kimoja ndani ya Makao Makuu ya Wilaya. Wale walioko pale, wananchi na wafanyakazi wa Serikali Kuu walipo pale wanategemea kisima kidogo sana ambacho kilichimbwa na Wamisionari. Hata kituo cha afya ambacho kiko pale kinategemea maji kutoka kituo cha misheni. (*Makofii*)

Ninaomba ufanuzi kwamba suala la Bahi, Serikali inalitizama kwa jicho gani? Ninaomba jicho la huruma sana kwa wananchi wa Bahi pale *centre* ambao wanatumia maji kutoka misheni, siku misheni wakikorofisha au wakikataa wananchi wale sijui watatumia maji kutoka wapi? Naomba ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana naye kwamba kuna tatizo kubwa katika Wilaya mpya ya Bahi. Katika mipango ambayo tunayo kwanza tuna mpango wa kufanya usanifu ili tupate maji ya kutosha kwa Wilaya zote nchini na hasa hizi mpya. Sasa kwa tatizo hili lipo, tutaangalia uwezekano wa kutengeneza kamradi ka *quick wins* ili tuweze kututua angalau kisima kimoja au viwili viwe vinafanya kazi katika mji ule. (*Makofii*)

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Wakati nachangia kwa maandishi nilipongeza kuanza mradi wa Chalinze awamu ya pili. Lakini kwa kuwa baadhi ya maeneo yaliyotajwa kwenye mradi huo kama Kiwangwa, Msinune, Ludiga, Kisanga yana matatizo makubwa sana ya maji na kwa kuwa mradi huo utakamilika Oktoba, 2012; je, Serikali ina mpango wowote wa dharura wa kuwasaidia wananchi wa maeneo hayo kwa sababu hali ni mbaya sana?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna huo mradi ambao ni mkubwa sana unaoendelea. Sasa kwa suala la kuangalia vijiji anavyovitaja ni Halmashauri ya Wilaya ambayo ndiyo intatakiwa iainishe na iweke vipaumbele katika mipango yake. Sisi tutafuatilia utekelezaji ambao wameshaainisha. (*Makofii*)

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kupata ufanuzi. (*Makofii*)

Katika Sera ya Maji kwa sasa hivi tunalo tatizo, kwa mfano milimani kule Lushoto. Katika mandishi yangu nilimuuliza Waziri, tatizo la maji katika Mji wa Lushoto pamoja na vijiji vya Mlola. Bahati mbaya kwa sasa kule juu milimani tunaanza kupeleka sera ya kuchimba visima. Ni kweli kwamba kuchimba visima ni tatizo kubwa na maji hayapatikani mlimani. Tumezoea maji yanayoshuka kwa nguvu za mvutano (*gravity*). Hivi kwa nini Serikali isingepeleka nguvu zaidi katika utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji na maji ambayo yanashuka kwa *gravity* ndiyo yakatumika zaidi katika maeneo ya milima badala ya kuchimba visima?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitolee ufanuzi hoja ya Mheshimiwa Shekifu, Mbunge wa Lushoto kama ifuatavyo:-

Naomba nikubaliane naye kwamba tutaweka msisitizo katika hifadhi ya mazingira ili tuwe na vyanzo ambavyo ni endelevu. (*Makofii*)

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia Mji Mdogo wa Loliondo na Mji wa Waso na kijiji cha Sakala kwamba ni maeneo ambayo yanakuwa kwa kasi sana kutokana na neema ya hivi karibuni ambayo tumepata umeme, *Inshallah*, pengine mwishoni mwa mwezi ujao, umeme utawashwa katika Mji huo wa Loliondo. Na vilevile hivi punde barabara ya lami itaanza kujengwa kutokea Mto wa Mbu hadi Loliondo mpaka *Cranes Camp*. Lakini vilevile tumekuwa na wageni karibu sasa ni wageni wa kudumu wanaokwenda kwa Babu wa Samunge kupata kikombe. Watu wamekuwa wengi sana

katika maeneo haya ambayo nimeyataja. Lakini miundombinu ya maji ni ya tangu mwaka 1979 ambapo Wilaya ya Ngorongoro ilianzishwa. (*Makofi*)

Naomba ufanuzi, je, tunaweza kupata visima vine, viwili katika Mji Mdogo wa Loliondo, viwili katika Mji Mdogo wa Waso na kimoja katika kijiji cha Sakala? Nashukuru Katibu Mkuu pia ananisikiliza hapa, Christopher Sayi ni mwema, mtaratibu sana. Ahsante. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajibu lile linalohusu Mji wa Waso, Loliondo kwa sababu pale Loliondo tunajua *data zake*, kuna watu 197,000 lakini maji yanayopatikana ni kidogo. Lakini usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni umekamilika na kazi ya kuongeza maji na kuweka miundombinu itaanza katika awamu ya pili mwaka ujao wa fedha. (*Makofi*)

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa ushauri kidogo pamoja na kuipongeza Serikali kwa mipango mizuri sana ya kuhakikisha wananchi wanaishi mjini na vijijini wanapata maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilikuwa nimeipongeza Serikali kwa mikakati yake ya kuwafikisha wananchi wa Jiji la Dar es salaam pamoja na Pwani maji ya kutosha itakapofika mwaka 2014. Lakini katika mchango wangu nikawa nimeonyesha wasiwasi wangu kwamba endapo wafadhili hawatatoa fedha kwa ajili ya mradi huo, pengine mradi wa kuwafikisha wananchi maji Dar es Salaam utasimama. Je, Serikali sasa inatoa tamko gani, endapo wafadhili watashindwa kuleta fedha kwa wakati ili wananchi wa Mkoa wa Dar es salaam na Pwani waweze kupata maji kama tulivyoahidi katika llani na katika ahadi ya Rais wetu? Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Makilagi kama ifuatavyo:-

Kwanza katika mpango maalum ambao Serikali tayari tumeishauweka, *commitment* ya wafadhili ipo thabiti, hakuna mahali popote ambapo katika zile fedha ambazo tumeweka, tunategemea kwamba watajitoa. Lakini kama litatokea tatizo kama hilo, Serikali itaziba pengo hilo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Najua kabisa Ubungo siasa ni maji! Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. NYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu yaliyotolewa na Waziri ambayo yanakinzana kiwango fulani na tamko lillotolewa na Serikali baada ya Kikao cha Baraza la Mawaziri, niseme tu kwamba kuhusiana na masuala ya udhaifu wa kiutendaji wa DAWASA, DAWASCO, masuala ya miundombinu, sijaridhika na majibu. Kwa hiyo, nitaendelea tu na kusudio ambalo nililiwasilisha toka mwezi Juni, Ofisi za Bunge la kuwasilisha Hoja Binafsi kuhusiana na matatizo ya maji Mkoa wa Dar es salaam. (*Makofi*)

Lakini ningeomba kupata ufanuzi tu kwa sasa kuhusu jambo moja, kwenye hotuba ya Waziri ukurasa wa 83, amezungumzia kuhusu mradi wa kuboresha huduma za maji safi na usafi wa mazingira katika maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dar es salaam. Kuna maeneo mbalimbali Jimbo la Ubungo ambayo hayaguswi na mtandao wa DAWASCO; maeneo ya Mpiji Majohi, maeneo ya Msakusi, maeneo ya Msigani, baadhi ya maeneo ya Mavurunza na maeneo mengine yakiwemo ya Kwembe. Nataka kujua tu kama huu mpango wa maji pembezoni ambao umetengewa takriban shilingi bilioni nne kama utagusa maeneo yote hayo na lini visima vya Kilungule, King'ong'o na Mavurunza vitazinduliwa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi hoja ya Mheshimiwa John Mnyika kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa nakubaliana naye kwamba kuna maeneo ambayo maji ni tatizo. Lakini sasa hivi DAWASA inaendelea kuchimba visima katika maeneo hayo ya Mavurunza, King'ong'o, Malambamawili, Kilungule, Mbagala, Sandali, Chang'ombe, Mburahati na maeneo mengine.

Kwa hiyo, ni kazi ambayo inaendelea na nategemea baada ya muda si mrefu, visima vile vitakuwa vimekamilika. (*Makof*)

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Sehemu kubwa ya Mkao wa Manyara ipo katika Ukanda wa Bonde la Ufa kwa hiyo, kuna maji mengi sana ardhini. Lakini cha kusikitisha ni kwamba kuna baadhi ya vijiji hakuna hata tone la maji na baadhi ya viongozi wetu ambao wametembelea kama Kiteto, Mheshimiwa Waziri Mkuu alijionea mwenyewe, akasema atamuagiza Waziri wa Maji na yeze aje ajiridhishe, Mheshimiwa Rais alitembelea Minjingu akasikitika akasema ataleta maji haraka sana. Hadi leo ahadi hizo hazijatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba ushauri kwamba Serikali inaweza sasa kuwakodisha wananchi waweze kujichimbia hata visima wenyeve kuliko kungojea miradi hii ya *World Bank* ambayo ina molongo mkubwa sana wa urasimu, waweze kupewa hata *excavator* hata moja kwa Mkao ili wananchi waweze kujichimbia visima? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Umbulla kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa Mkao wa Manyara kwa sehemu kubwa uko ndani ya Bonde la Ufa na maeneo mengi hata kama ukitaka kuchimba kisima, unaenda zaidi ya mita 200 ndiyo unaweza ukapata maji; na maji unayoweza kuyapata yanaweza yakawa na matatizo ya *fluoride*. Kulingana na mpango ambao tunao, bado tutaendelea kufanya juhud zaidi ili kusudi mipango ambayo ipo iweze kutekelezeka. Hatuwezi kusema tuwaachie wananchi kwa sababu sisi tumewaaahidi wananchi tutawapatia maji, kwa hiyo, tutafanya hiyo kazi. Na suala la kuwapatia vifaa, mimi nafikiri Halmashauri sasa ndiyo inaweza ikaangalia kama inaweza ikanunua vifaa kwa ajili ya kuchimba visima. Lakini tunalo Shirika la *DDCA* ambalo ni la Serikali, tunaweza tukawapeleka pale wakafanya hiyo kazi. (*Makof*)

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza niseme tu kwamba kuna tatizo la jumla la Kiserikali kwamba siku zote Bajeti ni ndogo, kwamba sungura ni mdogo. Lakini kimsingi ni tatizo la ujumla la Serikali. Sasa labda niende moja kwa moja kwenye swali langu la msingi. Wakati nachangia hoja, nimeainisha kwamba Mkao wa Kigoma ni Mkao mbao una vyanzo vyote vya maji; una Ziwa Tanganyika, la pili kwa kina kirefu duniani na maji yake yanatumika, ni maji safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mito ya kutosha kama Kigoma lakini kama Taifa, kwa sababu Tanzania mpaka sasa ni nchi ya 11 kwa mito mingi duniani. Kwa hiyo, tunakosa maji kwa sababu tu ya utekelezaji. Kwa hiyo, mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi hapa, Mkao kama wa Kigoma ambao una vyanzo vyote vya maji kiasi kile, leo watu wanaopata maji ni asilimia 27 tu. Lakini zaidi hata kwenye Bajeti yake, Mkao wa Kigoma ni mionganoni mwa Mikoa mitatu ya mwisho kabisa kwa kiwango kidogo cha fedha ambazo zimetengwa. Naomba ufanuzi. (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Kafulila kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa kulingana na sera yetu ya maji ni kwamba kila Halmashauri ina mipango yake ya kuendeleza na tumesema kwamba wananchi ili kusudi waweze kuona miradi ambayo wanaweza kuiendesha, sasa kama wataona kuchukua maji kwenye Ziwa, zile gharama wataweza kuziendesha, basi watachagua chanzo kama ni Ziwa. Lakini tukashauri kwamba visima ni zaidi sana kuendesha kwa sababu maji ya Ziwa yana gharama kubwa ya umeme na gharama ya kutibu maji yale. Maji ya visima kidogo ni safi. Sasa wananchi wenyeve wanaamua kwa kushauriana na yule Mtalaam Mshauri ambaye kila Halmashauri imemwajiri. Sasa ukisema Mkao, maana kuna Mkao na Vijiji, lakini ukisema Mji wa Kigoma, Mheshimiwa Waziri ametolea maelezo. (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongeze kidogo tu, labda nizungumzie kwanza Mji wa Kigoma. Kwa muda mrefu kwa kweli Ndugu yangu Kafulila, tunajua Mji wa Kigoma umekuwa na matatizo ya maji na tatizo kubwa pale ilikuwa siyo maji, maji yapo Ziwan pale, tatizo ilikuwa ni namna ya kuya-*pump* kutoka kule Ziwan kuyapeleka kwenye matenki, halafu kuyapeleka kwa wanywaji.

Sasa kila mmoja, kwa kweli pamoja na wananchi wa Kigoma tunakubali kabisa kwamba juhudhi ambazo Serikali imefanya katika siku za karibuni na wakati mimi nikiwa Naibu Waziri wa Maji, nakumbuka hili suala tumelishughulikia, tuliazima baadhi ya *pumps* kutoka Mwanza. Lakini kubwa zaidi ilikuwa ni kuhakikisha kwamba umeme unapatikana kwa ajili ya ku-*pump* maji kuyapeleka kule. Tulipofanya juhudhi hizo, kiasi cha upatikanaji wa maji katika Mji wa Kigoma, sasa hivi itakuwa ni tofauti na ilivyokuwa. Lakini tukiendelea sasa kwenye Wilaya zingine, programu hii aliyoleze Mheshimiwa Waziri ya vijiji kumi, nadhani kila mahali katika Wilaya zote ndiyo ipo katika hali ambayo ameielezea, tumefikia hatua ambayo tunarekebisha watalaam sasa wapatikane. Unajua bado tupo nyuma kidogo katika kuwapata hawa watalaam, lakini hatua si sawa na ilivyokuwa katika miaka iliyopita. (*Makof*)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi naomba niipongeze Serikali sana kwa majibu yake mazuri hasa upande wa maji ya Ziwa Victoria. Lakini ninaiomba Serikali tu ijaribu kutumia busara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Ihelele ndipo kwenye chanzo kikuu cha maji yanayokwenda Kahama, Nzega na sehemu zingine. Eneo la Ihelele pale hakuna maji hata kidogo, wananchi wanatazama matenki yale na maji wanayatazama, ndipo kwenye chanzo. Naiomba Serikali itumie busara wananchi wa Ihelele wapate maji. Serikali inasemaje? (*Makof*)

MWENYEKITI: Maji Ihelele, Mheshimiwa Naibu Waziri, ufanuzi!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Ndassa kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa Ihelele ndiyo chanzo cha maji yanayokwenda Shinyanga na Kahama. Katika awamu ya kwanza hatukuweza kutoa maji pale, lakini sasa kuanzia mwaka huu wa fedha, tunapeleka maji Ihelele. (*Makof*)

MHE. VICK P. KAMATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Geita wamechoka na siasa, wanachohitaji sasa ni maji. Kuna maneno maneno ya wanasiasa wachache yanaendelea kule kuhusu maji kutoka Ziwa Victoria kuja Nungwe na Nyankanga, wanasema kwamba chanzo hicho hakina maji safi na salama. Lakini kwa taarifa nilizonazo mimi ni kwamba maji yale yalishapelekwa maabara, yakathibitishwa kwamba ni safi na ni salama kwa matumizi ya binadamu. Je, Serikali inatoa ufanuzi gani, maana wananchi wa Geita sasa wanahitaji maji, wanateseka sana. (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Vick Kamata kama ifuatavyo:-

Kwanza tumewaelekeza kabisa Halmashauri ya Geita kwamba Madiwani mwanzoni walikuwa wanapinga kwamba maji yale yasichukuliwe kwa sababu hayana ubora. Lakini tumefanya vipimo kwenye maabara, wamethibitisha yale maji ni safi na tumetoa kibali kwamba yale maji yanaweza kusambazwa katika Mji wa Geita. (*Makof*)

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Wananchi wa Ngara wapo macho na wanafuutilia mjadala huu kwa umakini sana na wamenitumia messages walipomsikia Mheshimiwa Waziri akisema kwamba tutapata msaada wa bilioni 50 kutoka *ADB* (Benki ya Maendeleo ya Afrika), bilioni 15 ya *DFID* (Uingereza) na bilioni 30 ya Ujerumani. Wameniomba niulize Serikali, katika hali hiyo wangeomba wananchi wa Ngara nao

wakumbukwe hata kama wapo pembezoni mwa nchi, kilomita 1600 kutoka Dar es salaam. Wananchi wote katika vijiji 73 hawajui maana ya maji safi na salama. Naomba ufanuzi! (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho Mheshimiwa Waziri amezungumza ni kwamba vile vijiji ambavyo tayari usanifu umekamilika na kwamba kwa Bajeti hii hatukuweza kusema waanze kutangaza *tender* ya kujenga miundombinu, ndiyo tunataka kufanya sasa tuongeze vijiji kufikia *mid year* ya *December*. Kwa hiyo, kama Ngara vile vijiji tayari vimeshafanya usanifu, vinasubiri fedha, tutaangalia uvezekano wa kuviingiza. (*Makof*)

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufanuzi, Serikali wanafahamu kwamba Longido ni Wilaya kame na kwa sasa chanzo cha maji kinachotumika pale kimekauka kabisa. Ni siku yoyote tu shule zitafungwa na Kituo cha Afya nacho kitafungwa. Je, Serikali inasema nini kuhusu kuokoa hali hiyo ili wananchi wa Longido pamoja na shule zilizopo zisifungwe? Je, Serikali inaweza kutoa udharura wa kuokoa hali hiyo? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Laizer kama ifuatavyo:-

Nakubali kuwa Longido ni Wilaya mojawapo kati ya Wilaya ambazo ni kame. Sasa sera yetu kwa mwaka huu tunataka tujielekeze zaidi katika maeneo ambayo ni magumu kama ya Longido, tutaendelea kuchimba mabwawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutafanya kazi hiyo. (*Makof*)

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii. Katika swali langu na katika kuchangia hoja yangu ya maandishi, nilijenga hoja kwa Waziri kwamba Mji Mdogo wa Ifakara sasa hivi una watu takriban wanakaribia 130,000. Lakini Serikali mwaka 2004 ilitoa bilioni moja kwa ajili ya mradi mkubwa wa Kiburubutu unaoanzia katika Mto Lumemo na mwaka 2009 imetoa shilingi bilioni 2.5. Lakini sasa hivi mradi ule umesimama na hali ya Ifakara ni mbaya sana. Je, Waziri anatuhakikishajie wananchi wa Ifakara watapata maji ya uhakika na ukizingatia hela nyingi zimeishatumika katika mradi ule? Ahsante. (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Susan Kiwanga kama ifuatavyo:-

Ninavyofahamu ni kwamba Mheshimiwa Waziri ameshatoa jibu la matatizo ya Mji wa Ifakara. Kwa hiyo, tutaendelea na hilo jibu. (*Makof*)

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Ukiangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 118, walijiri mkandarasi anaitwa *Engineering Research Associate* tarehe 31 Julai, 2009 katika Wilaya ya Kasulu. Lakini ukiangalia tena kwenye ukurasa wa 140, Halmashauri ambazo watalaam washauri wanaandaa taarifa za awali na kuainisha kazi zitakazofanyika, Kasulu bado inasomeka pale. Sasa kama mtu ni *Engineer* umemwajiri mwaka 2009, mwezi Mei, 2011 bado anasema ndiyo anaandaa, sijui sasa hapo Wizara inaonyesha kwamba haiwasimamii hawa wakandarasi ambao wanaajiriwa. (*Makof*)

Lakini tatizo kubwa vile vijiji vya Jimbo langu la Manyovu na Kasulu, vile vijiji vyote havijafanyiwa chochote na watu kweli wanalamika, na tungeomba sasa Wizara ione umuhimu wa kuona kwamba Kigoma nayo sasa siyo suala tu la kuja hapa kuomba omnia. Nyie hamuwezi kuifirkiria kabla ya Obama hajasimama kuongea?! (*Makof/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Obama kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa tukubaliane kwamba anayesimamia hawa Watalaam Washauri ni Halmashauri ya Kasulu, ndiyo wanaosimamia. Kwa hiyo, sasa kama kuna tatizo la utekelezaji ambalo liko ndani ya mkataba na sisi kama watu ambao tunafanya *monitoring*, tutakwenda kufuatilia na kuliangalia. (*Makof*)

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza naomba Mungu amponye haraka Mheshimiwa Mwандосya ili aje tuungane pamoja. Pia napenda kuishukuru Serikali kwa ajili ya Mradi wa *World Bank*. Kwa upande wetu Jimbo la Nkenge angalau vijiji saba tayari vimepata maji na vitatu vilivyochimbwa maji hayakutoka bali tunaomba ifanyike utaratibu mwininge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo napenda kuchangia ambalo nimeliongelea katika kuchangia kwa maandishi, ni kwamba Wilaya yetu ya Misensi imezungukwa na Mto wa Kagera ni mto mzuri wenyewe maji safi amba hata *Kagera Sugar* inatumia maji hayo kump na kumwagilia kwenye miwa. Mimi nahoji Serikali au ningependa kuelewa hivi ni kwa nini isitusaidie kutumia hayo maji kwa ajili ya Wilaya yetu ya Misensi ili tupate maji safi, ukizingatiwa Wilaya yetu ni mpya tunatumia visima vya watu binafsi wakati maji yametuzunguka na hatuna hata mamlaka ya maji katika Wilaya nzima. Naomba Serikali iwajibu wananchi wa Nkenge ni namna gani ya kufanya angalau na sisi tufaidi maji katika Wilaya yetu ya Misensi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Assumpter Mshama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niwapongeze wananchi wa Nkenge katika vijiji saba tayari wameshafanikiwa kuchimba visima na sasa hivi kinachoendelea katika awamu hii kwenda kuvijengea miundombinu. Sasa kwa mipango ya baadaye maana hivi visima inawezekana visikidhi mahitaji tutaangalia uwezekano wa kutumia maji ya Mto Kagera. (*Makofii*)

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tatizo la maji katika Jimbo la Kwimba ninalotoka sasa hivi ni dharura siyo tatizo la kawaide tena, wananchi wa Ngudu Mjini wanunua maji kwa shilingi 500/= kwa ndoo. Wananchi wa Hungumalwa wanunua maji kuanzia shilingi 400/= na kuendelea kwa ndoo. Wananchi wa Kata ya Ilula hasa wale wa kijiji cha Manai hawana maji hata ya kununua kwa bei yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuamini kwamba *this government is dysfunctional*, sitaki kuamini hivyo, hivyo basi ninamuomba Waziri aende Kwimba akaangalie matatizo yaliyopo Kwimba na hatimaye aje na ufumbuzi. Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi hoja ya Mheshimiwa Leticia Nyerere, kuwa naomba nikubali kwamba nitaenda kuangalia matatizo yaliyopo kule. (*Makofii*)

MHE. AGNESS E. HOKORORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wanawake wa Mkoa wa Mtwara wamekuwa wakitumia muda mwinci kuhangaika na tatizo la maji, mbali ya kutembea umbali mrefu lakini pia wamekuwa wanatumia saa nyngi kusubiria au kungojea maji.

Je, Serikali haioni kwamba sekta hii ya maji haijachangia katika kuwapunguzia wananchi wa Mtwara umaskini kwa kuwa hasa tukizingatia kuwa zaidi ya asilimia 50% ya wananchi wa Tanzania ni wanawake na kwa hiyo walipaswa washiriki moja kwa moja katika shughuli za kimaendeleo ili kuinua uchumi na Pato la Taifa kwa ujumla. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Hokororo kama ifuatavyo:-

Kwanza nakubali kwamba sekta ya maji ina mchango wa kuchangia katika kuondoa umaskini na ndiyo maana tumeanzisha hii mipango ambayo tunafikiria ni endelevu kwa kila Halmashauri lakini kwa Mji wa Mtwara Waziri ameshaelezea mipango iliyopo ambayo itaongeza upatikanaji wa maji pale. (*Makofii*)

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Katika vijiji vingi vya Mkoa wa Mtwara matatizo ya upatikanaji wa maji yamepelekea wakulima wengi kuchagua kutumia *sulphur* ya maji badala ya *sulphur* ya unga. Na *sulphur* ya unga

inasemekana kwamba siyo rafiki sana wa mazingira, na hii ni kutokana na ukosefu wa maji ambapo *sulphurya* maji inahitaji kuchanganya na maji kwa hiyo maji hayapatikani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo na ni kikwazo kwa Kilimo Kwanza, lakini llani yetu ya Uchaguzi ya CCM imeagiza kwamba kufikia mwaka 2015 upatikanaji wa maji mijini uwepo kwa asilimia 95 na vijijiini kwa asilimia 75.

Ukiangalia mijini ongezeko lake ni asilimia tisa ambapo kwa kulinganisha na miaka mitano iliyopita iliongezeka kwa asilimia nane. Kwa vijijiini ongezeko lake ni asilimia 17.2 ukilinganisha na asilimia nne kwa miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka njue Serikali ina mkakati gani mahsuswa kuhakikisha kwamba upatikanaji wa maji vijijiini unaongezeka kwa hii asilimia 17 na hii itaweza kuhakikisha kwamba utekelezaji wa Kilimo Kwanza unakwenda vizuri. Ahsante. (*Makof*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, analosema Mheshimiwa Wambura ni kweli kwamba tumeamua kujituma kufanya zaidi vijijiini, lakini kama nilivowaeleza wakati natoa maelezo pale mwanzo huwa mgumu, kwa hiyo, tumepata matatizo huko mwanzo sasa tumefika mahali ambapo tuna vijiji zaidi ya 1,000 ambavyo viro tayari kwa utekelezaji. Lakini nitumie nafasi hii kusema kwamba hatua inayofuata sasa haitakuwa tena ya vijiji kumi kumi isipokuwa tutakuwa tunachukua vijiji kulingana na *coverage* ya maji. Kama kuna maeneo ambako pako nyuma zaidi vijiji vitakavyoingia kwenye mpango vitakuwa vingi zaidi kwa ajili ya kusukuma maendeleo ya upatikanaji wa maji katika maeneo kulingana na hali halisi. (*Makof*)

Kwa hiyo, tunaweka katika mpango wetu wa maendeleo wa miaka mitano tumeeleza vizuri sana na tumeweka *resources* na maji mionganini mwa vipaumbale kwa hiyo tunadhani tutasukuma zaidi kuelekea huko tulikokusudia kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

MWENYEKITI: Tuisikie Singida Mheshimiwa Diana Chilolo.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, wakati nauliza swali la nyongeza kwenye swali la msingi la Mheshimiwa Ritta Kabati, nililizila kero ya maji ya Wilaya ya Iramba, Kata ya Kinyangiri pamoja na Kengege na zingine, Naibu Waziri alinijibu vizuri sana kwamba Mheshimiwa Diana wewe tulia Bajeti yangu inakuja nitakupa ufanuzi, lakini sijaona ataje kabisa Kata hizo nilizozitaja ambazo zina kero kubwa sana toka enzi ya Uhuru. (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi wa swali la Mheshimiwa Diana Chilolo kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa kwenye sera yetu Halmashauri za Wilaya ndiyo zinaainisha vipaumbale vya vijiji ambavyo wanataka watekeleze kwa mwaka ule, na fedha hizi ambazo tumeziweka kwenye Bajeti zinakwenda kwenye vijiji vile ambavyo Halmashauri zenywewe ambazo na yeye Mheshimiwa Mbunge nina hakika anakuwa sehemu ya ile Halmashauri. Kwa hiyo, watashauriana na kupanga kuona vijiji anavyovitaka vipate maji viweze kuingia katika vipaumbale vipi. (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongezee kidogo tu juhudhi ambazo mimi niliziona katika Mkao wa Singida zinazosaidia upatikanaji wa maji, kwa sababu hatuwezi kuiachia Serikali kufanya kila kitu. Kule Singida na hasa Manyoni na nafikiri Mheshimiwa Chilolo ni shahidi kabisa, nimeona kwa kutumia Sheria ya *PPP* wao wamejitatihidi wanatumia madhehebu kupata vyanzo vingine vya maji.

Kwa mfano Mji wa Manyoni, Shirika la Damu Azizi ya Yesu ndilo linalochimba visima halafu linauzia Mamlaka ya Maji na Mamlaka inawauzia wananchi. Kwa kufanya hivyo upatikanaji wa maji umeongezeka. (*Makof*)

Kwa hiyo, nadhani tungeangalia pia kwamba tuangalie njia mbalimbali za kupata maji kama walivyofanya wale wa Manyoni na jinsi wanavyofanya pia wenzetu katika Mkao mMzima

wa Singida kwa kupata maji kutumia taasisi zingine mbalimbali hususani Mmashirika ya Ddini. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bwege, samahani Mheshimiwa Bungara. (*Kicheko*)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, wala hujasema jina baya, ni jina zuri sana hilo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hoja zangu nilimtaka Waziri aje Kilwa kuangalia matatizo ya mradi wa maji wa Mpala na Hospitali ya Kilwa, je, Waziri utanikubalia kuja Kilwa, ukinikubalia hilo tu basi shughuli yangu mimi imekwisha. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwenda Kilwa siyo *issue*, hilo ni jambo la kawaida tu kwenda Kilwa. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Bwege.

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Bwege kwamba yale maneno aliyosema kwamba hospitali ya Kilwa haina maji yalinikuna sana na mimi nilitaka kujua kwamba kwa nini hospitali nzima haina maji, nilimpata Mkuu wa Mkao wa Lindi na yeye amenithibitishia maji yapo na leo amepeleka Waandishi wa Habari kuonesha kwamba maji yanatoka. (*Makofi*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwanza kabisa naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Wasira kwa majibu yake mazuri ya kutupa matumaini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo naomba nirejee kwenye kitabu ambatanishi cha Bajeti kinachozungumzia miradi ya Benki ya Dunia ambacho kinasema Halmashauri ambazo zimepata kibali cha kutangaza zabuni kwa ajili ya kutafuta wakandarasi kujenga miundombinu ya maji ni pamoja na Halmashauri yangu ya Wilaya ya Songea ambapo Jimbo la Peramiko lipo ndani ya Halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa za uhakika kabisa nilizopewa na Waziri huyo amepewa nafasi ya kutangaza zabuni katika mradi mmoja tu wa maji wa kijiji cha Maweso na kuna matarajio ya mradi wa maji wa kijiji cha Lugagala kuititia Muungano Zomba na kuteremka vijiji vingine.

Hoja yangu ya msingi inabaki katika kijiji cha Lilondo ambacho wananchi toka mwaka 2006 walishachangia jumla ya shilingi milioni 24, kijiji cha Mkongotema na Magingu ambao wameshachangia si chini ya milioni 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa majibu na matumaini mazuri niliyopewa na Waziri kwamba tayari Ujerumanu na Benki ya ADB wameahidi kutoa fedha ili kufidia pengo hilo, na kama hawatazitoa Serikali imekubali kubeba jukumu hilo, naomba leo Waziri anithibitishie wale wananchi wa Mkongotema na Magingo wanaskia, wananchi wangu wa Lilondo wanaskia na vijiji hivyo vingine nilivyovitaja, hiyo fidia itakayoletwa ama fedha hizo zitakazoletwa kuititia Mfuko Mkuu (Hazina) zitapelekwa katika vijiji hivyo ambavyo nimevisema vina kero kubwa ya maji, wanagombania maji na tumbili na nyani huko chini kwenye visima hawapati maji salama. (*Makofi*)

Je, watakuwa *considered* sasa katika huo mpango, ningombwa sana nipate hayo majibu na wenywewe leo walisema kwa kweli watasikiliza hata kama Bunge tutamaliza usiku hawatalala mpaka waone haya majibu yakoje. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili liliwasilishwa vizuri sana na Mheshimiwa Mhagama jana, katika majibu yangu nimesema vijiji vya

aina hiyo hapa nchini tunavyo vingi na ndiyo maana tukasema ni lazima tutafute namna nyingine inayoweza kuongeza utekelezaji.

Ushauri wangu ni kwamba ikiwa tutapata nyongeza ya fedha na zikaenda katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea, nashauri kwamba Wilaya ya Songea ambayo ndiyo inayoamua *priority* inakwenda wapi, nisitisite juu ya kijiji anachokizungumza Mheshimiwa Mhagama ili *effort* ambayo imetolewa ya shilingi milioni 24 kama mchango isionekane ni adha kwa wananchi wale. (*Makof*)

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia. Katika kitabu cha nne cha Makadirio katika Wizara hii ukurasa wa 87 kuna billioni 38.5 ambazo zimetengwa kwa ajili ya mradi wa maji kule Kimbiji, wananchi wale maeneo yao yamechukuliwa muda mrefu kwa ajili ya mradi huu wa maji lakini hawajalipwa fidia, nilichokuwa nataka kujua kutoka kwa Waziri, je, ni kiasi gani cha fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kuwalipa fidia na fidia zao wazitegemee lini?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi hoja ya Mheshimiwa Ndugulile kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa maeneo yale ambayo tunataka kuchimba visima tulishaainisha maeneo ambayo yana mita 60 kila kisima. Sasa maeneo yale yote tulishayafidia na tukasema kwamba awamu itakayofuata baada ya mradi huu wa Kimbiji na Mpera tutaangalia maeneo makubwa zaidi. Sasa hiyo ni awamu nyingine lakini kwa awamu ya sasa ni maeneo yale ambayo tayari tumeshayalipa fidia. (*Makof*)

MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wakati nachangia niliweza kuainisha matatizo mawili makubwa, moja ni shida kubwa ya maji Mjini Namanyere na nyingine ni juu ya matumizi ya maji ya Bwawa la Kawa. Rais tayari alikwishatoa ahadi maji Namanyere ni taabu kubwa. Watalaam wakapinda migongo, wakaibua mradi wa billioni moja na nusu ili kuongeza kiwango kinachotolewa pale.

Je, Serikali itatupatia huduma hiyo sasa? Lakini kwenye mradi ule wa Nkundi katika Bonde la Kawa nikasema kwamba bwawa lile limetumia zaidi ya bilioni moja na milioni 92.

Vijiji vya Kalundi na Nkundi havina maji, nataka tamko la Serikali; je, Serikali itapeleka maji katika vijiji hivyo viwili?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kusema tu kwamba katika sera ya maji, kama kuna bwawa lipo mahali maji yale ni mali ya Serikali kwa hiyo bwawa lile ambalo lipo Kawa, yale maji yatatumika kwa matumizi ya wananchi ambao wapo karibu na vijiji vile. Kwa hiyo, sasa tutaangalia katika mipango yetu pamoja na Halmashauri tuweze kuona ni namna gani tutatengeneza miundombinu ili wananchi walopo waweze kutumia chanzo hiki cha Kawa. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed alikuwa amekupania kweli leo Naibu Waziri lakini sasa simuoni hapa, Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa wanawake wa Mara wanateseka sana na maji, na kwa kuwa vijiji vinavyozunguka Mgodi wa *North Mara* wanawake wale wanapata sana shida kwa sababu vyanzo vya maji vilichafuka na kemikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa ilitolewa hapa kwamba kuna visima vimechimbwa na Waziri wa Mazingira kitu ambacho sivyo, kwa hiyo ningependa kujua Wizara inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba inawapatia wananchi wale vyanzo vya maji safi na salama kwa kuchimba visima haraka sana kwa sababu wananchi wale wanateseka. (*Makof*)

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kabisa tatizo la wananchi wa vijiji vinavyozunguka Mgodi wa Nyamongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshirikiana na mgodi ule lakini Wizara kwanza ilikwenda kule kutazama ubora wa maji yale na ilishatoa taarifa na kwamba visima vimechimbwa ni kweli, ila bado havijajengewa, lakini tunataka kushirikiana na Mgodi wa Nyamongo katika kuongeza zaidi ubora na upatikanaji wa maji kwa vijiji vyote ambavyo vinazunguka pale viro kama saba. (*Makofii*)

MHE. MODESTUS D. KILIFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi nililizia juu ya Kata ya Mawindi na Kata ya Ipwani kwamba wananchi wale waliomba wapate maji ya kutegwa kutoka Mto Mpeng'o na upembuzi yakinifu umefanyika imeonekana utagharimu zaidi ya bilioni nane na Wilaya nzima ya Mbarali imeletewa milioni 600 kati ya hizo milioni 400 kwa ajili ya miundombinu na milioni 110 kujenga uwezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wananchi walikuwa na matumaini kwamba sasa watapata huduma hiyo ya maji na wameshirikishwa kuchanga fedha pamoja na kuandaa maeneo ya kupita maji kwa maana ya mtaro; je, Serikali ipo tayari sasa kuingiza nguvu yake ili kusaidia hawa wananchi ambao wanamatumaini lakini kwa fedha ambazo zimeletwa Mbarali haziwezi kumudu kukidhi haja ya mradi huo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Kilifi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza maeneo haya ambayo anayazungumza ni kweli kwamba kuna wasanifu ambao walipewa kazi hiyo na walileta hizo gharama. Lakini hizo gharama wamezipelea kwenye Halmashauri, sasa Halmashauri kwa mradi mkubwa namna hii hawana uwezo. Tunataka tuangalie kwa baadaye tuone kama Serikali inaweza ikaongeza nguvu pale. (*Makofii*)

MHE ABDUL R. MTEKETA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu nataka kuzungumzia kuhusu vyanzo vya maji kwa sababu vyanzo vingi vya maji vinafujwa na kuharibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kilombero sasa hivi mabwawa kama 20 yameshakauka na mito kama 40, je, Serikali ina mpango gani wa kulinda hivyo vyanzo vya maji katika Wilaya ya Kilombero?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekwishaweka mpango na Bunge lako hili limepitisha Sheria namba 11 ya mwaka 2009 ya rasilimali za maji. Sheria hii ndiyo ambayo sasa kinachotakiwa ni kuitekeleza sheria pamoja na regulations zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukitumia sheria hiyo basi tutaweza kutunza vyanzo vya maji. Lakini pia tukitegemea Serikali Kuu peke yake ndiyo itunze vyanzo vya maji hili ndugu zangu halitawezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Waziri wa Mazingira hapa alieleza kwa ufasaha akasema kutunza vyanzo vya maji ni wajibu wa wananchi wote, wakulima, wafugaji, tutumie sheria hii na kanuni zake ili tuweze kuvitunza. (*Makofii*)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Wasira na Mheshimiwa Eng. Lwenge, kwa kumwakilisha vyema Waziri mwenye dhamana ya maji kwenye kutoa hoja na kujibu maswali; sisi tunamwombea sana Mwenyezi Mungu, amrejeshee afya yake na aweze kurudi hapa Bungeni.

Itakumbukwa kwamba, katika mchango wangu nimeeleza tatizo pana la maji katika Wilaya ya Simanjiro, nikitoa mfano wa Kata za Naisinye, Mererani, Endayamtu na Shambalai, ambazo watoto wanapinda miguu kutokana na aina ya maji yanayopatikana. Ninatambua sana mazungumzo yanayoendelea kati ya Waziri Mkulo na Watu wa *BADEA* na Watu *OPEC Fund* kwa ajili ya maji ya Olkesumeti, lakini bado mpango huu utachukua muda mrefu. Hoja yangu ni kwamba, mpango ule wa dharura wa bilioni 1.8 wa kuweza kuwanusuru Wananchi wa Simanjiro ambao mifugo yao inahamia Kilindi na Handeni; fedha hizo zitatoka lini kuweza kuwasaidia Wananchi hawa wa Olkesumeti ambao sasa hivi wanalazimika kuhama? Nilikuwa naomba kauli ya Serikali katika eneo hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi kwa Mheshimiwa Ole-Sendeka, kama ifuatavyo:-

Kwanza, katika mazungumzo ambayo yanaendelea kati ya *BADEA* pamoja *ELIPS* ni vizuri kuweza kufadhilli mipango ambayo usanifu umeshakamilika kwa ajili ya Mji wa Olkesumeti. Tunafuatilia ili tuweze kukamilisha mazungumzo hayo. (*Makofii*)

Kuhusu mpango wa haraka (*quick win*), angalau wa kunusuru, naomba aniacie tutalitazama tuweze kuona nini tunaweza tukafanya na hizo fedha ziweze kupatikana ili kazi iweze kufanyika.

MHE. SILVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, maji yaendayo Dar es Salaam na chanzo cha maji cha Mto Ruvu kinapita katika maeneo ya Mji wa Kibaha, lakini bado maeneo mengi ya Mji wa Kibaha hayana maji na katika Programu ya Maji illyoanza mwaka 2009 katika vijiji 15 vilivyochedguliwa, pamoja na mshauri sanifu ku-mobilize Wananchi wakatoa michango yao mbalimbali na kuhifadhi kwa ajili ya Programu ya Maji, kwa muundo wa miamba katika Mji wa Kibaha; ni mitaa minne tu iliyofanikiwa kupata visima na visima hivyo bado maji yake si safi, kwa maana ya kuwa na chumvi nyingi. Sasa mitaa 11 iliyobakia haina maji na Wananchi wamekuwa *desperate*, hawajui wafanye nini ili waweze kupata maji safi. Halmashauri ilipofanya bidii kuomba *DAWASCO* waweze kuwapatia maji, bado suala hili limekuwa na kigugumizi kiasi kwamba, hata Madiwani wanataka kuja kumwona Waziri kujua waeleze nini kwa Wananchi.

(i) Ningependa Mheshimiwa Waziri anipe ufanuzi ni lini mitaa hii itafanyiwa utaratibu mbadala wa kupata maji kutoka chanzo cha Mto Ruvu ili na wao waweze kufaidi maji bila kuyaangalia yakielekea Dar es Salaam peke yake?

(ii) Ni lini tutapata mamlaka ambayo itaweza kusimamia maji katika Mji huu Mkuu wa Mkoa wa Pwani na unaoendelea kukua kwa haraka? Nitafurahi kama Waziri ataungana na mimi ili tuweze kututua tatizo hili kwa kuutembelea Mji wa Kibaha kuainisha na kujua matatizo haya ya maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Koka, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, huu Mpango Maalum wa Dar es Salaam, utahusisha pia Mji wa Kibaha na Bagamoyo; kwa hiyo, maeneo haya ambayo Mheshimiwa Mbunge anayazungumzia, tutayashughulikia katika Mpango huu. Mpango huo ambao upo ni katika muda huu mfupi, lakini katika muda mrefu lazima tupate maji ya kutoka Ruvu Juu.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Nami naomba nitoe mchango wangu au niulize maswali yangu kwa Mheshimiwa Waziri kwani hili linakugusa hata wewe mwenyewe Mwenyekiti huko Kongwa. Naomba nizungumzie tatizo la kupata taarifa katika Halmashauri zetu za matumizi ya fedha na upatikanaji wa takwimu sahihi ambazo niliziliza kwenye maswali yangu au nilleleza mchango wangu na pia taratibu mbovu za ununuzi wa vifaa kama vile *machine* au pampu ambazo ni mbovu za Kichina.

Nilizungumzia na kutolea mfano wa Hanang, ambapo mimi nilikuwa Diwani na nilieleza kitu ambacho nakijua na nyaraka ninazo hapa kama zinahitajika kwa ushahidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa iliyotolewa na Serikali tarehe 14 Februari, ilisema kwamba, Visima 15 vya Hanang vilichimbwa na vinane vinatoa maji. Taarifa iliyotolewa na Halmashauri hiyo hiyo kwenye Kikao cha Kamati ya Fedha tarehe 25 Februari, 2011 inasema, nyaraka zimepelekwa kwenda kukaguliwa kwa sababu kuna taratibu ambazo ni mbovu na zina dosari. Lingine, nilitoa mfano wa Kisima cha Gehandu, kimechimbwa mwaka 1968.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, swali sasa.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu nauliza kwamba; katika huo mpango wa uongo unaotolewa na Halmashauri zetu kwa Serikali; je, mna mpango gani na mnachukua hatua zipi? Mheshimiwa Waziri atujibu swali hilo. (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, hatuna mpango wa uongo ambaou unafanywa na Halmashauri, kwa hiyo, naomba afute hiyo kauli ya uongo haipo. Halafu pili, taratibu mbovu za manunuzi, nafikiri taratibu za manunuzi zimepitishwa na Bunge hili, sheria ipo ya kununua vifaa vya maji na vitu vingine; kwa hiyo, zinazingatiwa taratibu hizo. Ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilijilishe Bunge hili kwamba, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Hanang na kwamba mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Halmashauri na Mheshimiwa Rose Kamili naye ni Mjumbe wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang. Kwa hiyo, kama Halmashauri itakuwa imesema uongo ni pamoja na yeye ambaye ni Mjumbe.

Nilihakikishie Bunge lako kwamba, kati ya Halmashauri ambazo zinajitahidi mojawapo ni Halmashauri ya Wilaya ya Hanang. Pamoja na hela kidogo inayotoka kwenye Bajeti ya Serikali, Halmashauri ile imekuwa ikishirikiana na Wananchi wa Wilaya ya Hanang, Kanisa la Katolika kupitia BMDD na NGOs mbalimbali ikiwepo ADRA na *Living Water* na tumechimba visima tukishirikiana na Halmashauri yenye.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Rose asipende kusema uongo pamoja na yeye kuwa mmoja wa Wajumbe wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang. (*Makof*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda hauko upande wetu waliosimama walikuwa 76, lakini 23 hawajapata nafasi, naomba mniwie radhi dakika zilizobaki ni ndogo sana.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Tshs. 1,067,627,000/=
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i>	Tshs. 2,557,806,000/=
Kif. 1004 – <i>Information, Education and Communication</i>	Tshs. 155,310,000/=
Kif. 1005 - <i>Legal Services Unit</i>	Tshs. 225,839,000/=
Kif. 1006 – <i>Procurement Management Unit</i>	Tshs. 549,266,000/=
Kif. 1007 – <i>Management Information System</i>	Tshs. 220,983,000/=
Kif. 1008 – <i>Internal Audit Unit</i>	Tshs. 297,381,000/=
Kif. 2001 – <i>Water Resource Assessment and Exploration</i>	Tshs. 3,190,593,000/=
Kif. 2002 - <i>Central Stores</i>	Tshs. 152,362,000/=
Kif. 2003 – <i>Water Laboratory</i>	Tshs. 766,442,000/=
Kif. 2004 – <i>Directorate of Irrigation and Tech. Serv.</i>	Tshs. 0
Kif. 3001 – <i>Urban Water Supply and Sewerage</i> Tshs. 1,138,735,000/=	
Kif. 4001 – <i>Rural Water Supply</i>	Tshs. 4,081,384,000/=
Kif. 5001 – <i>Water Development and Management Inst.</i>	Tshs. 578,539,000/=
Kif. 6001- <i>Drilling and Dam Construction Agency</i>	Tshs. 0

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 49 – Wizara ya Maji

Kif. 1001 – *Administration and General*.....Tshs. 26,148,024,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning*Tshs. 3,856,701,000/=
Kif. 2001 – *Water Resource Assessment and Exploration*..... Tshs. 32,763,724,000/=
Kif. 2003 – *Water Laboratory*Tshs. 1,527,392,000/=
Kif. 2004 – *Directorate of Irrigation and Techn. Service*.... Tshs. 0
Kif. 3001 – *Urban Water Supply and Sewerage*Tshs. 313,547,996,000/=
Kif. 4001 – *Rural Water Supply*Tshs. 50,795,126,000/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilitrudia)

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU) (K.n.y. WAZIRI WA MAJI):
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi ilijadili Taarifa ya Makadirio na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, fungu kwa fungu na kuyapitisha bila mabadiliko; hivyo basi, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja illolewa iamuliwe)
(Hoja illamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2011/2012 yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Kwa jinsi hiyo, Bunge limepitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji. Tatizo la maji ni kubwa, tunawatakia kila la heri Wizara katika kushughulikia tatizo hili ambalo ni moja ya kero kubwa sana kwa Watanzania wote. Naona kuna Waheshimiwa Wabunge wawili wamesimama, bado tuna dakika nyingi sana.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nitumie Kanuni ya 68(1), ambayo inasema, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote kusema maneno kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo asubuhi ilikuja hoja mbele ya Bunge lako kuhusu utaratibu ambao ulikiukwa na ulilidharaulisha Bunge. Hatua ya mwisho kabisa Bunge lilitrudiwa kuunda Kamati Teule, ambayo itafuatilia kuona ni jinsi gani ambavyo Bunge limedhalilishwa kutohakana na kitendo cha Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kurejeshwa. Tukiangalia Katiba, Ibara ya 63(2), naomba noisome: *"Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho Chombo Kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya Wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii."*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge limekubaliana kwa kauli moja kuunda Kamati Teule, lakini wale watuhumiwa bado watakwenda kuchunguzwa wakiwa katika nyadhifa zao. Ningemba tuangalie utaratibu huu, kweli utakuwa umezingatia misingi ya Utawala Bora na Haki? (Makof)

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka mwongozo wako tarehe 18, siku ya maswali kwa Waziri Mkuu, nilisimama kuuliza swali. Kabla sijamalizia swali Spika alinikatiza, kwa hiyo, hata swali lenyewe halikuelewaka na leo sikusudii kuuliza hilo swali kwa sababu sijui nimwulize nani.

Kwa kuwa Spika ameelekeza swali langu kwenye ofisi yake, sasa nilitaka kujua kama kuna Kanuni ya kumwuliza Spika maswali na kama haipo ingepaswa basi iwekwe siku ya kumwuliza Spika maswali, kwa sababu kuna maswali mengi sana yanayohusu Bunge ambayo hatutakuwa na mtu wa kumwuliza. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine; tuna Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge); ni kazi gani ambayo huyo Waziri atafanya kama tunashindwa kuuliza maswali yanayohusu Ofisi za Wabunge? (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine tumewachagua watu watano kukaa kwenye Kiti hicho; Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyevitii Watatu; ni Kanuni ipi ambayo Spika anaitumia kumfokea Mbunge au Waziri kwa sababu tuliwachagua ili mtimize Shughuli za Bunge; sitegemei kwamba tuliwachagua ili mumfokee Waziri au Mbunge? Nataka ufanuzi. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutakubaliana kwamba, kwa kweli muda wetu hauturuhusu kuendelea kwa sasa kwa sababu tumekubaliana tutakuwa tunamaliza saa 7.15 kwa jinsi hiyo miongozi hii itatolewa ufanuzi wakati mwingine muafaka. Kwa sasa naoamba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni ya leo.

(*Saa 7.17 mchana Bunge lilitishwa hadi saa 10.00 jioni*)

(*Saa 10.00 jioni Bunge lilitrudia*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu kwa hatua inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 - Wizara ya Katiba na Sheria

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Katibu. Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri, kwa ajili ya kutoa hotuba yake, nataka nitumie dakika hizi chache kutoa ufanuzi ufuatao:-

Asubuhi ya leo, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, alinitaka nitoe Mwongozo kuhusiana na suala lilioljitekeza leo asubuhi na hoja ilikuwa kwamba; kwa nini wahusika watakaochunguzwa na Kamati Teule wasisimamishwe kazi kwanza ili Kamati iweze kufanya kazi yake. Majibu yake ni kwamba; kwa mujibu wa Kanuni ya 53(8), inasomeka hivi: "Mbunge ye yeyote hataruhusiwa kufufua jambo lolote ambalo Bunge lilikwisha kuli amua ama katika Mkutano wake huo uliopo au ule uliotangulia, wala kuwahisha shughuli za hicho chombo ambacho tumekipa kazi. Kwa jinsi hiyo, jambo hilo tuiachie hiyo Tume yetu itakayoundwa na Mheshimiwa Spika, ambayo itatajwa majina yake kwa wakati mwafaka pamoja na hadidu za rejea za hiyo Tume kwa wakati huo na itafanya kazi kufuatana na maelekezo ya Mheshimiwa Spika.

Kwa hiyo, sisi tusijiingize kwenye kutaka nani asimamishwe kazi au iweje. Baada ya Mwongozo huo, naomba sasa nimwite Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Celina Kombani, aje tuendelee.

Mheshimiwa Waziri, karibu. (*Makof*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako

Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Musa Siliima, kwa kupoteza wazazi wao wote wawili. Mungu awape nguvu na uvumilivu katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa tena kwa awamu ya pilii, kulongoza Taifa letu. Pia namshukuru sana kwa namna ya pekee, kwa heshima kubwa aliyonipa kwa kunteua kuiongoza Wizara hii nyeti ya Katiba na Sheria. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais pamoja na Watanzania kwa ujumla kwamba, nitajitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu, kufanikisha malengo ya Wizara na hatimaye Taifa letu lipate maendeleo. Pia nampongeza Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Makamu wa Rais. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Awamu ya Saba ya Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Mpanda Mashariki na kwa kuteuliwa kwake kwa mara ya pilii na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hatimaye kuthibitishwa kwa kura nyingi na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walopewa nyadhifa za kuiongoza Wizara mbalimbali katika Serikali hii ya Awamu ya Nne. Vilevile, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Kwanza Mwanamke kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mbunge wa Dole na Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kwa kuchaguliwa kwao kuwa Wenyeviti wa Bunge hili. Wote nawatakia mafanikio mema katika kuliongoza Bunge letu Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Jaji Mohamed Chande Othman, kwa kuteuliwa kuwa Jaji Mkuu wa Tanzania na hivyo kuiongoza moja ya mihimili mitatu ya dola. Ninaahidi kumpa ushirikiano mkubwa katika utendaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kuwa Wajumbe wa Kamati hii. Ninaishukuru kwa dhati Kamati chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge; na Makamu wake Mheshimiwa Angella Jasmine Kairuki, Mbunge, kwa ushirikiano, maoni na ushauri wao. Kamati hii yenye Wajumbe walibobea katika fani mbalimbali ikiwemo fani ya sheria, imekuwa msaada sana kwangu katika kutekeleza majukumu yangu kwa kutumia ushauri na uzoefu wao. Maoni walijotupatia wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2011/2012, yamesaidia sana kuiboresha Hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kutoa pongezi za pekee na kuwashukuru kwa dhati, Mawaziri walionitangulia kuwasilisha hoja zao hususan Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda na Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Mbunge wa Jimbo la Kilosa na Waziri wa Fedha, kwa hotuba zao nzuri ambazo zimetoa mwelekeo wa ujumla katika masuala ya Mipango, Uchumi, Mapato na Matumizi na shughuli za Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012. Aidha, naendelea kuwashukuru Wananchi wa Jimbo langu la Ulanga Mashariki, kwa kuwa na imani nami mpaka nikapita Ubunge bila kupingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Katiba na Sheria, imekabidhiwa dhamana ya kusimamia utoaji haki, udumishaji wa haki za binadamu na kuishauri Serikali katika masuala ya utawala wa sheria, kwa lengo la kudumisha amani, usalama, utilivu na kuweka mazingira mazuri ya maendeleo, hasa wakati huu ambapo nchi yetu ipo katika mfumo wa uchumi wa soko huria, vyama vingi vya kisiasa na utandawazi. Pamoja na jukumu hilo, Wizara hii inawajibika kujenga mfumo wa sheria ambaa utakidhi mahitaji mapya ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na

kiteknolojia. Katika kufanikisha dhamana hii, Taasisi zilizo chini ya Wizara hii zinazotekeleza majukumu haya ni kama zifuatazo:-

- (a) Mahakama ya Tanzania ngazi ya Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu inayohusisha Divisheni za Biashara, Kazi na Ardhi, pamoja na Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo;
- (b) Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali;
- (c) Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania;
- (d) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;
- (e) Tume ya Utumishi wa Mahakama;
- (f) Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (*RITA*); na
- (g) Chuo cha Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea na utekelezaji wa majukumu na mipango yake kwa kuzingatia llani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005-2010, Malengo ya Milenia, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), Mpango Mkakati wa Wizara, pamoja na ahadi na maagizo mbalimbali ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, lengo la hotuba hii ni kueleza hali ya utekelezaji wa Ahadi za Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, malengo ya Wizara na makadirio ya bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika mwaka 2010/2011, ilikuwa na malengo yafuatayo:-

- (a) Uimarishaji wa Utoaji wa Ushauri wa Kisheria nchini;
- (b) Usimamizi wa Haki za Binadamu na Masuala ya Katiba;
- (c) Utayarishaji wa Miswada ya Sheria na Hati mbalimbali;
- (d) Usikilizaji na Uendeshaji wa Mashauri nchini;
- (e) Utafiti na Mapitio ya Sheria mbalimbali;
- (f) Uimarishaji wa Shughuli za Usajili, Ufilisi na Udhamini;
- (g) Uboreshaji wa Mfumo wa Habari, Elimu na Mawasiliano;
- (h) Ujenzi wa Mahakama na Ofisi kwa ngazi mbalimbali;
- (i) Kuendelea na utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria na Miradi ya Maendeleo;
- (j) Usimamizi na Uendeshaji wa Vyuo vya Mafunzo;
- (k) Usimamizi wa Maadili ya Majaji na Mahakimu;
- (l) Kuboresha Maendeleo na Ustawi wa Watumishi; na
- (m) Kushughulikia masuala Mtambuka

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali, imeendelea kutekeleza jukumu la kuimarisha eneo la utoaji wa ushauri wa kisheria kuhusu masuala ya Mikataba ya Kibiashara, Kikanda, Katiba na Haki za Binadamu, uandishi na urekebu wa sheria; kuiwakilisha Serikali katika mashauri mbalimbali ya jinai na madai ndani na nje ya nchi na kuendelea kuongeza idadi ya Mawakili wa Serikali, ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wa utaalamu mahususi na kuwapatia vitendea kazi ili kuwawezesha kumudu majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali, imeweza kushughulikia Mikataba 318 na kutoa ushauri wa kisheria kwa Wizara mbalimbali ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Rais na Ofisi ya Waziri Mkoo. Pia, Ofisi imekuwa inaendelea kukagua Mikataba ya Manunuzi na kuitolea ushauri wa kisheria. Aidha, Mikataba 82 iliyohitaji maoni na ukaguzi (*vetting*) ilishughulikiwa. Ofisi pia ilishiriki katika majadiliano ya Mikataba baina ya Serikali na Makampuni, Taasisi na hata Serikali za nchi nyingine. Kwa mfano, Mchakato wa Utengamano wa Afrika Mashariki; SADC; Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali, imeendelea kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali na katika Mikataba inayoihusu Serikali pamoja

na Asasi zake. Pia katika kutekeleza jukumu hilo, imekuwa ikishiriki katika Timu za Serikali za Majadiliano (*Government Negotiating Team- GNT*). Kama wengi wetu tunavyoolewa, Mikataba wowote hujumuisha Sekta ya Kisheria, ya Ufundu, kutegemea Sekta inayohusika na pia masuala ya kifedha. Huo ndiyo msingi wa Serikali kuendelea na matumizi ya timu za wataalam (*GNT*) ili kuwezesha utaalalm mbalimbali ujumuike kwa pamoja pale Serikali inapokuwa katika majadiliano ya Mikataba. Aidha, Mawakili wa Serikali wameendelea kutoa ushauri katika masuala ya kisheria na uendeshaji wa mashauri ya jinai na madai mbalimbali. Pia Ofisi imeanza kuangalia usahihi wa Mikataba katika nyanja za kiufundi na kifedha ili kujiridhisha kama inakidhi maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine iliyochukuliwa na Serikali ni ya kuurekebisha Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kuitenganisha Divisheni ya Madai na Sheria za Kimataifa iliyokuwa inashughulikia masuala ya Mikataba na uendeshaji Mashauri kuwa Divisheni mbili tofauti, moja ikijikita katika kushughulikia Mikataba ya Kibiashara na ile ya Mahusiano ya Kimataifa na nyingine ikijikita katika kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya madai katika Mahakama na pia katika vyombo vya upatanishi. Mabadiliko haya yanalenga kuwaimarisha Mawakili wetu kuweza kuwa na ueledi kutohana na utaalalm na uzoefu katika maeneo watakayoyashughulikia (*Specialization*). Baadhi wataimarishwa na kuwafanya wabobee katika Mikataba ya aina mbalimbali, ikijumuisha utaalalm katika maeneo ya madini, mafuta, gesi asili, kodi, uzalishaji umeme, teknohama na mengine. Wakati wengine wataimarishwa ili wabobee katika uendeshaji wa mashauri katika Mahakama za ngazi mbalimbali na katika mabaraza ya usuluhishi mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri wenye mapendekezo ya kuanzisha utaratibu wa kisheria wa kuitambua kada ya Mawakili Jamii (*Paralegals*) ili waweze kutoa msaada na huduma za kisheria kwa Wananchi hususan wale wa vijiji, ambako kwa sasa hakuna huduma za Mawakili wa Kujitegemea (*Advocates*). Aidha, Wizara kwa kushirkiana na Taasisi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali (*NGOs*), imeendelea kutoa huduma za kisheria kwa Wananchi wasio na uwezo wa kugharimia huduma hizo. Sanjari na hilo, katika siku ya Msaada wa Sheria (*Legal Aid Day*), inayoendeshwa na *Tanganyika Law Society* chini ya Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Sheria, jumla ya Wananchi 688; kati yao wanawake wakiwa 249 na wanaume 439, walipewa huduma na msaada wa kisheria katika mashauri ya migogoro ya ardhi, ndoa na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu chini ya utekelezaji wa Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Sheria, imefanya upembuzi yakinifu kwa lengo la kuanzisha mtandao wa msaada wa kisheria (*Legal Aid Literacy Network*). Taarifa ya upembuzi huu tayari imejadiliwa na wadau na mapendekezo ya kuundwa kwa Sekretarieti ya Uratibu chini ya Chama cha Wanasheria Tanganyika (*Tanganyika Law Society*), yametekelezwa kwa kuajiri watumishi wanne na ofisi imefunguliwa kwenye Jengo la IPS na wataanza kazi mwezi Agosti, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi wa Haki za Binadamu na Masuala ya Katiba; Wizara yangu kwa kushirkiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, iliendelea kushughulikia malalamiko ya Wananchi kwa kutoa ushauri wa kisheria, kutoa elimu kwa umma, kufanya uchunguzi na utafiti juu ya masuala yanayohusu haki za binadamu na Utawala Bora. Tume ilipokea jumla ya malalamiko mapya 1,333 na ya zamani 7,542. Malalamiko 1,042 yalipatiwa ufumbuzi na kufungwa, sawa na asilimia 12 ya malalamiko yote yaliyofunguliwa. Malalamiko 7,833 bado yanaendelea kushughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuutiliaji wa malalamiko ya Wananchi pia ulifanyika kuititia uchunguzi na usikilizwaji wa hadharani juu ya vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu na misingi ya Utawala Bora vinavyofanyika katika sehemu zenye migogoro ya ardhi na madini. Usikilizwaji huo ulijumuisha Watendaji, Wananchi na Wawekezaji katika Wilaya 15 katika Mikoa ya Tanga, Manyara, Mara, Shinyanga, Rukwa na Morogoro. Aidha, idadi ya Wananchi walipewa ushauri wa kisheria nayo iliongezeka. Jumla ya walalamikaji 624 walipewa ushauri na msaada wa kisheria. Kutohana na malalamiko haya, mashauri 14 yamefunguliwa katika Mahakama za Dar es Salaam na Pwani na yanasmamiwa na Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ilifuatilia hali na haki za watoto walioko katika vizuo kwa kukagua vituo 65 wanakozuiwa watu ikiwemo magereza, polisi, mahabusi za watoto na shule ya maadilisho ili kubaini hali za watoto, sababu za kuwepo katika sehemu hizo na mbinu za kuwaepusha katika mazingira hayo. Taarifa yenye mapendekezo imepelekwa katika taasisi husika kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Vile vile, Tume kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali, inaendelea kukamilisha Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (*The National Human Rights Action Plan for the Promotion and Protection of Human Rights*) kama ilivyoazimiwa katika Tamko la Vienna la mwaka 1993 (*The 1993 Vienna Declaration*), ambapo nchi zote Wanachama wa Umoja wa Mataifa, walitakiwa kuanzisha Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu. Mpango huo ukikamilika utaonesha Dira na Mikakati ya kukuza, kulinda na kutetea haki za binadamu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009, Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa (*United Nations Human Rights Council*), iliweka utaratibu mpya wa kupima Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa (*Universal Periodic Review - UPR*), jinsi zinavyotekeleza mikakati mbalimbali ya Umoja wa Mataifa kuhusu masuala ya haki za binadamu ambapo nchi hupimwa kila baada ya miaka minne. Aidha, Wizara yangu kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 iliandaa taarifa na kuiwasilisha katika Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatarajiwa kufanyiwa tathmini ifikapo mwezi Oktoba, 2011. Vilevile, kwa upande mwingine, Taarifa ya 17 kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa kuhusu uondoaji wa aina zote za ubaguzi wa rangi imekamilika na itawasilishwa kwenye Kamati inayohusika na masuala ya kuzuia ubaguzi wa rangi. Taarifa hizi zinatusaidia kujenga taswira nzuri kwa nchi yetu na hivyo kuwafanya wadau wa maendeleo kutusaidia katika kuzikabili changamoto zinazotupunguzia kasi ya maendeleo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, iliandaa na kushiriki kikamilifu kwenye Maadhisho ya Siku ya Haki ya Binadamu Duniani, ambayo huadhimishwa tarehe 11 Disemba ya kila mwaka. Kaulimbi ya mwaka 2010 iliwa "Paza Sauti, Kemea Ubaguzi" (*Speak Up, Stop Discrimination*). Mheshimiwa Spika ndio aliyekuwa mgeni rasmi katika Maadhisho hayo. Kwa niaba ya Wizara, tunamshukuru sana. Maadhisho hayo yanatukumbusha wajibu wetu wa kuhudumia Wananchi kwa kuzingatia Utu na Misini ya Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza kauli ya Mheshimiwa Rais alioitoa tarehe 30 Disemba, 2010 kuhusu dhamira ya Serikali kuanzisha mchakato wa kuandika Katiba mpya ya Nchi, Wizara yangu imeandaa Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Nchi na kuuwasilisha Bungeni. Muswada huo unalenga kuanzisha Tume ya Kuratibu Maoni ya Wananchi na kuweka utaratibu wa kufanya kazi hiyo. Baada ya Muswada huo kuwasilishwa Bungeni, Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala iliwasilisha kwa wadau kwenye Mikutano iliyofanyika Dodoma, Dar-es Salaam na Zanzibar. Endapo Muswada huo utajadiliwa na kuitishwa na Bunge na kisha kuidhinishwa na Rais kuwa Sheria, tutakuwa katika nafasi nzuri ya kuendelea na mchakato wa kuandika Katiba mpya. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuwe mstari wa mbele katika kuwaelimisha Wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika mchakato huo wa kuandika Katiba mpya.

Mafanikio ya mchakato huo yatatokana na sisi Wabunge kuwa na mtazamo chanya juu ya mapendekezo haya ya Serikali yanayolenga kufanya mabadiliko ya Katiba ya nchi. Aidha, ninawashukuru Wananchi na vikundi mbalimbali, vilivyotoa na vinavyoendelea kutoa michango yao ya maoni kuhusu uandaaji wa Muswada utakaowezesha kuandikwa kwa Katiba mpya. Pia naishukuru Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa maoni iliyoyatoa baada ya mashauriano yaliyofanywa kati ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwanasheria Mkoo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Wataalam wao. Mashauriano hayo yamesaidia katika kuboresha Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa maelezo ya ziada na yanukuliwe kwenye *Hansard*, ambayo hayako kwenye kitabu changu kuhusu *Progress Report* au Maendeleo ya Mchakato wa Katiba kama ifuatavyo:-

Baada ya Muswada wa Mabadiliko ya Katiba uliosomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Tatu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 5 Aprili, 2011, Serikali iliondoa Hati ya Dharura iliyotumika kuwasilisha Muswada kwa madhumuni ya kuendelea kupata maoni zaidi kutoka kwa Wananchi. Tangu wakati huo, Serikali imefanya mambo yafuatayo:-

Kwanza, imetoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Katiba kwa kuelezea maudhui yake, ikiwemo kuunda Tume ya Kukusanya Maoni kutoka kwa Wananchi; kuweka utaratibu wa kukusanya maoni; kuweka mamlaka ya kuunda Bunge la Katiba; na kuweka utaratibu wa kuhalalisha Katiba mpya.

Pili, kati ya mwezi Aprili hadi Juni, 2011, kumekuwepo na vikao vinne vya mashauriano juu ya yaliyomo katika Muswada kati ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Wataalam wao. Vikao vilivyo fanyika ni vine; kikao kimoja kimefanyika Tanzania Bara na vikao vitatu vimefanyika Tanzania Visiwani. Mashauriano yaliyofanyika yalilenga katika kuleta maridhiano ya kuwa na uelewa wa pamoja.

Tatu, Serikali imefanya uchambuzi wa maoni mbalimbali yaliyotolewa na Wananchi, Vyama vya Siasa na Wadau wengine, ambayo baadhi yake yamezingatiwa na Baraza la Mawaziri katika kuuboresha Muswada.

Nne, Muswada umetafsirwa katika Lugha ya Kiswahili.

Tano, Kamati ya Baraza la Mawaziri la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiongozwa na Waziri Mkuu na Ujumbe wa Baraza la Mapinduzi ukiongozwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Wataalam, watakutana kwa ajili ya kupitia Muswada kwa pamoja ili kuuboresha zaidi. Baada ya maridhiano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Muswada pamoja na marekebisho yake, utawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya pili na mara ya tatu. Kwa kuzingatia ratiba ya Bunge, inatarajiwa katika siku zijazo itafanyika Semina kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu maudhui ya Muswada huu kabla haujawasilishwa Bungeni na tunategemea kwamba, Bunge la mwezi Novemba, Muswada huu utawasilishwa rasmi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuandaa Miswada ya Sheria na kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, kwa ajili ya kujadiliwa na hatimaye kupitishwa na kuwa Sheria za Nchi. Hadi kufikia mwezi Juni, 2011, jumla ya Miswada 12 iliandaliwa na kufikishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Kati ya Miswada hiyo, Miswada minne ilipitishwa na kuwa Sheria za Nchi na Miswada minane iliyobaki inafanyiwa kazi na Kamati za Kudumu za Bunge. Kati ya Sheria zilizopitishwa, Sheria 20 zilifanyiwa marekebisho, Sheria Ndogo 436 pamoja na Hati za Serikali, zimeandikwa au kuhakikiwa na baadaye kuchapishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliendelea kuandaa Sheria Ndogo zikiwemo Kanuni zinazoandalika chini ya Sheria mbalimbali, Sheria ndogo za Halmashauri za Majiji, Wilaya na Miji. Aidha, Ofisi hii kwa kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, imetafsiri Sheria zipatazo 11 na Muswada mmoja toka Lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili na zimeshaanza kutumika. Sheria hizo ni Sheria ya Watoto (Sura ya 15), Sheria ya Kinga na Uhibiti wa UKIMWI (Sura ya 431), Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sheria ya Ubua baina ya Umma na Watu binafsi ya mwaka 2010, Sheria ya Tafsiri ya Sheria (Sura ya 1), Sheria ya Kanuni ya Adhabu (Sura ya 16), Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Sura 20), Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010 na Sheria ya Misitu (Sura ya 323) na Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imekuwa ikifanya juhudzi za kupunguza mashauri ya madai, katiba na jinai katika Mahakama zote nchini. Katika mwaka 2010/11, Mahakama ya Rufani imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la usikilizaji mashauri haya na utoaji haki. Jumla ya mashauri 2,172 yalikuwepo kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010 na mashauri 685 yalipokelewa

kwa mwaka 2010/2011 na kuwa na jumla ya mashauri 2,857. Kati ya haya, mashauri 798 yalisikilizwa na kutolewa uamuzi. Mashauri hayo yaliyosikilizwa ni sawa na asilimia 28 ya mashauri yote yaliyokuwepo, baada ya Mahakama ya Rufani kufanya vikao 21 kati ya vikao 23 vilivyopangwa. Mashauri yanayoendelea kusikilizwa ni 2,059.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11 Mahakama Kuu ilipokea mashauri 9,453 mapya na kufanya kuwa na jumla ya mashauri 20,385. Kati ya hayo, mashauri 10,932 yalikuwepo toka Mwaka wa Fedha wa 2009/2010. Jumla ya mashauri 9,669 yalisikilizwa na kuhitimishwa kwa mwaka 2010/2011. Mashauri yaliyosikilizwa ni sawa na asilimia 47 ya mashauri yote yaliyokuwepo. Mashauri 10,718 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa. Usikilizaji wa mashauri hayo ni matokeo ya kufanya vikao 78 kati ya 156 vilivyopangwa kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi illuanza Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 ikiwa na Mashauri 154 na ilipokea mashauri mapya 266 na kufanya jumla ya mashauri kuwa 420. Mashauri 144 yalisikilizwa na kuhitimishwa na mashauri 276 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa kwa mujibu wa Sheria za zamani za kazi. Mashauri yaliyosikilizwa ni sawa na asilimia 34.3 ya mashauri yote yaliyokuwepo.

Mahakama hii pia illuanza Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 ikiwa na mashauri 1,333 na ilipokea mashauri 1,067 mapya na kufanya jumla ya mashauri 2,400. Mashauri 893 yalisikilizwa na kuhitimishwa na mashauri 1,507 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa kwa mujibu wa Sheria mpya za kazi. Mashauri yaliyosikilizwa ni sawa na asilimia 37.2 ya mashauri yote yaliyokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha utatuzi wa migogoro ya kiajira na kikazi nchini, Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi illandaa na kuendesha mafunzo ya siku mbili kwa Watumishi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*CMA*) pamoja na baadhi ya Wadau wa Divisheni ya Mahakama ya Kazi, juu ya namna ya kupunguza wingi wa marejeo yanayoletwa kwenye Divisheni ya Mahakama ya Kazi kutokea Tume. Wadau pia walipewa nafasi ya kutoa tathmini yao juu ya utendaji wa Divisheni hii pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi na kutoa maoni yao juu ya namna ya kuboresha utendaji wa taasisi hizi katika kushughulikia migogoro ya kiajira na kikazi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi illuanza Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 ikiwa na mashauri 4,141 na ilipokea mashauri 2,313 mapya na kufanya jumla ya mashauri kuwa 6,454; mashauri yaliyosikilizwa 1,371 na mashauri yaliyosalia ni 5,083. Mashauri hayo yaliyosikilizwa ni sawa na asilimia 21.2 ya mashauri yote yaliyokuwepo. Aidha, Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi iliweza kukaa vikao 21 tu kati ya vikao 45 vilivyopangwa kufanyika kulingana na bajeti iliyopatikana. Vikao hivi vilifanyika katika Mikoa ya Mwanza, Mbeya, Arusha, Kilimanjaro, Mtwara,Tabora na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha na kuharakisha usikilizaji wa mashauri yanayohusu ardhi, Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi ilianzisha Programu Maalum ya Kusikiliza Mashauri kwa lengo la kupunguza mlundikano wa mashauri yaliyokuwepo ijulikanayo kama *Case Back Log Program*. Programu hii imeanzishwa ili kusikiliza mashauri ya ardhi kwa njia ya vikao katika Kanda za Mahakama Kuu zenyé mashauri mengi. Awamu ya kwanza ya Programu hii imeanza kutekelezwa katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Dodoma, Tabora, Mwanza, Mbeya na Dar es Salaam. Aidha, Mheshimiwa Jaji Kiongozi aliwapangia Waheshimiwa Majaji 16 kusikiliza mashauri ya ardhi na waliweza kusikiliza mashauri 526. Kati ya hayo, mashauri 352 yalisikilizwa na kuhitimishwa katika muda wa wiki sita. Mashauri hayo yaliyosikilizwa na kuhitimishwa ni sawa na asilimia 67 ya mashauri yote yaliyopangwa kusikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara illuanza Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 ikiwa na mashauri 288 kutoka mwaka 2009/2010 na kupokea mashauri 154 mapya na kufanya kuwa na jumla ya mashauri 442. Kati ya hayo, mashauri 174 yametolewa uamuzi na mashauri 268 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa. Mashauri yaliyotolewa uamuzi ni sawa na asilimia 39 ya mashauri yote yaliyokuwepo. Mahakama pia imekamilisha uanzishwaji wa maktaba ya elektroniki, ambayo imewezesha baadhi ya nakala za hukumu na sheria kupatikana katika tovuti ya Mahakama ya Biashara (www.comcourt.go.tz). Aidha, Mahakama imeanzisha mfumo wa upatikanaji wa taarifa za mashauri kuititia ujumbe wa simu za mkononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama za Hakimu Mkazi zilanza mwaka 2010/2011 zikiwa na mashauri 20,256 na ilipokea mashauri 28,096 mapya na kuzifanya kuwa na jumla ya mashauri 48,352. Kati ya haya, mashauri 19,760 yalisikilizwa na kuhitimishwa. Mashauri yaliyosikilizwa na kuhitimishwa ni sawa na asilimia 41 ya mashauri yote yaliyokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama za Wilaya, Mwaka wa Fedha wa 2009/2010 kulikuwa na jumla ya mashauri 27,062 yaliyobaki na mashauri 57,227 mapya yalifunguliwa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na kufanya jumla ya mashauri 84,289 kuwepo katika Mahakama hizo. Kati ya haya, mashauri 47,677 yalisikilizwa na mashauri 36,612 yanaendelea kusikilizwa. Mashauri yaliyosikilizwa ni sawa na asilimia 57 ya mashauri yote yaliyokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama za Mwanzo ziliwu na mashauri 40,316 kutoka mwaka 2009/2010. Mwaka 2010/2011 mashauri 303,032 ilipokelewa na kufanya kuwa na jumla ya mashauri 343,340. Kati ya hayo, mashauri 219,693 yamesikilizwa, sawa na asilimia 64 ya mashauri yote yaliyosikilizwa na kubakia mashauri 123,647.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imefanikiwa kukamilisha mchakato wa kuanza kuwatumia wahitimu wa Shahada ya Kwanza ya Sheria kwenye Mahakama za Mwanzo. Waraka wa Utumishi Namba 1 wa Mwaka 2010, unaohusu Muundo wa Utumishi wa Kada zilizo chini ya Mahakama ya Tanzania, unaweka pamoja na mambo mengine, sifa ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo kuwa na Shahada ya Kwanza ya Sheria. Muundo huu umeanza kutumika tangu tarehe 1 Julai, 2010. Utaratibu hu unakusudiwa kutoa fursa kwa wenyewe mashauri kuwakilishwa kisheria kwenye Mahakama za Mwanzo na Mawakili. Aidha, utaratibu huo utasadia kupunguza tatizo la uhaba wa Mahakimu lilokuwa likisababishwa na Mahakimu wahitimu wa Stashahada kuondoka kwenda masomoni mara tu baada ya kuajiriwa ili kupata Shahada ya Kwanza ya Sheria, ambayo ingewavezesa kuwa Mahakimu Wakazi. Wizara katika kutekeleza azma hii, inao mpango wa kuanza kuajiri wahitimu wa Shahada ya Kwanza ya Sheria. Mahakimu waliopo sasa wasiokuwa na shahada wataendelea kutoa huduma kwenye Mahakama hadi hapo watakapokuwa wamejiendeleza zaidi na kupata shahada ya sheria au kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza jukumu la uendeshaji wa mashauri nchini, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hadi kufikia Juni 2011 ilikuwa na jumla ya Mashauri ya Madai 557. Mashauri hayo ni yale yaliyofunguliwa dhidi ya Serikali. Yapo pia mashauri kumi ambayo Serikali imeyafungua dhidi ya watu binafsi. Mashauri hayo yapo katika hatua mbalimbali za kusikilizwa na kutolewa maamuzi ya Mahakama. Kati ya mashauri hayo, mashauri 23 yameamuliwa na yamefikia ukomo, sawa na asilimia nne ya mashauri yote na mashauri 26 yamesikilizwa, sawa na asilimia tano ya mashauri yote yaliyoamuliwa katika ngazi ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Ofisi pia ilipokea jumla ya maombi ya madai 271 yaliyofunguliwa mahakamani dhidi ya Serikali na kati ya hayo, maombi 23 yalisikilizwa na kutolewa maamuzi. Aidha, yapo mashauri ya madai ambayo Serikali imeamuliwa na Mahakama kuyalipa lakini Serikali imeyakatia rufaa. Hali kadhalika, jumla ya migogoro minne ya masuala ya upatanishi (*arbitration*) inayohusu Serikali ilishughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ilipokea mashauri ishirini ya Kikatiba yaliyofunguliwa na Wananchi kwa mwaka 2009/2010 na mwaka 2010/2011. Pia mashauri mawili yanayohusu mgombea binafsi yalifunguliwa katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (*The African Court of Justice and Human Rights*). Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2010/2011, mashauri 38 yalifunguliwa na Wananchi pamoja na wanaharakati. Kati ya hayo, mashauri 30 yapo Mahakama Kuu na Mashauri manane yapo Mahakama ya Rufani. Hata hivyo, mashauri manne tayari yameshatolewa uamuzi na Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuitilia Divisheni ya Mashtaka, iliendelea kutekeleza jukumu lake la kuendesha mashtaka ya jinai katika Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu na Mahakama zilizo chini ya Mahakama Kuu na pia iliendelea kuratibu kazi ya vyombo pelelezi. Katika kutimiza wajibu huu, mafanikio makubwa yamepatikana katika uratibu wa upelelezi na uendeshaji wa mashauri

yaliyohusisha mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi, udanganyifu, utakasishaji wa fedha haramu na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Wizara yangu iliendelea kushirikiana kikamilifu na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Mamlaka mbalimbali katika kutokomeza mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi, tofauti na miaka mitatu iliyotangulia ambapo jumla ya matukio 54 ya mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (*Albino*) yalitokea. Jitihada zilizofanywa na Serikali kupitia vyombo vyetu vyenye dhamana na utoaji wa haki-jinai zilifaulu kudhibiti wimbi la mauaji hayo na ni tukio moja tu ndilo lilitokea kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 na hadi sasa Jamhuri imeshinda mashauri yote manne yaliyokwisha sikilizwa na Mahakama Kuu na mashauri matatu yaliyosikilizwa na Mahakama ya Rufani na inajizatiti kufanya hivyo kwa mashauri mengine yaliyosalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kujiimarisha katika mapambano dhidi ya aina zote za rushwa zilizoainishwa katika sheria zilizopo. Kwa namna ya kipekee, Wizara yangu imejishughulisha kwa karibu sana na mashauri yanayohusu rushwa kubwa na ubadhirifu wa mali za Umma (*Grand Corruption and Serious Fraud Offences*). Jumla ya majalada 192 yaliyohusu rushwa kubwa na ubadhirifu, yalipokelewa kutoka vyombo vyetu upelelezi vya TAKUKURU na Jeshi la Polisi ambapo majalada 82 yaliandaliwa hati za mashtaka na kupewa kibali cha kushtaki, majalada mawili yalifungwa baada ya kuridhika kuwa ushahidi usingetosheleza kuthibitisha mashtaka. Majalada 92 yalirudishwa kwa vyombo husika kwa ajili ya kufanyiwa upelelezi zaidi. Majalada 16 yaliyobaki yanaendelea kufanyiwa kazi na Divisheni ya Mashtaka. Sanjari na kuwafikisha watuhumiwa wa rushwa kubwa mahakamani, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanzisha Kitengo kipywa katika Divisheni ya Mashtaka kitakachokuwa na jukumu la urejeshaji na uchukua ji wa mali (*Assets Recovery and Forfeiture Section*) illyopatikana kwa njia ya uhalifu kwa washtakiwa wanaopatikana na hatia ya makosa ya aina hiyo Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeendelea kuendesha mashauri yanayohusiana na matumizi mabaya ya madaraka na wizi wa fedha kutoka akaunti ya madeni ya nje (*EPA*), yaliyofunguliwa takriban miaka miwili iliyopita. Kati ya mashauri 13 ya *EPA* yaliyofunguliwa mahakamani, shauri moja limetolewa uamuzi na washtakiwa wawili wametiwa hatiani na usikilizaji wa mashauri yaliyobaki unaendelea katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisitu. Aidha, mashauri tisa yanayohusu usafishaji wa fedha haramu (*money laundering*) na shauri moja linalohusu uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira katika eneo la maji ya Bahari ya Hindi yameendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Wizara yangu katika kutekeleza Mpango wa kutenganisha Shughuli za Upelelezi na Uendeshaji Mashtaka katika ngazi ya Mahakama za Wilaya na Mahakama ya Hakimu Mkazi, ilifanikiwa kupokea mashauri ya jinai 13,656. Kati ya hayo, mashauri 1,627 yalirudishwa kwa ajili ya upelelezi zaidi na mashauri 12,029 yaliyofikiswa Mahakamani na Mashauri 6,294 yalitolewa uamuzi, sawa na asilimia 52.3 ya mashauri yote yaliyofikiswa Mahakamani. Mashauri 5,538 bado yanaendelea kushughulikiwa. Uendeshajiji wa Mashauri ya makosa ya jinai uliofanywa na Mawakili wa Serikali katika ngazi hizi za Mahakama umechangia kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu kutoka wastani wa wafungwa 45,000 hadi 35,000 kwa mwaka 2010/2011. Aidha, mpango huo umeendelea kutekelezwa katika ngazi ya wilaya, ukiwa unazihusisha Mahakama za Wilaya za Makao Makuu ya Mikoa 15 kati ya 17 yenye Ofisi za Kanda za Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Sanjari na hatua hii, mchakato wa kupata majengo kwa ajili ya ofisi za mikoa iliyosalia unaendelea kwa msaada wa Mamlaka ya Miji na Wilaya pamoja na Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Sheria nchini. Sanjari na mpango huo, Wizara yangu kwa kushirikiana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imejipanga kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utenganishwaji wa upelelezi na uendeshaji wa mashtaka ili Wananchi wafahamu umuhimu wao katika uendeshaji wa mashauri ya jinai hasa pale wanapotakiwa kutoa ushahidi, jambo ambalo limekuwa likisumbua sana katika baadhi ya mashauri na hivyo kuwa chanzo cha ucheleweshaji wa uendeshaji wa mashauri nchini. Mafanikio mengine yaliyoanza kupatikana kutokana na utekelezaji wa mpango huo ni kuanzishwa kwa Jukwaa la Kitaifa la Haki Jinai linalounganisha pamoja vyombo vyote vinavyosimamia utekelezaji wa Haki Jinai nchini. Pamoja na kuwepo kwa mafanikio hayo, bado mpango huo unakabiliwa na

changamoto nyingi ambazo zimepunguza kasi ya utekelezaji wake. Mojawapo ikiwa ni uwezo mdogo wa Serikali kifedha na rasilimali watu katika kuyawezesha maeneo ya ofisi yanayopatikana yaanza kufanya kazi za uendeshaji mashtaka kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kuwezesha jukumu la uendeshaji mashauri mbalimbali Mahakamani, imeendelea na zoezi la kukamilisha uwekaji wa mtandao wa kompyuta ujulikanao kama *Casedocket Management System*, utakaowezesha kuhifadhi kumbukumbu na utunzaji wa nyaraka mbalimbali zinazohusu mashauri ili kuwawezesha Mawakili wa Serikali katika shughuli za uendeshaji wa mashauri nchini. Mtandao huo ukikamilika, utapunguza gharama za kusafirisha mafaili kutoka sehemu moja hadi nyingine. Aidha, mtandao huo pia utakuwa na mahusiano na mitandao mingine inayotumika hivi sasa kwenye Mahakama katika usikilizaji wa mashauri nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010, mashauri arobaini na manne yalifunguliwa kupinga matokeo ya Ubunge kwenye Majimbo mbalimbali. Hadi sasa mashauri kumi yameisha katika hatua za awali na kubaki mashauri thelathini na manne.

Kati ya mashauri hayo yaliyobaki, mashauri matano yapo tayari kusikilizwa na yataendelea kwa tarehe tofauti kwa kuzingatia muda maalum wa kusikilizwa, ambao ni miaka miwili baada ya uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, ilifanya mapitio ya sheria mbalimbali ili ziweze kukidhi mahitaji ya jamii. Tume iliendelea kufanya mapitio ya sheria zinazosimamia Sekta ya Mifugo kwa lengo la kuandaa mapendekezo yatakayolenga kuifanya sekta hiyo kuwa ya kisasa na endelevu zaidi. Rasimu ya awali ya taarifa ya mapitio ya sheria hizo imeandalila na utafiti wa sheria husika umepangwa kufanyika katika Mikoa ya Arusha, Manyara, Morogoro, Kilimanjaro, Dodoma, Shinyanga, Mara na Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume hii imekamilisha utafiti wa sheria za mila zinazofuata mkondo wa ukoo wa mama (*matri/lineal*). Utafiti uliolenga kuboresha sheria hii ulifanyika katika Wilaya za Nachingwea na Ruangwa Mkoani Lindi; Masasi na Nanyumbu Mkoani Mtwara; Ulanga, Kilosa Ifakara na Mvomero Mkoani Morogoro; na Namtumbo na Mbinga Mkoani Ruvuma. Taarifa ya utafiti huo imekwisha kuandaliwa na itawasilishwa kwenye ngazi za juu kufanyiwa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuondoa ukandamizaji dhidi ya wanawake, Serikali imeanzisha mchakato wa kufanya mapitio ya Sheria ya Mirathi na Uriithi na Sheria ya Ndoa. Waraka kuhusu ukusanyaji wa maoni ya Wananchi juu ya sheria hizo umeandalila na unasubiri kujadiliwa na Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza azma ya kuziimarisha na kuzioanisha sheria zinazohusu mapambano dhidi ya rushwa, Wizara katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, imeanzisha mchakato wa kuitafsiri katika Lugha ya Kiswahili, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329, ili Wananchi wengi waweze kuelewa maudhui ya Sheria hii. Kazi ya kutafsiri Sheria hii ambayo bado inafanywa na wataalam, inatarajiwa kukamilishwa katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamin (RITA) unashughulikia ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu muhimu za maisha ya binadamu kwa kusajili vizazi, ndoa, talaka na vifo. Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, idadi ya vizazi 625,670, vifo 73,810, ndoa 23,108, talaka 69 na watoto 33 wa kuasili walisajiliwa. Aidha, Wakala umeendelea kusimamia mirathi na kufunga mirathi ya zamani 14 ikilinganishwa na 13 iliyofungwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010. Wakala pia umeendelea kuandika na kutunza wosia mbalimbali. Mwaka 2010/2011 Wakala umefanikiwa kuandika na kutunza wosia zipatazo 36. Aidha, bado ipo haja ya kuendelea kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu uandikaji wa wosia pamoja na kupeleka huduma hii karibu na Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala umeendesa kampeni za kuhamasisha kuhusu uandikishaji na usajili wa vizazi na vifo katika Wilaya tano za Dodoma, Kinondoni, Mbeya, Igunga

na Ngorongoro. Sanjari na usajili, ufilisi na udhamini, wakala ulishiriki katika Wiki ya Maadhimisho ya Utumishi wa Umma pamoja na kufanya usajili kwa Waheshimiwa Wabunge Mjini Dodoma. Aidha, mafunzo ya huduma ya kuandika na kutunza wosia yalitolewa kwa Wananchi ili kuwapa mwamko wa uandikaji wosia ili kupunguza kwa kiwango kikubwa migogoro mingi inayotokea katika masuala ya mirathi. Ili kulipa msukumo suala hili, naomba niwahimize Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwa mfano kwa kuandika na kutunza wosia kwa kutumia Wakala huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wakala huu, imeendelea kutoa mafunzo ya uandikishaji wa vizazi na vifo katika ngazi ya wilaya na vijiji kwa watumishi wapatao 309 walio kwenye ngazi za Makatibu Tawala wa Wilaya, Wasajili Wasaidizi, watumishi walio katika vituo vya tiba, Maafisa Uhamiaji, Maafisa Usalama, Maafisa Tarafa, Watendaji wa Kata, Serikali za Mitaa na Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika masuala ya ufilisi na udhamini, Wakala umepewa mamlaka ya kisheria ya kuwa mpokezi na msimamizi rasmi wa watu na makampuni yaliyofilisiwa na Mahakama. Aidha, jumla ya miunganisho ya wadhamini wa Asasi 203 ilisajiliwa. Wakala pia umeendelea kuimarisha shughuli za udhamini kwa kuzitembelea Asasi mbalimbali zilizoandikishwa kwa nia ya kuwakumbusha wadhamini wajibu wao wa kulinda mali za Asasi hizo kwa kuleta marejesho kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 15 Julai, 2011 Wakala uliteuliwa na Mahakama Kuu kuwa mfilisi rasmi wa Kampuni ya Kufua Umeme iitwayo *Independent Power Tanzania Limited (IPTL)*. Majukumu ya Wakala ni kutoa notisi ya ufilisi kwa Kampuni ya *IPTL* na kufanya matayarisho ya Taarifa ya hali halisi ya Kampuni hii (*statement of affairs*), kufanya makubaliano kati ya msimamizi rasmi na wadeni wa *IPTL*, kukusanya mali na ugawaji wa mali kwa wadeni na wanahisa pamoja na kuhakikisha uendeshaji wa shughuli za *IPTL*. Hata hivyo, mnamo tarehe 12 Agosti 2011, Wakala umepata amri ya Mahakama ya kusitisha kwa muda shughuli za Ufilisi wa *IPTL* mpaka hoja za pande zote mbili zitakaposikilizwa na Mahakama mnamo tarehe 24 Agosti, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Wizara yangu iliendelea kutoa elimu kwa umma kuititia njia mbalimbali zikiwemo kurusha vipindi vya moja kwa moja na vile vya kurekodiwa vya runinga na redio; ushiriki wa pamoja wa Taasisi zote katika maonesho mbalimbali yakiwemo Maonesho ya NaneNane yaliyofanyika mwezi wa Agosti mwaka 2010 hapa Dodoma ambapo Wananchi zaidi ya 7,200 walihudumiwa; Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika mwezi Juni, 2011 Jijini Dar es Salaam ambapo Wananchi zaidi ya 6,700 walihudumiwa na siku ya msaada wa sheria kwa umma iliyoadhimishwa tarehe 11 Desemba, 2010 katika mikoa kumi ambapo Wananchi 688 walipewa elimu na msaada wa kisheria. Siku hii hufanyika kila mwaka kwa ushirikiano kati ya Wizara kuititia Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria (*LSRP*) na Chama cha Mawakili Tanzania Bara (*TLS*). Aidha, Wizara na Taasisi zake ziliendelea kuanzisha na kuboresha njia nyingine za mawasiliano na Wananchi kwa kutumia tovuti, vipeperushi na machapisho mbalimbali ili kuwawezesha Wananchi wengi zaidi kupata habari na elimu kwa urahisi zaidi.

Wizara pia imeandaa Mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano (*Information Communication Strategy*), kwa kuititia Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria, kwa lengo la kuboresha mawasiliano kati ya Wananchi na Wizara. Mkakati huu utaanza kutumika mara baada ya kupata maoni ya wadau. Sanjari na hatua hizi, Wizara pia imeunganishwa na Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano. Hatua hii itapunguza gharama za mawasiliano. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, inatarajia kuzindua tovuti yake iitwayo www.agctz.go.tz mwezi Septemba, 2011 ili kuwzesha utoaji wa taarifa zinazohusu shughuli za ofisi hiyo kwa ujumla. Kwa jinsi tovuti hiyo ilivyoandalialiwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itakuwa imeunganishwa na Wizara na Taasisi wadau katika Sekta ya Sheria mbali ya Wizara na Taasisi nyingine za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika kutekeleza uamuzi wa kujenga Mahakama Kuu katika kila Mkoa, katika mwaka 2010/11 imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Jengo la Mahakama Kuu Bukoba na tayari makabidhiano ya awali yamefanyika. Aidha, mchakato wa kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya pili wa Jengo la Mahakama Kuu Shinyanga

umekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza Mwaka wa Fedha wa 2011/2012. Pia, taratibu za ukarabati wa Jengo la Mahakama Kuu Dar es Salaam zimekamilishwa kwa kumpata Mkandarasi na Mkatuba umesainiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu tayari imesaini Mikataba na wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Mahakama za Mwanzo za Magoma - Korogwe, Ngorongoro MJini Wilaya ya Ngorongoro, Kerokore - Bukoba Vijiji na Boma Ng'ombe - Hai na shughuli za ujenzi zimekwishaanza. Aidha, ukarabati wa majengo ya Mahakama za Mwanzo za Mgandu na Mwamagambe - Manyoni umeanza. Ukamilishaji wa ujenzi wa Mahakama za Mwanzo za Tingi - Mbanga, Mbondo - Nachingwea, Laela na Msanzi - Sumbawanga na Robanda - Serengeti hakuweza kutekelezwa kutokana na ufinyu wa bajeti. Ujenzi na ukarabati wa Mahakama hizo utaendelezwa katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana (2010/2011), Bunge lako Tukufu lilitaarifiwa kuwa ujenzi wa Mahakama za Mwanzo ishirini za Kawe - Kinondoni, Kigamboni - Temeke, Maili Moja - Kibaha, Kisarawe MJini - Kisarawe, Mwanga MJini - Mwanga, Buguruni - Ilala, Gairo - Kilosa, Usevya - Mpanda, Mkomazi - Korogwe, Lukuledi - Masasi, Makuyuni - Monduli, Mafinga - Mufindi, Makongorosi - Chunya, Bunda MJini - Bunda, Sangabuye - Ilemela, Ulyankulu - Urambo, Songea MJini, Mtowisa - Sumbawanga, Bariadi MJini - Bariadi na Terati - Simanjiro, ungeanza baada ya kupata kibali toka Benki ya Dunia. Ujenzi huu ulishindikana kuanza kwa kuwa kibali hakutolewa kwa sababu ya kutokukubaliana kuhusu michoro ya majengo. Nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, sasa kibali kimeshatolewa na mshauri mwelekezi ameshapatikana. Aidha, taratibu za Sheria ya Manunuzi ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi zimeshatangazwa kwenye vyombo vya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika kutekeleza na kusimamia Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Sheria, kwa mwaka 2010/2011, iliiwezesha Mahakama ya Tanzania kukarabati na kuboresha Masjala na ofisi za takwimu katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, kwa lengo la kuongeza ufanisi wa huduma ya kupohea, kutunza na kutumia kwa usahihi nyaraka za mshauri mbalimbali yanayosajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria na Miradi ya Maendeleo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Taasisi nyininge, imeendelea kuboresha na kuimrisha shughuli za upeletezi wa makosa ya jinai kwa Jeshi la Polisi. Kwa mwaka 2010/2011, zabuni ya ununuza wa vifaa vya kisasa vya upeletezi wa makosa ya jinai imekwihatolewa na taratibu za manunuza ya vifaa hivyo zipo katika hatua ya kukamilishwa. Pia Programu hii, imeendelea kutoa mafunzo ya mbinu za upeletezi na haki za binadamu ili kuhakikisha uzingatiaji wa haki za binadamu kwa Maafisa na Askari wakati wakitekeleza majukumu yao. Jumla ya Maafisa na Askari 260 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ya mbinu za kisasa za upeletezi na matumizi ya teknohama katika shughuli za upeletezi wa makosa ya jinai na utakatishaji wa fedha haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Programu hii, imeliwezesha Jeshi la Polisi kuweka miundombinu ya mahabusu za watoto kwenye vituo vikubwa vya Polisi katika Mkoa wa Mbeya ili kutekeleza Sheria ya Watoto kwa kulinda haki zao. Ujenzi wa mahabusu ya watoto utakamilishwa Mwaka wa Fedha wa 2011/12. Programu hii pia imelisaidia Jeshi la Polisi kuanzisha dawati la jinsia na watoto katika Vituo vya Polisi. Aidha, vituo vitatu vya Polisi vya Chang'ombe - Temeke, Bomang'ombe - Moshi na Magu viko katika hatua za kufungua dawati hili ili kutoa fursa ya kupohea malalamiko ya unyanyasaji wa watoto na kijinsia kupitia mpango maalum wa upokeaji wa malalamiko na utoaji wa ushahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu hii katika kuboresha na kuimrisha taaluma na ujuzi wa wanasheria nchini, imeliwezesha Baraza la Taaluma ya Sheria (*Council of Legal Education*), kuanzisha ofisi itakayojitegemea kwa ajili ya uratibu na usimamizi wa taaluma ya sheria nchini, badala ya kutegemea majengo ya Mahakama. Vilevile, Wizara yangu kupitia Programu hii imeendelea na ujenzi wa majengo ya Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (*The Law School of Tanzania*), kwa awamu mbili. Ujenzi wa awamu ya kwanza unaohusisha majengo ya

utawala, maktaba, nyumba za watumishi, kantini, madarasa na jengo la mazoezi ya usikilizaji na uendeshaji mashauri unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa likiwemo Shirika la Maendeleo la Uingereza (*DFID*), ambalo kupitia Mradi wa Kupambana na Rushwa (*Tackling Corruption Project – TCP*), limetoa msaada wa kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa Divisheni ya Mashtaka na Taasisi nyingine nne za Serikali ikiwemo Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi, Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi katika Sekta ya Umma (*PPRA*), TAKUKURU na Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (*FIU*).

Katika mwaka 2010/2011, Mradi huu umeiwezesha Divisheni ya Mashtaka kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo waendesa mashtaka 110 juu ya kushughulikia uhalifu utokanao na vitendo vya rushwa na udanganyifu, kufanya tafiti, kuendeleza mpango wa kujenga mfumo wa utunzaji kumbukumbu na kununua vitendea kazi vilivyo saidia kutekeleza majukumu yake. Aidha, Mradi mwingine unaohusu Mpango wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania (*MKUMBITA*), unaotekelizwa na Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara yangu, umesaidia kuwezesha kuwepo kwa mazingira bora ya uwekezaji kwa kufanya mapitio mbalimbali ya sheria ikiwemo Mikataba ya Kibashara na uboreshaji wa mfumo wa uendeshaji na usikilizaji wa mashauri nchini, kwa lengo la kuharakisha utoaji wa haki kwa Wananchi na kuvutia wawekezaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Mradi huu umesaidia kufanya mapitio ya mfumo wa madai (*Review of the Civil Justice System*), ambapo sheria mbalimbali na kanuni zinazohusu mfumo wa haki za madai zinarejewa ili ziweze kukidhi mahitaji ya sasa ya kijamii, kiuchumi, kislasa na kiteknolojia. Mradi huu umeiwezesha Tume kukusanya hukumu mbalimbali kutoka Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu, kwa kuzipitia na kuandika kwa kifupi mambo yote ya msingi ya kisheria (*Legal Principles*), yaliyojadiliwa na kuamuliwa katika mashauri husika na kuyaweka kwenye tovuti ya Tume hiyo kwa ajili ya kuwarahisishia wadau mbalimbali kusoma na kuelewa misingi ya kisheria iliyotumika kufikia hukumu hizi. Aidha, Mradi huu pia umegharimia mapitio ya Sheria za Ardhi na Sheria za Kazi, kwa lengo la kutatua matatizo ya kisheria kuhusiana na migogoro ya ardhi, kiajira na kikazi kati ya waajiri na waajiriwa. Mradi huu pia unapitia mfumo wa Sheria za Ardhi kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata hadi Mahakama Kuu. Rasimu ya Waraka wa Majumuisho (*Position Paper*) kuhusu sheria hizi imeandalila kwa ajili ya kuanza shughuli za utafiti katika sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kupata uhisani wa Shirika la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) katika kuwajengea uwezo wa kitaalamu Mawakili kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali, Wanasheria na Wataalam wengine walio katika Wizara na Idara za Serikali, kwa kuwapatia mafunzo katika nyanja za kujadili, kuandika na kuhakiki Mikataba, kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa hatua zote za majadiliano ya Mikataba ili kuweza kubaini matatizo kabla ya Mikataba kusainiwa na hatimaye kuwa na Mikataba yenye maslahi kwa Taifa. Wanasheria na Wataalam kutoka katika Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali katika Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Ofisi ya Waziri Mkoo, Wizara ya Maliasili na Utalii, Nishati na Madini, Uchukuzi, Ujenzi pamoja na Mamlaka ya Mapato (*TRA*), Kituo cha Uwekezaji (*TIC*), Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*TAA*), Mamlaka ya Bandari (*TPA*) na Shirika la Mafuta ya Petroli (*TPDC*), wameshiriki katika mafunzo yaliyoendeshwa katika maeneo saba tofauti yanayohusu:-

International Practice for Negotiating Contracts in the Extractive Industry; Legislative Drafting of law Related to investment Contracts in the Extrative Industry; Negotiating Fiscal Investment Agreements in the Extractive Industry; Negotiating Public Private Partnership (PPP) Investment Agreements; Legislative Drafting of Large Scale Investment Contracts in the Mineral Sector; Contract Management Practices for large Scale Investment Contracts; and Negotiating Bilateral Investment and Double Taxation and Managing their Impact on Large Scale Investments.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama imeundwa kuhakikisha inasimamia maadili, utendaji kazi bora, pamoja na uwajibikaji wa Majaji na Mahakimu ili kurudisha heshima na imani ya Wananchi kwa Mahakama ya Tanzania, chombo ambacho kinategemewa kutoa haki sawa kwa wote na kwa wakati. Tume kwa mwaka 2010/11, imeshughulikia masuala ya

nidhamu sita ambapo Mahakimu wanne walirejeshwa kazini, mmoja shauri lake bado linaendelea kushughulikiwa na mmoja amefukuzwa kazi. Tume hii pia, ilitekeleza kazi mbalimbali zinazohusu uratibu wa ziara za kuitangaza kwa Wananchi na Watumishi wa Mahakama pamoja na kuendesha mikutano mitatu ya Watumishi wa Mahakama na vikao vitatu vya Wajumbe wa Kamati za Mikoa na Wilaya zilizopo Pwani, Tanga na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania ilianza rasmi uendeshaji wa mafunzo mwezi Machi, 2008, hadi sasa imesajili jumla ya wanafunzi 2,084. Kwa mwaka 2010/11, Taasisi hii ilisajili wanafunzi wapya 594 ikilinganishwa na lengo la kusajili wanafunzi 600. Wanafunzi 607 waliokuwa wanaendelea na mafunzo walihudhuria mafunzo kwa vitendo (*field placement*) katika sehemu mbalimbali za kazi nchini. Aidha, Mtaala wa Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ulihuishwa na Kanuni mpya za kuendesha mafunzo zillipitishwa kwa nia ya kuboresha mfumo wa utoaji mafunzo na upimaji wa wanafunzi katika mitihani. Taasisi hii pia iliendeleza ushirikiano na Shirika la Mawakili la Uingereza liitwalo *International Senior Lawyers Project*, ambapo Mawakili wa Kujitegemea 48 kutoka Nchini Uingereza walitoa mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Jijini Dar es Salaam kwa kushirikiana na Mawakili na Wahadhiri wa hapa nchini. Ushirikiano huu uliwezesha kutoa mafunzo kwa viwango vya kimataifa hususan kwenye maeneo ya Mbinu za Uwakili (*Advocacy Skills*), Maadili na Kazi ya Uwakili (*Professional Practice and Ethics*), Mwenendo wa Mashauri ya Jinai (*Criminal Procedure and Practice*), Mwenendo wa Mashauri ya Madai (*Civil Procedure and Practice*) na Uandishi wa Mikataba na Hati za Kisheria (*Legal Drafting Skills*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kuwa baadhi ya wanafunzi wanaojiunga na Taasisi hii hawana uwezo wa kugharimia mafunzo yao na kwa kuwa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu haiwaruhusu wanafunzi hao kupata mikopo kwa ajili ya kugharimia mafunzo, Serikali imekuwa ikitoa fedha kuitilia Wizara yangu kwa ajili ya kuwakopesha wanafunzi wahitaji. Mikopo hii inasimamiwa na Bodi ya Uendeshaji ya Taasisi hii. Tangu mwezi Agosti, 2008 hadi sasa, wanafunzi 1,369 wa Taasisi hii wamekwishapewa mikopo yenye jumla ya shilingi 3,842,172,560. Ili kulipatia ufumbuzi suala hili, Serikali inaendelea kutafakari utaratibu wa kudumu wa utoaji mikopo kwa wanafunzi wahitaji wa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu pia inasimamia Chuo cha Uongozi wa Mahakama - Lushoto (*Institute of Judicial Administration*). Chuo hiki kilianzishwa mwaka 1999 kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ngazi ya Cheti na Stashahada. Mafunzo ya Cheti cha Sheria yanawaandaa wanachuo kuwa makarani wa mahakama, watunzaji wa kumbukumbu za mahakama, maafisa wa sheria wasaidizi, maafisa tawala na waandishi wa habari za mahakama. Mafunzo ya Stashahada ya Sheria yanawaandaa wanachuo kuwa na ufahamu wa misingi na kanuni na sheria na utekelezaji wake katika utatuzi wa migogoro. Chuo kinaendesa mafunzo ya muda mfupi, semina zinazohusu Utawala Bora na utoaji wa ushauri wa masuala ya Utawala Bora. Aidha, chuo kuitilia kituo cha msaada wa sheria (*IJA, Legal Aid and Education Trust*) kinatoa ushauri wa kitaalamu kwa Wananchi wanaohitaji msaada wa kisheria, ambao wanashindwa kumudu gharama za Mawakili. Kituo pia kinatoa mafunzo na kufanya utafiti katika nyanja za haki za binadamu, usawa wa kijinsia, Utawala Bora na maeneo mengine ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Chuo kimeendesa mafunzo mbalimbali na kutoa wahitimu 450. Aidha, Chuo kimeendeleza ujenzi wa hosteli ya wanachuo wa kike, yenye uwezo wa kuchukua wanachuo 300; kimeandaa mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano 2010/2011- 2014/2015 na pia kimejenga tanki kubwa lenye uwezo wa kuhifadhi lita milioni moja za maji. Aidha, Viongozi wa Chuo hicho walipata nafasi ya kutembelea *Justice College* huko Pretoria ili kujifunza jinsi wenzetu wanavyoendesa mafunzo kazini kwa Mahakimu katika kuboresha utendaji kazi wa Mahakimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kutekeleza masuala mtambuka yanayohusu kupambana na maambukizi ya UKIMWI, kuzuia rushwa na kuzingatia suala la jinsia katika mipango ya maendeleo. Aidha, katika kutekeleza mpango wa kudhibiti maambuzi ya UKIMWI mahala pa kazi, Wizara yangu kwa kushirikiana na taasisi zake, iliendelea kuwapatia watumishi mafunzo ya namna ya kujikinga na maambukizi mapya ya ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na kuwapatia fedha kwa ajili ya kununua lishe bora. Ili kufahamu maendeleo ya afya za watumishi, baadhi walipata fursa ya kupima kwa hiari afya zao. Wizara pia iliendesa mafunzo ya

kuwaelimisha watumishi kuhusu madhara ya rushwa katika utumishi wa umma. Aidha, katika kusimamia madhara ya rushwa na maadili, Kamati za Maadili zilizoundwa ndani ya Wizara na taasisi zake, ziliendelea kuchukua hatua zinazostahili kwa watumishi walibainika na tuhuma dhidi ya rushwa pamoja na ukosefu wa maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa masuala ya jinsia katika mipango ya maendeleo, Wizara yangu imeteua waratibu wa madawati ya jinsia na kuwapatia mafunzo ili waweze kutekeleza majukumu yao katika kuratibu na kusimamia uzingatiaji wa masuala ya jinsia mahali pa kazi. Vilevile, elimu juu ya masuala ya jinsia imetolewa kwa watumishi 69 na kwa Waheshimiwa Majaji na Mahakimu 359 kuititia juhudzi za Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuleta ufanisi na tija katika utoaji haki na kuboresha utendaji kazi, Wizara imewapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ya fani mbalimbali watumishi 695 wa kada zote, nje na ndani ya nchi, ikiwa ni pamoja na mafunzo kazini (*on job training*). Watumishi 133 walijiriwa katika nafasi za Uwakili wa Serikali, Uhakimu na kada nyngine ili kujaza nafasi zilizokuwa wazi, watumishi 297 walipandishwa vyeo na watumishi 232 walithibitishwa kazini na katika vyeo vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara yangu katika kutekeleza dira yetu na majukumu yake, bado yapo mambo mengi ambayo hayajapata ufumbuzi wa uhakika.

Vyombo vyetu vya utoaji haki vinajitahidi lakini havijafikia kiwango cha kuwa kimbilio la wote wanaotaka haki likiwa ndiyo lengo la dira yetu. Mambo yanayochangia kutofikiwa kiwango hicho ni:-

(a) Ufinyu wa bajeti ambao umesababishwa na uwezo mdogo wa Serikali kifedha kutokidhi mahitaji ya Wizara yanayoongezeka kutokana na majukumu ya Wizara kupanuka;

(b) Upungufu mkubwa wa rasilimali watu hasa kwenye vyombo vyake vya utoaji haki kwa Wananchi unasababisha kuendelea kuwepo kwa mlundikano wa mashauri Mahakamani;

(c) Uwezo mdogo wa Wananchi walio wengi kuvifikia vyombo vya kutoa haki na huduma za kisheria, pia uelewa mdogo wa Wananchi kuhusu mfumo uliopo wa sheria na Mahakama nchini;

(d) Kuwepo kwa tabia ya kudai na kupokea rushwa na tabia zisizozingatia matakwa ya taaluma kwa baadhi ya watumishi katika Sekta ya Sheria kunakosababisha Wananchi kukosa imani na vyombo vya utoaji haki;

(e) Mazingira ya kazi yasiyoridhisha kwa watumishi wengi katika Sekta ya Sheria yanayotokana na uhaba wa vitendea kazi muhimu kama vile vyombo vya usafiri, upungufu wa majengo ya ofisi na samani, vitabu vya sheria, nyumba za watumishi, maslahi duni kwa Watumishi wa Serikali kunakosababisha baadhi kuacha kazi na kutokutumika kwa teknolojia ya kisasa katika uendeshaji wa mashauri;

(f) Kuchelewa kwa ujenzi wa Mahakama ya Rufaa na Mahakama za Mwanzo pamoja na Jengo la Makao Makuu ya Wizara;

(g) Suala la mikopo kwa wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu iliyopo inawaruhusu wanafunzi wa shahada ya kwanza (*undergraduate*) tu kupata mkopo na siyo wahitimu wa shahada ya kwanza wanaojunga na Taasisi hii.

(h) Suala la *no objection* kutoka *World Bank* ambalo linasababisha shughuli nytingi ama kutofanyika kwa wakati uliopangwa au kuchelewa kufanyika kwa sababu ya kutopata hiyo *status ya no objection*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kwamba, changamoto zilizoainishwa kimsingi zinatokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara kila mwaka wa fedha kutokana na udogo wa Pato la Taifa, Wizara yangu imeanza kubaini ufumbuzi wa changamoto hizo kwa kutayarisha mikakati na malengo mbalimbali katika Mpango na Bajeti ya Mwaka 2011/2012 kwa kutumia fedha zitakazoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kulingana na vipaumbele vya Wizara. Pia kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha pamoja na miongozo mbalimbali ya Serikali inayohimiza usimamizi na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali fedha na watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele vitakavyochochea ufumbuzi wa changamoto hizo vimejikita katika kutekeleza malengo ya 2011/2012, ambayo ni uendeshaji wa Mfuko wa Mahakama, kuongeza kasi ya ajira kwa Mahakimu na Mawakili wa Serikali ikiwa ni pamoja na uteuzi wa Majaji, uimarishaji wa Divisheni ya Huduma za Kisheria kwa Umma, ufuatilaji wa suala la rushwa katika ngazi zote za utoaji haki, kuongeza kasi ya usikilizaji na uendeshaji wa mashauri mbalimbali nchini ili kulipatia ufumbuzi suala la mlundikano wa mashauri mahakamani na msongamano wa mahabusu na wafungwa magerezani, uimarishaji wa utoaji wa ushauri wa kisheria nchini, utafiti na mapitio ya sheria mbalimbali, usimamiaji wa haki za binadamu na Utawala Bora na uimarishaji na uboreshaji wa vyuo vya mafunzo vinavyosimamiwa na Wizara. Pia uratibu wa mchakato wa Katiba mpya, utoaji wa elimu kwa umma, uimarishaji wa shughuli za usajili, ufilisi na udhamini, uboreshaji wa maendeleo ya watumishi na utekelezaji wa masuala mtambuka ya UKIMWI, Rushwa na Jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yote irekodiwe katika *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango na Malengo ya Wizara kwa Mwaka 2011/2012, kwanza ni kuhusu uendeshaji wa Mfuko wa Mahakama napenda kulishukuru Bunge lako Tukufu ambalo katika Mkutano wake wa Kwanza lilijadili na kuitisha Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama Na. 4 ya mwaka 2011, ambayo pamoja na mambo mengine inaaniszha Mfuko wa Mahakama ambao utaongeza uhuru na uwezo wa Mahakama katika kutekeleza jukumu lake la msingi. Ni matumaini ya Wizara yangu kwamba, kuwepo kwa Mfuko huu kutasaidia kuongeza ufanisi katika Mahakama, hususan kupunguza mlundikano wa mashauri kwa kiwango kikubwa. Aidha, kwa kuanzia, Serikali kwa mwaka wa fedha 2011/2012 imetenga shilingi bilioni 20 kwa ajili ya usikilizaji wa kesi Mahakamani, fedha hizi zitagawanywa kuanzia Mahakama ya Mwanzo hadi Mahakama ya Rufani kwa uwiano wa majukumu yatayotekelawa kwa kila ngazi ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni uteuzi wa Majaji, Ajira za Mahakimu na Mawakili wa Serikali. Napenda nitoe shukrani kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudu zake za kuendelea kuteua Majaji ili kupunguza mrundikano wa mashauri na kuongeza ufanisi katika ngazi ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Hadi sasa idadi ya Waheshimiwa Majaji imefikia kumi na tano (15) kwa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu ina jumla ya Waheshimiwa Majaji hamsini na nane (58). Kwa upande wa Mahakimu wapo 1,118, kati ya hao Mahakimu Wakazi 335, Mahakimu wa Mahakama za Wilaya 25 na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 758 na Mawakili wa Serikali ni 362. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inatarajia kuongeza idadi ya ajira za Mahakimu na Mawakili wa Serikali ili kukidhi mahitaji ya usikilizaji na uendeshaji wa mashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni uimarishaji wa Divisheni ya Huduma za Kisheria kwa Umma. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara itaendelea kuimarisha Divisheni ya Huduma za Kisheria kwa umma (*Public Legal Service Division*) kwa kuijengea uwezo wa vitendea kazi pamoja na kuajiri wataalam wa sheria wa kutosha ili kusaidia shughuli za kuratibu utoaji huduma za ushauri wa kisheria kwa jamii ya watu wasio na uwezo wa kulipia huduma hizo ili kufanikisha azma ya Wizara ya haki sawa kwa wote. Aidha, kuimarishwa kwa Divisheni hii kutawezesha kuwa kiungo muhimu kinachowezesha taasisi mbalimbali za watu binafsi na vikundi vingine vya kisheria nchini vinavyotoa msaada wa kisheria kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia mwongozo utakaotayarishwa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni mapambano dhidi ya rushwa. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) itaendelea kutekeleza mkakati wa Kitaifa wa kupambana na kuzuia rushwa. Sanjari na utekelezaji wa mkakati huu suala la rushwa katika Taasisi za Wizara litaendelea kufuatiliwa katika ngazi zote ili kubaini wala rushwa na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria. Aidha, kamati za maadili katika Wizara zitaimarishwa pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi juu ya athari za rushwa na mbinu za kuepuka vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, ni usimamizi wa usikilizaji na uendeshaji wa mashauri nchini, ili kukabiliana na changamoto ya ucheleweshwaji wa usikilizaji wa mashauri, Wizara yangu kupitia Mahakama ya Tanzania imeendelea kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kisasa kwa kuweka mfumo wa kieletroniki wa kurekodi mwenendo wa mashauri katika Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu Dar es Salaam pamoja na Divisheni za Mahakama Kuu ya Ardh, Biashara na Kazi. Hatua hii itasaldia kupunguza muda wa usikilizaji wa mashauri na upatikanaji wa nakala za hukumu ikilinganishwa na hapo awali ambapo mwenendo mzima wa mashauri ulikuwa ukiandikwa kwa mkono. Aidha, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara kupitia Mahakama ya Tanzania ina mpango wa kuweka na kuanza kutumia teknolojia hiyo katika Mahakama Kuu Kanda za Tabora, Mwanza, Bukoba, Arusha, Dodoma na Moshi pamoja na Mahakama ya Hakimu Mkazi, Kisutu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania katika ngazi zote na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, katika mwaka 2011/2012 itaongeza kasi ya usimamizi wa usikilizaji na uendeshaji wa mashauri mbalimbali nchini. Aidha, katika ngazi ya Mahakama ya Rufani, Mahakama hiyo imepanga kufanya vikao 30 katika vituo mbalimbali vya Mahakama Kuu ambako Mahakama ya Rufani huwa inafanya kazi. Vituo hivyo ni Arusha, Bukoba, Dar-es Salaam, Dodoma, Iringa, Mbeya, Mwanza, Mtwara, Sumbawanga, Tanga, Tabora na Zanzibar. Katika vikao hivyo, inatarajiwa kusikiliza jumla ya mashauri 1,140. Pia Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi imepanga kusikiliza na kuhitimisha mashauri 300 kwa sheria ya zamani na mashauri 600 kwa Sheria mpya. Mahakama hii itaendelea na ukarabati na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Ofisi lililoko Kinondoni, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Mahakama Kuu inatarajia kufanya vikao 260 katika kanda zake zote 13 za Arusha, Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Mbeya, Moshi, Mtwara, Mwanza, Songea, Sumbawanga, Tabora na Tanga na jumla ya mashauri 11,600 yatasikilizwa. Aidha, Mahakama Kuu Divisheni ya Ardh ina mpango wa kuboresha mazingira ya usikilizaji mashauri kwa kutumia mfumo wa teknolojia, kuimarisha mpango maalum wa usikilizaji wa mashauri (*case backlog program*) kwa awamu ya pili na ya tatu ambapo mashauri 960 yatasikilizwa na kuhitimishwa. Pia Mahakama hii itaendesha vikao 30 katika Masjala ndogo za Mahakama ili kuondoa mlundikano wa mashauri ya Ardh na Nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara itaendelea kusikiliza mashauri 225 ya kibiashara na kutoa uamuzi wa haki kwa kutumia vyombo vya teknolojia ya kisasa. Aidha, Mahakama hii pia itaendelea na ukarabati wa jengo ambalo litatumika kuanzisha masjala ndogo Mbeya. Sanjari na hayo Divisheni hii itaandaa na kukamilisha mchakato wa kanuni za kuendesha mashauri zitakazoleta mapinduzi katika kusimamia mashauri ya Kibiashara. Kwa upande wa Mahakama za Hakimu Mkazi jumla ya mashauri 23,712, Mahakama za Wilaya mashauri 57,212 na Mahakama za Mwanza mashauri 263,631 yatasikilizwa na kuhitimishwa katika mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Divisheni ya Mashtaka kwa mwaka 2011/2012 itaendelea kuendesha mashauri 7,099 ya makosa ya jinai ambayo hayajahitimishwa pamoja na mashauri mpya. Aidha, mashauri 534 ya madai na maombi ya madai 248 yaliyokuwepo pamoja na mpya yatakayopokelewa yataendelea kuendeshwa katika ngazi mbalimbali za Mahakama. Vile vile, Ofisi hii itaendelea kuendesha mashauri 32 ya Kikatiba na yanayohusu Haki za Binadamu katika Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, ni uimarisaji wa utoaji wa ushauri wa Kisheria nchini. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kuimarisha eneo la utoaji wa ushauri wa kisheria kuhusu masuala ya Mikataba, Katiba na Haki za Binadamu, Uandishi na Urekebu wa Sheria pamoja na kuiwakilisha Serikali katika mashauri mbalimbali ya jinai na madai ndani na nje ya nchi kwa kuwajengea uwezo wa kitaaluma Mawakili wa Serikali na Waendesha Mashtaka. Vilevile, katika kuhakikisha kwamba nchi inaendeshwa kwa misingi ya utawala wa kisheria na kutoa huduma bora kwa wananchi wake mapema, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kujengewa uwezo wa kuajiri watumishi wenye sifa na taaluma mbalimbali. Ofisi hii pia itaendelea kukiimarisha Kitengo chake cha takwimu kwa kuajiri idadi ya kutosha ya wataalam wa takwimu kwa lengo la kuonyesha takwimu za mchango wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kuokoa fedha ambazo Serikali ingedaiwa kila mara iwapo mashauri yote yanayoendeshwa Mahakamani ingeshindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, ni utafiti na mapitio mbalimbali ya Sheria. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara yangu kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, imepanga kuendelea kukamilisha taarifa za miradi ya utafiti wa Sheria za Kilimo, Mifugo, Mfumo wa Haki za Madai, Sheria inayohusu Uwekezaji wa Ushirika hasa Uwekezaji katika Ardhi pamoja na kupitia hukumu za Mahakama ya Rufaa na za Mahakama Kuu kwa Lengo la kubainisha hoja za kisheria zilizojadiliwa na kuziweka kwenye tovuti ya Tume (*Civil Justice Review Portal and Dynamic Website*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, usimamiaji wa Haki za Binadamu na Utawala Bora. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itaendelea kushughulikia na kukamilisha malalamiko 7,833 yaliyopokelewa miaka iliyopita. Aidha, Tume itaimarisha matawi yaliyopo mkoa wa Lindi, Zanzibar, Mwanza na kukamilisha ufunguzi wa ofisi huko Pemba kwa lengo la kutoa huduma za ushauri na misaada ya kisheria kwa wananchi wanaohitaji. Tume pia inataraja kuandaa mfumo mpya ambao utawezesha wananchi kutoa taarifa za uvunjifu wa haki za binadamu na utawala bora kwa kupitia simu za mikononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume pia itaendelea kupitia sehemu zenye migogoro ya ardhi, madini na hifadhi za Taifa kati ya wananchi, wawekezaji na vyombo vingine. Aidha, itachunguza ukiukwaji wa haki za binadamu wanaotendewa watu wenye ulemavu wa akili na matatizo ya mimba kwa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inataraja kuandaa na kukamilisha Ripoti kuhusu Mkataba wa Afrika na Haki za Binadamu na Watu na kuiwasilisha kwenye Tume inayohusika na mkataba huo. Ripoti kuhusu Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni itajadiliwa na Kamati husika ya kimataifa kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, ni uimarisaji na uboreshaji wa Vyuo vya Mafunzo. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo itaendelea kutengeneza vitini na vitabu vya miongozo ya kufundishia (*Student Manuals na Teaching Manuals*); kudahili na kutoa mafunzo kwa wanafunzi 800 ikiwemo kuwawezesha wanafunzi hao kufanya mafunzo kwa vitendo maeneo ya kazi; kuanzisha mfumo wa kisasa wa menejimenti ya kumbukumbu za wanafunzi na mitihani na kuboresha mahusiano baina ya Taasisi na wadau mbali mbali wa ndani na nje (*Networking*). Aidha, Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto kitaendelea kutoa mafunzo kulingana na mahitaji ya soko la ajira hususan katika fani ya sheria na programu mbalimbali za elimu zitakazoongeza ufanisi katika utendaji wa watumishi wa Mahakama wakiwemo Majaji na Mahakimu, ujenzi wa hostel ya wanachuo wa kiume, ukarabati wa majengo yaliyochakaa pamoja na kudahili wanachuo 1500.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi, ni uratibu wa mchakato wa Katiba Mpya. Kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hotuba yake, Wizara yangu itaendelea na jukumu la kuratibu mchakato wa kuwepo kwa Katiba Mpya. Aidha, katika kuratibu na kusimamia jukumu, hilo kwa mwaka wa fedha 2011/2012 wananchi wataendelea kuelimishwa kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 iliyopo ili isadie ukusanyaji wa maoni ya wananchi kwa ajili ya kuandika Katiba Mpya. Vilevile, katika kuhakikisha jukumu hilo linakamilishwa vyema, muundo wa Wizara yangu umerejewa ili kukidhi zoezi la uratibu na usimamizi wa

mabadiliko ya Katiba. Muundo huu umerejewa kwa kuongezewa Idara mpya ya Katiba na Usimamizi wa Maendeleo ya Utoaji Haki (*Constitution and Justice Monitoring Division*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na moja, utoaji wa eimu kwa umma. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa umma kwa kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano ulioandaliwa. Aidha, masuala ya elimu kuhusu mchakato wa kutayarisha Katiba Mpya, mfumo wa usimamizi, uboreshaji wa Sheria, usikilizaji na uendeshaji wa mashauri nchini, utahamasishwa kuititia vyombo vya habari, magazeti, vipeperushi, machapisho mbalimbali pamoja na mikutano na warsha. Tume pia itaendelea kutoa ellmu kwa umma juu ya hali na haki za watoto walio katika mkinzano na sheria hasa walio katika vizuio vya magereza, polisi, mahabusu za watoto na shule ya maadilisho ili kuwaepusha kwenye mazingira hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na mbili, uimarishaji wa shughuli za Usajili, Ufilisi na Udhamini. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wakala utaendelea na mpango wa ununuzi na usambazaji wa vifaa vya usajili; kampeni za uhamasishaji na usajili wa vizazi na vifo. Wakala utatua mafunzo juu ya umuhimu wa kusajili matukio muhimu kwa jamii, na asasi mbalimbali zikiwemo za kidini na zisizo za kiserikali. Aidha, Wakala kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo utaanza kutekeleza mpango ya usajili wa watoto walio chini ya miaka mitano (*Under Five Birth Registration Initiative*) na usajili wa watoto walio kati ya miaka sita hadi 18 (*Six to Eighteen Birth Registration Initiative*). Zoezi hilo litafanywa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uandikaji wa wosia, Wakala una mpango wa kutoa mafunzo kwa wananchi kuititia vyombo vya habari na kwa Taasisi mbalimbali ili kuongeza mwamko na uelewa wa uandikaji wa wosia kwa lengo la kupunguza migogoro inayotokea katika masuala ya mirathi. Mpango wa huduma hii utaanishwa katika ngazi ya kanda pindi Mawakili wapya watakapoajiriwa katika kanda hizo. Hatua hii itapunguza usumbufu uliopo kwa wananchi kufuata huduma hiyo katika Makao Makuu ya Wakala. Aidha, katika mwaka 2011/2012, huduma za Kitengo cha huduma za ufilisi kitaimarishwa kwa kuwapatia mafunzo na stadi stahili wanasheria wanaoshughulikia masuala ya ufilisi. Sheria za ufilisi zitafanyiwa mapitio upya kwa kushirikiana na wadau kwa lengo la kuziunganisha kuwa sheria moja ya ufilisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na tatu, ufumbuzi wa mrundikano wa wafungwa na Mahabusu Magerezani. Mahakama itaendelea kutumia Kamati ya Haki Jinai ambayo inajumuisha wadau wote wa masuala ya makosa ya jinai. Kamati hii pamoja na kazi zake, ni kutafuta suluhisho la mlundikano wa wafungwa magerezani na uharakishwaji wa mashauri, Aidha, Mahakama kwa kushirikiana na Idara za Polisi, Magereza, Ustawi wa Jamii na Divisheni ya Mashitaka itaendelea na juhudzi za kulipatia ufumbuzi tatizo la mrundikano wa wafungwa na mahabusu magerezani. Vikao vya kusukuma mashauri katika ngazi ya Taifa hadi Wilaya vitaendeshwa kwa lengo la kubaini na kutoa ufumbuzi wa tatizo la ucheleweshaji wa mashauri Mahakamani. Mahakama katika ngazi zote zitaendelea kutoa dhamana kwa washitakiwa wa makosa yanayodhaminika kisheria na kutoa adhabu mbadala ya kifungo kwa mujibu wa sheria kwa washitakiwa wanaopatikana na hatia. Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI itatoa Elimu kwa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji ili kuwapangia kazi Wafungwa wanaopewa adhabu mbadala. Mahakama pia itaendelea na utaratibu wa kutumia mfumo wa *Individual Calendar* ili kuharakisha usikilizaji wa mashauri ya jinai ambapo kila Jiji atapangiwa ratiba ya kushughulikia mashauri kwa muda maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na nne, ni kuhusu uboreshaji wa Maendeleo ya Watumishi. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kuwapeleka watumishi wake wa Kada zote kwenye mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili kuwajengea uwezo katika kumudu majukumu ipasavyo. Aidha, Tume itaendelea kuboresha maendeleo ya watumishi wa Mahakama kwa kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Maadili, Utendaji kazi bora pamoja na uwajibikaji wa Mahakimu ili kurudisha heshima na imani ya wananchi kwa mahakimu na Mahakama ya Tanzania. Pia, itaendelea kuratibu ziara za kuitangaza kwa wananchi na watumishi wa

Mahakama pamoja na kuendesha mikutano ya watumishi wa mahakama na vikao vya wajumbe wa Kamati za Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru Viongozi na Watendaji Wakuu na watumishi wote katika Wizara yangu kwa ushirikiano waliounesha katika kutayarisha Mpango na Bajeti hii na kuijamilisha pamoja na ushirikiano mzuri wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa muda mfupi niliokaa katika Wizara hii. Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wakuu wa Taasisi wa Wizara yangu nikianzia na Mheshimiwa Jaji Mkuu, Mohamed Chande Othman; Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Frederick Mwita Werema; Mheshimiwa Jaji Kiongozi, Fakih A. R. Jundu; Mheshimiwa Katibu Mkkuu, Wizara ya Katiba na Sheria Oliver P.J. Mhaiki; Nailbu Mwanasheria Mkkuu wa Serikali, George M. Masaju; Msajili wa Mahakama ya Rufaa, Francis Mutungi; Mkurugenzi wa Mashtaka, Elezezer M. Feleshi; Msajili wa Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara, Mheshimiwa John Kahyoza; Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Celina Wambura ambaye amestaafu mwezi uliopita na Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Japheti Sagasii. (*Makofii*)

Aidha, nawapongeza wafuatuo kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa walizonazo, Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Mheshimiwa Jaji Aloysius Mujulizi; Msajili wa Mahakama Kuu, Mheshimiwa Ignas Kitus; Msajili wa Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi, Mheshimiwa David Mrango; Msajili wa Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi, Mheshimiwa Mohamed Gwae; Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mary Massay; Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufili na Udhamini Phillip Saliboko na Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania Dokta Gerald Ndika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wizara ya Katiba na Sheria na Serikali kwa ujumla, napenda kuwashukuru sana wadau wetu wa maendeleo kwa kuendelea kushirikiana nasi katika kuboresha Sekta yetu ya Sheria. Wadau hao wa maendeleo ni Denmark (*DANIDA*), Canada (*CIDA*), Benki ya Dunia (*WB*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Watoto (*UNICEF*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (*UNDP*) na Uingereza (*DFID*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru wananchi na wadau wengine kutoka Sekta Binafsi na kutoka vyombo vya habari, vyuo vya elimu vinavyoshughulika na masuala ya sheria kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Sekta ya Sheria. Aidha, shukrani zangu za dhati ziwaendee Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yao katika kuboresha utendaji wa Wizara yangu ili itoe mchango wake muhimu katika utoaji haki kwa wote na kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2011/2012, ili Wizara ya Katiba na Sheria iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2011/2012, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi bilioni mia moja thelathini na nane, milioni mia saba ishirini na tatu, laki tisa na hamsini na sita elfu na mia sita (138,723,956,600) kwa ajili ya matumizi ya Wizara. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni tisini na saba, milioni mia tano kumi na saba, laki tatu arobaini na sita elfu na mia sita (97,517,346,600) ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shillingi bilioni ishirini na tisa, milioni mia tisa tisini na moja, laki saba na ishirini na nane elfu (29,991,728,000) ni mishahara, na shilingi bilioni sitini na saba, milioni mia tano ishirini na tano, laki sita kumi na nane elfu (67,525,618,000) ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Fedha za Matumizi ya Maendeleo ni shilingi bilioni arobaini na moja, milioni mia mbili na sita, laki sita na kumi elfu (41,206,610,000). Kati ya fedha hizo, shilling bilioni tatu, milioni mia moja na sita, laki saba tisini na mbili elfu (3,106,792,000) ni fedha za ndani wakati shilingi bilioni thelathini na nane, milioni tisini na tisa laki nane kumi na nane elfu (38,099,818,000) ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio hayo ya fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa mafungu kumi na mbili kama ifuatayo:-

FUNGU 12 TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA

Matumizi ya Mishahara	Sh.	122,305,000/=
Matumizi Mengineyo	Sh.	1,000,000,000/=

	Matumizi ya Maendeleo (Ndani) Sh.	-
	Matumizi ya Maendeleo (Nje) Sh.	-
	Jumla	Sh. 1,122,305,000/=
FUNGU 16 OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI		
Matumizi ya Mishahara Sh. 1,369,636,000/=		
Matumizi Mengineyo Sh. 7,832,865,000/=		
Matumizi ya Maendeleo (Ndani) Sh. -		
Matumizi ya Maendeleo (Nje) Sh. 1,401,000,000/=		
	Jumla	Sh. 10,603,501,000/=
FUNGU 18: MAHAKAMA KUU		
Matumizi ya Mishahara Sh. 7,952,289,000/=		
Matumizi Mengineyo Sh. 9,347,213,000/=		
Matumizi ya Maendeleo (Ndani) Sh. -		
Matumizi ya Maendeleo (Nje) Sh. -		
	Jumla	Sh. 17,299,502,000/=
FUNGU 19: MAHAKAMA ZA WILAYA NA MWANZO		
Matumizi ya Mishahara Sh. 12,577,835,500/=		
Matumizi Mengineyo Sh. 6,591,501,000/=		
Matumizi ya Maendeleo (Ndani) Sh. -		
Matumizi ya Maendeleo (Nje) Sh. -		
	Jumla	Sh. 19,169,336,000/=
FUNGU 35: DIVISHENI YA MASHTAKA		
Matumizi ya Mishahara Sh. 3,256,906,000/=		
Matumizi Mengineyo Sh. 3,541,330,000/=		
Matumizi ya Maendeleo (Ndani) Sh. -		
Matumizi ya Maendeleo (Nje) Sh. 5,663,957,000/=		
	Jumla	Sh. 12,462,193,000/=
FUNGU 40 MAHAKAMA		
Matumizi ya Mishahara Sh. 1,483,224,000/=		
Matumizi Mengineyo Sh. 28,487,488,000/=		
Matumizi ya Maendeleo (Ndani) Sh. 3,106,792,000/=		
Matumizi ya Maendeleo (Nje) Sh. 10,439,299,000/=		
	Jumla	Sh. 43,516,803,000/=
FUNGU 41: WIZARA YA KATIBA NA SHERIA		
Matumizi ya Mishahara Sh. 1,494,146,000/=		
Matumizi Mengineyo Sh. 3,306,963,000/=		
Matumizi ya Maendeleo (Ndani) Sh. -		
Matumizi ya Maendeleo (Nje) Sh. 15,667,754,000/=		
	Jumla	Sh. 20,468,863,000/=
FUNGU 55: TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA		
Matumizi ya Mishahara Sh. 1,426,388,000/=		
Matumizi Mengineyo Sh. 2,392,285,000/=		
Matumizi ya Maendeleo (Ndani) Sh. -		

Matumizi ya Maendeleo (Nje)Sh. 824,918,000/=
Jumla Sh. 4,643,591,000/=

FUNGU 59 **TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA**
 Matumizi ya Mishahara Sh. 524,180,600/=
 Matumizi Mengineyo Sh. 1,000,000,000/=
 Matumizi ya Maendeleo (Ndani) Sh. -
 Matumizi ya Maendeleo(Nje) Sh. 616,350,000/=
Jumla Sh. 2,140,530,600/=

FUNGU 60: **MAHAKAMA YA KAZI**
 Matumizi ya Mishahara Sh. 247,915,000/=
 Matumizi Mengineyo Sh. 1,096,009,000/=
 Matumizi ya Maendeleo (Ndani) Sh. -
 Matumizi ya Maendeleo
 (Nje) Sh. 1,665,200,000/=
Jumla Sh. 3,009,124,000/=

FUNGU 64: **MAHAKAMA YA BIASHARA**
 Matumizi ya Mishahara Sh. 248,872,000/=
 Matumizi Mengineyo Sh. 1,000,000,000/=
 Matumizi ya Maendeleo (Ndani) Sh. -
 Matumizi ya Maendeleo (Nje)Sh.1,391,340,000/=
Jumla Sh. 2,640,212,000/=

FUNGU 90: **MAHAKAMA YA ARDHI**
 Matumizi ya Mishahara Sh. 217,996,000/=
 Matumizi Mengineyo Sh. 1,000,000,000/=
 Matumizi ya Maendeleo (Ndani) Sh. -
 Matumizi ya Maendeleo (Nje) Sh. 430,000,000/=
Jumla Sh. 1,647,996,000/=

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makusanyo ya maduhuli. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara yangu inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni mbili, milioni mia tatu na mbili, arobaini na nane elfu (2,302,048,000) kama maduhuli ya Serikali. Mchanganuo wa makusanyo kwa kila fungu husika ni kama ifuatavyo:-

Fungu 12	-	Sh.	-
Fungu 16	-	Sh.	14,001,000/=
Fungu 18	-	Sh.	278,001,000/=
Fungu 19	-	Sh.	982,002,000/=
Fungu 35	-	Sh.	-
Fungu 40	-	Sh.	130,007,000/=
Fungu 41	-	Sh.	2,002,000/=
Fungu 55	-	Sh.	5,131,000/=
Fungu 59	-	Sh.	-
Fungu 60	-	Sh.	-
Fungu 64	-	Sh.	824,900,000/=
Fungu 90	-	Sh.	<u>66,004,000/=</u>

Jumla - Sh. 2,302,048,000/=

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, napenda kuwashukuru watendaji wote wa ofisi yangu pamoja na wote walionisaidia kwa njia moja au nyingine. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumejipanga, tumedhamiria na tutatekeleza, naomba mtupe muda tuyafanye hayo ambayo tuliyapanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja illtolewa iamulliwe*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Celina Kombani, kwa hotuba yako nzuri sana tunakushukuru sana.

Sasa kwa haraka haraka niwatambulise wageni kabla ya kuendelea wageni wa Mheshimiwa Waziri watoto wake Goodluck na Joel, karibuni sana, mama anafanya kazi nzuri. Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri Kombani, ni Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Oliva Muhaiki, karibu Katibu Mkuu; Jaji Kiongozi Mahakama Kuu, Faki Abdallah Jundu; ahsante sana. Jaji Mfawidhi, Mahakama Kuu *Division* ya Kazi, Mheshimiwa Regina Mtebezi Rweyemamu; Jaji Mfawidhi wa Mahakama ya Kanda ya Dodoma, Mheshimiwa Mary Shangali; Jaji Mfawidhi, Mahakama Kuu Tanga, Mheshimiwa Kipenka Mussa; Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Kipenka Mussa kabla ya kwenda kwenye huduma ya Mahakama alikuwa ni Katibu wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, karibu sana Mheshimiwa Jaji Kipenka. Jaji Mfawidhi Mahakama ya Biashara, Mheshimiwa Robert Makaramba; karibu sana. Jaji Mahakama Kuu ya Tanzania na Mkuu wa Chuo cha Mahakama Lushoto, Mheshimiwa Alyoce Mujuizi, Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu Moshi, Mheshimiwa Stella Mugasha; Jaji Mahakama Kuu Dodoma, Mheshimiwa Mwanaisha Kwariko; Jaji Mahakama Kuu Dodoma, Mheshimiwa Sivangwila Mwangesi. (*Makofii*)

Pia wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri Kombani, Waziri wa Katiba na Sheria kutoka Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania wanaongozwa na Mheshimiwa wa Tume hiyo ambaye ni Mheshimiwa Profesa Jaji Ibrahim Hamisi Juma; yuko Jaji Mstaafu Ernest Mwaipopo, Bi, Ester Manyesha; yuko Profesa Sufiani Bukurura; yuko Albert Msangi, lakini pia yuko Katibu Mtendaji wa Tume hiyo ambaye amekuwa ni mtumishi wa Bunge kwa miaka minge hapa ndugu Japhet Sagasii. (*Makofii*)

Katika majukwaa ya wageni wako wasajili wa Mahakama na Wakurugenzi kama mpo Wasajili na Wakurugenzi kama Mahakimu Wafawidhi. Tungependa pia kuwatambua Mahakimu Wakazi kutoka Mkoa wa Dodoma, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo Mkoa wa Dodoma na watumishi kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, karibuni sana. (*Makofii*)

Pia ningependa kuwatambua wageni wa Mheshimiwa Tundu Lissu, Waziri kivuli Wizara ya Katiba na Sheria na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hiyo, amba ni Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida amba wanatoka Chama cha CHADEMA, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani, karibuni sana Dodoma, Mbunge wenu anafanya kazi nzuri. (*Makofii*)

Bila kupoteza muda sasa naomba nimwite msemaji wa Kamati kuhusiana na Wizara hii, karibu sana Mheshimiwa Blandes. Anasimama Mwanasheria Blandes kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati.

MHE. GOSBERT B. BLANDES – (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na kabla sijaanza kusoma taarifa ya Kamati ya Bunge, niruhusu kwanza nitoe shukrani kwa wananchi wa Jimbo la Uchaguzi la Karagwe, kwa kunihamini na kunichagua tena kuwa Mbunge wao. Imani wallyonipa nitaiheshimu kwa kuchapa kazi, wananchi wote wa Karagwe napenda kuwahakikishia kwamba nawapenda sana kuliko mchele wa Shinyanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niwashukuru watendaji wote wa vyombo vya habari hapa nchini, hususan redio Karagwe na redio Fadeko ambazo ziko Jimboni kwangu kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kutoa huduma kwa wananchi wa Jimbo la Karagwe. Namshukuru mke wangu mpenzi Gorola na watoto wetu Comfort Blandes pamoja na wadogo zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha

2010/2011 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11), naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba, Sheria na Utawala kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala ilikutana tarehe 30/5/2011, katika ukumbi wa Ofisi Ndogo ya Bunge Dar es Salaam kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na kuchambua kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012. Wizara hii ina Mafungu 12 kama ifuatavyo:-

- (i) Tume ya Utumishi wa Mahakama - Fungu 12
- (ii) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Fungu 16
- (iii) Mahakama Kuu - Fungu 18
- (iv) Mahakama za Wilaya - Fungu 19
- (v) Mkurugenzi wa Mashtaka - Fungu 35
- (vi) Mahakama - Fungu 40
- (vii) Wizara ya Katiba na Sheria - Fungu 31
- (viii) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
- Fungu 55
- (ix) Tume ya Kurekebisha Sheria - Fungu 59
- (x) Mahakama ya Kazi - Fungu 60
- (xi) Mahakama ya Biashara - Fungu 64
- (xii) Mahakama ya Ardhi - Fungu 90

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi nyingine zilizotajwa kuwa chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ni pamoja na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhaminini (*RITA*), Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (*Law School of Tanzania*) na Chuo cha Uongozi wa Mahakama (*Institute of Judicial Administration*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa mwaka wa Fedha 2010/2011. Wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka 2010/2011, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi wa sekta hii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya ushauri ulizingatiwa na kufanyiwa kazi kama ifuatavyo:-

(i) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Wizara kwa ujumla kuongezewa Bajeti, Kamati ilielezwa kwamba suala hili linaendelea kuboreshwa taratibu kuzingatia hali ya fedha Kitaifa;

(ii) Tume ya Haki za Binadamu kushughulikia malalamiko 481 yaliyobaki juu ya kuhifadhi haki za binadamu na utawala, Kamati ilijulishwa kuwa Tume ilishughulikia mashauri 195 na mashauri 286 yaliyobaki yako katika hatua za mwisho uchunguzi wake kukamilika. Tume

haikufanikiwa kumaliza mashauri yote kutokana na ugumu wa kupata kumbukumbu kwani baadhi yake ni za miaka ya 1970;

(iii) Kuanzishwa kwa Mfuko wa Mahakama ndani ya kipindi cha mwaka mmoja, Serikali kuititia Bunge imepitisha Sheria iliyounda Mfuko wa Mahakama na tayari Serikali imeshatenga bajeti kwenye Mfuko huu ya Sh. 20,000,000,000/-, hivyo mwaka huu Mfuko huo utaanza kufanya kazi;

(iv) Serikali kuandaa Mkakati maalum wa kukarabati majengo chakavu ya Mahakama, ujenzi wa Mahakama sanjari na nyumba za Mahakimu, mkakati uliopo ni kukarabati majengo ambayo hayajachakaa sana na kwa yale yaliochakaa yatabomolewa na kujengwa upya. Aidha, mkakati mwininge ni kila inapoengewa Mahakama pia na nyumba za watumishi zijengwe ili kupunguza tatizo la nyumba za watumishi wa Mahakama;

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda mengine nitayaruka lakini naomba *Hansard* iyarekodi kwamba ndiyo taarifa ya Kamati yetu.

(v) Ujenzi wa Mahakama Maalum za Rushwa, Kamati ilifahamishwa kuwa agizo hili halikutekelezwa kutokana na ufinyu wa bajeti, kwa sasa mashauri ya rushwa yataendelea kusikilizwa na Mahakama zilizopo;

(vi) Chuo cha Mahakama cha Lushoto (*Institute of Judicial Administration*) kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kutoka katika Mahakama za Mwanzo na Wilaya, Kamati ilijulishwa kuwa suala hili halijatekelezwa kutokana na ufinyu wa bajeti; na

(vii) Usawa wa maslahi baina ya Wanasheria wa Serikali na wale waliopo Tume ya Kurekebisha Sheria na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Kamati ilielezwa kuwa Timu ya Wataalam iliundwa na imewasilisha mapendekezo Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma ili suala hili lishughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizojiteza. Kutokana na maelezo ya kina na ufanuzi wa hoja mbalimbali zilizojiteza, Kamati iliridhika na utendaji wa Wizara ikilinganishwa na malengo waliyokuwa wamewekewa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011, kwa Taasisi zote na Mafungu husika. Pamoja na hayo, changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria zilianishwa kama ifuatavyo:-

(i) Ufinyu wa bajeti ambao umesababishwa na uwezo mdogo wa Serikali kifedha kutokidhi mahitaji ya Wizara kutokana na majukumu kuongezeka, mfano kuanzishwa kwa Taaasi, Vitengo, Kurugenzi na Majaji wengi kuteuliwa ambao kwa pamoja wanahitaji kuhudumiwa;

(ii) Mazingira duni ya kufanya kazi na ukosefu wa vitendea kazi muhimu kama vile magari, ofisi, samani, nyumba za watumishi na kutotumia teknolojia ya kisasa katika kuendesha mashauri;

(iii) Upungufu mkubwa wa rasilimali watu unaosababisha mrundikano wa mashauri Mahakamani;

(iv) Ukosefu wa maadili katika Utumishi wa Umma; na

(v) Kutokuwepo kwa Mikopo kwa Wanafunzi wa Taasisi ya mafunzo ya Wanasheria kwa vitendo kutokana na Sheria ya Utoaji Mikopo kuruhusu Mikopo kutolewa kwa Shahada ya Kwanza tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije katika maoni na mapendekezo ya Kamati. Baada ya kuelezea utekelezaji wa maagizo ya Kamati, mafanikio na changamoto zilizoikabili Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mahakama:-

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuishukuru na kuipongeza Wizara kwa juhudzi zake, Kamati inashauri Taasisi za Mahakama kufanya bidii zaidi pamoja na changamoto walizonazo ili kuweza kupunguza malalamiko ya ucheleweshaji wa kesi Mahakamani ambao umekuwa unasababisha msongamano wa mahabusu na wafungwa Magerezani pamoja na kuliingiza Taifa kwenye ghamama zisizo za lazima za kuwalisha, kuwavisha na kuwapatia huduma nyinginezo mahabusu na wafungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wataendelea kuwa na imani kubwa na Mahakama endapo wataelewa nafasi ya Mahakama katika kuendeleza amani ya nchi, utatuzi wa migogoro na kuichukulia kama chombo kinachofanikisha maendeleo ya kiuchumi.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba mrundikano wa mahabusu na wafungwa Magerezani unawenza kuepukika iwapo utaratibu wa kutoa vifungo vya nje au hata kutoa adhabu za kufanya shughuli za maendeleo nje ya Mageresa (*extra Mural Punishment*) utatumika kwani wengi wa mahabusu na wafungwa kwa hivi sasa kesi zao ni ndogo kama vile uzembe na uzururaji ambazo hata hivyo, wengi hususan vijana hujingiza kwenye makosa hayo kwa sababu ya kukosekana kwa shughuli mahsusizi za kufanya au kukosa elimu ya ujasiriamali ambapo wangeweza kujajiri na kujipatia kipato wao wenywewe;

(iii) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali mbaya kwenye upande wa Mahakama hivi sasa, ambapo Mahakama moja ya Mwanzo imekuwa inahudumia Tarafa zaidi ya moja kwa baadhi ya maeneo, Kamati inashauri Serikali ianze Mikakati ya kujenga Mahakama kila Tarafa na pale ambapo Mahakama hazipo basi wananchi wa eneo hilo wachague sehemu ambapo huduma ya Mahakama ya Mwanzo itatolewa. Kamati inasikitishwa sana na taarifa kwamba katika Mwaka wa Fedha 2010/ 2011, Serikali ilitenga fedha za maendeleo kwa ajili ya Mahakama za Mwanzo mpya tano (5) tu nchi nzima, pamoja na kwamba hazikujengwa kikamilifu.

Sambamba na hilo, Kamati inashauri Serikali iajiri vijana wengi waliomaliza Shahada ya Sheria ili waweze kutoa huduma kwenye Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mahakama Kuu:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Wizara itafakari umuhimu wa kujenga Mahakama Kuu chache kila mwaka kwani baadhi ya Mikoa haina Mahakama Kuu na hivyo kuwa chanzo cha ucheleweshaji wa Kesi na mrundikano wa Mahabusu na wafungwa.

Hivyo, Wizara kwa kutumia miundombinu iliyopo itafute njia ya kupata mapato na hivyo kuweza kukamilisha lengo hilo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile kuna uhaba mkubwa wa Majaji katika Mahakama zote, Serikali inashauriwa ifanye kila jithhada ya kuongeza idadi ya Majaji na Mahakimu lakini kwa angalizo kuwa Majaji wanaoteuliwa wanakidhi sifa na vigezo ili kupunguza mashauri mengi ambayo yanahitaji kusikilizwa na kuondoa mrundikano wa Mahabusu na wafungwa ambao wanakaa muda mrefu bila kesi zao kusikilizwa ili wananchi wapate haki kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali:

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Sheria nyingi zimekuwa zikiandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Pamoja na sababu nyingi zilizotolewa, Kamati inaamini umefika wakati sasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iwe na Kitengo cha Wataalam wa Lugha watakaoweza kufanya tafsiri ya Sheria inayotungwa kwa lengo la kuwawezesha wananchi wengi wasiojua lugha ya Kiingereza kufuatilia Sheria inayohusika. Kamati inapendekeza Sheria zote zinapoletwa Bungeni zije kwa lugha zote mbili ya Kiswahili na Kiingereza.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa tatizo la mikataba mibovu ambayo Taifa limekuwa likiingia hasa na Makampuni ya kigeni, Kamati inashauri Wizara itengeneze programu za muda mfupi na mrefu kwa wataalam wetu ili waweze kupata mafunzo ndani na ndani ya nchi na hivyo kupata ujuzi na uelewa wa kuandika mikataba, hususan ya Kimataifa. Aidha, Kamati

inashauri wataalam wetu kuzingatia uzalendo na maslahi ya Taifa katika kutayarisha mikataba hii.
(*Makofii*)

(iii) Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa nchi yetu iko kwenye mchakato wa mabadiliko ya Katiba. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya dhamira ya Serikali kuanzisha mchakato wa mabadiliko ya Katiba ya Nchi katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, ya Salaam za Mwaka Mpya kwa wananchi tarehe 31 Desemba 2010, Serikali illela Bungeni Muswada unaokusudia kuweka masharti ya uanzishaji wa Tume, pamoja na Sekretarieti kwa madhumuni ya kuendesha na kusimamia mchakato wa mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Muswada huo kusomwa Bungeni, Kamati ilianza kukusanya maoni mbalimbali ya wananchi pamoja na maoni kutoka Vyama vya Siasa, Viongozi wa Dini na Asasi zingine za Kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hivi sasa Kamati imekwisha pokea maoni ya Wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Jukwaa la Katiba, Chama cha Wanawake Wanasheria (*Tanzania Women Lawyers Association*), Kituo cha Wanawake cha Msada wa Sheria (*Women's Legal Aid Centre*), Kituo cha Taifa cha Msada wa Sheria (*National Organisation for Legal Assistance*), Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*Legal and Human Rights Centre*), Chama cha Wanasheria Tanganyika (*Tanganyika Law Society*), Kitivo cha Sheria chuo kikuu cha Dar es Salaam na Mzumbe na wadau wengine wengi. Kamati bado inaendelea kupokea maoni zaidi na kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishukuru pia Serikali kwa kuwa siku na kukubali kuufanya maboresho Muswada huo ikiwa ni pamoja na kuuandika kwa lugha ya Kiswahili kama ilivyopendekezwa na Kamati baada ya kupokea maoni mengi ya Wadau walioshauri iwe hivyo.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imejipanga vema na inashauri Serikali iharakishe marekebisho ya Muswada huo na kuyaleta mapema Bungeni ili tumalizie hatua zilizobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mahakama ya Ardhi. Kwa vile kwa sasa migogoro ya ardhi katika ngazi ya Kijiji na Kata inashughulikiwa na Mabaraza ya Ardhi ya Kijiji kwa mujibu wa *The Courts (Land Disputes Settlements) Act. No. 2 ya Mwaka 2002* ambapo katika Kifungu cha Sita, Msimamizi Mkuu wa Mabaraza haya ni Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa maana ya Watendaji wa Vijiji ambapo ufanisi wake umeonekana kuwa wa hali ya chini, Kamati inashauri kuwa, ni vema mfumo wa Mabaraza hayo ukabadilishwa na kuwa chini ya usimamizi wa Mahakama ili migogoro hii iweze kutatuliwa kwa haraka na watu amba wana utaalam wa masuala haya ya ardhi na hivyo kuondoa migogoro mingi ambayo kila siku inaendelea kuibuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kamati ilipata maelezo kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ambayo kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Na. 7 ya Mwaka 2001 (iliyorekeblishwa 2002) Kifungu cha 3, Tume hii ni ya Muungano, Kamati ilielezwa kwamba kwa upande wa Zanzibar hakuna Mahabusu ya Watoto. Kinachofanyika ni kuwatenganisha tu wakati wa kulala usiku lakini muda wote wa mchana huchanganyika na watu wazima kinyume na haki za binadamu na utawala bora. Suala hili pia ilielezwa liko hata upande wa Tanzania Bara ambapo kuna mahabusu za watoto chache sana hivyo kufanya maeneo mengine watoto kuchanganywa na mahabusu ya watu wazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inalionia jambo hili siyo sahihi kwani si tu kwamba linawadhalilisha watoto bali pia linakwenda kinyume na Kifungu cha tano (5) cha Sheria ya Mtoto, Sura ya 58 (*Section five (5) of Young Offender Decree, Cap. 58* na Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009) Kamati inaelekeza Sheria ifuatwe kwa kujenga maeneo maalum kwa ajili ya watoto na kuhakikisha kwamba watoto hawa wanaendelea na elimu au kupatiwa elimu wakiwa mahabusu kwa lengo la kuwaandaa kuwa raia wema kwa maisha ya baadaye. Vilevile inashauriwa kwamba, ni vema Mahakama za Watoto zikaongezwa kama Sheria ya Mtoto inavyoagiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Tume ya Utumishi wa Mahakama. Ibara ya 112(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeanzisha Tume ya Ushauri wa Uteuzi wa Majaji na Ajira ya Mahakimu ambayo inaitwa Tume ya Utumishi wa Mahakama. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutunga Sheria ya Mfuko wa Mahakama, ambao kwa kiasi kikubwa utapunguza matatizo yaliyopo hivi sasa. Hata hivyo, Kamati inaamini kwamba pamoja na kiasi cha fedha zilizotengwa Sh. 20,000,000,000/= kimetoa kipaumbele kwa ajili ya umalizaji wa kesi, ni vema kiasi hicho kitumike kuongeza idadi ya ajira ya Majaji na Mahakimu kuliko vikao vya posho na usafiri ambavyo vinagharimu sana. Aidha, ili kupunguza suala la rushwa katika sekta ya Mahakama, ni vema Watumishi hao wakaandaliwa mazingira mazuri ya kazi hasa ukizingatia kwamba kazi zao zinawafanya waishi katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile suala la mikopo kwa wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo lina matatizo, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia mambo yafuatayo:-

- Serikali ipitie upya mfumo wa utoaji wa Shahada ya Kwanza ya Sheria kwa Vyuo vyote ili kuoanisha mfumo huo, kwa vile kwa sasa kuna Vyuo vinyavotoa Shahada ya Sheria kwa miaka mitatu na vingine miaka minne na hivyo, kuwe na mfumo mmoja uliokubalika. Aidha, ikitukubaliwa ni miaka minne, basi ule mwaka wa nne ndio uwe wa Mafunzo kwa Vitendo na uunganishwe moja kwa moja kwenye Shahada ya Kwanza ili Bodi ya Mikopo iendelee kuwahudumia;

- Sheria iliyoanzisha Bodi ya Mikopo iletwe Bungeni kuboreshwa ili iruhusu kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Shule ya Sheria kwa Vitendo na hivyo wasipate usumbufu wa kusoma bila kuwa na uhakika wa maisha yao hasa ukizingatia hali ya maisha ya sasa ilivyo; na

- Wizara itenye fedha kwa ajili ya Mikopo ya Wanafunzi hao ili kuondokana na ufadhili unaotolewa na taasisi nyingine ambao hauna uhakika na kuondoa migomo isiyo ya lazima kwa wanafunzi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati kuptitia Vifungu vya Wizara hii, ilibaini Wizara imeweka fedha nyingi kwenye vifungu vya posho, vikao na usafiri. Hata hivyo, Kamati imefuatilia takwimu za Majaji na Mahakimu na kuelezwu kwamba kuna sehemu nchini hazina kabisa mahakama. Wananchi hufunga safari ndefu kutafuta haki zao na kwa gharama. Mwanya huu huwabagua na hawatendewi haki. Upungufu mkubwa uliopo ni kama ifuatavyo:-

- Nchi nzima kuna Mahakama za Mwanzo 974 zinazofanya kazi na mahitaji ni Mahakama za Mwanzo 1105 hivyo kuwa na upungufu wa Mahakama za Mwanzo 131. Mahakama hizo zinahudumiwa na Mahakimu wapatao 758 tu;

- Nchi nzima kuna Mahakama za Wilaya zipatazo 105, upungufu ni Mahakama 24. Mahakama zilizopo zinahudumiwa na Mahakimu wa Wilaya wapatao 27 na Mahakimu Wakazi wapatao 143. Mahitaji ni kila Mahakama ya Wilaya inatakiwa iwe na Mahakimu Wakazi wapatao wanne (4); na

- Nchi nzima kuna Mahakama Kuu zipatazo 13 tu na Majaji wapatao 58 na hivyo Kamati inashauri kila Mkoa uwe na Mahakama Kuu na Majaji waongezekere.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kwamba ni vema fedha nyingi zilizotengwa kwa ajili ya posho na usafiri zikatumika kuajiri Mahakimu wa kutosha ili kusaidia upungufu mkubwa uliopo ambao ndiyo chanzo kikuu cha ucheleweshwaji wa kesi na mrundikano wa mahabusu na wafungwa Magerezani. Aidha, Serikali iwe na mpango madhubuti wa kujenga Mahakama katika kila Wilaya na Mikoa mipya iliyoanzishwa.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imeendelea kukabiliwa na ufinyu mkubwa wa bajeti hata baada ya Kamati kushauri katika bajeti iliyopita waongezewe lakini imeshindikana, Kamati inaendelea kusisitiza Wizara hii kuongezewa bajeti ili kesi nyingi ziweze kusikilizwa jambo ambalo linalalamikiwa na wanachi wengi na kudhani hazisikilizwi kwa sababu ya rushwa wakati tatizo ni bajeti. Aidha, Kamati inashauri kuwa Serikali iboreshe miundombinu ya Chuo cha Lushoto ambacho kinaendesha Mafunzo ya Uhakimu na Watumishi mbalimbali wa Mahakama ili tuweze kukabiliana na upungufu uliopo kwa kutoa mafunzo kwa Mahakimu na Watumishi mbalimbali wa Mahakama. (*Makof*)

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata muda wa kutembelea Wakala wa Usajili na Ufisili wa Mdhamsini (*RITA*). Kamati ilielezwa majukumu yanayotekelawa na *RITA* japo kwa kiasi kikubwa kutokana na ufinyu wa Bajeti, majukumu hayo yanatekelezwa katika mazingira magumu. Pamoja na hali hiyo, bado Kamati inaiponjeza Wakala kwa jitihada kubwa ya kufanikisha malengo yao japo Mara nyingi wamekuwa wanapata changamoto katika ufanikisha majukumu yao kutokana na Sheria zinazowaongoza, kukinzana na nyingine kupitwa na wakati. Kamati inapendekeza kwa Serikali kuzileta Sheria zinazokinzana na sheria nyingine ili zifanyiwe marekebisho na hivyo kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya *RITA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mahakama Kuu, Kitengo cha Kazi. Kamati inaiponjeza Mahakama ya Kazi kwa kufanya kazi kubwa japo katika mazingira magumu. Kamati haikufurahishwa na taarifa ya Mheshimiwa Waziri aliyotoa mbele ya Kamati kuhusu Mahakama hii kwani inaonyesha wazi, kwamba Mahakama hii inatekeleza majukumu yake chini ya kiwango kutokana na idadi ndogo ya Watendaji wa Mahakama hii na sababu kubwa ya upungufu huu ni ufinyu wa Bajeti. Kamati inazidi kuishauri Serikali kuongeza Fungu la Bajeti ya Mahakama hii ili iweze kufanikisha malengo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mahakama Kuu, Kitengo cha Biashara. Kamati inaiponjeza Serikali kwa hatua za makusudi ilizochukua na hivyo kuiwezesha Mahakama Kuu kitengo cha Biashara kukamilisha Maktaba ya Elektroniki na hivyo kuwezesha nakala za hukumu na baadhi ya Sheria kupatikana katika tovuti ya Mahakama ya Biashara. Kamati inashauri Serikali izidi kuiwezesha Mahakama hii ili ifanye shughuli zake kwa ufasaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Tume ya Kurekebisha Sheria. Kamati imebaini kwamba hivi sasa kuna uwepo wa Sheria nyingi zilizopitwa na wakati na hivyo kuathiri mfumo wa utoaji haki. Kamati inashauri Wizara kulfanyia kazi jambo hili mapema iwezekanavyo na hivyo kuleta mbele ya Bunge lako Sheria zote zenye matatizo ya aina hiyo ili ziweze kurekebishwa. Moja ya mfano wa Sheria hizo, ni Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii muhimu ili niweze kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia, nawashukuru Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Katiba na Sheria na Mheshimiwa Jaji Frederick Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa Ushirikiano mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Vile vile, nawashukuru Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria na Wakuu wa Taasisi pamoja na Maafisa Waandamizi wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano waliotupatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nawashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2010/2011. Uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala mbalimbali kuhusu Sekta za Sheria, Uendeshaji, Haki za Binadamu na Utawala Bora umesaidia kufanikisha kazi hii kwa ufanisi. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mwenyekiti; Mheshimiwa Angellah J. Kairuki, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mjumbe; Mheshimiwa John P. Lwanji, Mjumbe; Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mjumbe; Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mjumbe; Mheshimiwa Fakharia K. Shomar, Mjumbe; Mheshimiwa Zahra A. Hamadi, Mjumbe; Mheshimiwa Mussa H. Kombo, Mjumbe; Mheshimiwa Felix F. Mkosamali, Mjumbe; Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mjumbe; Mheshimiwa Azza H. Hamad, Mjumbe; Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mjumbe;

Mheshimiwa Jaddy S. Jaddy, Mjumbe; Mheshimiwa Tundu A. Mughwai Lissu, Mjumbe; Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina, Mjumbe na Mheshimiwa Jason S. Rweikiza, Mjumbe. (*Makofii*)

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Kaimu Katibu wa Bunge Ndugu John Joel na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Charles J. Mloka na Ndugu Peter Magati, Grace Bidya na Asia Ninja, Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu vema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake, kama yalivyowasilishwa na Mtoha hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Wakili kwa kutusomea hotuba hiyo kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Lakini kabla hujaeendelea kwa ajili ya maandalizi baada ya hotuba itakayofuata mchangiaji wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Maulida Komu na nadhani tutakuwa na nafasi sana sana mbili tu, wa pili atakuwa Mheshimiwa Angella Kairuki. Sasa kabla sijamwita msoma hotuba wa Kambi ya Upinzani nimeona baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanatokatoka nje wanafuatilia redio na kadhalika, hakuna sababu ya kutoka nje mpaka *half time* Simba moja, *Coastal* bila. (*Makofii/Kicheko*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA, KATIBA NA UTAWALA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile tumeshapongezana na kupeana shukrani za kutosha; kwa kuzingatia matakwa ya kanuni ya 151 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2007, inayohusu salamu za pongezi na kwa kutambua ufinyu wa muda wa nusu saa nilionao, naomba uniruhusu niokoe muda wa majadiliano kwa kufanya kile ninachowajibika kukifanya kwa mujibu wa kanuni ya 99(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri wa Katiba na Sheria imeanzishwa kwa mujibu wa kipengele cha 12 cha Nyongeza ya Waraka wa Rais uliochapishwa kama Tangazo la Serikali Na. 494 la tarehe 17 Desemba 2010. Majukumu ya Ofisi hii yameainishwa katika Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la mwaka 2010 (*The Ministers [Assignment of Ministerial Functions] Notice, 2010*) lilichapishwa katika Gazeti la Serikali kama Tangazo la Serikali Na. 494A la tarehe 17 Desemba 2010. Kwa mujibu wa Nyongeza ya Pili ya Tangazo hilo, pamoja na mengine, Ofisi ya Waziri wa Katiba na Sheria imekasimiwa majukumu ya masuala ya Kikatiba, uendeshaji na utoaji wa haki, uendeshaji mashtaka na haki za binadamu na majukumu mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya majukumu haya ni ya Kikatiba kwani yamewekwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Kwa mfano, kwa mujibu wa Ibara ya 4(1) ya Katiba, shughuli zote za mamlaka ya nchi zinazohusu uendeshaji na utoaji wa haki "... zitatekelezwa na kudhibitiwa na vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutekeleza utoaji haki...." Vyombo hivyo viwili, kwa mujibu wa Ibara ya 4(2) ni Mahakama ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mahakama ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, kwa mujibu wa ibara ya 107A(1), "mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama."

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu mengine ya Kikatiba ya Ofisi ya Waziri wa Katiba na Sheria ni pamoja na Katiba yenyewe. Vile vile, masuala yote yanayohusu uendeshaji wa mashtaka ni ya Kikatiba kwa mujibu wa Ibara za 59B(1) na (2) za Katiba zinazounda Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye "... atakuwa na uwezo wa kufungua, kuendesha na kusimamia mashtaka yote nchini." Aidha, haki za binadamu nayo pia ni masuala ya Kikatiba kufuatana na Sehemu ya Tatu ya Sura ya Kwanza ya Katiba yenyе kufafanua haki za binadamu na wajibu muhimu na Sehemu ya Kwanza ya Sura ya Sita yenyе kuunda Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na kuipa mamlaka na majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgawanyo wa madaraka na uhuru wa Mahakama. Mfumo wetu wa Kikatiba na kiutawala umejengwa katika misingi ya mgawanyo wa madaraka na

uwajibikaji iliyowekwa na Katiba. Ibara ya 4(1) na (2) ya Katiba inaweka msingi wa Kikatiba wa mgawanyo wa madaraka baina ya vyombo vyenye mamlaka ya utendaji, vyombo vyenye mamlaka ya kutekeleza utoaji haki na pia vyombo vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Vyombo hivi vitatu vya dola havitakiwi na wala haviwezi, kujitenga katika utekelezaji wa majukumu yao ya Kikatiba. Hata hivyo, pamoja na mahusiano kati yao, vyombo vya dola vinatakiwa kuwa huru katika utekelezaji wa majukumu yao. Ndio maana Ibara ya 107B ya Katiba inaelekeza kwamba: "Katika kutekeleza mamlaka ya utoaji haki, Mahakama zote zitakuwa huru na zitalazimika kuzingatia tu masharti ya Katiba na yale ya sheria za nchi." (*Makofii*)

Hii ni muhimu zaidi kwa vyombo vya utoaji haki kwani bila uhuru huo, vyombo hivyo vinaweza kujikuta vikihatarisha au kukiuka haki za watu kwa kuegemea zaidi kwa mamlaka nydingine hasa hasa Serikali. Hii ni kwa sababu, katika utekelezaji wa majukumu yake ya kikatiba na kisheria ya kila siku, Serikali hujikuta ikiingilia haki mbalimbali za wananchi. Vitendo hivyo mara nydingi huishia katika vyombo vya utoaji haki kwa ajili ya maamuzi yao. Bila kuwa huru, vyombo vya utoaji haki vinaweza kujikuta vikiwezesha Serikali kuingilia haki za kimsingi za wananchi au kuhalalisha ukiukwaji wa haki za binadamu za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu urais wa kifalme na uhuru wa Mahakama. Kwa muda wote wa uhai wetu kama Taifa huru, mfumo wetu wa kikatiba na wa kisiasa umejengwa juu ya nguzo moja kuu ambayo mwanazuoni wa Kenya, Profesa H.W. Okoth-Ogendo, aliwahi kuiita Urais wa Kifalme (*Imperial Presidency*). Hii inatokana na ukweli kwamba katika mfumo huu, Rais ana madaraka makubwa sana sio tu ya kiutendaji bali pia ya kiutungaji sheria kwa vile, kwa mujibu wa Ibara 62(1) ya Katiba, Rais ni sehemu ya Bunge. Vile vile Rais ana kivuli kirefu cha kikatiba katika utekelezaji wa masuala mbalimbali ya Kimahakama kwa kutumia mamlaka makubwa aliyonayo katika uteuzi wa viongozi wote wa ngazi za juu za Mahakama. Kwa mfano, chini ya mfumo wetu, Rais anamteua Jaji Kiongozi na majaji wote wa Mahakama Kuu ya Tanzania [ibara ya 109(1) ya Katiba] na Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na majaji wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania [ibara ya 118(2) na (3)]. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Rais anatekeleza wajibu wake Kikatiba wa kuteua majaji kwa mashauriano na Tume ya Utumishi wa Mahakama [ibara ya 109(1) na 113(1)] na Jaji Mkuu [ibara ya 118(3) ya Katiba]. Hata hivyo, ni muhimu kutambua na kusisitiza ufinyu wa mamlaka ya ushauri kwa mujibu wa Katiba yetu. Hii ni kwa sababu chini ya Ibara ya 37(1) ya Katiba, "... Rais atakuwa huru na hatalazimika kufuata ushauri atakaopewa na mtu yeoyote, isipokuwa tu pale anapotakiwa na Katiba hii au na sheria nydingine yoyote kufanya jambo lolote kulingana na ushauri anaopewa na mtu au mamlaka yoyote."

Vile vile, kwa mujibu wa Ibara ya 112(2) ya Katiba, wajumbe wote wa Tume ya Utumishi wa Mahakama ni wateuliwa wa Rais na kwa sababu hiyo, Rais anashauriwa na watu alioamateua yeeye mwenyewe na halazimiki kufuata ushauri wao! Katika mazingira haya ya Kikatiba, ni rahisi kwa Rais kuteua watu kuwa Majaji au viongozi wa juu wa Mahakama ya Tanzania kutokana na vigezo vingine nje ya utaalami au uzoefu wao wa kitaaluma. Aidha, katika mazingira haya, ni rahisi kwa wateuliwa wa Rais kuamini kwamba wameteuliwa kwenye nafasi kwa nasaba zao na ukaribu wao na Rais au watu wake wa karibu na kwa hiyo wanajiona wana deni la kulipa fadhila kwa Rais kwa kufanya maamuzi yatakayompendeza yeeye au Serikali yake. Mfumo huu wa Kikatiba unajenga mazingira ya wateuliwa wa Rais kujipendekeza kwake au kwa Serikali yake (*sycophancy*) ambayo matokeo yake ni uendeshaji na utoaji haki ullojaa woga au upendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba mazingira haya ya Kikatiba yanatishia moja kwa moja uhuru wa Mahakama ya Tanzania na hayana budi kuangaliwa upya katika mjadala wa Kikatiba unaoendelea sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, badala ya madaraka ya Urais wa Kifalme juu ya Mahakama ya Tanzania kupunguzwa ili kuwe na uwiano bora zaidi wa mgawanyo wa madaraka kati ya Serikali na Mahakama ili kulinda uhuru wa Mahakama, Sheria ya Uendeshaji Mahakama, 2011 iliyotungwa na Bunge hili Tukufu katika Mkutano wake wa Tatu, imemwongezea Rais madaraka makubwa zaidi katika uendeshaji wa Mahakama. Kwa mujibu wa kifungu cha 7(1) cha Sheria hiyo, Rais ndiye atakayemteua Mtawala Mkuu wa Mahakama na ndiye anayeamua masharti ya ajira ya Mtawala Mkuu wa Mahakama [kifungu cha 7(6)]. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 9, mamlaka ya

nidhamu juu ya Mtawala Mkuu wa Mahakama ni Rais. Sheria hii vile vile inampa Rais hata mamlaka ya kuanzisha au kuvunja nafasi za Kimahakama na zisizokuwa za Kimahakama baada ya kushauriwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama [kifungu cha 21(1)].

Kama ambavyo nilipata kusema wakati natoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Muswada wa Sheria hiyo, kifungu hiki kinakwenda kinyume na matakwa ya ibara ya 36(1) ya Katiba inayompa Rais mamlaka ya kuanzisha au kufuta ofisi za utumishi wa umma "... bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyomo katika Katiba hii na sheria nyingine yoyote...." Nafasi za Kimahakama kama za Majaji na Mahakimu zimewekwa ama na Katiba yenyewe au na sheria nyinginezo na kwa hiyo Rais hana mamlaka ya kuzianzisha au kuzifuta!

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama vile vile inatishia uhuru wa Mahakama kwa kuruhusu wanasiwa na watendaji wa Serikali kusimamia nidhamu za watumishi wa Kimahakama. Kwa mfano, chini ya kifungu cha 50(5), Kamati za Maadili ya Watumishi wa Kimahakama za Mikoa zimepewa wajibu wa kushughulikia nidhamu za Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu Wakazi wa mikoa husika. Kamati hizi zinaoongozwa na Wakuu wa Mikoa amba pia wanateua wajumbe wengine wawili kati ya wajumbe sita wa Kamati [kifungu cha 50(1)]. Kama ambavyo nimepata kusema wakati nilipowasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Muswada wa Sheria hii, utaratibu huu unahatarisha uhuru wa Mahakama kwa sababu Wakuu wa Mikoa "... wana tabia ya kuingilia utendaji wa Mahakama zetu na mara nyingi ni wakiukaji wa sheria na taratibu za nchi yetu. Mara nyingi Mahakama ni vyombo pekee katika mikoa vyenye mamlaka kisheria ya kuwadhibiti pale wanapokiuka miiko ya kisheria ya kazi zao."

Mheshimiwa Naibu Spika, kivuli hiki kirefu cha Urais wa Kifalme katika uongozi na utekelezaji wa mamlaka ya utoaji haki wa Mahakama ni tishio kwa uhuru wa Mahakama na utekelezaji wa majukumu yake. Licha ya viapo vyao vya kutenda haki bila hila, woga au upendeleo, wateuliwa wa nafasi mbalimbali za uongozi au utendaji wa Mahakama wana uwezekano mkubwa wa kujiona wanawajibika kwa mamlaka yao ya uteuzi, yaani Rais. Aidha, watendaji wa Mahakama amba wanawajibika kinidhamu kwa mamlaka zinazoonozwa na watendaji wa Serikali na makada wa Chama Tawala kama Wakuu wa Mikoa wanakuwa na woga wa kushughulikia kesi zinazowahu watendaji na makada hao na/au Serikali wanayoiwakilisha. Dalili za woga huu ni nyingi na zitazidi kuongezeka kwa sababu ya Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama. Tayari tumeanza kusikia taarifa za baadhi ya Wakuu wa Mikoa kuwafuata Mahakimu ili kuulizia mwelekeo wa kesi zinazohusu wanachama au viongozi wa Vyama vya Upinzani hasa hasa CHADEMA. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba huu ni muda muafaka, sambamba na mjadala wa mfumo mpya wa Kikatiba, kuyashughulikia masuala haya ili Mahakama ya Tanzania iondokane na kivuli kirefu cha Urais wa Kifalme na kuiwezesha kuwa huru kutenda haki kwa mujibu wa viapo vya watendaji wa Mahakama ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu amlipae mpiga Zomari. Pengine tishio kubwa kuliko mengine yote kwa uhuru wa Mahakama za Tanzania limekuwa sio tu kuingiliwa na wanasiwa na watendaji wakuu wa Serikali. Tishio kubwa zaidi ni lile la Serikali kutumia udhibiti wake wa hazina ya Taifa kuinyima Mahakama rasilimali za kuiwezesha kutimiza wajibu wake Kikatiba. Kama nilivyosema katika hotuba yangu wakati nawasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Uendeshaji Mahakama, moja ya matatizo makubwa yanayokabili Mahakama zetu nchini ni pamoja na vipaumbele vyake kutozingatiwa katika migawanyo ya bajeti za Serikali za kila mwaka. Wasiofutilia kauli za Serikali Bungeni wanaweza kufikiri kwamba haya ni maneno ya kila siku ya Wapinzani wasioona mema mengi ambayo Serikali mbalimbali za CCM na mtangulizi wake, *TANU*, zinadaiwa kuyafanya katika kipindi cha miaka hamsini ya uhuru wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wengine fikra hizo, naomba niwakumbushe kauli ya aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria wakati huo, Mheshimiwa Dokta Mary M. Nagu, wakati alipowasilisha hotuba ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2006/2007 na naomba nimnukuu: "... Changamoto zilizoainishwa kimsingi zinatokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa kila mwaka wa fedha. Mara nyingi na kwa kipindi kirefu, kiasi kinachotolewa huwa hakilingani na mahitaji halisi ya Wizara." Mwisho wa kunukuu.

Naomba niwakumbushe pia kauli ya mrithi wa Mheshimiwa Dokta Nagu katika Wizara hiyo Mheshimiwa Mathias M. Chikawe wakati wa hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2009/2010, naomba ninukuu tena: "... Changamoto zilizoainishwa kimsingi zinatokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara yangu kila mwaka wa fedha. Mara nydingi kiasi kinachotolewa huwa hakilingani na mahitaji halisi ya Wizara na hata kiasi kidogo kinachotengwa hakitolewi kwa wakati na wala hakitolewi chote, jambo ambalo linaathiri sana Mpango Kazi wa Wizara yangu." Kama nitakavyoonesha kwingineko katika hotuba hii, hoja hizi za 'Sungura Mdogo' ndio zimekuwa wimbo wa Serikali kila mwaka kuhusu bajeti za Wizara ya Katiba na Sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya miundombinu ya Mahakama zetu ni ya kusikitisha na haisameheki kwa upande wa Serikali ambayo ndio yenyenye udhibiti wa hazina ya umma. Kwa mfano, wakati Serikali imejenga majengo mapya ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa yote na Wilaya zote na Wizara mbalimbali katika kipindi cha miaka hamsini ya uhuru wetu, Kanda nane kati ya kumi na tatu za Mahakama Kuu ya Tanzania zimeendelea kutumia majengo yaliyorithiwa kutoka dola ya kikoloni. Kanda nne kati ya tano zilizobaki na Divisheni tatu za Mahakama Kuu, yaani Divisheni ya Biashara, ya Kazi na ya Ardh za zinatumbua majengo yaliyoazimwa au kuchukuliwa kutoka taasisi nyingine za umma! Ni Kanda moja tu za Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Bukoba ambayo imejengewa jengo jipya ya Mahakama katika kipindi cha miaka hamsini ya Utaifa wetu na hata hilo moja halijakamiliha hadi leo!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa karibu miaka thelathini tangu kuanzishwa kwake, Mahakama ya Rufani ya Tanzania ilikuwa ikichangia jengo moja na Masjala Kuu ya Mahakama Kuu, Dar es Salaam. Mwaka 2004, ukarabati wa jengo la iliyokuwa Hoteli ya Forodhani wa kulifanya kuwa Makao Makuu ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania ulianza. Ukarabati huo ulikamiliha na jengo kuanza kutumika mwaka 2006. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kwamba Serikali imeamua sasa kuliiza Jengo hilo kwa wawekezaji wapya wa iliyokuwa *Kempinski Kilimanjaro Hotel* ili libomolewe na eneo lake liguezwe kuwa maegesho ya magari ya wageni wa hoteli hiyo! Kwa hatua hii, Mahakama Rufani ya Tanzania itatakiwa ikapangishiwa tena mahali pengine pa kufanyia kazi zake za utoaji haki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali imeridhia jengo la Mahakama ya juu kabisa katika mfumo wetu wa kimahakama na wa kikatiba libomolewe ili wageni wa *Kempinski Kilimanjaro Hotel* wapate maegesho ya magari yao, Serikali imetenga shilingi sifuri kwa ajili ya Fungu 40 kasma 6313 inayohusu ukarabati wa Mahakama ya Rufaa! Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli rasmi Bungeni kama taarifa za kuuzwa kwa Jengo la Mahakama ya Rufani ya Tanzania na mipango ya kulibomoa ili eneo lake liguezwe kuwa maegesho ya magari ni za kweli. Kama ni za kweli, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iliambie Taifa Mahakama ya Rufani ya Tanzania itahamishiwa wapi ili kupisha wageni wa *Kempinski Kilimanjaro Hotel* kuegesha magari yao!

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuachana na mpango huo wa aibu mara moja kwa sababu unarudisha nyuma mafanikio yote yaliyopatikana kwa Mahakama ya Rufani ya Tanzania kuwa na jengo lake yenye na hivyo kupunguza mrundikano wa Majaji, Mawakili, watumishi wa Mahakama na wadau wa kesi ambaa umekuwepo kwa miaka mingi katika jengo la Masjala Kuu ya Mahakama Kuu ya Tanzania. Ni Serikali ya aina gani hii inayobomoa majengo ya mhimili mkuu wa dola kama Mahakama ili kutafuta nafasi ya watu wanaokwenda kujiburudisha hotelini kuegesha magari! Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ituepushie fedheha na aibu hii kwa nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoonesha kwenye hotuba yangu ya tarehe 15 Aprili mwaka huu, hali ya miundombinu ya Mahakama za chini ya Mahakama Kuu ni mbaya kama ilivyoona kwa Mahakama za juu. Hata hivyo, licha ya hali hii mbaya, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 500 tu kwa ajili ya Fungu 40 kasma 6310 inayohusu ujenzi na ukarabati wa Mahakama za Wilaya. Aidha, kasma 6312 inayohusu ujenzi na ukarabati wa Mahakama za Mwanza imetengewa shilingi milioni 500 vile vile. Hali hii mbaya ya miundombinu ya Mahakama ya Tanzania na mafungu haya kidogo yaliyotengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wake peke yake ni ushahidi wa kutosha kwamba mfumo wa uendeshaji na utoaji haki katika nchi yetu haujawahi kupewa kipaumbele na Serikali kwa miaka yote hamsini ya uhuru wetu. Kwa bahati mbaya huu sio

ushahidi pekee wa Serikali kupuuzia vipaumbele vya mfumo wetu wa uendeshaji na utoaji haki kwa miaka yote ya uhuru wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hajjawahi kutokea kwa Rais wa nchi hii au mawaziri wake kushindwa kufanya safari yoyote ndani au nje ya nchi kwa sababu ya ufinyu wa fedha zilizotengwa kwa ajili hiyo. Wote tu mashahidi kwamba kwa mwaka huu peke yake, Bunge hili Tukufu limeidhinisha zaidi ya shilingi billioni 135 kwa ajili ya safari za Rais na matumizi mengineyo ya Kitaifa! Rais na Baraza la Mawaziri ndio wanaounda mhimili wa kwanza wa dola la Tanzania. Aidha, hatujawahi kuambibiwa kwamba Bunge hili Tukufu limeshindwa kufanya Mkutano wake hata mmoja, au mikutano ya Kamati zake za Kudumu, kwa sababu ya ufinyu wa bajeti au 'udogo wa sungura.' Bunge hili Tukufu linaunda mhimili wa pili wa dola letu. Hata hivyo, imekuwa ni jambo la kawaida kwa Mahakama ya Tanzania, mhimili wa tatu wa dola la Tanzania kushindwa kufanya vikao vyake kwa sababu ya ufinyu wa bajeti inayotengwa kila mwaka kwa ajili hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za Serikali yenyejuu ya jambo hili zinaonyesha jinsi ambavyo Urais wa Kifalme umedhoofisha uwezo wa Mahakama ya Tanzania kutekeleza wajibu wao wa kikatiba wa kuwa "*mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano*", kutumia maneno ya ibara ya 107A(1) ya Katiba. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Mahakama ya Rufani ilipanga kufanya vikao ishirini na mbili vya kusikiliza kesi za rufaa. Hata hivyo, kutohana na kutokeleza fedha kulingana na mahitaji yake halisi, Mahakama hiyo iliweza kufanya vikao kumi na sita tu hadi kufikia mwezi Machi 2011. Vile vile, Mahakama Kuu katika Kanda mbalimbali kumi na tatu zilipanga kufanya jumla ya vikao 124 katika kipindi hicho. Hata hivyo, kutohana na kutokeleza fedha zinazolingana na mahitaji halisi ya vikao hivyo, Mahakama Kuu iliweza kufanya vikao kumi na tano tu na Kanda sita hazikufanya kikao hata kimoja!

Mheshimiwa Naibu Spika, sio Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani tu ambazo zimekwazwa kutekeleza wajibu wao kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Hali ni mbaya zaidi katika Mahakama za chini. Kwa mfano, wakati ambapo Mahakama za Mahakimu Wakazi na za Wilaya ziliikuwa na uwezo wa kusikiliza kesi 110,000 katika mwaka wa fedha 2010/2011, kwa ukomo wa bajeti waliowekewa na Serikali, Mahakama hizo zimeweza kusikiliza mashauri 27,000 au 24.6% ya uwezo wao. Aidha, Mahakama za Mwanzo ziliikuwa na uwezo wa kusikiliza kesi 242,000 kama zingeweza kutumia uwezo wa watumishi waliopo kwa sasa, licha ya upungufu mkubwa wa Mahakimu unaozikabili Mahakama za Mwanzo nchini. Hata hivyo, kwa sababu wa kupewa fedha pungufu, Mahakama za Mwanzo zimeweza kusikiliza takriban mashauri 70,000 tu au 28.9% ya uwezo wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla wake, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Mahakama ya Tanzania imeweza kusikiliza 29% tu ya mashauri ya madai na jinai kwa kutumia idadi ya Majaji na Mahakimu waliopo kwa sasa na kwa kutumia miundombinu haffu iliyopo. Ukweli ni kwamba kiasi hicho ni kikubwa hasa hasa ikitiliwa maanani kwamba katika kipindi hicho hicho, ukomo wa bajeti iliowekewa Mahakama ya Tanzania ilikuwa 23.5% ya mahitaji yake halisi. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, kiasi halisi kilichotolewa bila kujali kilitolewa lini kilikuwa 23% ya mahitaji halisi kwa mwaka huo!

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira haya, magereza hayawezi kuacha kujaa mahabusu ambao wanateseka na kuozea magerezani sio kwa sababu wana hatia yoyote bali kwa sababu hakuna Hakimu au Jaji wa kusikiliza kesi zao au kwa sababu walipo hawajatengewa fedha za kuwawezesha kusikiliza kesi hizo. Katika mazingira ya namna hii, maneno ya Ibara ya 107A(2)(b) ya Katiba yetu kwamba katika kutoa uamuzi wa mashauri ya madai na jinai kwa kuzingatia sheria, Mahakama zinatakiwa "... *kutochelewesha haki bila sababu ya kimsingi*" yanaonekana kama ni kejeli na dhihaka ya kikatili na kifedhuli kwa wale wote wanaotaabika magerezani kwa sababu ya kesi zao kutokusikilizwa kwa wakati. Katika hali hii, dira ya Wizara ya 'haki kwa wote kwa wakati' ingeonekana kama kichekesho kinachowafaa zaidi Ze Comedy kama isingekuwa inahusu maisha ya binadamu wanaoteseka magerezani bila kuwa na hatia yoyote!

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika hotuba yangu kwenye Bunge hili Tukufu mnamo tarehe 15 Aprili 2011, kwa sababu ya kuzinyima Mahakama fedha zinazolingana na mahitaji yao halisi na hata zinazolingana na ukomo wa chini uliowekwa na Hazina, "... Mahakama ya Tanzania imekuwa ni mdeni mkubwa na sugu." Takwimu za madeni ya Mahakama zetu yanayotokana na kushindwa kulipia vifaa, huduma na stahili mbalimbali za Majaji, Mahakimu na watumishi wengine wa Mahakama zinapatikana katika ukurasa wa 92-93 wa Taarifa Rasmi (Hansard) ya Majadiliano ya Bunge ya Kikao cha Nane cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Tanzania cha tarehe hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya Mahakama ya Tanzania kuwa mdeni mkubwa na sugu wa wagavi wa vifaa, huduma na wa stahili za Majaji, Mahakimu na watumishi wengine wa Mahakama kuna athari kubwa katika utendaji wake. Kwanza, kama alivyosema aliyekuwa Jaji Mkuu wa Tanzania, Augustino S.L. Ramadhani wakati alipotuhutubia Waheshimiwa Wabunge juu ya Nafasi ya Mahakama Katika Uongozi wa Nchi: "Ni vigumu sana kwa Jaji anayeishi katika nyumba inayodaiwa kodi kuweza kusikiliza na kutoa hukumu katika kesi za mwenye nyumba na mpangaji au kesi yoyote ya uvunjwaji mkataba. Lazima Jaji atoe boriti kwenye jicho lake ili aweze kutoa (sic!) kibanzi kwenye jicho la mwingine"! Wanasheria wanapenda kusema 'haki sio tu lazima itendeke lakini vile vile lazima ioneokane kuwa imetendeka.' Majaji ambaeo ni wadeni sugu wanawezaje kuonekana wametenda haki kwa wadeni sugu wengine wanaokwenda Mahakamani kudai malipo ya madeni yao! (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, athari ya pili, ni kwamba kuwa mdeni sugu kunaiondolea Mahakama heshima na hadhi yake mbele ya jamii na hasa hasa mbele ya watendaji wa mihimili mingine ya dola kama Serikali na Bunge. Napenda kumnuuu Jaji Mkuu Ramadhani tena: "Kila nilipokwenda mikoani nilikwenda ofisini kwa Mkuu wa Mkoa na kwa Mkuu wa Wilaya kutoa heshima zangu na kusaini kitabu cha wageni. Wakuu wa Mikoa wachache walitoka ofisini mwao kunilaki nje. Wengine walibakia ofisini mwao na kutuma mwakilishi kuja kunipokea ili nikamkute Mkuu wa Mkoa ofisini mwake ingawa Jaji Mkuu amefunga safari kutoka Dar es Salaam kumfuatia yeye. Kuna wakati nilikwenda Wilaya moja na nikaambiwa kuwa Mkuu wa Wilaya aliondoka jana yake kuanza likizo ya mwaka! Hivi kweli Mkuu wa Wilaya asingeweza kuahirisha likizo kwa siku moja tu kukutana na Jaji Mkuu. Ikkumbukwa kwamba Jaji Mkuu ndiye anayemuapisha Rais ili aweze kushika madaraka ya juu kabisa katika Taifa naye DC ni mwakilishi wa huyo Mheshimiwa Rais Wilayani humo." Kama Jaji Mkuu haheshimiwi kiasi hiki na Wakuu wa Mikoa na Wilaya, maamuzi ya Mahakama yake yanawezaje kuheshimiwa na watendaji hawa wa Serikali? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa mdeni sugu pia kunaiondolea Mahakama ya Tanzania imani kwa wagavi wa wa vifaa na huduma mbalimbali zinazohitajika kwa uendeshaji bora wa Mahakama. Kupotea kwa imani hiyo ya wagavi kuna athari kubwa za kiutendaji na hata kifedha. Kama inavyosema Taarifa ya Kikosi Kazi cha Ofisi ya Rais, Uratibu na Utawala Bora juu ya Ukaguzi wa Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo (20) Chini ya Ufadhilli wa Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria (*LSRP*) ya Machi, 2011: "Kumekuwepo na tabia sugu ya Mahakama kuchelewesha kulipa wakandarasi wa miradi ya ujenzi kwa wakati, hivyo kusababisha ujenzi wa Mahakama kuchelewa. Hivi sasa wapo wakandarasi wengi ambaeo hawavutiwi na kazi zinazotolewa na Mahakama. Na wakati mwingine wakandarasi hulazimika kupandisha gharama za ujenzi ili kufidia ucheleweshaji wa malipo unaotarajiwa kujitekeza kutoptana na urasimu wa Mahakama." (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sungura mdogo hakubaliki tena. Imekuwa jadi kwa Serikali kutoa sababu za ufinyu wa bajeti kuhalalisha kuinyima Mahakama fedha za kutosha kutimiza dira ya Wizara ya Katiba na Sheria ya 'Haki kwa Wote na kwa Wakati.' Visingizio hivi vya 'sungura mdogo', 'ufinyu wa bajeti' na kadhalika vimerudiwa rudiwa katika bajeti za kila mwaka za Wizara hii. Kwa mfano, akitoa hotuba ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2004/2005, aliyekuwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu alilieleza Bunge hili kwamba katika mwaka 2003/2004, "... Sekta ya Sheria kwa ujumla wake imeendelea kukabiliwa na matatizo ambayo yanaathiri kasi na ufanisi wa utendaji. Matatizo hayo yametokana hasa na ufinyu wa Bajeti ya Serikali. Ufinyu huo wa Bajeti umeendelea kuathiri utoaji na usimamizi wa haki na utawala wa sheria." (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake ya Bajeti kwa mwaka 2005/2006, Mheshimiwa Mwapachu alirudia tena hoja ya 'udogo wa sungura': "... Wizara kwa ujumla wake imeendelea kukabiliwa na matatizo ambayo yanaathiri kasi na ufanisi wa utendaji. Matatizo hayo yanatokana hasa na Bajeti ya Serikali kutoweza kukidhi mahitaji halisi ya asasi za Wizara." Kama tulivyoonesha, visingizio hivi vilirithiwa na Serikali ya Awamu ya Nne ya Rais Mheshimiwa Dokta Jakaya Kikwete kama ushahidi wa hotuba ya bajeti ya mwaka 2006/2007 iliyotolewa na Mheshimiwa Dokta Nagu unavyothibitisha. Vile vile, katika hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2007/2008, Mheshimiwa Dokta Nagu alirudia "... kuwepo matatizo makubwa ya ufinyu wa bajeti" kama moja ya changamoto zilizosababisha Wizara kutotekeleza kikamilifu na kwa ufanisi baadhi ya majukumu yake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba pekee ambayo haikuzungumzia kabisa tatizo la 'ufinyu wa bajeti' au 'udogo wa sungura' ni ile iliyotolewa na Mheshimiwa Chikawe wakati alipowasilisha bajeti ya mwaka 2008/2009. Hata hivyo, mwaka ullofufata kama tulivyoekwisha kuonesha, Mheshimiwa Chikawe alirudi kundini kwa kurejea tena dhana hiyo ya 'sungura mdogo'! Mheshimiwa Chikawe aliendelea jadi ya 'ufinyu wa bajeti' na 'sungura mdogo' kwenye Bajeti ya Wizara ya mwaka jana pale aliposema kwamba: "... Wizara yangu bado inakabiliwa na changamoto nyingi katika vyombo vyake vya utoaji haki nchini.

Aidha, changamoto nyingi zinazoikabili Wizara ni pamoja na uwezo mdogo wa Serikali kifedha na rasilimali watu katika vyombo vyake vya utoaji haki kwa wananchi wake na kusababisha kuendelea kuwepo kwa mrundikano wa mashauri ya jinai na madai kwa kiwango kikubwa...." Aidha, Mheshimiwa Chikawe alikiri kwamba licha ya idadi ya watumishi wa kada mbalimbali wa Mahakama kuongezeka, "... bado uwezo wa Serikali kifedha ni mdogo kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi katika utoaji wa haki hapa nchini. Pia Wizara yangu ina upungufu wa nyenzo za kufanya kazi kama magari, ofisi, samani na nyumba za watumishi. Changamoto hizi zinaathiri utekelezaji wa azma ya Serikali ya upatikanaji wa haki kwa wote mapema na kupunguza tija ya Taasisi mbali mbali zilizoko chini ya Wizara."

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria hajasema katika hoja yake ya leo kwamba fedha anazoomba Bunge hili Tukufu liidhinishe kwa Wizara yake kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo kwa mwaka huu wa fedha hazitoshi wala bajeti hii ni finyu na wala hajasema kwamba sungura huyu ni mdogo. Hii ni licha ya ukweli kwamba Serikali hajatenga fedha zozote za maendeleo kwenye Fungu 18 la Mahakama Kuu na Mahakama za Mahakimu Wakazi tangu mwaka wa fedha 2010/2011-2011/2012. Aidha, kwa kipindi hicho hicho, hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwenye Fungu 19 linalohusu Mahakama za Wilaya na za Mwanzo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimya wa Mheshimiwa Waziri kuhusu suala la utoshelevu wa fedha anazoomba ziidhinishwe na Bunge hili Tukufu sio wa ajabu, kwani katika utafiti wangu kwa ajili ya hotuba hii, sijaona yeoyote kati ya Mawaziri wote waliomtangulia Mheshimiwa Waziri wa sasa wa Sheria na Katiba aliyewahi kuliambia Bunge hili Tukufu kwamba bajeti walizokuwa wanaziombea idhini ya Bunge hazitoshi. Kwa sababu hiyo, pengine haitakuwa makosa kwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuchukulia ukimya wa Mheshimiwa Waziri katika jambo hili kuwa ni imani yake kwamba fedha anazoomba mwaka huu zitatosheleza mahitaji yote ya Wizara yake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Mheshimiwa Waziri ameliambia Bunge hili Tukufu kwamba bajeti ya mwaka jana ilikuwa finyu ndio maana majukumu ya utoaji haki hayakutekelezwa kwa ufanisi. Maneno haya ya bajeti finyu na sungura mdogo ni utetezi ambao unapaswa kupuuzwa na Bunge hili Tukufu. Ni maneno yanayokuja kama *after thought* baada ya Serikali kushindwa kutekeleza wajibu wake. Kwa jambo hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli kama bajeti hii ya mwaka huu inatosheleza mahitaji yote yatakayoiwezesha Mahakama ya Tanzania kutoa haki kwa wote kwa wakati kama ilivyo dira ya Wizara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itakiri kwamba fedha zilizotengwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya Mahakama ya Tanzania hazitatosha kuiwezesha kutekeleza wajibu wake

kikatiba, basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe pungufu ya fedha hizo kutoka kwenye Fungu Na. 98 la Wizara ya Ujenzi, Kasma Na. 4168 inayohusu 'Miradi Maalum ya Ujenzi wa Barabara' ambalo baada ya shilingi bilioni 95 kuchotwa na kupelekwa Wizara ya Uchukuzi, sasa limebakisha shilingi bilioni 253.075. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaanmini kwamba kama ilikuwa halali kwa Serikali kutoa shilingi bilioni 95 kutoka kwenye Fungu hilo baada ya kuwa zimekwishaidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi na kuzipeleka kwenye Fungu Na. 62 la Wizara ya Uchukuzi, haiwezi ikawa haramu kwa Serikali hiyo hiyo kutoa fedha nyingine kutoka Fungu hilo hilo na kuzipeleka kwenye mafungu yote yanayohusu Mahakama ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujisadi Mahakama. Inaelekea kwamba Mahakama ya Tanzania nayo imekumbwa na aina ya kansa inayojukana kitaalamu kama *fisadiosis*, au kwa jina lilirozoleka hapa kwetu, ujisadi ambayo imesambaa kila mahali katika mfumo wetu wa kiutawala. Dalili za kuenea kwa kansa hii katika Mahakama ni pamoja na matumizi mabaya ya fedha za umma zinazotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo ya Mahakama ya Tanzania. Naomba kuthibitisha jambo hili kwa kutumia mradi wa ujenzi wa majengo ya Mahakama chini ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria (*Legal Sector Reform Program*) ambayo imekuwa ikifadhiliwa na nchi wafadhili pamoja na Benki ya Dunia kwa karibu miaka mitano sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya *LSRP*, Mahakama ya Tanzania ilipanga kujenga majengo kumi ya Mahakama na kukarabati mengine kumi yaliyochakaa kila mwaka kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008. Fedha za utekelezaji wa miradi hiyo zimekuwa zikitolewa na wafadhili katika bajeti ya maendeleo kupitia mradi wa *LSRP* kila mwaka. Hata hivyo, kwa mujibu wa Taarifa ya Kikosi Kazi cha Ofisi ya Rais, "utekelezaji wa miradi hiyo umekuwa haqidhishi kiasi kwamba wafadhili wamefikia hatua ya kutishia kujitoa na kusitisha ufadhili wao". Ukaguzi wa miradi hiyo uliofanywa na Kikosi Kazi hicho unaonesha kwamba, hadi sasa ni Mahakama tatu tu zilizoweza kujengwa na kukamilika kwa kipindi chote hicho. Mifano michache ya dalili za kansa ya ujisadi kwenye miradi hiyo inatosheleza kuthibitisha uwepo wa tatizo hili ndani ya Mahakama. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya majengo yaliyotarajiwa kukarabatiwa chini ya *LSRP* ni jengo la Mahakama ya Mwanzo ya Kirua Vunjo, Wilayani Moshi Vijijini katika Mkoa wa Kilimanjaro. Kwa mujibu wa Taarifa ya Kikosi Kazi cha Ofisi ya Rais, jengo la Mahakama hiyo "kwa nje limekarabatiwa vizuri na kumalizika. Hata hivyo, kwa ndani jingo hilo lina mipasuko kwenye kuta na sakafuni. Aidha, mbaa za dari zimeliwa na mchwa na kusababisha *ceiling board* zote kuanguka chini. Kwa ujumla, kazi iliyo fanyika hairidhishi na hajafikia kiwango kilichotarajiwa kulingana na thamani ya fedha iliyotumika." Cha ajabu kabisa ni kwamba "mkandarasi alikwishakabidhi jengo toka mwaka 2009 na kulipwa fedha yake yote ikiwemo *retention money*." (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa jengo la Mahakama ya Mwanzo ya Basotu katika Wilaya ya Hanang, Mkoa wa Manyara nao umegubikwa na utata wa ujisadi. Kwa mujibu wa Taarifa ya Kikosi Kazi cha Ofisi ya Rais, ingawa ujenzi wa Mahakama hiyo umekamilika kwa 75%, mkandarasi ameshalipwa 95% ya fedha zake "... ijapokuwa hadi sasa mkandarasi ameshindwa kumaliza kazi na kukabidhi mradi." Timu ya ukaguzi ya Kikosi Kazi cha Ofisi ya Rais ilibaini kwamba Wakala wa Majengo ya Serikali (*TBA*) "... waliruhusu mkandarasi kulipwa kiasi kikubwa cha fedha ambacho hakilingani na kazi iliyokwahafanyika." (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo ya Bereko katika Wilaya ya Kondo, Mkoani Dodoma nao umezua maswali juu ya uadilifu wa wahusika. Ujenzi huo ulitakiwa kuwa wa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza ilitakiwa kumalizika tarehe 20 Julai, 2008. Kwa mujibu wa Taarifa ya Kikosi Kazi cha Ofisi ya Rais, "... Mahakama ilikwishamlipa mkandarasi shilingi 141,704,940 ikiwa ni pamoja na *advance* kwa ajili ya awamu ya pili. Hata hivyo, malipo hayo yaliyofanyika kabla ya mkandarasi hajamaliza na kukabidhi kazi za awamu ya kwanza na wala bila kuwepo mkataba wowote kwa ajili ya awamu ya pili ya ujenzi huo." Aidha, "... hakukuwepo mchanganuo *Approved Bill of Quantities*, zinazoainisha kazi zitakazofanywa na mkandarasi katika awamu hiyo ya pili." Kwa sababu hizo, hadi sasa ni vigumu kujua gharama halisi za mradi huu wa Mahakama ya Bereko kwa vile hakuna mkataba mahususi kwa ajili ya kazi hiyo ya ujenzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine ya ujenzi wa Mahakama ambayo imeonyesha dalili za *ufisadiosis* ni Mahakama ya Mwanzo ya Shelui, Wilayani Iramba katika Mkoa wa Singida; Mahakama ya Mwanzo ya Ilolangulu, Wilayani Uyui katika Mkoa wa Tabora; Mahakama ya Mwanzo ya Makuyuni katika Wilaya ya Monduli, Mkoani Arusha na Mahakama ya Mwanzo ya Mwanga Mjini katika Wilaya ya Mwanga, Mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kikosi Kazi cha Ofisi ya Rais kilichokagua miradi hiyo kilibaini kwamba jengo la Mahakama ya Mwanzo ya Shelui "... liko katika hali isiyordhisha"; kwa Ilolangulu "... mkandarasi hakuweza kukamilisha kazi katika muda ... uliopangwa kutokana na sababu zisizokuwa na msingi pamoja na usimamizi hafifu", lakini *TBA* ilimwidhinishia malipo "... wakati kazi ilikuwa haijaanza kufanya ambapo ...alilipwa fedha zote"! (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mahakama ya Mwanzo ya Makuyuni, ujenzi wake haujaanza na kiwanja kilichokuwepo mwanzoni kimechukuliwa na Halmashauri baada ya kukaa muda mrefu bila kuendelezwa." Aidha, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Monduli "... hajawahi kujua kama Mahakama ya Mwanzo ya Makuyuni imo katika mpango wa kujengwa chini ya *LSRP*." Kama ilivyokuwa kwa Makuyuni, Kikosi Kazi cha Ofisi ya Rais kiliambiwa kwamba ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo ya Mwanga Mjini nao ulikuwa bado haujaanza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashangazwa na kusikitishwa sana na utendaji wa aina hii wa Mahakama ya Tanzania. Kama taasisi inayosimamia sheria na iliyojaa wanasheria kama Mahakama ya Tanzania inaweza kufanya malipo ya mamiloni ya shilingi za walipa kodi bila kuwepo mkataba wa kazi inawezaje kuwardhisha Watanzania kwamba maamuzi mbalimbali juu ya haki na wajibu wa wananchi yanafanywa na watu wanaojuu kweli sheria za nchi yetu na sio na vihiyo wa sheria! Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazitaka mamlaka husika kuwachukulia wote waliohusika hatua stahiki haraka iwezekanavyo ili kurudisha imani ya Watanzania kwa Mahakama ya Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utendaji wa aina hii sio tu unatilia shaka uadilifu wa watendaji wa kimahakama na uwezo wao wa kitaaluma, bali pia unawapa nguvu wale wote ambao wamehusika katika kuudhoofisha mfumo wetu wa utoaji haki kwa kuwapa hoja kwamba Mahakama ya Tanzania haina uwezo wa kusimamia fedha zake. Mfano mzuri wa hatari hii ni Taarifa yenyeze ya Kikosi Kazi cha Ofisi ya Rais. Baada ya madai kwamba ofisi ya Msajili wa Mahakama ya Rufaa ya Tanzania "... haina wataalam wa fani nydingine zaidi ya wanasheria ambao kazi yao ya msingi ni kwenda mahakamani ... na kwamba wanasheria hawafundishwi utawala wa fedha wawapo chuoni "... lakini hivi sasa kila mtu Mahakamani anatamani awe msimamizi mkuu wa fedha ...", Taarifa hiyo ilipendekeza kwamba "... muundo wa uongozi wa Mahakama urekebishwe kiasi kwamba kuwepo na kada mbili, ya utawala na ile ya wanasheria. Kada ya sheria ishughulikie masuala ya kuendesha kesi mahakamani na kada ya uongozi wa Mahakama ihusike na mambo yote ya utawala ikiwemo kusimamia miradi ya maendeleo ya Mahakama."

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba haikuwa bahati tu kwamba mwezi mmoja baada ya Kikosi Kazi cha Ofisi ya Rais kuwasilisha Taarifa yake Serikalini, Muswada wa Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama uliletwa Bungeni chini ya Hati ya Dharura na kupitishwa kuwa sheria baada ya siku mbili za mjadala! Nimeshaeleza madhara ya Sheria hii kwa uhuru wa Mahakama ya Tanzania kutenda haki bila hila, woga au upendeleo. Taarifa ya Kikosi Kazi cha Ofisi ya Rais ilikuwa ni *Farasi wa Troy* (*Trojan Horse*) katika vita ya Urais wa Kifalme dhidi ya Mahakama ya Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mchakato wa Katiba Mpya. Tarehe 11 Machi 2011, Serikali ilichapisha Muswada wa Sheria ya Mapitio ya Katiba ya mwaka 2011 (*The Constitutional Review Bill, 2011*) katika Gazeti la Serikali la tarehe hiyo. Muswada huo uliletwa katika Mkutano wa Tatu wa Bunge hili Tukufu kwa Hati ya Dharura. Hata hivyo, baada ya upinzani mkubwa dhidi ya Muswada huo kujitokeza karibu nchi nzima, Serikali ililazimika kuuondoa katika ratiba ya shughuli za Bunge kwa maelezo kwamba itaufanya marekebisco na kuurudisha Bungeni katika Mkutano huu

wa Bunge. Hata hivyo, licha ya Muswada huo kuwepo katika ratiba ya awali ya shughuli za Bunge, baadaye ratiba hiyo ilifanyiwa mabadiliko kwa kuuondoa Muswada kwenye ratiba hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, danadana yote hii inaonesha jinsi suala la utaratibu wa namna ya kupata Katiba mpya kwa ajili ya nchi yetu lilitivo muhimu. Tofauti na kauli za awali za Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba sheria inayoweka utaratibu wa kupatikana kwa Katiba mpya ina umuhimu mkubwa wa karibu sawa na Katiba yenyewe. Utaratibu wa kidemokrasia, shirikishi wa makundi makuu ya kijamii na ulio wazi utapeleke na nchi yetu kuwa na Katiba mpya ambayo sisi wote tutaweza kujivunia. Kwa upande mwengine, utaratibu uliojaa ukiritimba wa kirasi, unaohodhiwa na watu au taasisi chache na unaofanyika gizani na/au kwa siri utaleta Katiba mpya kwa jina tu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba katika hali ya sasa ya kisiasa ya nchi yetu, utaratibu huu hauwezi kukubalika na wananchi walio wengi na utasababisha machafuko makubwa ya kisiasa na kijamii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya, Serikali inaelekewa kufikiri kwamba inaweza kuwalazimisha Watanzania kukubali utaratibu wa aina hiyo. Hii ni kwa sababu Kambi Rasmi ya Upinzani imepata nakala ya Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Mapitio ya Katiba, 2011 iliyo fanyiwa marekebisho ambayo inatazamiwa kuleta Bungeni kwa tarehe ambayo haijulikani bado. Rasimu ya Muswada huu inathibitisha kwamba Serikali haina nia yoyote ya kuweka utaratibu wa kidemokrasia, ulio shirikishi wa makundi makuu ya kijamii na kisiasa katika kupata Katiba Mpya. Kwa upande mwengine, Rasimu inapendekeza utaratibu wa kupata Katiba Mpya uliojaa urasimu na unaoendeleza hodhi ya Urais wa Kifalme ambayo ndiyo imekuwa hulka kuu ya mfumo wetu wa kikatiba na kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rasimu ya Muswada inapendekeza kumpa mamlaka makubwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa mashauriano na/au makubaliano na Rais wa Zanzibar ya kuteua Tume ya Kupitia Katiba yenyewe wajumbe wasiozidi thelathini. Aidha, Rasimu ya Muswada inapendekeza kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa mashauriano na/au makubaliano na Rais wa Zanzibar ataipatia Tume hiyo hadidu za rejea na muda wa kumaliza kazi yake na kuwasilisha taarifa. Utaratibu huo huo wa mashauriano na makubaliano utatumika katika uteuzi wa Katibu wa Tume na Sekretariati ya Tume ambayo itateuliwa na Waziri wa Katiba na Sheria kwa makubaliano na Waziri mwenzake wa Zanzibar. Katibu na wajumbe wa Sekretariati wanatakiwa kuwa watumishi wa umma ambao hata kwa mujibu wa utaratibu wa sasa wa kikatiba, wanawajibika kwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Mapitio ya Katiba inaendeleza pia mfumo wa Urais wa Kifalme kwa mapendekezo juu ya uwasilishaji wa taarifa ya Tume. Hapa inapendekeza kwamba Tume ya Mapitio ya Katiba itawasilisha taarifa yake kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Rais wa Zanzibar.

Aidha, baada ya mashauriano na makubaliano na Rais wa Zanzibar na baada ya kumalizika kwa taratibu za ndani zinazohusu utungaji wa sera, Rais atamwelekeza Waziri kuwasilisha Muswada wa Katiba katika Bunge la Katiba kwa ajili ya kupitishwa kwa vifungu vya Katiba." Pendekezo hili ni la hatari kubwa. Kwanza, kumalizika kwa taratibu za ndani zinazohusu utungaji wa sera maana yake ni kwamba mpaka Baraza la Mawaziri lirdhie Muswada huo ndio utapelekwa kwenye Bunge la Katiba! Kwa mujibu wa Katiba, wajumbe wote wa Baraza la Mawaziri ni wateuliwa wa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa Urais wa Kifalme pia unaonekana katika mapendekezo yanayohusu Baraza la Katiba. Kwa mujibu wa kifungu cha 20 cha Rasimu ya Muswada, Rais kwa makubaliano na Rais wa Zanzibar na baada ya kushauriwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na yule wa Zanzibar ataunda Baraza la Katiba na kuteua wajumbe wake. Baada ya kuundwa, Baraza la Katiba litateua Spika na Naibu Spika ambao watatakiwa kutoka katika sehemu tofauti za Jamhuri ya Muungano. Spika na Naibu Spika watatakiwa kula kiapo mbele ya Makatibu wa Baraza la Katiba ambao ni Katibu wa Bunge wa sasa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar wa sasa. Wote hawa, kwa mujibu wa Katiba na Katiba ya Zanzibar ya 1984, ni wateuliwa wa Rais na/au wa Rais wa Zanzibar na wanatakiwa kula kiapo kwa Rais! (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Mapitio ya Katiba inapendekeza kwamba kazi ya Baraza la Katiba iwe moja tu: kutunga Katiba Mpya na mambo yanayohusiana nayo. Baada ya kufanya kazi hiyo, Baraza litakuwa limejifuta lenyewe, ijapokuwa kujifuta huko kwa Baraza hakutamzuia Rais kuliunda upya Baraza siku za baadaye likiwa na wajumbe wale wale kwa lengo la kufanya mabadiliko ya Rasimu ya Katiba Mpya kabla Rasimu hiyo haijapitishwa! Rasimu inapendekeza kwamba ili Katiba Mpya ipitishwe ni lazima ipate ridhaa ya theluthi mbili ya wajumbe wote wanaotoka Tanzania Bara na idadi hiyo hiyo ya wajumbe wanaotoka Tanzania Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Mapitio ya Katiba inapendekeza pia kwamba Katiba Mpya ipatiwe nguvu na uhalali wa kisheria kwa kupitia kura ya maoni itakayoratibiwa na kusimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushirikiana na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Tume hizi mbili kwa mashauriano na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar ndizo zitakazotengeneza swali litakaloulizwa kwenye kura ya maoni. Utaratibu utakaotumika katika kura ya maoni ni ule unaotumika katika chaguzi za kawaida katika nchi yetu, yaani Sheria ya Uchaguzi wa Taifa, Sura ya 343, Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292 na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar, 1984. Ijapokuwa kura ya maoni itaamuliwa kwa wingi wa wapiga kura (*simple majority*), Rasimu ya Muswada inapendekeza kwamba ili kura hiyo iwe halali ni lazima angalau 65% ya wapiga kura wote walijandikisha Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar washiriki katika kupiga kura. Rasimu ya Muswada inapendekeza kwamba Rais ndiye atakayeamua, kwa namna atakavyoona inafaa, kuanza kutumika kwa Katiba Mpya! (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli rasmi kama Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Mapitio ya Katiba ndio inawakilisha msimamo wa Serikali juu ya mchakato wa kutungwa kwa Katiba Mpya. Kama ni hivyo, basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuweka wazi msimamo wake Muswada huu haukulaliki hata kidogo.

Kwanza, Kambi Rasmi ya Upinzani haikubaliani na mamlaka makubwa yanayopendekezwa kupewa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Rais wa Zanzibar chini ya Muswada huu. Urais wa Kifalme kama kanuni kuu ya kikatiba na kisiasa ndiyo ambayo imetufikisha hapa tulipo leo: Taifa lenye wananchi maskini, liliojaa ufisadi, lisilojali demokrasia na haki za binadamu na lenye kuongozwa na watawala wasiowajibika kwa wananchi au kwa vyombo vya uwakilishi vya wananchi. Mfumo huu hauwezi kutumika tena kulipatia Taifa letu Katiba Mpya ya kidemokrasia itakayokidhi mahitaji ya karne hii na nytingine zijazo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mapendekezo ya Rasimu ya Muswada hayakubaliki kwa sababu yanaweka mchakato wa Katiba Mpya kwenye huruma na/au fadhila ya Rais wa Zanzibar na siasa za Zanzibar kwa ujumla. Kwa mapendekezo haya, Rais wa Zanzibar asipokubaliana na jambo lolote linalohitaji ridhaa yake basi mchakato mzima utasimama au kusitishwa. Aidha, endapo katika kura ya maoni inayopendekezwa, theluthi mbili ya Wazanzibari hawatakubaliana na Katiba Mpya basi Katiba hiyo haitapitishwa hata kama inakubaliwa kwa kiasi kikubwa na wananchi wa Tanzania Bara. Mustakabali wa Taifa letu hauwezi kuwekwa tena rehani kwenye siasa za Zanzibar na kwenye matakwa ya Wazanzibari kwa kiasi hicho. Kuhusiana na jambo hili, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba Rais wa Zanzibar ahushishwe tu katika masuala ya kikatiba ambayo ni ya Muungano tu. Nje ya masuala hayo, Rais wa Zanzibar hana sababu yoyote ya kuhusishwa na mchakato wa kikatiba unaohusu mambo ya Tanzania Bara. (*Makof*)

Aidha, wajumbe wa Tume ya Mapitio ya Katiba ambao watatoka Zanzibar wahusike tu katika mchakato wa masuala ya kikatiba ambayo ni ya Muungano tu. Vile vile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza wananchi wa Zanzibar washiriki katika kura ya maoni inayohusu mfumo mpya wa Muungano tu. Hii ndio kusema kwamba, kama vile ambavyo viongozi, wawakilishi na wananchi wa Tanzania Bara hawajashirikishwa katika mchakato wa kikatiba wa Zanzibar kwa sababu ulihusu mambo yasiyokuwa ya Muungano, vivyo hivyo viongozi, wawakilishi na wananchi wa Zanzibar wasishiriki katika mchakato wa kikatiba wa mambo yasiyokuwa ya kikatiba kwa upande wa Tanzania Bara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia historia halisi ya Muungano wetu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba wakati umefika kwa wananchi wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kuamua kwa mara ya kwanza katika historia yetu na kwa uhuru kabisa kama wanataka kuendelea kuwa na Muungano na wa aina gani. Hili halijawahi kufanyika na ndio maana Muungano umeendelea kuwa kero kwa wananchi wengi wa nchi hizi mbili. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba, suala la ridhaa ya wananchi ni la umuhimu mkubwa na ni lazima lishughulikiwe kwanza kabla ya mchakato unaopendekezwa na Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Mapitio ya Katiba kuanza na/au kupitishwa. (*Makof*)

Aidha, kwa kuzingatia historia yetu halisi ya kikatiba na kisiasa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza mfumo mpya wa kutunga Katiba Mpya ambao hautatawaliwa na kivuli kirefu cha Urais wa Kifalme. Kikubwa hapa ni kwamba, badala ya wajumbe wa Tume ya Katiba kuteuliwa na Rais kama inavyopendekezwa na Rasimu ya Muswada, wajumbe hao wateuliwe kutokana na mapendekezo ya Vyama vya Siasa, hasa hasa vile ambavyo vina uwakilishi Bungeni, taasisi zisizokuwa za Kiserikali na za kitaaluma, makundi maalum ya kijamii pamoja na Serikali yenye.

Aidha, badala ya Sekretariati ya Tume kujazwa warasimu wa Serikali ambao ni wateuliwa wa Rais kama inavyopendekezwa, Sekretariati hiyo itokane na wajumbe watakaoteuliwa na Tume yenye na ambao watawajibika moja kwa moja kwa Tume yenye badala ya kuwajibika kwa Rais kama ilivyo sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina imani, sio tu na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, bali pia na mfumo mzima wa kisheria na kitaasisi unaoendesha chaguzi za nchi yetu. Mfumo huu na watendaji wake wameonesha wazi kutokuwa huru na kutumiwa na Chama cha Mapinduzi kuchakachua matokeo ya chaguzi mbalimbali hapa nchini. Kwa maana hiyo, Tume ya Uchaguzi ya Taifa na ile ya Zanzibar, haiwezi kuachiwa jukumu kubwa la kuendesha kura ya maoni kwa ajili ya kupata Katiba Mpya. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba Serikali ilete Bungeni Muswada wa Mapendekezo ya Mabadiliko ya Katiba na ya Sheria husika za Uchaguzi kwa lengo la kuiunda upya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa lengo la kuhakikisha inasimamia zoezi la kura ya maoni kwa uhuru na bila upendeleo kwa Chama Tawala. Muswada huu vile vile utatoa fursa kwa Bunge hili Tukufu kutunga vifungu vinavyowezesha Katiba Mpya kutungwa ambavyo havipo kwa Katiba ya sasa. Kutofanya marekebisho haya kutafanya sheria yoyote ya kuweka utaratibu wa kupata Katiba Mpya kuwa batili kwa kwenda kinyume na matakwa ya Katiba ya sasa ambayo hairuhusu Katiba Mpya kutungwa ila inaruhusu tu marekebisho ya Katiba yenye. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uendeshaji wa mashtaka ya jinai. Mamlaka ya Uendeshaji wa Mashtaka ya Jinai imekasimiwa kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mujibu wa Ibara ya 59B(2) ya Katiba. Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 59B(4), katika kutekeleza mamlaka yake, "Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa huru, hataingiliwa na mtu yeyote au na mamlaka yeyote na atazingatia ... nia ya kutenda haki, kuzuia matumizi mabaya ya taratibu za utoaji haki na maslahi ya umma." Kanuni hii kuu imetamkwa pia na kifungu cha 8 cha Sheria ya Utumishi wa Mashtaka ya Taifa, Na. 27 ya 2008 (*National Prosecutions Service Act, 2008*) ambayo pia imefafanua na kutilia nguvu mamlaka haya ya kikatiba. Kwa mujibu wa Sheria hii, Mkurugenzi wa Mashtaka ana mamlaka sio tu ya kudhibiti mashtaka yote ya jinai bali pia kuratibu shughuli za upelegelezi wa makosa ya jinai [kifungu cha 16(1)]. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 17(1) na (3), Mkurugenzi ana uwezo wa kutoa maelekezo ya maandishi kwa ofisa yeyote wa umma ili apatiwe taarifa yoyote inayohusu upelegelezi au uendeshaji wa mashtaka ya jinai na ofisa huyo anatakiwa kutii maelekezo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kumwezesha Mkurugenzi wa Mashtaka kutekeleza wajibu wake wa kikatiba kwa uhuru kamili na bila woga au upendeleo, Mkurugenzi wa Mashtaka amewekewa kinga ya ajira yake. Kwa mujibu wa kifungu cha 19(1) na (2) cha Sheria ya Utumishi wa Mashtaka ya Taifa, sifa, masharti na mafao ya ajira ya Mkurugenzi wa Mashtaka yatakuwa sawa na yale ya ajira ya Jaji wa Mahakama Kuu. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 19(3), Mkurugenzi wa Mashtaka hawezi kuondolewa kwenye madaraka yake isipokuwa kwa kushindwa kutimiza wajibu wake kwa sababu ya ugonjwa au kwa kukiuka Kanuni za Maadili ya Kitaaluma ya

Maafisa wa Sheria, Mawakili wa Serikali na Wanasheria Walioko kwenye Utumishi wa Umma chini ya Sheria ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali, Sura ya 268 ya Sheria za Tanzania. Hii ndio kusema kwamba, kwa mujibu wa Sheria Na. 27 ya 2008, utaratibu wa kumwondoa Mkurugenzi wa Mashtaka kwenye ajira yake hauna tofauti na utaratibu wa kumwondoa Jaji wa Mahakama Kuu kwenye ajira yake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba utaratibu huu wa kikatiba na kisheria umempa Mkurugenzi wa Mashtaka nyenzo za kutosha kisheria za kupambana na uhalifu mkubwa hapa nchini na vile vile kuzuia matumizi mabaya ya mfumo wa uendeshaji na utoaji haki na hasa hasa ya mfumo wa mashtaka ya jinai. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashangazwa na kusikitishwa na kushindwa kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kufungua na/au kuendesha mashtaka yanayohusu matukio makubwa ya ujisadi ambayo yametikisa Taifa letu Serikali ya Awamu ya Nne ilipoingia madarakani miaka sita iliopita. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua uwepo Mahakamani wa kesi kadhaa za ujisadi zinazowahusu aliyekuwa Waziri wa Viwanda na Biashara wa zamani Basil Mramba na aliyekuwa Katibu Mkoo wa Wizara ya Fedha Gray Mgonja na maafisa kadhaa wa ngazi za kati wa Benki Kuu ya Tanzania. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiamini kwamba hawa ndio wahuksika pekee wa matukio yote ya ujisadi ambaa umelitia Taifa letu hasara kubwa. Hii ni kwa sababu tangu mwaka 2007, ushahidi wa kutosha unaowaunganisha viongozi na maafisa waandamizi wa Serikali ya Awamu ya Tatu na wa Awamu ya Nne na maswahiba wao wa kibiashara umetolewa hadharani mara baada ya Katibu Mkoo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) akisaidiwa na mimi mwenyewe kusoma Orodha ya Mafisadi (*The List of Shame*) katika Mkutano wa Hadhara wa Mwembe Yanga, Temeke, Dar es Salaam tarehe 18 Septemba 2007. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ushahidi wa maandishi uliotajwa katika Orodha ya Ujisadi na nyaraka nyingine zinazohusiana na Orodha hiyo zinaonesha kuhusika kwa viongozi wa ngazi za juu kabisa Serikalini katika kashfa kubwa za Meremeta Limited, Tangold Limited, Deep Green Finance Limited, Kagoda Agricultural Company Limited, Kiwira Coal Mine, Radar ya BAE Systems, Richmond, Dowans na nyinginezo nyingi. Kushindwa kuwachukulia hatua stahiki wahuksika hawa, pamoja na kutupiana mpira kati ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mkurugenzi Mkoo wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kunathibitisha sio mapungufu ya kisheria bali mapungufu ya uwezo wa kiutendaji kama sio wa kimaadili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010 /2011, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ilishughulikia kesi kubwa za rushwa zipatazo ishirini na tisa ambazo zilihusisha thamani ya fedha ya shilingi bilioni 288. Kati ya kesi hizo, kesi za wizi wa fedha za Benki Kuu ya Tanzania (*EPA*) ziliikuwa na thamani ya shilingi bilioni 37, uhujumu uchumi shilingi bilioni 12, kuisababishia Serikali hasara shilingi bilioni 225, kusafisha fedha haramu shilingi bilioni 10 na wizi wa kutumia silaha shilingi bilioni 4.1. Kwa kuzingatia hata Rais Kikwete mwenyewe alishawahidi kukiri kwamba fedha za *EPA* zilizoibwiwa ziliikuwa jumla ya shilingi bilioni 133, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutamka Bungeni ni kwa nini Mkurugenzi wa Mashtaka hajaona busara ya kuwashtaki wezi wa mabilioni yaliyobaki ya *EPA* hadi sasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya mapungufu hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa tamko rasmi kwa Bunge hili Tukufu kama huu sio muda muafaka kwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali kumshauri Rais kuunda Mahakama Maalum kwa mujibu wa kifungu cha 19(4) cha Sheria ya Utumishi wa Mashtaka ya Taifa kwa lengo la kuchunguza suala la kumwondoa madarakani Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kushindwa kutekeleza wajibu wake wa kikatiba na kisheria. Aidha, kwa vile ajira ya Mkurugenzi Mkoo wa TAKUKURU haina kinga za kisheria ilizo nazo ajira ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa tamko kwa nini hadi sasa Rais hajaona busara ya kutumia mamlaka yake chini ya Ibara ya 36(1) na (2) ya Katiba kufuta uteuzi wa Mkurugenzi Mkoo wa TAKUKURU kwa kushindwa kutekeleza wajibu wake kisheria. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubambikizaji raia kesi za uongo. Kama nilivyoonesha mwanzoni, Mkurugenzi wa Mashtaka ana jukumu kikatiba na kisheria kuzuia matumizi mabaya ya utaratibu wa utoaji haki. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitishwa na kushindwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kuzuia matumizi mabaya ya utaratibu wa utoaji haki ambayo yamekithiri ndani ya Jeshi la Polisi kwa Askari Polisi kukamata na kufungulia wananchi kesi za uongo zinazohusu tuhuma za makosa makubwa ya jinai ambayo hayana dhamana kisheria. Kwa mujibu wa Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa mwaka 2002/2003 iliyochapishwa mwezi Mei 2005, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (*CHRAGG*) iligundua kwamba malalamiko mengi iliyoyapokea kuhusu Jeshi la Polisi "...yaligusia polisi kubambikizia raia kesi...." Taarifa hiyo inathibitisha kwamba msongamano wa mahabusu katika magereza yetu kulingana na idadi ya wafungwa ni ishara ya "... kushindwa kwa mfumo wa dhamana chini ya Sheria ya Mwenendo wa Jinai, Sura ya 20 ya Sheria." (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia mfano wa kesi kubwa alizofunguliwa Diwani wa Kata ya Bumera katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo kwa mwaka 2005-2010, Mheshimiwa Tengera Marwa. Mwaka 2008 Mheshimiwa Marwa alizushiwa tuhuma ya mauaji na kufunguliwa kesi ya mauaji *Pl Na. 11 ya 2008* katika Mahakama ya Wilaya ya Tarime. Sambamba na kesi hiyo ya mauaji, Mheshimiwa Marwa pia alizushiwa kesi ya ujambazi wa kutumia silaha na kufunguliwa Kesi ya Jinai Na. 469 ya 2008 katika Mahakama hiyo hiyo. Baada ya kuteseka gerezani kwa zaidi ya mwaka mmoja kwa sababu kesi zote mbili hazina dhamana kisheria, Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kutumia mamlaka yake ya *nolle prosequi* alifutwa Mheshimiwa Marwa mashtaka yote mawili na hivyo akaachiliwa huru. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Mheshimiwa Tengera Marwa kuchukua fomu za uchaguzi ili aweze kutetea kiti chake cha Diwani wa Kata ya Bumera wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2010, tarehe 5 Agosti 2010 alikamatwa tena na kufunguliwa kesi ya jinai ujambazi wa kutumia silaha Na. 255 ya 2010 katika Mahakama ya Wilaya ya Tarime. Mwezi Septemba 2010, kesi hiyo nayo ilifutwa kwa *nolle prosequi* ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Hata hivyo, Mheshimiwa Marwa hakuachiwa nafasi ya kuwa huru kwa muda mrefu kwani muda mfupi kabla ya Uchaguzi Mkuu, alikamatwa tena na kufunguliwa kesi nydingine ya mauaji yenye *Pl Na. 39 ya 2010*. Sambamba na kesi hiyo ya mauaji, pia alifunguliwa kesi tena ya ujambazi ya kutumia silaha Na. 465 ya 2010. Kesi ya mauaji *Pl Na. 39/2010* ilifutwa kwa Mara nydingine tena kwa *nolle prosequi* ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliyotolewa mapema mwaka huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, matumizi mabaya ya mfumo wa utoaji haki dhidi ya Mheshimiwa Tengera Marwa hayakwisha kwani tarehe 5 Mei 2011 alifunguliwa kesi nydingine ya mauaji yenye *Pl Na. 21 ya 2011* na kwa hiyo ameendelea kuteseka kwenye Gereza la Rumande la Wilaya ya Tarime. Katika kipindi hicho, Mheshimiwa Marwa amefunguliwa kesi tatu za mauaji na tatu ujambazi wa kutumia silaha. Katika kipindi hicho hicho, Mheshimiwa Marwa amefutiwa kesi za mauaji mara mbili na kesi za ujambazi wa kutumia silaha mara mbili. Kesi mbili zilizobaki zinaonesha Mkurugenzi wa Mashtaka ameishiwa nguvu kwa sababu ya *nolle prosequi* zake zote kupuuzwa na uongozi wa Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Tarime na Rorya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mabaya ya mfumo wa uendeshaji na utoaji haki ya namna hii ni makosa ya jinai kwa mujibu wa kifungu cha 102 cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania na adhabu yake ni kifungo cha miaka saba kwa mujibu wa kifungu cha 104 cha Sheria hiyo. Pamoja na ukweli huo, Mkurugenzi wa Mashtaka hajachukua hatua zozote za kisheria dhidi ya maafisa husika wa Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Tarime na Rorya. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli rasmi Bungeni kama ni sera ya Serikali kwa Jeshi la Polisi kupuza mamlaka ya kikatiba na kisheria ya Mkurugenzi wa Mashtaka pale mamlaka hayo yanapokuwa tofauti na maslahi au matakwa ya Jeshi la Polisi au watendaji wake. (*Makofî*)

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe tamko ni kwa nini hadi sasa Mkurugenzi wa Mashtaka hajachukua hatua zozote za kisheria kuwfungulia mashtaka ya jinai ya matumizi mabaya ya utaratibu wa uendeshaji na utoaji haki watendaji wote wa Jeshi la Polisi, Kanda Maalum ya Tarime na Rorya kwa kuendelea kumtesa gerezani Mheshimiwa Diwani Tengera Marwa licha ya *nolle prosequi* kadhaa za Mkurugenzi wa Mashtaka. Vile vile Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe kauli kama, kutohana na matukio kama haya ya matumizi mabaya

ya utaratibu wa uendeshaji na utoaji haki, huu sio wakati muafaka kwa Serikali kuleta Muswada wa Mabadiliko ya Sheria mbalimbali za jinai ili kufuta vifungu vinavyozuia watuhumiwa wa makosa makubwa ya jinai kupatiwa dhamana na hivyo kuondoa kabisa uwezekano wa Jeshi la Polisi la kukiuka haki za binadamu kwa kutumia sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu haki za binadamu. Sehemu ya Tatu ya Sura ya Kwanza ya Katiba inahusu haki za binadamu na wajibu muhimu. Kwa mujibu wa Ibara ya 30(3) ya Katiba, jukumu la kuhifadhi na kulinda haki na wajibu muhimu zilizotolewa na Katiba ni wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Ili Mahakama Kuu itimiza wajibu wake huo, mwaka 1994 Bunge hili Tukufu lilitunga kwa mujibu wa Ibara ya 30(4) Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu wa Binadamu, Sura ya 3 ya Sheria za Tanzania. Kifungu cha 15 cha Sheria hiyo kinamtaka Jaji Mkuu, baada ya mashauriano na Waziri kutunga kanuni zitakazoweka utaratibu wa namna ya kufungua na kuendesha kesi zinazohusu ukiukwaji wa haki na wajibu wa binadamu. Hadi leo hii hakuna Jaji Mkuu hata mmoja ambaye ametunga kanuni hizo, miaka 17 baada ya kutungwa kwa Sheria yenye.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake ni kwamba watu wengi wameshindwa kufungua mashauri yanayohusu haki na wajibu wa binadamu kwa kukosekana utaratibu wa kikanuni uliofikiriwa na kifungu cha 15 cha Sheria hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli Bungeni ni kitu gani kimekwamisha utungwaji wa kanuni husika cha kifungu hicho. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine kizingiti kikubwa zaidi kwa utekelezaji wa haki na wajibu muhimu wa binadamu zilizotolewa na Katiba imekuwa ni masharti ya kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu wa Binadamu kinacholazimu Mahakama Kuu kuwa na Majaji watatu wakati wa kusikiliza kesi hizo. Katika mazingira halisi ya Mahakama Kuu ya nchi yetu yenye uhaba mkubwa wa Majaji, imekuwa na vigumu kwa Majaji watatu kupatikana kwa wakati mmoja ili kusikiliza na kuamua kesi zinazohusu haki za binadamu. Matokeo yake ni kwamba kesi nydingi zinakaa muda mrefu Mahakamani hadi wadaawa wanakata tamaa na kuziachia. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali iandae Muswada wa Marekebisho ya Sheria hiyo ili kurudisha utaratibu wa zamani wa kesi za haki za binadamu kusikilizwa na Jaji mmoja. Hii itarahisisha wadaawa kwenda Mahakamani kudai haki zao za msingi na Mahakama Kuu kuyafanya maamuzi maombi ya wadaawa hao kwa wakati muafaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo mengine yanayohusu utekelezaji wa haki za binadamu yanababishwa na Mahakama ya Tanzania yenye na hasa hasa majaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani ya Tanzania. Tofauti na ilivyokuwa miaka ya mwanzo ya utekelezaji wa haki za binadamu ambayo ilishuhudia kesi nydingi zikiamuliwa na Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani, kuanzia miaka ya katikati ya tisini na kuendelea Mahakama zetu za juu zimeingiwa na hofu ya kufanya maamuzi yanayohusu haki na wajibu wa msingi kama zilivyoainishwa na Katiba. Badala yake, Mahakama zetu za juu zimekuwa mabingwa wa kujificha katika kichaka cha masharti ya kiufundi na mara nydingi kesi zenye masuala ya msingi na muhimu kisheria zimetupiliwa mbali kwa sababu tu ya kuwepo makosa ya kiufundi ya kisheria wakati zinafunguliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hofu hii ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani inashangaza na kusikitisha sana kwa sababu inakwenda kinyume moja kwa moja na matakwa ya Ibara ya 107A(2)(e) ya Katiba inayoitaka Mahakama "... kutenda haki bila kufungwa kupita kiasi na masharti ya kiufundi yanayoweza kukwamisha haki kutendeka." Aidha, kama nilivyoonesha mwanzoni, Ibara ya 107B ya Katiba inazipa uhuru Mahakama zote katika utekelezaji wao wa mamlaka ya utoaji haki. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba moja ya sababu zinazofanya Mahakama ya Tanzania kudharaulika na kupuuzwa na wananchi na watendaji wa Serikali ni pamoja na kuabudu huku kwa masharti ya kiufundi hasa hasa yanapoonekana kwamba yatakwamisha haki kutendeka! (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii zilizoainishwa na Katiba vile vile zimewekewa utaratibu mwingine wa kikatiba na kisheria. Sehemu ya Kwanza ya Sura ya Sita ya Katiba inaunda Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (*CHRAGG*) na kuipa majukumu na mamlaka ya kuyatekeleza majukumu hayo.

Kwa mujibu wa Ibara ya 130(1) ya Katiba, majukumu ya *CHRAGG* ni pamoja na kuhamasisha hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii; kupokea malalamiko ya uvunjaji wa haki za binadamu na kuyachunguza na kama itabidi, kufungua mashauri Mahakamani ili kuzuia uvunjaji wa haki za binadamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 129(2) na (3) ya Katiba, *CHRAGG* inaundwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wengine wasiozidi watano na Makamishna Wasaidizi, ambao wote wanateuliwa na Rais baada ya mashauriano na Kamati ya Uteuzi. Kwa mujibu wa Ibara ya 129(5), ukomo wa kushikilia nafasi ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wote ni vipindi viwili vya miaka mitatu mitatu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina taarifa kwamba, kwa sababu ya ukomo huo wa kikatiba, *CHRAGG* kwa sasa haina Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wala Makamishna kwa sababu walikuwepo walishafikisha ukomo wa ofisi zao na Rais hajateua wengine wapya. Kama taarifa hizi ni za kweli basi inatoa ujumbe mbaya sana kwa wananchi kwamba masuala ya haki za binadamu na wajibu muhimu kwa jamii sio kipaumbele cha Serikali. Dhana hii inatiliwa nguvu na ukweli kwamba katika mwaka huu wa fedha, jumla ya shilingi 824,918,000 ambazo ni fedha zote za maendeleo zilizotengwa kwa *CHRAGG* ni fedha za kutoka nje. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuthibitisha ukweli wa taarifa hizi na kulieleza Taifa ni kwa nini hali hii imeruhusiwa itokee. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni chini ya uongozi wa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman A. Mbowe kwa ushauri na ushirikiano uliowezesha maandalizi ya maoni haya. Aidha, niwashukuru familia yangu, mke wangu mpenzi Alicia Bosensera na mapacha wetu Agostino Lissu na Edward Bulali kwa kuendelea kuvumilia upweke unaotokana na *Daddy* kuwa mbali muda mwingi kwa sababu ya majukumu mazito ya Kibunge. Aidha, niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Singida Mashariki kwa imani na nguvu wanayonipa kila siku kwa kuendeleza msimamo wetu thabiti wa kukataa kunyanyaswa, kunyonywa na kupuuzwa na *Ndaa ya Njou!*

Mwisho, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru viongozi, wanachama na wapenzi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wananchi wote wa Tanzania ambao wameendelea kutuunga mkono na kututia nguvu katika kipindi hiki muhimu katika historia ya nchi yetu. Nawaomba waendelee kutuunga mkono na kututia nguvu katika siku ngumu na za majaribu makubwa zinazokuja! (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya marefu, naomba kukushukuru na wewe binafsi na naomba kuwasilisha. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Tundu Lissu kwa hotuba yako na kabla hatujaingia kwenye wachangiaji ambao kama nilivyosema watakuwa wawili, labda niseme tu juu ya ninavyomfahamu Mheshimiwa Tundu Lissu. Pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuna Ukumbi kama huu unaitwa Nkrumah, kuna sheria zisizoandikwa za vyuo na sheria moja katika hiza ilikuwa inasema; "Mwanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Chuo Kikuu yaani *Njuka* haruhusiwi kusema ndani ya ukumbi wa Nkrumah katika mkutano wa hadhara. Mwanafunzi peke yake aliyejunja mwiko huo akiwa *first year* alikuwa ni Tundu Lissu. (*Makof/Kicheko*)

Sasa namwita Mheshimiwa Maulida Komu na atafuatiwa na Mheshimiwa Agellah Kairuki.

MHE. MAULIDAH ANNA VALERIAN KOMU: Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama kwenye ukumbi huu Mtukufu leo hii kutokana na kuzorota kwa afya yangu na kuwashukuru wale wote wanaoniombea na namwomba Mwenyezi Mungu atairudisha kama ilivyo kuwa *Inshallah*, Amina. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii leo ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana. Wizara ya Katiba na Sheria, Katiba ndio kichwa cha nchi, moyo ndio sheria za nchi, kimojawapo kikifeli hakuna kitu kitafanyika hapo. Kinachonishangaza naomba kabla ya yote uniruhusu kwanza nisome hii ni Katiba ya Nchi, naomba unipe nafasi nisome

machache tu kwenye ibara ambazo zinazungumza kuhusu ukweli na uaminifu na utu wa mtu ndani ya nchi yake. Kwenye Ibara hii ya 9 (h) inasema kwamba "Tuhakikishe kwamba Sheria za Nchi zinalindwa na zinatekelezwa" na nytingine inasema kwamba "Aina zote za dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa, uonevu au upendeleo zinaondolewa ndani ya nchi. Vile vile (J) inasema kwamba "Shughuli za uchumihaziendeshwi kwa njia zinazoweza kusababisha ulimbikizaji wa mali au njia kuu za uchumi katika mamlaka ya watu wachache binafsi".

Mheshimiwa Naibu Spika, siongei hayo, hayo yamo ndani ya Katiba ya Nchi ambayo ndio kichwa na ukiangalia hayo yote niliyozungumza hakuna hata moja linalotekelzezeka. Nchi hii leo imekuwa tuseme kama alivyosema baba yangu Ali Hassan Mwinyi kichwa cha mwendawazimu. Kila mmoja anafanya anavyoona yeye kwa upande wake itamsaidia yeye. Hakuna ambaye yuko katika nchi hii amekabidhiwa madaraka, aliyopo ndani ya nchi hii anayefanya kazi kwa kumuonea huruma Mtanzania aliyeko kijiji ni anayehangaika. Sheria zinatungwa hapa, tunazitunga sisi wenywewe na cha ajabu ni kwamba, sisi ndio tulioletwa na wananchi katika jengo hili kwa ajili ya wao. Sasa kama sisi tumeletwa na wananchi kwa ajili ya wao halafu sisi ndio tunatangulia kuvunja sheria na kufanya vituko vya ajabu na kujibu masuala ya wananchi hapa kiholela holela sijui tunakwenda wapi. Utaona mtu anasimama anasema kitu cha maana hapo mbele ya ukumbi huu, Waziri mhusika anacheka, unacheka nini, kitu gani kinakuchekesha, wakati kinachozungumzwa ni kitu cha uchungu ndani ya nchi hii kinachoendeshwa vibaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimesoma kwenye hotuba ya Waziri kumbe wao ndio wasimamiaji wakubwa wa sheria na wao ndio wasimamiaji wakubwa wa mikataba. Nilikwenda kwenye semina ya TAKUKURU kama wiki moja au mbili zilizopita nyuma, nilishtushwa kusikia eti mwekezaji anakuja ndani ya nchi hii anaanza kuwekeza, anaanza kufanya anavyotaka halafu ndio tunakaa tunafanya mikataba. Mungu wangu! Tumekuwa tunafanya *experiment*. Maana yake vijana wa leo wanakwambia sioi kabla sijaangalia. Sasa ina maana na sisi tunafanya hivyo mpaka mwekezaji aangalle, afanye anavyotaka halafu eti ndio tuje tumpe ridhaa. Kama tunafanya hivyo, naomba kuanzia leo jambo hilo likome. Hii nchi tumekabidhiwa na wananchi. Serikali iliyoko madarakani imewekwa na wananchi. Hawana haki ya kufanya kitu kama wananchi hawakutaka kitu kile, mpaka wananchi watafutwe waambiwe sasa tunasema aah wananchi wako mbali. Basi sasa kama wananchi wako mbali nini maana ya kuwa na Bunge, kwa sababu wao ndio wametuleta hapa. Kama tutakaa hapa tunashabikia vitu vya ajabu eti kwa sababu ni Mwana-CHADEMA, kwa hiyo kitakachozungumzwa na Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Freeman Mboge hata kama kikiwa mseto, nicheke nishangilie, hamna. Hamna vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kuna kitu kikubwa zaidi katika nchi kinaweza kikaangamia kama tutajaza mikataba ya ajabu ajabu. Ikiwa kweli hilo linatendeka nilishtuka siku ile, nilishtuka sana na *privileges* na *rights* tunazowapa wawekezaji katika nchi hii ni za ajabu halafu tunalia hatuna kipato. Katiba ni makubaliano, Katiba sio ya kuifanya utani, tunataka kurudisha kama alivyosema Waziri Kivuli wangu hapa kwamba Serikali iliyowekwa na wananchi ndio wakae wapendekeze wanavyotaka wao halafu warudishe kwa wananchi halafu wananchi wakubaliane na wao yanakwenda wapi hayo, kwani kuna haraka ya nini. Tuwasikilize kwanza wananchi wa makundi mbalimbali, wanaelewa matakwa mbalimbali, wa makundi mbalimbali tuwasikilize wanawake wanasema nini, vijana wanasema nini, siku hizi watoto wamekalambuka, wana mabaraza yao ya wanafunzi kwenye mashule, wanazungumza utashangaa mtoto anavyozungumza. Tuwasikilize, tuwape haki wote kwanza, kisha tukae kitako tuyachekeche hayo tutoe Katiba ambayo itaiweka nchi hii kwenye misingi ya haki ya utawala. Sio tunataka tu kuleta kuvutana vutana hapa na kuzungumza vitu vya ajabu ili nimpendekeze fulani afurahi apendezewe aone raha, hapana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye sheria, sheria tunazitunga hapa, nani kijiji ni anazijua sheria hizo. Leo tulikuwa kwenye semina ya akinamama na unyanyasaji unaofanywa kwa akinamama, sheria zipo zilitungwa, lakini mama gani kule kijiji ni anajua kwamba kuna sheria gani ina haki naye, ananyanyasika, anateseka hajui pa kukimbia. Tunasema kwamba kuna mpango wa kusaidia kwenye hotuba ya Waziri kwamba eti huko vijiji kutakuwa na wanasheria wa kuwasimamia wananchi kwenye haki zao wakati wanakwenda kwenye mambo ya Mahakama. Wanajua hao wananchi kama kuna kitu kama hicho. Mnajua kwamba kuna kitu kama hicho kikienda kule kwa wananchi anaingia Polisi bure anatoka kwa pesa, mnaelewa hayo? Kama

tunataka kufanya haki basi kule kule kwenye Halmashauri zetu tuanze kwanza kuwapa elimu Madiwani wetu. Madiwani waelewe sheria zinavyokwenda na haki za wananchi kwenye maeneo yao. Madiwani tuwape nguvu, fedha na haki ya kwenda kule kuwafundisha wananchi wao kuwaambia haki zenu ni moja, mbili, tatu, nne na kuwafungua macho, hawajui wale na eti wale ndio waliotuleta hapa. Tumejua hapa kwa ajili yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tuko mbali, tukifanya utani hii nchi ambayo sisi tulioko huko hatufuati sheria halafu tunasema kwamba eti walioko chini hawafuati sheria, wanachukua sheria mkononi, wanachomana moto wanatiana matairi tunawaonea. Tuanze kujitakasa sisi wenyeewe kwanza, tuanze kujua sisi wenyeewe kwanza tuna msimamo wa aina gani. Huwezi ukamwambia eti Polisi aende akamkamate mtu aliyefanya vibaya kule nje amlete Polisi yeye mwenyeewe mshahara wake ni shilingi 10,000/=, halafu eti amtoe hivi hivi bila ya kumwambia ebu fanya basi na mimi, haiwezekani! Yale yale aliyojasema hapa Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba tunasema siku zote sungura, huyu sungura atakuwa lini tembo. Siku zote sungura, sungura, hiyo kauli sasa ife, Mwenyezi Mungu anasema ninapokupa ukawa huna shukrani basi nitazuia kukupa. Tunapopata kile tunachopata hiyo hiyo trilioni sitana *point* tunayopata ambayo leo bajeti ya shilingi trilioni 11 wakati hatuna makusanyo ya trilioni saba au nane, tunasubiri watu watusaidie, tunapofika hapo tu ndio sheria hazifanyi kazi, tunapofika hapo tu ndio tunasema Mahakama haina vitendea kazi, tunapofika hapo ndio tunazungumza tuvute busara, tuvute hekima jamani sungura mdogo. Tukubali kula hasara ya kutumia kidogo tulichonacho kwa ajili ya kutaka kuleta kingi. Kama hutaki kutumia kile kidogo ulichonacho na kingi hupati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi yote tuliyonayo inatuhinda nini kuiendeleza na leo tunataka kutunga sheria hapa tuseme wawekezaji tuwakabidhi ardhi waje muone jinsi wananchi watakavyonyanyasika, wawekezaji wachache tu wapo hapa wanaleta mpaka mpishi, mfagaji kutoka kwao, tunaambiwa nini eti Watanzania hatuna uwezo wa kufanya kazi ni wavivu na sisi tunakubali. Je, tulishawapa hizo sheria hawa wananchi au tulishawafundisha hao wananchi au tulishawapa *moral* ya kufanya kazi wakashindwa. Kama vijana wamejaa barabarani huko wanalipuka nyie mnasema hawafuati sheria, watafuata sheria wanazijuaje, wamesoma wapi hizo sheria hawa vijana, hawajui sheria yoyote zaidi ya kuvuta *bhangi* na kula unga basi ndio sheria yao na ndivyo walivyokuwa na sisi wenyeewe ndio tumewaacha wafike hapo walipofika, halafu sisi wenyeewe tunawalaamu kwa nini wamefika hapo. Ni kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina nguvu nimeishiwa, lakini nasema hivi kama tusipoangalia uozo ulioko sasa hivi tujuue tunapokwenda miaka minne, mitano mbele tunakwenda kubaya tutageuka kama mende tutaanguka chali na tutashindwa kumpata wa kutuokoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Maulidah Komu kwa mchango wako na pole sana kwa kuugua tunakuombea kheri. Mheshimiwa Angella Kairuki.

MHESHIMIWA ANGELLA J. M. KAIRUKI: Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Kabla yako Mheshimiwa Waziri alisimama. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

MWONGOZO WA SPIKA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima kwa kutumia kanuni namba 68(7) na kwa mujibu wa kanuni namba 64(g).

Mheshimiwa Naibu Spika, namheshimu sana sana, dada yangu Mheshimiwa Maulidah Komu. Vile vile nina uvumilivu kusikiliza wengine, lakini inapotokea kwamba kuna sababu ya kusimama hapa inabidi nifanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Maulidah Komu alisema kwamba kuna wawekezaji wanaoanza shughuli kabla ya makubaliano au mikataba kuingiwa, ingependeza sana kama tutapata kujua mwekezaji huyu ni nani ili tuweze kufuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mheshimiwa Maulidah alisema kwamba kuna maswali yanayoulizwa na Waziri anacheka. Hili ni jambo ambalo wananchi wakilisikia na kama ni kweli halipendezi, ingependeza kujua ni Waziri gani ambaye anacheka kwa sababu lugha hiyo kwa kweli inadhalilisha na kama kuna Waziri ambaye amefanya hivyo ni vyema basi akisimama hapa na akaomba radhi kwa sababu kwa mujibu wa majukumu tuliyopewa hatupaswi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Angella Kairuki!

MHE. ANGELLA J.M. KAIRUKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naamini dakika zangu zitabaki pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kabisa kabla sijazungumza chochote *ni-declare interest* kwamba nilishafanya kazi katika Wizara ya Katiba na Sheria hususan Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwanza kabisa naomba kulpongeza sana Wizara ya Katiba na Sheria kwa kazi kubwa ambayo inaifanya kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Jaji Mkuu Chande, pamoja na Mheshimiwa Jaji Werema, Mwanasheria wetu Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niseme kwamba bajeti hii ni ndogo sana. Ukiingalia kwa tarakimu, shilingi bilioni 138.7 inaweza ikaonekana ni fedha nyangi sana, lakini wote kabisa tunafahamu majukumu mazito yaliyopo katika Wizara hii. Majukumu mazito ambayo mnajua kabisa, Wizara hii imechanganyika pamoja na mhimili wa Mahakama. Wote mnafahamu bajeti ambazo zimekuwa zikitolewa kwa Bunge pamoja na Serikali. Kwa ujumla, kwa kweli fedha hizi hazitoshi. Upungufu huu mkubwa wa bajeti kwa Wizara ya Katiba na Sheria utaleta athari kubwa sana. Athari ya kwanza ni kufukuzwa katika majengo ya ofisi ambayo wamepangisha. Ofisi ya *DPP* inalipa takriban shilingi bilioni 1,489,000,000 kwa ajili ya kodi katika majengo ambayo wanapangisha. Ofisi hizi ziko katika Mikoa ya Shinyanga, Mbeya, Arusha, Dar es Salaam, (*Sukari House* na Benjamin Mkapa) kwa kweli ni fedha nyangi sana. Hivyo basi, ningependa Serikali iangalie namna ifanye iwezavyo, jamani wote hapa ni waathirika wa sekta hii, kama si sisi moja kwa moja, lakini ndugu zetu na wananchi ambaa tunawawakilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bajeti hii Mawakili wa Serikali watashindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo, watashindwa kuhudhuria Mahakamani kama wanavyopaswa, itakwamisha kabisa mfumo mzima wa uendeshaji wa kesi na itapelekea kuongezeka kwa mrundikano wa kesi Mahakamani na jambo hilo litasababisha msongamano wa mahabusu. Wote tunajua hili litazidi kuchelewesha upatikanaji wa haki nchini. Mwaka 2008 Bunge letu lilipitishwa Sheria ya *National Prosecution Services Act* inayotoa madaraka ya kutenganisha upelelezi na shughuli za uendeshaji wa mashtaka. Sasa kwa bajeti hii kwa kweli *DPP* ametengewa shilingi bilioni tatu na kama shilingi bilioni 1.48 inakwenda kwenye kodi za majengo, nikiwa kama mwakilishi wa wafanyakazi, maslahi mbalimbali ya wafanyakazi yatakwamishwa na ningemshauri *DPP* apeleke kwenye posho za wafanyakazi na majengo tusubiri kwanza, Serikali itafute fedha nyagine na haiwezekani nusu nzima ya bajeti tukaipeleka kwenye majengo wakati yako majengo mengi kabisa ya Serikali yako wazi. Vile vile, tutapelekea matumizi mabaya ya rasilimali watu ambayo itakaa ofisini bila ya kufanya kazi yoyote, waende Mahakamani kufanya nini, wataishia kukaa maofisini, kwa kweli si haki mliangalie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, inatakiwa weledi wa hali ya juu kwa Mawakili wa Serikali. Lakini kwa fedha hizi watawapeleka vipi mafunzo jamani? Kuna changamoto mpya mbalimbali katika maeneo ya utakasishaji wa fedha haramu, katika maeneo ya wizi kupitia mitandao ya kompyuta, majadiliano ya mikataba, uandishi wa mikataba, uandishi wa sheria pamoja na urekebu wa sheria. Ni dhahiri kabisa, bajeti hii lazima iboreshwe pamoja na kwamba Mawakili hawa wa Serikali waliongezewa

mshahara katika miaka ya hivi karibuni, lakini bado kwa majukumu wanayoyafanya mishahara yao ni midogo sana. Huwezi kulinganisha na hauna uwiano sawa ukilinganisha na taasisi zingine na vyombo vinavyofanya upelelezi kama vile TAKUKURU na vinginevyo. Wanapokwenda Mahakamani, TAKUKURU wamekuwa wameshafanya upelelezi lakini Wakili huyo wa Serikali jamani ndiye anayeendesha mashtaka, ndiye anayeonekana kwa ndugu wa mtuhumiwa yule. Watu hawa hawalipwi *risk allowance*, wanatiwa kwenye majaribu makubwa na hatari kubwa. Watu hawa hawalipwi *communication allowance*. Inafika wakati mtu yuko Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu anatakiwa awasiliane na Ofisi ya CID Temeke lakini hana fedha ya kufanya mawasiliano. Jamani, atumie fedha yake ambayo hana. Wenzetu wengine kwenye Taasisi za Upelelezi wamekuwa wakipewa posho ya mafuta, Mawakili hawa wa Serikali hawaipati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka wiki mbili zilizopita wakati wa mgomo ule wa vituo vya mafuta nilipigwa simu na baadhi ya Mawakili hawa wakilalamika, wengine walifika wakati hata kwenda ofisini ilikuwa tabu, hawakuwa na nauli. Nieleze ukweli, mimi mwenyewe nimeshakuwa na bosi wangu wa zamani yuko pale Ndugu Kyuki anakumbuka kuna nyakati nilikuwa nikimtania, watu walifika wakati wanakopa mshahara wanabakiwa na shilingi 8,000/= kama mshahara. Nilikuwa nikimtania hivi, siku nikiamka asubuhi ukinipigia simu kwa nini Angellah umechelewa nikikwambia sijaja sina nauli utanifanya nini? Nimeona *priority* yangu nihudumie wanangu, siwezi kuacha kula nikatenga nauli ya mwezi mzima jamani, tuwaangalie watu hawa wanateseka na haikubaliki. Hususan watu hawa endapo wataamua wagome, aidha kwa sababu za msingi, kweli hana nauli au anaweza akaamua kusema sina na kumbe anayo. Kesi hizi kama tunavyofahamu kwenye Kesi za Madai zinaweza zikasikilizwa upande mmoja, Mheshimiwa Tundu Lissu atakubaliana na mimi hapo na mnajua ikisikilizwa *ex parte*, madhara yake kwa Serikali ni makubwa. Lakini kwa Kesi za Jinai madhara yake ni kwa mwananchi yule ambaye anazidi kuteseka mahabusu, tuwaangalie watu hawa. Kwa hiyo, tunapopitisha bajeti hii mtaiona ni kubwa lakini kwa kweli ni ndogo na haikubaliki machoni mwa binadamu yejote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawakili hawa wa Serikali wengine ni Mawakili wa Kujitegemea. *Wame-sacrifice*, wameamua kuitumikia nchi hii. Viko vivutio vingi katika *Private Firms* huko nje lakini wamekuwa wazalendo na wanafanya kazi kuititia Serikali hii. Wanakosa posho mbalimbali ambazo wangeweza kuzipata na vivutio vingine huko nje. Jamani muwafikirie muwape *non practising allowance* ili muweze kuwa-retain.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala la posho ya nyumba, kwa *nature* ya kazi ambazo wanazifanya jamani zinahatarisha. Mimi binafsi nilishiriki kuendesha kesi ya Babu Seya natolea tu mfano, ziko kesi nyingine nyingi za hatari, unakuta mtu anapangisha nyumba *let us say* ya mtuhumiwa wa madawa ya kulevyta, humo humo ni nyumba ya ndugu wa mtuhumiwa huyo. Kweli jamani? Ni hatari! Tuwasaidie watu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo Wakala wa Majengo kuna nyumba ambazo zimebakni na kuititia Shirika letu la Nyumba la Taifa kipaumbele wapewe watumishi hawa jamani. Kwanza itawasaidia wawe karibu na ofisini na itawasaidia wasitumie gharama kubwa katika usafiri. Lakini kwenye vyombo vya usafiri, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma waangalie namna ya kuwapatia mikopo ya magari na waweze kuwa-guarantee ili mtu anavyoanza kazi angalau aweze kupata chombo cha usafiri na ikibidi mikopo ya nyumba na *pension* zao baadaye zitumike kama *security*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Jengo la Sukari *House* wana Mawakili wa Serikali takriban 20 mpaka 40. Lakini wanatumia chombo kimoja cha usafiri na tuna fahamu Mji wetu wa Dar es Salaam ulivyo *scattered* na tunafahamu Mahakama zetu pia ambazo zimesambaa sana. Kwa hiyo, nitoe rai kwa Waziri aangalie namna ya kutafuta vyombo vingine vya usafiri ili kuweza kuwasaidia kuwahudumia watumishi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuongelea suala la upandishwaji wa vyeo. Niwapongeze wamepandisha Mawakili wengi vyeo, lakini ukiangalia tathmini wako ambao bado wana vyeo ambavyo havistahili na viko chini sana. Kwa hiyo, niombe ifanyike tathmini ili kila

mwenye cheo chake apate haki ambayo anaistahili kulingana na miaka ambayo amefanya kazi pamoja na uzoefu wake. Hapo angalau nimegusa kidogo ingawa sijamaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niingie kwenye Mahakama. Tumeelezwa shilingi bilioni 20 zimetengwa kwenye Mfuko wa Mahakama na tunafahamu sote kuna tatizo kubwa la mrundikano wa kesi. Napenda Mheshimiwa Waziri atakavyokuja kufanya majumuisho yake hapa atueleze. Tunafahamu kuna mpango wa kupunguza mrundikano wa kesi ambao uko kwenye awamu ya pili. Lakini ukiangalia kuna mashauri 2,857, yaliyosikilizwa ni mashauri 789. Hivi sasa yamebaki mashauri 2098 na yeze ametueleza watapunguza mashauri 960. Hii ni asilimia 28 jamani. Katika mashauri 2,098 upunguze mashauri 960 ya nyuma unatesa watu na bado kuna mashauri mapya mengi yanaendelea kufunguliwa. Napenda atueleze wanatumia vigezo gani katika kupunguza mrundikano huo wa kesi? Haziwezi kufanana! Katika Mahakama ya Mwanza labda imekaa miezi sita, Mahakama ya Wilaya labda imekaa mwaka mmoja na Mahakama Kuu mwaka au zaidi. Kuwe na vigezo, ni kesi ipi wanaitathmini kama ni ya muda mrefu na imekaa kwa muda gani kwa ngazi husika na aina ya kesi yenye. Natambua Wizara ya Sheria imefanya *Case Flow analysis*. Napenda atueleze ni mapendekezo gani ambayo yamependekezwa *case flow analysis* hiyo na ni yapi ataanza kuyatekeleza?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni Wazee wa Baraza, Wazee hawa wa Baraza wanafanya kazi kubwa lakini ukiangalia kiwango cha posho ambayo wamekuwa wakilipwa ni ndogo sana na haiendani na kazi kubwa wanayoifanya. Pia niongelee jengo la Mahakama ya Rufani. Kwa habari ambazo nimezikia kuna mipango ya kuifanya Mahakama hii kuwa maegesho. Kwa kweli hili halikubaliki hususan ukiangalia historia kubwa iliyopo katika utoaji wa haki hapa nchini kuhusiana na jengo hili na haswa ukizingatia liko karibu na Mahakama Kuu pamoja na jengo la Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia nirudi kidogo kwenye ofisi ya *DPP*. Tulielezwu hapa kupitia Sheria ya *NPS* kwamba ofisi hii itakuwa Mamlaka inayojitegemea. Wenzetu wote wa Afrika Mashariki ni Mamlaka zinazojitegemea, ni Tanzania peke yake *DDP* amebanwa. *DDP* sio Mamlaka Ajiri, akitaka kuajiri lazima kupata kibali cha Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Akiwa na mtumishi mzuri amemfundisha, *DAG* anaweza akaamua kumhamisha. Kwa hiyo, umefika wakati sasa Waziri kwenye majumuisho yake atueleze kikwazo ni nini na ni lini *DDP* atakuwa ni Mamlaka inayojitegemea na Mamlaka Ajiri?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni Mfumo ambao Mwanasheria Mkuu wa Serikali anautumia katika Kanda mbalimbali Mikoani. Kwa mfumo uliopo sasa, Kanda zile watu wa *DDP* wamekuwa wakitumika kuendesha mashauri ya Idara zingine zilizoko Makao Makuu. Kwa kweli ukizingatia tumeanzisha mchakato wa kutenganisha Upelelezi na Mashtaka, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Angella Kairuki, tunakushukuru sana kwa mchango wako na kwa kweli umeonesha uzoefu mkubwa. Dakika zangu zimebaki chache sana nilimwona Mheshimiwa Machali kama unaweza kutumia dakika moja na si zaidi kwa ulichonacho.

TAARIFA

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa. Wakati nimesimama nitaka kumpatia Mheshimiwa Mary Nagu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwezesaji na Uwekezaji taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8). Ni kwamba Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anachangia amezungumza kwamba baadhi ya Mawaziri huwa wanachekache. Naomba nimkumbushe hata hapahaha wakati Mheshimiwa Tundu Lissu alipokuwa akizungumza wapo walikuwa wanachekache japo sitaki kuwa-mention. Lakini pia wakati Waziri wa Maji alipokuwa akihitimisha Hoja yake leo mchana hata simu ziliikuwa zinapigwa na alikuwa akichekacheche vilevile. (*Makof*)

Kwa hiyo naomba taarifa hiyo aipokee na pili kuhusiana na suala zima la wawekezaji.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sendeka naomba ukae. Nilimalize la Mheshimiwa Machali. Ile 68(8) inasema hivi: "Vilevile Mbunge yeoye anaweza kusimama mahali pake na kusema taarifa na kwa ruhusa ya Spika atatoa taarifa au ufanuzi kwa Mbunge anayesema wakati huo ambapo Spika atamtaka Mbunge huyo aketi chini ili apokee maneno hayo." Kwa kuwa lilishasemwa zamani kwa utaratibu huo ukiutumia Mheshimiwa Machali uko nje ya utaratibu.

Mheshimiwa Ole Sendeka!

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, sina hoja tena, hoja yangu ilikuwa ni kumpa taarifa hiyo.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Dakika zangu kama nilivyosema zimekwisha sana, naomba tusikilizane Waheshimiwa Wabunge. Nitaanza na Mwongozo ambaa aliuomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwezesajili na Uwekezaji, Mheshimiwa Mary Nagu katika mambo mawili. Yeye ametumia Kanuni ya 64(1)(f) na (g). Alichokizungumza ni kwamba Mawaziri wanachekachecha. Katika namna aliyoitumia ni lugha ambayo kwa kweli upande wa Mawaziri kwa Kanuni hiyo ni lugha ya kuudhi. Ni lugha ya kuwafanya kama vile hawako *serious* na mambo.

La pili kwamba Serikali inaruhusu wawekezaji kuwekeza bila kuingia mikataba, nalo sioni uzito wake ameliweka katika msingi gani. Lakini mwongozo wangu ni huu ufuatayo:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Maulida Komu alikuwepo hapa wakati unatoa maelezo yake na baadaye akatoka. Lakini kabla ya kuchangia alinifahamisha kwamba hali yake ya kiafya haikuwa nzuri. Ninachohisi ni kwamba kwa kweli alikuwa hajisikii vizuri, kwa hiyo tumsamehe tu bure. Kwa hiyo, mwongozo ninaoutoa ni kwamba, jambo hili kwa kweli Mheshimiwa Maulida Komu ni mtu mzima, Mbunge makini, naamini alikuwa hajisikii vizuri tu ndiyo imesababisha hali hii.

Naomba nimalizie kuhusu mwongozo aliuomba Mheshimiwa Lekule Laizer asubuhi. Ili tusiweke viporo tunaelekea mwisho. Mheshimiwa Lekule Laizer alionomba mwongozo kwamba ninyi Waheshimiwa Wabunge mmetuachagua sisi, Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Naibu Spika, Wenyevit wa Bunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Viongozi wengine tunaoongoza Bunge hili lakini kuna wakati tunawakaripia. Niseme tu kwa hili kama linajitokeza kwa kweli hatupaswi kuwakaripia kwa sababu ninyi ni wapiga kura wetu na yeoye aliyechaguliwa kwa kura kwa kweli huwa hawezu kumkaripia mpiga kura wake. Kwa hiyo, katika eneo hilo kwa kuwa sisi ni binadamu endapo tunakosea tunaomba radhi. (*Makof*)

Lakini la pili, ni suala la Ofisi za Wabunge na Bajeti ya Bunge, maswali yake bado yataendelea kuulizwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu au Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali itajibu pamoa na ukweli kwamba sasa masuala ya Ofisi za Wabunge yatahamishiwa chini ya Tume ya Huduma za Bunge lakini kwa vile Bajeti ya Serikali inayowasilishwa hapa Bungeni inawasilishwa chini ya Waziri Mkuu bado katika utaratibu wetu wa maswali, Mheshimiwa Mbunge akitaka kupata ufanuzi wa jambo hilo haiwezekani kumuuliza Mheshimiwa Spika au Katibu wa Bunge. Bado maswali yatakwenda kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makof*)

Baada ya Mwongozo huo nina hakika hakuna kilichobaki kwa shughuli zilizopangwa leo zimekamilika, tutaendelea tena na Wizara hii kuimalizia saa saba na nusu mchana. Kwa jinsi hiyo basi naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 12.32 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 25 Agosti, 2011 saa tatu asubuhi)

